**11 JUNI, 2026**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Arobaini na Nane – Tarehe 11 Juni, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**SPIKA:** WaheshimiwA Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:**

Maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ENG. MSHAMU A. MUNDE):**

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha *(Monetary Policy Statement)* kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mheshimiwa Abdallah Chikota.

Na. 569

**Ujenzi wa Vituo vya Afya Chawi na Mnima**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza: -

Je, lini fedha za ujenzi wa Vituo vya Afya vya Chawi na Mnima zitatolewa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Jimbo la Nanyamba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 hadi kufikia 2025/2026 Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 2.7 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Mji Nanyamba, Vituo vya Afya Kitaya na Nyundo pamoja na ukamilishaji wa maboma nane ya zahanati katika Halmashauri ya Mji Nanyamba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 300 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya Hospitali ya Halmashauri ya Mji Nanyamba.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu kwenye vituo vya afya 364 vinavyoendelea na ujenzi kote nchini, kisha kuendelea na ujenzi wa vituo vipya vya afya katika kata zitakazokidhi vigezo, zikiwemo Kata za Chawi na Mnima katika Halmashauri ya Mji wa Nanyamba. Ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, Kata ya Mnima na Kata ya Chawi zina idadi kubwa sana ya watu. Kwa kuwa kata hizi zimeainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi, je, Serikali sasa itamke rasmi ni lini ujenzi huo utaanza?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; ninaipongeza Serikali kwa kutupa watumishi 60 katika mgao wa hivi karibuni, lakini kama alivyoainisha hapo tuna vituo vya afya sita na Hospitali ya Mji wa Nanyamba bado idadi ya watumishi haitoshelezi.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutuongezea watumishi katika vituo vya afya na Hospitali yetu ya Mji wa Nanyamba? Ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Jimbo la Nanyamba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia vituo hivi na kweli vimo kwenye ilani yetu ya uchaguzi ya mwaka 2025 hadi 2030. Tutaendelea kutekeleza ujenzi wa vituo hivi. Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tumekwishatenga bajeti ya kujenga vituo 111 katika kata zote

ambazo zimekidhi vigezo na tutaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivi.

Mheshimiwa Spika, la pili, anashukuru Serikali kwa kuendelea kupeleka watumishi, kupitia vibali ambavyo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliruhusu tuajiri watumishi 5,000 nchi nzima tutaendelea kuongeza watumishi katika vituo vyetu vya afya ili waendelee kutoa huduma ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amezamiria kuacha tabasamu kwa Watanzania. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, TAMISEMI walituahidi kujenga vituo vya kimkakati na kuna halmashauri ambazo tayari fedha zilitoka tangu Bunge lililopita, na kuna halmashauri ambazo hatujapata. Nilipowasiliana na Mheshimiwa Profesa Shemdoe akasema mchakato unaendelea, lakini hadi sasa mchakato huu haujakamilika, hususani sisi watu wa Makete, Kituo cha Matamba ambacho kiko katika hizo fedha ambazo tunasubiri kutoka Hazina.

Je, ni lini Serikali itatoa fedha hizo ili Kituo cha Matamba kianze kujengwa, kwa sababu kinahudumia takribani kata tano na wananchi wa pale wamekwama kwa muda mrefu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Festo, Mbunge wa Jimbo la Makete kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tulifanya ziara Makete na tukajionea wananchi walivyo na ari, wanavyoiamini Serikali yao inavyoendelea kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu tayari liliidhinisha fedha za kwanza ambazo zilikwenda katika vituo vya afya vya kimkakati katika majimbo 120. Tayari tumekwishawasilisha kwa wenzetu Wizara ya Fedha zaidi ya majimbo 94 ambayo mwaka

huu wa fedha zinakwenda kuidhinishwa zaidi ya shilingi bilioni 23.5 kwa ajili ya kukamilisha vituo vya kimkakati ambavyo majimbo hayajapata.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Festo pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine kwamba tutaendelea kujenga vituo hivi na tayari tumeshawasilisha maombi Wizara ya Fedha. Ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Katika Kata ya Hunyari Serikali imejenga kituo cha afya, lakini hakuna jengo la upasuaji na hili swali hapa nimeuliza mara 300 kidogo.

Je, ni lini sasa Serikali itapeleka fedha za jengo la upasuaji kwenye Kituo cha Afya Hunyari?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Getere, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ilijielekeza kwanza kujenga majengo ya *OPD* ili wagonjwa wetu waendelee kupata huduma, lakini pia nimhakikishie Mheshimiwa Getere pamoja na wanajimbo na wananchi wanaowahudumia kwamba tutaendelea kutenga fedha kuhakikisha tunakamilisha miundombinu hii katika kata hizi. Miongoni mwa kata ambazo zitapokea fedha kata 111, vituo 111 vya afya kukamilisha majengo ambayo yaendelee kutoa huduma katika majimbo yetu na vituo vyetu. Ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnesta.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Zahanati ya Tabata A ni zahanati ambayo imefunguliwa mwaka 1976 na hivi sasa ninavyoongea inahudumia kwa siku wagonjwa 300 mpaka 350. Zahanati hii inategemewa na kata zaidi ya nne zinazozunguka maeneo hayo.

Je, Serikali wako tayari kuipandisha hadhi zahanati hii kuwa kituo cha afya ili iweze kutoa zile huduma stahiki kulingana na hayo mazingira ambayo nimeyaeleza kwa kuwa tayari zahanati hii ina sifa zote kabisa za kupandishwa kuwa kituo cha afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kaiza kama alivyoliuliza.

Mheshimiwa Spika, *nature* ya Jimbo la Segerea ni miongoni ya majimbo yenye idadi kubwa ya watu. Kwa hiyo, nimwelekeze Mkurugenzi kuleta maombi maalum Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ili tuweze kulipokea na kuanza mchakato wa kuipandisha zahanati hii kuwa kituo cha afya na iendelee kutoa huduma kwa Wana-Segerea. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Lufungija.

**MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia. Nilitaka kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba Kituo cha Afya cha Tarafa ya Kashishi kilichopo katika Kata ya Kashishi ni kituo cha afya kinachojengwa kwa mapato ya ndani. Sasa yapata miaka mitano tunalo jengo la wagonjwa wa nje na jengo la maabara. Changamoto kubwa tuliyonayo ni jengo la wazazi ambalo tayari msingi umeshajengwa.

Je, ni lini jengo hilo litapatiwa fedha na Serikali ili kuweza kukamilika liweze na kutoa huduma kwa wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lufungija, Mbunge wa Jimbo la Ulyankulu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha miundombinu hasa katika eneo la afya ya mama na mtoto. Nimhakikishie Mheshimiwa Lufungija kwamba kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tutaendelea kutenga fedha na nilimuahidi tutakwenda jimboni nikaone huo msingi ambao tayari halmashauri wameshaanza ili tuweke msisitizo katika ujenzi wa jengo hili la mama na mtoto. Ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Stella Ikupa.

Na. 570

**Kamati za Watu Wenye Ulemavu**

**MHE. STELLA I. ALEX** aliuliza: -

Je, Kamati za Watu Wenye Ulemavu zilizoanzishwa katika ngazi za Mikoa na Wilaya zinafanya kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kamati za Watu Wenye Ulemavu zimeanzishwa kwa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Na. 9 ya mwaka 2010, ikiainisha majukumu ya Kamati ambayo ni pamoja na kufuatilia upatikanaji wa huduma muhimu kama afya, elimu, ajira, ulinzi wa jamii na miundombinu jumuishi, kushauri Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri kuhusu masuala ya watu wenye ulemavu, kufuatilia utekelezaji wa mipango na bajeti zinazohusu watu wenye ulemavu, kupokea na kujadili changamoto zinazowakabili watu wenye ulemavu na kupendekeza ufumbuzi. Aidha, utekelezaji wa majukumu ya kamati hizi katika ngazi ya kijiji/mtaa, wilaya na mkoa yamefikia 52%.

Mheshimiwa Spika, kupitia kamati hizo jumla ya watu wenye ulemavu 328,733 wametambuliwa kote nchini, wakiwemo wanaume 162,464 na wanawake 166,269. Utambuzi huu umeiwezesha Serikali kupata takwimu sahihi zinazosaidia katika upangaji, utekelezaji na ufuatiliaji wa huduma mbalimbali za kijamii kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kusimamia na kuhakikisha kamati hizi zinaendelea kufanya kazi kwa mujibu wa sheria. Ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ikupa.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini haya yaliyoelezwa kwenye jibu la msingi utekelezaji wake unategemea vikao, jambo ambalo halifanyiki kwenye mikoa na halmashauri nyingi hapa nchini. Ninaomba nitumie nafasi hii kuipongeza Kamati ya Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kamati hizi vikao vyake havitumii gharama kubwa; je, Serikali ina kauli gani kuhusu kutenga fedha kwa ajili ya kuziwezesha kamati hizi kufanya kazi kwa mujibu wa sheria?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Stella Ikupa Alex kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali tumeendelea kutenga fedha, na niendelee kuwasisitiza na kuwakumbusha wakuu wetu wa mikoa wote na halmashauri zote nchini kuendelea kutenga fedha na kuhakikisha vikao hivi vinakaliwa kwa ajili ya kutatua changamoto ambazo zinawapata ndugu zetu walemavu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa utashi wake tayari amekwishaongeza idadi kubwa ya walemavu katika Bunge lako Tukufu ili waweze kusema yale ya kwao ambayo yanawasibu na Serikali iweze kuyachukua na kuyapatia ufumbuzi. Ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa mimi mwenyewe ni mdau wa watu wenye ulemavu na ni balozi pia, lakini pia niko katika Kamati ya Mkoa ya Watu Wenye Ulemavu; ni kwa nini sasa hizi Kamati pamoja na nia nzuri sana ya kuanzisha hizi Kamati bado hazijaweza kujengewa uwezo ili kujua nini wanatakiwa wafanye kwa ajili ya watu wenye ulemavu? Na ndio maana bado kuna changamoto hata ya mikopo, bado watu wenye ulemavu wengi kwenye halmashauri zetu hawapatiwi mikopo inavyotakiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa. Dkt. Kabati, Mbunge wa Jimbo la Kilolo, Mkoani Iringa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali tumeendelea kutenga bajeti na nimesema kwenye jibu la msingi kwamba tumefikia 52%. Mwanzo ni mzuri, hatujamaliza bado changamoto hizi. Tunaendelea kusisitiza uwepo wa Kamati hizi na kuleta mezani mashauriano ya namna gani tunaweza kuwafikia ndugu zetu wenye ulemavu na kutatua changamoto zao.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia kwenye ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu maeneo mbalimbali, namna anavyozungumza na watu wenye ulemavu, anakaa nao na kuwasikiliza na huwa hata hawasikilizi kupitia *microphone,* huwa anakwenda moja kwa moja kuwasikiliza.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa akitufundisha namna gani ya kuwasikiliza watu wenye ulemavu na kutatua changamoto zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ni kwamba Kamati ya TAMISEMI ikiongozwa na Mheshimiwa Kyombo, Mwenyekiti wetu walisisitiza namna bora zaidi ya kuwafikia watu wenye ulemavu katika ile mikopo ya 10% ili waweze kupata mikopo hiyo. Ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa. Tunaendelea Mheshimiwa Kamonga.

Na. 571

**Kutenga Bajeti na Kuziboresha Barabara za Vijijini**

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA** aliuliza: -

Je, Serikali imeandaa mkakati gani wa kuzitambua, kuzitengea bajeti na kuziboresha barabara za vijiji vyenye uzalishaji mkubwa ili zipitike msimu wote?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Jimbo la Ludewa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)* inaendelea kuziainisha na kuzitambua barabara zote ambazo haziko kwenye mtandao wa *TARURA* zinazopita kwenye uzalishaji mkubwa ili ziweze kuingizwa kwenye mtandao wa barabara wa *TARURA* na kufanyiwa matengenezo ikiwemo barabara za Wilaya ya Ludewa.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Ludewa, Serikali imetambua na kujenga Barabara ya Kigasi – Milo – Amani ambayo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 imetengewa jumla ya shilingi milioni 369 kwa ajili ya ujenzi wa njia za zege *(concrete strips)* na shilingi milioni 200 kwa ajili ya kuweka changarawe eneo lenye urefu wa kilometa 10. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Barabara ya Mundindi – Njelela hadi Ngogomo imetengewa kiasi cha shilingi milioni 150 za ujenzi wa kiwango cha changarawe ambapo kazi itaanza kutekelezwa mara baada ya kipindi cha mvua kuisha.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali itajenga Barabara ya Amani – Ibumi ambayo ni muhimu kwa kilimo cha mahindi. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 barabara hii imetengewa shilingi milioni 367 na itajengwa kwa njia za zege *(concrete strips)* kuanzia kibao hadi yalipo maghala ya mahindi, ikijumuisha maeneo yote ya milima ikiwemo eneo la Mkelema. Ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Pamoja na hivyo nina maswali mawili madogo ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ile barabara inayoanzia Madope kwenda Madilu hadi Ilininda mpaka Mundindi ambako kuna chuma cha Liganga ni barabara muhimu sana, kuna nguzo nyingi, viazi na mazao mbalimbali yanatoka kule.

Je, Serikali iko tayari iwapo nitaleta andiko namna ya kuiboresha kwa kiwango kinachoweza kuhimili magari mazito ili waweze kutoa fedha kwa ajili ya utengenezaji huo?

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna barabara inayoanzia Mawengi kwenda Makonde, barabara hizi za mwambao ikiwemo ya Lumbila – Lifuma zinaenda kwenye miteremko mikali, kwa hiyo, zinahitaji ziko *concrete strips* na mitaro ili ku-*control* maji.

Je, Serikali iko tayari kuongeza fedha kwa ajili ya kuboresha barabara hizi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Jimbo la Ludewa, kwa hakika anachapa kazi kubwa sana katika kuwahudumia wananchi wa Jimbo la Ludewa. Mimi nimhakikishie kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, tutashirikiana na wewe Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Ludewa kuhakikisha kwamba barabara hizo zote muhimu zinapata fedha kwa ajili ya kuziboresha.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ziko barabara zikiwemo Barabara ya Madope na Madilu ambazo ni barabara muhimu sana kwa shughuli za kilimo na shughuli za usafiri na usafirishaji. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwanza tumekubaliana kwamba barabara zote muhimu katika wilaya zetu ikiwemo katika Wilaya ya Ludewa ziainishwe na zitengewe bajeti. Asilimia 60 ya bajeti ambayo tunaendelea kuitangaza sasa tutatoa kipaumbele cha juu zaidi kwenye barabara muhimu kama Barabara ya Madope na Madilu. Kwa hiyo, nimhakikishie

Mheshimiwa Mbunge kwamba tutahakikisha kwamba barabara hizi zinapelekewa fedha na zinajengwa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara ya Mawengi inapitisha magari mazito kwa sababu ya shughuli za kilimo na hususan viazi, mbao na mazao mengine. Nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali ina dhamira ya kuiboresha barabara ile kiwango cha changarawe kwa awamu ili iweze kupitisha mizigo mingi na kuhakikisha kwamba tunaboresha shughuli za kiuchumi kwa wananchi wa Ludewa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, kuna suala zima la kisera tumeliongea hapa sana kuhusiana na barabara za majimbo ambayo yapo mjini na vijijini, kwamba barabara za majimbo yenye vijiji vingi zipewe fedha zaidi kwenye bajeti. Serikali imefikia wapi kwenye kupanga fedha nyingi zaidi kwa majimbo wa vijijini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na nimpongeze sana kaka yangu Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini kwa kazi kubwa anayofanya ya kuwawakilisha wananchi wa Jimbo la Njombe Mjini.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunafahamu Halmashauri ya Mji wa Njombe ina jiografia za aina mbili; jiografia ya mijini, lakini pia vipo vijiji vingi ambavyo vina hali ya vijijini kabisa. Ndio maana Serikali kwa kutambua hilo, kwanza tumehakikisha Halmashauri ya Mji wa Njombe inaingia kwenye Mradi wa *TACTIC* na tayari tuna hatua nzuri ya maandalizi kuhakikisha kwamba tunatekeleza Mradi wa *TACTIC* Awamu ya

Tatu katika Halmashauri ya Mji wa Njombe kwa maana ya mitaa ya pale mjini.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali imeendelea kuongeza bajeti za *TARURA* ikiwemo katika Halmashauri ya Mji wa Njombe ili kuhakikisha vijiji vyote vinaendelea kujengewa barabara, lakini pia kufanya matengenezo ya mara kwa mara. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kwa kadri ya upatikanaji wa fedha kwa awamu kuboresha barabara za vijiji vya Halmashauri ya Mji wa Njombe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kafiti.

**MHE. KAFITI W. KAFITI:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi kwa kupata nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Ilemela, barabara yetu ya kutoka Ilalila kwenda Kabusungu mpaka Sangabuye barabara inayounganisha hospitali ya wilaya ni mbovu sana na hivyo kuleta shida kwa wananchi na watumiaji wa huduma za hospitali.

Ni lini Serikali itakwenda kutengeneza barabara hiyo na Waziri yupo tayari kutembelea wilayani kwangu kuweza kuangalia barabara hiyo na kuona umuhimu wa kuitengeneza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ni kweli kwamba baadhi ya barabara katika Jimbo la Ilemela kwa Mheshimiwa Kafiti Kafiti zimeathiriwa sana na mvua zilizomalizika kunyesha msimu uliopita. Hata hivyo, tunafahamu kwamba Halmashauri ya Ilemela ni moja ya halmashauri ambazo zimeendelea kuongezewa bajeti za barabara. Nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, katika mipango ya Serikali, moja ya kipaumbele cha kuboresha miundombinu ya barabara ni kupeleka barabara katika maeneo ya huduma za jamii kama shule na hospitali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara hiyo inaelekea eneo la hospitali ya halmashauri, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, nimuelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela na Meneja wa *TARURA* wa Wilaya ya Ilemela kuhakikisha wanafika kwenye barabara hiyo na kuipa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, katika 60% ya bajeti ambayo tumepewa kibali cha kutangaza hivi karibuni na tupo hatua za mwisho kupata makandarasi tuhakikishe barabara hiyo kutokana na umuhimu wa kwenda hospitali ya wilaya inajengwa na kufanyiwa matengenezo ili kurahisisha huduma za usafiri kwa wananchi na wagonjwa wanaotoka hospitali hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Swalle.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi. Mkoa wa Njombe ni kati ya mikoa ambayo ina mvua nyingi sana kwa mwaka na Jimbo la Lupembe barabara nyingi huwa zinakuwa zimeharibika, lakini shida kubwa fedha ya *TARURA* inachelewa kuja kwa ajili ya ujenzi wa hizi barabara.

Mheshimiwa Spika, ni upi mpango wa Serikali kupeleka fedha mapema Jimbo la Lupembe, tujenge hizi barabara kabla ya mvua nyingi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, barabara za Mkoa wa Njombe ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Jimbo la Lupembe, lakini pia na mikoa mingine ambayo ina mvua nyingi kwa mwaka, zinaathiriwa sana na mvua na matokeo yake mara kwa mara tumekuwa tukitumia fedha kurejea kujenga na kuboresha barabara zilezile.

Mheshimiwa Spika, hatua ambayo Serikali imechukua; kwanza, tumeanza kufanya *design* nzuri na bora zaidi ya

barabara ambazo zitajengwa kulingana na hali ya hewa ya kijiografia kwa maana maeneo yenye milima na mvua nyingi tutakwenda na *design* ya barabara ambayo itakuwa bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano katika Jimbo la Ludewa tumetenga bajeti kwa ajili ya kujenga barabara za *concrete strips* za zege za mistari ambazo zitasaidia kuhakikisha kwamba zinadumu kwa muda mrefu hususan kwenye maeneo ya milima na maeneo ya mvua nyingi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nikuhakikishie Mheshimiwa Enosy Swalle kwamba tutasimamia suala hilo kwa barabara za Jimbo la Lupembe Mkoa wa Njombe na majimbo mengine yenye hali ya hewa ya aina hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Kija.

**MHE. KIJA L. NTEMI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Mimi ninapenda kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba Mji wa Katoro ni mji ambao umekua sana na una mwingiliano wa watu wengi, lakini tunamshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, alitusaidia akatuletea fedha tukajenga mitaro kiasi na barabara nyingi za Mji wa Katoro hazipitiki.

Je, Serikali ina mpango gani kuingiza Jimbo la Katoro au Mji wa Katoro katika Mradi wa *TACTIC* ili uweze kujengwa na zile barabara zipitike, watu waweze kufika katika sehemu zao katika nyumba zao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ninaomba nimthibitishie Mheshimiwa *Engineer* Kija Ntemi, Mbunge wa Jimbo la Katoro kwamba Serikali inatambua kwamba Mji wa Katoro ni mji ambao unakua kwa kasi kubwa sana. Kuna ongezeko la shughuli za kiuchumi, lakini pia ongezeko la idadi ya watu na ndio maana

katika vipaumbele vya barabara tumeendelea kuhakikisha kwamba tunaongeza fedha za barabara katika Jimbo la Katoro.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nikuhakikishie tu kwamba tutaendelea kufanya hivyo; kwanza, kuhakikisha kwamba barabara zetu zinaendelea kujengwa na hasa kiwango cha zege na lami kwa kadri ya upatikanaji wa fedha kwenye bajeti, lakini pili tumeweka mpango kwamba barabara zote lazima zijengewe mifereji au mitaro ya kudumu ili iweze kusaidia barabara zetu kuhimili maji wakati wa mvua.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuingia kwenye *TACTIC*; mpango wetu wa *TACTIC* ulikuwa kwa ajili ya majiji, manispaa na miji na kwa hivyo tutaendelea kuona namna nyingine ya kuboresha barabara za Katoro badala ya Mradi wa *TACTIC*.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Mheshimiwa Sheila Lukuba.

Na. 572

**Ujenzi wa Mabweni Shule ya Sekondari Nanenane**

**MHE. SHEILA E. LUKUBA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga mabweni kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita katika Shule ya Sekondari Nanenane?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Sheila Edward Lukuba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Shule ya Sekondari Nanenane ilipandishwa hadhi na kupata kibali cha kuchukua wanafunzi wa kutwa wa kidato cha tano na sita ambapo kwa sasa ina wanafunzi wa kidato cha tano 101. Shule ya Nanenane iliyopo Manispaa ya Morogoro ipo kwenye mpango wa kujengewa mabweni kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuongeza miundombinu katika shule za Manispaa ya Morogoro kwa awamu ambapo kwa kipindi cha miaka mitano 2021/2022 – 2025/2026 Serikali imepeleka shilingi bilioni 7.36 kwa ajili ujenzi wa mindombinu ya shule katika Manispaa ya Morogoro.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali imetenga shilingi milioni 880 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 40 katika shule za sekondari zenye upungufu wa madarasa katika Manispaa ya Morogoro ikiwemo madarasa mawili katika Shule ya Sekondari ya Nanenane.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lukuba.

**MHE. SHEILA E. LUKUBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Kwanza kabisa nianze kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa na nzuri anayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwezi huu wa sita niliomba pesa katika Shule ya Sekondari ya Mkundi – Mlimani na mpaka sasa tumeshapokea fedha hizo kiasi cha shilingi milioni 528.99. Tunashukuru sana, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, itakapokamilika Mbunge wangu wa jimbo nina imani atakwenda kuizindua. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Shule ya Sekondari Nanenane, sasa ina idadi ya wanafunzi wa *A level* 227, lakini hakuna mabweni. Wanafunzi wamekuwa wakiishi kwa kupanga mtaani na kama tunavyojua umri wao ni umri wa makuzi na wengi wao wamekuwa wakijiingiza kwenye makundi ya vijana waharibifu na wengine pia kutokuzingatia masomo ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali yangu tukufu, chini ya uongozi wa Mama yetu Samia Suluhu Hassan, iweze kutujengea hayo mabweni katika hiyo Shule ya Nanenane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; Shule ya Sekondari Mgugu iliyopo Wilaya ya Kilosa ni ya kitaifa ya wasichana na shule hiyo inachukua mpaka wasichana wenye mahitaji maalum na sasa ina idadi ya wanafunzi 536. Je, lini Serikali itaongeza miundombinu ya mabweni katika shule hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nimpongeze sana Mheshimiwa Sheila Edward Lukuba, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Morogoro kwa namna ambavyo amekuwa msemaji na mwakilishi bora kwa wananchi wa Morogoro, lakini na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pili nipokee pongezi zake nyingi kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo ametekeleza. Sekta ya Elimu, imepelekewa fedha nyingi katika halmashauri zetu zote na shule nyingi zimeendelea kujengwa, madarasa na miundombinu mingine na kwa hakika Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, anastahili maua yake kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Lukuba kwamba tunafahamu Shule ya Sekondari ya Nanenane katika Manispaa ya Morogoro ni shule inayochukua kidato cha tano na

sita. Kwa mujibu wa sera yetu, mabweni ama *hostel* ni jambo muhimu katika shule zote za kidato cha tano na sita na ndio maana tumeiweka kwenye mipango yetu na tunaendelea na taratibu za kibajeti na mara tutakapokamilisha taratibu za kibajeti, tutahakikisha tunapeleka fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa mabweni katika shule hii.

Mheshimiwa Spika, suala la pili; zipo shule zenye mahitaji maalum kama shule hii ya Kilosa ya wasichana ambayo inahitaji mabweni. Nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali inatambua na tutaendelea kutenga fedha ili tuhakikishe tunaboresha mazingira ikiwemo kujenga mabweni katika shule zenye mahitaji maalum ikiwemo shule hii katika Wilaya ya Kilosa.

**SPIKA:** Ahsante.

Mheshimiwa Eric James.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kuniona. Katika Jimbo la Buchosa, Kata ya Iligamba ipo Shule ya Sekondari Iligamba. Wananchi kwa kushirikiana na Mbunge na Diwani wao wamefanikiwa kujenga jengo la bweni mpaka hatua ya lenta, lakini wamepungukiwa kiasi cha shilingi milioni 99. Je, Serikali ipo tayari kutamka hapa kwamba itawaunga mkono wananchi hawa kupeleka fedha hizo ili bweni liweze kukamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Mbunge wa Jimbo la Buchosa, Mheshimiwa Eric James Shigongo amefuatilia mara kadhaa kuhusiana na suala la ujenzi wa bweni katika shule kadhaa ikiwemo shule ambayo ameisema hivi leo.

Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie nafasi hii nikupongeze sana Mheshimiwa Mbunge, lakini pia wananchi na Menejimenti ya Halmashauri ya Buchosa kwa kuhakikisha kwamba

tunachangia nguvu zetu na mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa bweni.

Mheshimiwa Spika, nikuhakikishie dhamira ya Serikali ni kuboresha miundombinu ya elimu, ikiwemo ujenzi wa mabweni na utaratibu wa Serikali kwa shule zile za bweni za kidato cha tano na sita, ama shule zile za *O'level* za mahitaji maalum, Serikali inaendelea kutenga bajeti ili kupeleka fedha kuhakikisha kwamba mabweni hayo yanajengwa. Kwa hiyo, tutalifanyia tathmini pia bweni hilo likiwa linakidhi vigezo hivyo vya kisera ili tuweze kupeleka fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa bweni hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ni lini Serikali itaanza kujenga mabweni ya kidato cha tano kwenye Shule ya Sekondari ya Ndugu na Shule ya Sekondari ya Hezya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, shule zote za kidato cha tano na sita zimewekewa mpango kwa awamu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunajenga mabweni. Dhamira ya Serikali ni kuondoa umbali wa wanafunzi kwenda shule, lakini pia kuwaepusha na changamoto mbalimbali ambazo zinatokana na kutembea umbali mrefu kwenda shule.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba nikuhakikishie Mbunge wa Jimbo la Vwawa, Mheshimiwa Hasunga kwamba shule hizo ulizozitaja ikiwa ni za kidato cha tano na sita tutazipa kipaumbele kwenye bajeti zetu na ikiwa ni shule za *O' level* basi tutaona namna ambavyo halmashauri kwa kufanya *internal arrangement* wanaweza wakakubaliana kuanza ujenzi kwa awamu kama ni zinakidhi vigezo vya kuwa shule za mazingira hatarishi.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Shule ya Sekondari ya Kakoso imepandishwa hadhi na kuwa ya kidato cha tano na cha sita, haina mabweni na madarasa ya kutosha. Ni lini Serikali itaenda kujenga miundombinu katika shule hii? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Shule ya Sekondari Kakoso katika Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika ambayo ni shule ya kidato cha tano na sita ni miongoni mwa shule ambazo Serikali imeweka mpango kwa ajili ya kutekeleza kwa awamu ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ikiwemo madarasa, mabweni, maabara, maktaba na majengo mengine.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea, kwa kuwa zoezi hili ni endelevu tutaipa kipaumbele shule hiyo pia ili tukishakuwa tumeweka taratibu zetu za kibajeti vizuri, tuhakikishe shule hiyo inapelekewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu inayopungua.

**SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kuweza kunipatia fursa na mimi kukuuliza swali. Shule ya Amali ya Nyandoto, Serikali imejitahidi imekamilisha miundombinu ya awali kama vile madarasa, nyumba za walimu na vyoo, lakini shule ile imeshindwa kusajiliwa na kuanza kufanya kazi kwa sababu ya ukosefu wa mabweni na kwa sababu ilijengwa nje kabisa ya mji na makazi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali haioni kuna haja ya kutenga fedha za dharura ili kuweza kukamilisha miundombinu ile ya mabweni kuweza kulinda thamani ya uwekezaji mkubwa ambao mmeuweka na kutoa fursa kwa vijana wa Tarime kuweza kunufaika na elimu hii ya amali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali katika kuboresha mafunzo ya ufundi na amali kwa wanafunzi imekuwa ni kujenga miundombinu ya shule za amali za kihandisi na shule za amali za kawaida.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa Serikali imekwishajenga jumla ya shule 103, zikiwemo shule 74 za amali, ikiwemo shule ya Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko katika Jimbo la Tarime Mjini, lakini zipo shule 29 za amali za kihandisi. Ninaomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ujenzi wa shule hizi umekwenda kwa awamu. Tulianza na awamu ya kwanza takribani shilingi milioni 583 na tunafahamu zipo shule ambazo bado miundombinu haijakamilika. Tupo kwenye utaratibu wa kuhakikisha kwamba tunapeleka fedha kukamilisha miundombinu ambayo haijakamilika yakiwemo mabweni.

Mheshimiwa Spika, tutakwenda awamu ya pili kwa ajili ya kujenga karakana na miundombinu mingine ili kuziwezesha zile shule za amali ziweze kutoa mafunzo kwa vitendo kwa ufanisi mkubwa zaidi. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa tutahakikisha tunatoa kipaumbele kwenye shule hiyo ya amali katika Jimbo la Tarime Mjini.

**SPIKA:** Ahsante. Kwanza niwapongeze Mawaziri kwa namna mnavyojibu maswali vizuri. *(Makofi)*

Siyo wewe peke yako, wote pamoja na hata pale ambapo swali la Mbunge halihusiani na idara yako, lakini majibu mnayo. Inaonesha namna gani Mawaziri ambao mpo *dedicated* kwenye kazi zenu. *(Makofi)*

Nimpongeze vilevile Mheshimiwa Wanu, juzi nimemuona kwenye mitandao alikuwa anapita ziara kwenye viwanda, lakini akawa anapigia debe ajira. Ajira siyo *section* yake, lakini uchungu

wa wananchi wake na yeye akawa anaipigia debe ajira. Mawaziri niwapongeze sana kwa kazi nzuri mnayofanya. *(Makofi)*

Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Mwantona kwa niaba yake Mheshimiwa Baraka.

Na. 573

**Ujenzi wa Barabara ya Kilometa 26 kutoka Idweli hadi Ngumbulu - Rungwe**

**MHE. BARAKA A. U. MWAMENGO K.n.y. MHE. ANTON A. MWANTONA** aliuliza: -

Je, lini Barabara ya Idweli hadi Ngumbulu - Rungwe yenye kilometa 26 itajengwa ili ipitike mwaka mzima?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, Mbunge wa Rungwe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Idweli hadi Ngumbulu – Lugombo – Rungwe yenye urefu wa kilometa 26 ni sehemu ya barabara ya Wilaya ya *Number One* – Lugombo ambayo imekasimiwa ihudumiwe na *TANROADS*. Baada ya kukasimiwa, *TANROADS* imeanza kuifungua na kujenga barabara hii kwa kiwango cha changarawe ambapo katika mwaka wa fedha 2025/2026 jumla ya kilometa 13 zimefunguliwa. Aidha, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027, barabara hii imetengewa jumla ya shilingi milioni 216.24 kwa ajili ya kuendelea kuifungua na kuijenga kwa kiwango cha changarawe, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Baraka.

**MHE. BARAKA A. U. MWAMENGO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii kuuliza maswali kwa niaba ya Mheshimiwa Mwantona.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ukiangalia ni muhimu sana na ni kiungo muhimu sana kwenda kwenye vijiji na vitongoji kama Bujingijila na kule mwisho kwenda kuiunga na Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo.

Mheshimiwa Spika, sasa ni lini barabara hiyo itaanza kutengenezwa kwa pesa ambayo imetengwa kwa ajili ya mwaka wa fedha ambao unakuwa unaisha maana bado mpaka sasa hivi ninavyozungumza haijaanza kutengenezwa. Je, ni lini itaanza kutengenezwa sasa? Tunaomba majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; katika barabara zinazosumbua ndani ya majimbo yetu, mojawapo ni Barabara ya Matema kwenda Ikombe ambayo inakwenda kuunganisha Wilaya ya Ludewa na kipande kile cha upande wa Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kwenda kuitembelea barabara ile ili kuona uwezekano wa kuitengeneza kwa haraka? Kwa sababu inaunganisha Mkoa wa Mbeya na Mkoa wa Njombe. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, katika swali lake la kwanza ambalo linahusiana moja kwa moja na hii barabara, baada ya kuona hii barabara ni muhimu, ndiyo maana pamoja na kwamba haijaja *TANROADS* moja kwa moja, hata hivyo, Serikali imeamua *TANROADS* waweze kuisimamia na kuitengeneza na ndiyo maana tumeanza kuifungua kwa awamu kwa viwango vya *TANROADS* na tuna uhakika tutaikamilisha ikiwa ni pamoja na kuiweka changarawe.

Mheshimiwa Spika, tumetenga fedha kwa bajeti hii ambayo tumepitishiwa kwenda kuijenga na kuikamilisha. Kwa hiyo, tutaanza tu mara bajeti hii itakapoanza kutumika ili pale ambapo

tumeishia tuweze kuendelea kwa bajeti hii ambayo tumeitenga ili kuhakikisha kwamba wananchi hao wanaitumia hii barabara kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, pia kuhusu Barabara ya Matema kwenda Ludewa, barabara hii iko kwenye mipango ya kuifungua kwa awamu na tunatambua umuhimu wake, si tu kuunganisha Mkoa wa Mbeya na Mkoa wa Njombe, lakini pia ni barabara muhimu sana kwa ajili ya ulinzi ambayo inapita kando kando ya Ziwa Nyasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama Serikali tutaichukua kwamba barabara zote hizi za ulinzi ni barabara za kipaumbele. Kwa hiyo, ipo kwenye mpango na niko tayari kwenda kuitembelea barabara hiyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, hali ya hewa ya Tukuyu ni nzuri sana kwa sasa, lakini barabara ya kuanzia Katumba – Suma – Masebe - Kandete kutokea Tukuyu Mjini, ile barabara hakuna kinachoendelea mpaka sasa tangu mkandarasi alivyoiacha. Kwa hiyo wanawake na watoto na wananchi wote kwa ujumla wanateseka sana na vumbi. Sasa je, ni lini barabara hiyo itakamilika kwa ujenzi wa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, barabara hii ina mkandarasi na tulikuwa tumemlipa fedha ya awali asilimia kumi. Nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge, tunavyoongea sasa hivi tayari ameshalipwa tena asilimia tano na ninavyoongea sasa hivi tayari amesharudi kwa kasi na anaendelea kufanya kazi ili kukamilisha kazi ambayo amepewa kuifanya. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndumbaro.

**MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kutokana na upatikanaji wa makaa ya mawe malori 1,600 yanapita katikati ya Mji wa Songea ndani ya saa 24. Je, ni lini sasa Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara ya mchepuko ili kuondoa adha kwa wakazi wa Mji wa Songea?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nakiri pengine ni mara ya nne ama ya tano Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro kuuliza swali hili na hasa kuhusu barabara ya *bypass* kilometa 16. Barabara hii inajengwa kwa kusaidiana na wenzetu wa *World Bank* na tayari mkandarasi yuko *site*. Changamoto ilikuwa ni kulipa fidia.

Mheshimiwa Spika, ninavyoongea hivi Mheshimiwa Mbunge atakuwa shahidi kwamba Serikali imeshalipa fidia na sasa tunaanza kujenga ile *bypass* ikiwa ni pamoja na barabara ya kutoka Songea kuja Njombe, tutaishia Mtukila kilometa kama 100.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chacha.

**MHE. CHACHA M. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Geita ni mji ambao unakua kwa kasi kutokana na shughuli ambazo zinafanyika pale za madini, biashara na ongezeko la watu. Sasa natamani kufahamu Serikali ina mpango gani wa upanuzi wa barabara kutoka Mpomvu mpaka Buhalahala kama ilivyoandikwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2025 ili kuendana na hali halisi ya ukuaji wa Mji wa Geita? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, sijasikia barabara aliyoitaja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chacha.

**MHE. CHACHA M. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, upanuzi wa barabara ya kutoka Buhalahala mpaka Mpomvu kama ilivyoandikwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2025 imeandikwa kwamba kutakuwepo na upanuzi. Sasa nataka kufahamu mpango wa Serikali ni lini hasa itaanza upanuzi huu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ni kweli ipo kwenye ilani na ikishakuwa kwenye ilani iko kwenye mpango. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika miji yote ambayo inakuwa na kupanuka, hizi barabara zote zinakwenda kupanuliwa lakini italingana na mpango wa bajeti kwamba tutaanza mwaka huu; kwa sababu utekelezaji wa ilani siyo wa mwaka mmoja ni wa miaka mitano. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa katika kipindi hiki cha utekelezaji wa ilani, tutakwenda kufanya hiyo kazi ambayo tumeiahidi.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Abubakari Asenga.

Na. 574

**Fidia kwa Wananchi wa Ifakara – Mlimba**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA** aliuliza:-

Je, lini wananchi wanaoishi pembezoni mwa Barabara ya Ifakara – Mlimba wenye alama ya kijani watalipwa fidia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kufuatia maboresho ya Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007 na Kanuni zake za mwaka 2009, upana wa hifadhi ya barabara kuu na za mikoa uliongezwa kutoka mita 22.5 hadi mita 30 kutoka katikati ya barabara kwa kila upande. Kutokana na ongezeko hilo, Serikali italipa fidia kwa wananchi wote ambapo wapo ndani ya mita 7.5 wenye alama ya kijani pindi maeneo hayo yatakapohitajika. Hivyo, niwahakikishie wananchi wanaoishi pembezoni mwa barabara ya Ifakara kwenda Mlimba ambao nyumba zao zimewekewa alama ya "X" ya rangi ya kijani, kuwa watalipwa fidia wakati Serikali itakapoanza mpango wa upanuzi wa barabara hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, kwa kweli mimi naishukuru Serikali. Tutakumbuka miaka miwili iliyopita nilikuwa naomba barabara hii ianze kujengwa Ifakara kwenda Mlimba kutokea Njombe. Serikali ya Watanzania chini ya Chama Cha Mapinduzi na Waziri Ulega na Mheshimiwa Naibu Waziri ni watu bingwa sana, barabara imeanza, mkandarasi yuko *site* amelipwa pesa zake na anaendelea kufanya kazi. Sasa nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ni kuhusu fidia pia ya barabara ya Ifakara kwenda Kidatu ambayo barabara imekamilika, Mheshimiwa Waziri alinijibu hapa kwamba tathmini inafanyika upya kupitia Ofisi ya Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, tathmini ile imekamilika. Je, ni lini wananchi wale watalipwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuhusu fidia pia ya barabara ya mchepuko ya Ifakara kupitia Mbasa - Katidiga kutokea Daraja la Magufuli kwenda Malinyi, nayo wananchi zaidi ya miaka minne wanasubiri fidia. Je, ni lini fidia yao italipwa? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba nipokee shukrani za Mheshimiwa Mbunge kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ninaamini hizi shukrani 100% ni za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tulijibu kwamba tunapokuwa tumefanya ujenzi wa barabara kuna wananchi ambao kwa bahati mbaya wengine wanakuwa wamerukwa, ama wamepunjwa, ama hawaridhiki na malipo ya fidia, na ziko kamati ambazo huwa zinakuwa chini ya Mkuu wa Wilaya na kazi hii katika hii Barabara ya Kidatu - Ifakara suala hili lilijitokeza na Mheshimiwa Mbunge amelifuatilia sana.

Mheshimiwa Spika, timu ilienda uwandani, imefanya kazi na kweli ilibaini hayo mapungufu na tunavyoongea sasa hivi yale mahitaji au zile fidia ambazo ama zilikuwa zimepungua, ama watu wamerukwa, tunavyoongea sasa hivi taarifa zao ziko Hazina kwa ajili ya kuandaa fedha za malipo ili wananchi hao waweze kulipwa.

Mheshimiwa Spika, pia, kuhusu fidia zingine kama nilivyosema katika jibu la msingi, hatutamwondoa mtu kabla ya kulipa fidia, ikiwa ni pamoja na hiyo Barabara ya kutoka Ifakara kwenda Mlimba, lakini pia tutakapoanza Barabara ya Ifakara - Lupiro kwenda Malinyi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Patali.

**MHE. PATALI S. PATALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Barabara ya Isyonje - Kikondo ni barabara muhimu sana kwa uchumi wa Wana-Mbeya Vijijini. Ninatambua mkandarasi yupo *site* na hii barabara ni barabara ambayo inaunganisha Mkoa wa Mbeya pamoja na Mkoa wa Njombe, Wilaya ya Makete. Mkandarasi yupo *site* ameanzia Makete lakini kipande cha kilometa 22 ambacho ni Isyonje - Kikondo ndiyo kipande chenye usumbufu sana na hakijaguswa na mkandarasi. Sasa, kwa niaba ya

Wananchi wa Mbeya Vijijini, ni lini barabara ya hiki kipande cha kilometa 22 itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Hii barabara ni barabara ya kutoka Isyonje hadi Makete na Serikali tulianza upande wa Makete barabara ambayo mara kadhaa hata Mheshimiwa Festo Sanga amekuwa akiiulizia. Hizi barabara kwa sababu huwa ni ndefu tunazigawa kwa vipande, ili tukikamilisha kipande kingine tunahamia kipande kingine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hizo kilometa 22, kwa kuwa eneo hilo ni eneo la mvua nyingi na la miinuko na ilikuwa siyo rahisi kwa kweli kulikarabati vizuri katika kipindi hichi. Sasa ni kipindi ambacho mvua imepungua, nimwelekeze Meneja wa Mkoa wa Mbeya aweze kuhakikisha kwamba mkandarasi ambaye amepangwa kukarabati hilo eneo, anakarabati vizuri wakati Serikali inatafuta fedha kuanza kukijenga hicho kipande kwa kiwango cha lami kwa sababu tayari ilishasanifiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mfaume.

**MHE. ZUBERI Y. MFAUME:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya Bigwa - Kisaki tayari ilishapimwa na watu wa *Millenium Challenge Account* na wakabainisha watu wanaopaswa kulipwa fidia. Je, ni lini sasa Wizara itapeleka rekodi hizi *TANROADS* Mkoa ili iweze kuwafidia wananchi na kazi iendelee? Ahsante

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi, tukishasanifu tunafanya *evaluation* na tukishafanya *evaluation* mara nyingi tunakuwa tunakabidhi hizo taarifa Wizara ya Fedha ambao wanafanya maandalizi. Pale ambapo tunakuwa tumechelewa kupata fedha ya ujenzi tunaanza na yale maeneo ambayo hayana fidia wakati

tunasubiri kupata fedha tulipe ili tuweze kuwaondoa wale ambao sasa wanastahili kuondoka ili waweze kupisha barabara.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Barabara ya Bigwa - Kisaki ambapo tunaanza Bigwa mpaka Mvua hatutamwondoa mtu mpaka tuwe tumemlipa fidia yake.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Margaret Sitta.

Na. 575

**Ujenzi wa Barabara Kuunganisha Ulyankulu, Urambo na Sikonge**

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya lami itakayounganisha Wilaya tatu za Ulyankulu, Urambo na Sikonge?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, barabara inayounganisha Wilaya za Ulyankulu, Urambo na Sikonge inajumuisha sehemu ya barabara kuu na barabara ya mkoa kuanzia Ulyankulu – Urambo – Usoke – Tutuo hadi Sikonge yenye urefu wa kilometa 184 ambapo sehemu ya Urambo – Usoke kilometa 40 na Tutuo - Sikonge kilometa 16 ni za kiwango cha lami. Sehemu ya Usoke – Tutuo kilometa 69, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inaendelea na imefikia 40%. Aidha, kwa sehemu ya Urambo – Ulyankulu kilometa 59, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imepangwa kuanza katika mwaka wa fedha 2026/2027. Baada ya kazi za usanifu kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sitta.

**MHE. MARGARET S. SITTA**: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza, je, ni lini kazi ya usanifu itakamilika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kwamba, barabara inayotoka Tabora kwenda Kigoma inapita kwenye vijiji vingi vyenye watu wengi. Je, ni lini Serikali itaweka taa ili kuepusha ajali katika maeneo hayo yakiwemo maeneo ya Vumilia, Uhuru, Motomoto, Mbaoni, Itundu, Usisya, Usoke na Usongelani? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Urambo kwamba kazi ya usanifu, kwa mfano Tutuo - Usoke tuko 40%, na kuanzia Usoke kwenda Ulyankulu tumepanga kuanza usanifu kwa mwaka huu wa fedha unaokuja. Kwa kawaida inategemea na urefu wa barabara na nini kipo kwenye hizo barabara. Hata hivyo, tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika usanifu, muda ambao tunakuwa tumekubaliana na wahandisi washauri kwa kawaida huwa tunakwenda pamoja kwa sababu hakuna changamoto kubwa ambazo zinachelewesha usanifu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie kadiri mikataba itakapokuwa imeingiwa tutahakikisha kwamba tunawasimamia na wanakamilisha usanifu ndani ya muda, ili tuweze kuharakisha kuanza kuzijenga hizo barabara kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, nataka nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge wa Urambo na Watanzania kwa ujumla kwamba, baada ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kukamilisha barabara kwa kiwango cha lami kutoka Dodoma hadi Kigoma ambayo pia inapita katika Jimbo la Urambo, kumekuwa na kazi kubwa sana ya maendeleo na vijiji vimeendelea kukua kwa kasi sana.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wizara tulishawaelekeza mameneja wa mikoa, vijiji vyote ambavyo viko hasa kwenye barabara kuu watuainishie na kutupa idadi ya taa za barabarani ili wananchi hawa waweze, kwanza kuwa na usalama lakini pia waweze kufanya shughuli zao za kibiashara kwa muda mrefu zaidi katika vijiji vyao, ikiwa ni pamoja na vijiji ambavyo viko katika jimbo la Mheshimiwa Sitta, Mbunge wa Urambo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tayari mameneja wanaleta taarifa za mahitaji ya hizo taa na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutafunga taa katika vijiji vyote ambavyo vitakuwa vinasifa ya kufungiwa taa. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Pondeza.

**MHE. AMJADI USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi kwa kunipa nafasi. Ninaomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri swali dogo la nyongeza kwenye sekta ya barabara. Kuna barabara ile ya kutoka Babati mpaka Singida ambayo inatumiwa na magari ya nchi za jirani, ambayo yanachukua mizigo kutoka Bandari ya Tanga imeharibika sana. Je, Serikali ina mpango gani kuhusu kipande hiki? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli hii Barabara ya Babati - Singida na hasa kuanzia maeneo yale ya Gehandu imeharibika sana na hata Mbunge wa Hanang amekuwa akiongelea sana. Kama kuna barabara imeharibika ninakiri ni moja ya hiyo barabara. Timu ya wataalamu imekwenda ili kufanya tathmini ya haraka ili barabara hiyo tuweze kuiboresha haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika mipango ya mwaka huu moja ya barabara ambayo kwa kweli Serikali inaiangalia kwa umakini na kwa uharaka ni hii, kwa sababu sasa hivi inapitisha magari mengi sana hasa baada ya magari mengi yanayotoka Tanga. Magari ya Tanga yanapita katika hiyo barabara, kwa hiyo

imezidiwa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, hiyo barabara inaenda kukarabatiwa. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kapunda.

**MHE. BAZILIO K. MBWILO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali. Barabara ya kutoka Namanyere kwenda Bandari ya Kipili ndiyo tunayoitarajia iwe *feeder road* kwa ajili ya meli yetu ambayo itaanza kazi hivi karibuni; lakini vilevile, barabara hiyo ndiyo inayotegemewa zaidi na wafanyabiashara kutoka nchi jirani ya *Congo* kwa ajili ya kusafirisha mizigo yao, lakini barabara hii inapofika masika haipitiki hasa kwa magari makubwa.

Mheshimiwa Spika, je, kwa umuhimu huo Serikali itaanza lini kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami, ili kuwezesha mapato zaidi ya nchi kutokana na usafirishaji wa mizigo?*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba tu nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Nkasi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nataka tu nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi kama Wizara ama Serikali inaongea, tunajua sasa hivi wenzetu wa Uchukuzi wanaboresha na kukarabati meli zao ambazo zitapita Ziwa Tanganyika ikiwepo *MV Liemba* nadhani ipo kwenye hatua za mwisho kabisa hii, kuna meli nyingi ambazo zinakarabatiwa ambazo wenzetu wa ukanda wa Ziwa Tanganyika wanazitegemea, lakini pia hakutakuwa na maana kama barabara hazitaimarishwa.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge hii barabara tumeshaikamilisha usanifu na hata katika vitabu vyetu vya bajeti tumeshatenga kiasi cha fedha kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, ipo kutoka Namanyere - Katongoro – Kipili tunategemea kwamba kama tutapata kibali tutaanza

kuijenga na ndiyo maana tumeipangia fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Neema Majule.

Na. 576

**Kuanzisha Skimu za Umwagiliaji Dodoma**

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha skimu za umwagiliaji katika Mkoa wa Dodoma wenye tatizo la ukame?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Serikali inatambua changamoto ya ukame katika Mkoa wa Dodoma na umuhimu wa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika mkoa huo ili kuhakikisha uzalishaji endelevu wa mazao na kuimarisha usalama wa chakula. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya umwagiliaji katika Mkoa wa Dodoma ikiwemo ujenzi wa mabwawa matatu yaliyopo katika Wilaya za Chamwino (Membe), Mpwapwa (Msagali) na Kongwa (Ngomai) kwa ajili ya umwagiliaji, ujenzi wa skimu mpya nne pamoja na ukarabati wa skimu nane katika Wilaya za Chamwino na Bahi za mkoa huo.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali inaendelea na miradi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mabwawa nane mapya pamoja na skimu 20 katika Mkoa wa Dodoma. Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha uhakika wa upatikanaji wa maji kwa ajili ya shughuli za kilimo cha umwagiliaji. Serikali inaendelea na mkakati wa uchimbaji wa visima virefu ambapo jumla ya visima 31 vimeshachimbwa katika awamu ya kwanza katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Dodoma na visima 35

vitachimbwa kwa awamu ya pili ili kuwezesha wakulima wadogo wadogo ambao wapo kwenye maeneo yasiyo na mabwawa na mito kwa ajili ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, visima hivi vinategemea kuongeza upatikanaji wa maji na kuongeza eneo la umwagiliaji kwa zaidi ya hekta 22,000 jambo litakalosaidia kuongeza uzalishaji wa mazao na kupunguza athari za ukame.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Neema.

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba nishukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kweli ni kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi tutapata hayo mabwawa, lakini pia tunaendelea kupata visima virefu, lakini pia tunategemea maji mengi zaidi kutoka Ziwa Victoria kwa ajili ya kufanya mji wetu uwe na maji ya kutosha zaidi ya *domestic use*. Maji hayo pia yatatumika hata kwa ajili ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, sisi Dodoma tunapata mvua nyingi sana wakati wa masika, lakini maji yote haya huwa yanapotea tu kwa sababu hayana mahali pa kutunzwa. Je, Serikali haioni sababu sasa ya kufanya *surface survey* tu kuweza kuona maji haya yanakoelekea ili waweze kupata mabwawa mengi zaidi na hasa kuwaajiri sasa wanawake wengi na vijana kwenye kilimo hiki cha umwagiliaji? Hilo ni swali langu la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, zaidi ya skimu tulizo nazo, je, Serikali sasa ipo tayari kufanya miundombinu mingine kwa ajili ya watu walio jirani na hizo skimu waweze kutumia kilimo hiki cha umwagiliaji hata kwa *pump*? Hivyo uagizaji wa *pump* nyingi zaidi na mbegu bora ambazo zitaweza kufanya waweze kujikita kwenye kilimo hiki cha mwaka mzima badala ya kutegemea mvua. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Majule kwa maswali mazuri ya msingi na nimthibitishie tu kwamba Serikali tayari imeshafanya na inaendelea na mpango wake wa kufanya hii *surface survey* kwa ajili ya miradi mikubwa ya umwagiliaji na ndiyo maana utaona katika njia ya *SGR* kutokea Morogoro mpaka unafika hapa Dodoma Wizara ya Kilimo tukishirikiana na Wizara ya Uchukuzi pamoja na Wizara ya Ujenzi tunatarajia kujenga karibu mabwawa sita ambayo yatasaidia kukusanya maji yote yanayotokana na mvua ambayo yatasaidia kwenye kilimo. Kwa hiyo, tayari tuko katika mpango na tutaendelea na tutatoa taarifa baada ya kukamilika kwa jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuweka miundombinu mingine hiyo ni sehemu ya mradi ambao tunatekeleza, kwa hiyo, katika kila mradi ambao tunaufanya tunaweka hiyo *component* ya kuhakikisha kwamba wale ambao wako karibu ama pembezoni mwa mradi tunawasaidia kuwasogezea *pump* au kufanya *extension* ya ule mradi ili kuwasaidia wale wakulima. Kwa hiyo, tunafanya hivyo na tutaendelea kufanya hivyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha Baraka.

**MHE. ASHA R. BARAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Swali langu lilikuwa limelenga Wizara ya Ujenzi, lakini alikuwa...

**SPIKA:** Basi kaa chini, kaa chini. Mheshimiwa Mabula.

**MHE. MABULA J. MAGANGILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Jimbo la Msalala ni jimbo ambalo linaongoza kwa kilimo cha mpunga na 60% ya mpunga katika Mkoa wa Shinyanga unatoka Msalala, lakini ni jimbo ambalo linayo maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji kama Kata ya Mwakata, Igundu, Chela, Mwanengi na Kakola. Maeneo haya yanafaa kwa kilimo cha umwagiliaji na ni mabonde ambayo tunaweza kulima kwa misimu miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itapeleka mradi wa umwagiliaji katika maeneo haya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nimpongeze Mheshimiwa Mabula, Mbunge wa Msalala kwa maswali mawili ya msingi na bahati nzuri jambo lake tulishazungumza tangu juzi na jana na nilishamthibitishia baada ya kuzungumza na Mkurugenzi wa Tume kwamba katika yale maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha kwamba tunayafanyia *feasibility study* mabonde yote ni pamoja na haya mabonde aliyoyataja ikiwemo Mwakata, Kakola na Mwaningi pamoja na hayo mengine. Kwa hiyo, yapo katika mpango na baada ya kumaliza *feasibility study* maana yake sasa tutatangaza ili kupata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi.

**SPIKA: SPIKA:** Mheshimiwa Mattembe.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi. Ipo skimu ya umwagiliaji ya Bwawa la Msange, lakini skimu hii kwa sasa imesimama na imefikia 39%. Ningependa kufahamu ni lini sasa Serikali italeta fedha za kutosha ili kukamilisha skimu hii ambayo ni muhimu sana kwa Jimbo la wananchi wa Ilongero? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nimshukuru dada yangu Mheshimiwa Aysharose Mattembe, Mbunge wa Viti Maalum - Singida. Ni kwamba nilishatoa maelezo hapo awali kwamba Serikali sasa hivi tumeshapata *commitment* ya fedha kutoka Wizara ya Fedha kupeleka fedha tume karibu shilingi bilioni 25 kila mwezi na katika fedha hizo maana yake tunapeleka katika ile miradi ambayo tayari ilishakuwa imeanza na inakaribia kuisha, lakini na ile miradi ambayo iko zaidi ya 50% na mingine ambayo tayari tulishawapa wakandarasi katika muda uliokwisha. Kwa hiyo, Bwawa la Msange ni mojawapo ya ambalo tutapokea fedha hizo.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Edward Olelekaita.

**11 JUNI, 2026**

Na. 577

**Ukarabati wa Majosho – Kiteto**

**MHE. EDWARD O. KISAU** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka fedha za ukarabati wa majosho katika Vijiji vya Ndotoi, Enguserosidan na Laiser katika Kata ya Laiser – Kiteto?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naomba kujibu swali namba 577 la Mheshimiwa Edward Kisau Olelekaita, Mbunge wa Kiteto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa ujenzi na ukarabati wa majosho katika kudhibiti magojwa yanayoenezwa na kupe na mbung'o hapa nchini. Katika kutekeleza azma hiyo Serikali ilianza kutekeleza mpango wa ujenzi wa majosho tangu mwaka 2021/2022 ambapo hadi sasa jumla ya majosho 754 yamejengwa kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2022/2023, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilitumia kiasi cha shilingi milioni 92 kwa ajili ya kujenga na kukarabati majosho saba katika Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto kwenye Vijiji vya Nchinila, Loltepesi, Amei, Lembapuli, Loolera, Orkitikiti na Engong'ongare. Majosho hayo yalikamilika kwa 100% na yanafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuratibu ujenzi, ukarabati na uendelezaji wa miundombinu muhimu ya mifugo katika maeneo mbalimbali hapa nchini ikiwemo majosho ya Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za mifugo kwa wananchi kadri ya upatikanaji wa fedha. Aidha, natoa rai kwa halmashauri zote nchini, ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto kuhakikisha zinatenga fedha

kutoka katika mapato yao ya ndani kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya majosho ili kudhibiti magonjwa ya mifugo na kuongeza tija katika sekta ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninashukuru kwa majibu ya Serikali. Kwa kuwa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi imesema kila kijiji chenye mifugo kinastahili kuwa na josho na katika Kata za Sunya, Kijiji cha Asamatwa, Ndorokoni, Matui na Bwawani hakuna majosho. Nini kauli ya Serikali ya uhakika kwamba majosho yatajengwa kwenye vijiji hivi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili na hili ni maalum kidogo, Kata ya Dongo na Laiser ni kata zenye mifugo wengi sana karibu 151,000 halafu hazina josho hata moja. Nini kauli ya Serikali angalau basi kwa kuanza na hizi kata mbili ambazo hazina majosho kabisa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Olelekaita kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika majibu yangu ya msingi, Serikali inatambua umuhimu wa afya ya mifugo na ndiyo maana imewekeza majosho niliyoyataja yakiwemo ambayo yamejengwa katika baadhi ya vijiji kwenye Jimbo la Kiteto.

Mheshimiwa Spika, kauli ya Serikali kuhusu sera yake ya kila kijiji kuwa na majosho bado iko pale pale, changamoto kubwa tuliyonayo ni kwamba tuna maeneo makubwa na mahitaji ni mengi na kwa maana hiyo tunaenda kwa kasi kulingana na upatikanaji wa fedha na ndiyo maana nimeomba na nashauri kwamba halmashauri za wilaya na zenyewe pia zichangie katika mapato yao ya ndani ili tuweze kupunguza pengo kubwa ambalo lipo.

Mheshimiwa Spika, na mimi natambua eneo la Kiteto Mheshimiwa Naibu Waziri alipofanya ziara jambo kubwa lililojitokeza kwenye ziara hiyo ilikuwa ni mahitaji ya majosho. Kwa hiyo, tukipata fedha tutaweka kipaumbele katika maeneo ambayo yana mahitaji makubwa.

Mheshimiwa Spika, katika swali la pili kuhusu hizo kata mbili ambazo zina mifugo mingi, lakini hazina josho hata moja, majibu yangu ni yale yale kwamba Serikali tutajitahidi, tukipata fedha tutaelekeza nguvu kwenye maeneo hayo ambayo yana mifugo mingi na kwa halmashauri kwa sababu penye mifugo mingi pia kuna mapato mingi.

Kwa hiyo, ni vizuri pia Mheshimiwa Mbunge ambaye pia ni diwani katika halmashauri kujaribu pia kushawishi katika vikao kuelekeza fedha za ndani maeneo ambayo yana uzalishaji mkubwa wa mifugo ili pia kusaidia wafugaji waweze kudhibiti magonjwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Wilson.

**MHE. DKT. WILSON C. MAHERA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuweza kuuliza swali.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Butiama ni miongoni mwa wilaya ambazo zina wafugaji wengi wa mifugo, lakini ni wilaya ambayo zaidi ya vijiji 10 havina majosho kwa ajili ya kuoshea mifugo hasa Kijiji cha Mwibagi, Kijiji cha Nyanza, Kyawazaru Kwigutu, Magunga, Rwamkoma, Sirorisimba, Mlianza na Matongo.

Mheshimiwa Spika, swali je, lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kujenga majosho kwenye Wilaya ya Butiama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Wilson, Mbunge wa Butiama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika majibu ya msingi ya swali la msingi, tunatambua mahitaji ya majosho katika Jimbo la Butiama na ninampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Wilson ambaye ameshaandika barua rasmi ofisini kupitia kwa Katibu Mkuu na barua hiyo inakuwa ni mwongozo kwetu wakati tunatengeneza vipaumbele vya kukabiliana na tatizo hilo. Tunakushukuru sana na tutakupa majibu ya barua yako.

Mheshimiwa Spika, ombi langu, Waheshimiwa Wabunge wote ni Madiwani, tujitahidi sana kushawishi halmashauri zetu ambazo zinapata mapato kutokana na mifugo waweke kipaumbele katika eneo la majosho, kwa sababu majosho yanasaidia afya ya mifugo. Kwa hiyo, naomba tuendelee kuwa wasimamizi na washauri wazuri kwenye halmashauri zetu tuweze kupunguza tatizo la uhaba wa majosho kwenye maeneo yetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Malima.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mpwapwa ni kati ya wilaya zenye mifugo mingi hapa nchini, lakini tuna upungufu wa majosho na hasa katika Kata za Mima, Iwondo, Kimagai, Mlembule na Chunyu.

Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itakwenda kujenga majosho kwa ajili ya kulinda afya za wanyama wetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Malima, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, majibu yangu bahati mbaya au nzuri yanafanana. Matatizo ni kwamba tunazo rasilimali chache na mahitaji ni makubwa. Vyanzo vya kuweza kukabiliana na pengo hilo ni ama Serikali Kuu kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Halmashauri za Wilaya kupitia mapato ya ndani, lakini pia na Mifuko ya Maendeleo ya Wabunge na hapa nimpongeze Mheshimiwa Cherehani ambaye ndiye amerithi kwenye kiti nilikokuwa nakaa kabla sijateuliwa, nilipotembelea Jimbo lake la Ushetu nilikuta kulikuwa na ahadi ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Mpina ambayo ilikuwa haijatekelezwa ya kujenga josho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipoambiwa nikaahidi kwamba tutatekeleza kwa sababu ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri, namwona Mheshimiwa Ado anacheka kwa sababu ahadi ya Mheshimiwa Waziri haifi. Namshukuru sana Mheshimiwa Cherehani alitumia Mfuko wa Jimbo kujenga josho na amenialika niende kulifungua. Kwa hiyo, hicho ni chanzo kingine kizuri cha kutatua changamoto ya majosho. Yeye kwenye fedha za jimbo ameamua mwaka huu ni mwaka wa kuwekeza kwenye miradi ya mifugo, mwaka jana ilikuwa afya, mwaka huu ni mwaka wa eneo la mifugo. Mimi naona sasa hivi huyu ndiye Mheshimiwa Mbunge ambaye anaweza akaleta mfano wa namna ya kutumia vizuri Mfuko wa Jimbo katika kutatua changamoto tulizonazo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wetu umekwisha. Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Wageni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu; wageni 86 wa Mheshimiwa Waziri Mkuu wanafunzi na walimu wa Shule ya Msingi *Maria Mission* kutoka Wilaya ya Ubungo, Kibamba Jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika; wageni wa Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,

Mipango na Uwekezaji ambao ni Dkt. Tausi Kida - Katibu Mkuu Mipango; Dkt. Fred Msemwa - Katibu Mkuu Uwekezaji na Mheshimiwa Balozi Ombeni Sefue, Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu na Mjumbe wa Tume ya Taifa ya Mipango. *(Makofi)*

Wapo pia Ndugu James Maziku - Mkurugenzi Huduma kwa Wawekezaji wa Mamlaka ya Uwekezaji Maeneo Maalum ya Kiuchumi Tanzania (*TISEZA)*; Dkt. John Mduma - Mkurugenzi Mkuu Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi *(WCF);* Ndugu Benjamin Chilumba - Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Raslimali Watu, Tume ya Taifa ya Mipango; Dkt. Mursali Milanzi - Naibu Katibu Mtendaji Mipango ya Kitaifa; Dkt. Blandina Kilama - Naibu Katibu Mtendaji Biashara na Ubunifu na Ndugu Sostheness Kewe - Naibu Katibu Mtendaji, Ufuatiliaji, Tathmini na Utendaji Kazi. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Noela Mafuru - Mke wa aliyekuwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Taifa Mipango, Marehemu Lawrence Mafuru na Ndugu Lorraine Mafuru, mtoto wa aliyekuwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Mipango, Marehemu Lawrence Mafuru. *(Makofi)*

Yupo Profesa Fortunata Makene, *Director of Economic and Social Research Foundation*. *(Makofi)*

Pia, yupo Ndugu Rogathe Mbowe, Mwenyekiti wa CCM, Wilaya ya Ubungo. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Mkumbo ni Watendaji Wakuu wa Benki; Ndugu Tuse Mwaikasa, Mkurugenzi Mtendaji *Tanzania Bankers Association;* Ndugu Frank Nyabundege, Mkurugenzi Mtendaji Benki ya Maendeleo ya Kilimo na Ndugu Eric Chijoriga - Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Benki ya Biashara. *(Makofi)*

Pia, wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Mkumbo, hawa ni wadau wa maendeleo; Ndugu Marsha Macatta Yambi - Mkurugenzi Mtendaji wa *UN Global Compact* Tanzania; Ndugu Zena Amour - Mtaalam wa Sera za Kijamii *UNICEF,* Tanzania; Ndugu Godfrey Mulisa - Mratibu Ofisi ya *UNDP* Dodoma; Dkt.

Majaliwa Marwa - *Assistant Representative UNFPA* Tanzania; Ndugu Evance Siangecha - Mratibu wa Maendeleo, Ofisi ya Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa Tanzania na Ndugu Bahati Ulimwengu - Mwakilishi wa Sekta Binafsi. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Balozi Khamis Mussa Omar, Waziri wa Fedha; Ndugu Natu El-Maamry Mwamba - Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali; Ndugu Elijah Mwandumbya - Naibu Katibu Mkuu, Usimamizi wa Fedha; Ndugu Nsubili Joshua, Naibu Katibu Mkuu, Huduma za Hazina; Ndugu Meshack Anyingisye - Kamishna Usimamizi wa Bajeti; Dkt. Amina Msengwa - Mtakwimu Mkuu wa Serikali; Ndugu Benedicto Mgonya - Mwakilishi wa Gavana wa Benki Kuu na Ndugu Efraim Mdee - Mkurugenzi wa Sera na Mipango *TRA*. *(Makofi)*

Wageni Waheshimiwa Wabunge; wageni watatu wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa - Waziri wa Mifugo na Uvuvi, hawa ni viongozi wa Chama cha Ufugaji kutoka Mkoa wa Mara, Pwani na Manyara. *(Makofi)*

Wageni 10 wa Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya - Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, hawa ni viongozi wa CCM Wilaya ya Manyoni, Mkoa wa Singida. *(Makofi)*

Wageni saba wa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki, hawa ni Maafisa Elimu kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga ambao ni marafiki zake na wafanyabiashara kutoka Makete, Mkoani Njombe. *(Makofi)*

Wageni 39 wa Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Qambaji Nuwas ambao ni walimu na wakuu wa shule za msingi kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, Mkoani Manyara. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 76 wa Mheshimiwa Yagi Maulid Kiaratu ambao ni wanafunzi na walimu wa Shule ya Sekondari ya Kindai kutoka Mkoani Singida. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Sara Ally Msafiri, huyu ni Chifu kutoka Jamii ya Wafugaji kutoka Jimbo la Mvomero, Mkoani Morogoro. *(Makofi)*

Wageni 12 wa Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, hawa ni watumishi wa Ofisi ya Elimu kutoka Mbozi, Mkoani Songwe. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Fagason Aron Nkingwa ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Eric James Shigongo, Washirika wa *Mikocheni A Life Center* kutoka Kanisa la *T.A.G VCCT* kwa Mchungaji Dkt. Huruma Nkone, Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Pia wapo wageni 27 wa Mheshimiwa George Natany Malima ambao ni wachungaji na wake zao, Dinara Mima Mpwapwa, Mkoani Dodoma. Wake zao sijawaona bado. Hongereni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia kwa siku ya Jumatatu, tarehe 15 Juni, 2026 kutakuwa na semina itakayoendeshwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano kuhusu *scheme* za Hifadhi ya Jamii kwa wananchi waliojiajiri, *Hifadhi Scheme* na Mradi wa Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi, Kilimanjaro, zinazosimamiwa na Mashirika ya Hifadhi ya Jamii ya *PSSSF* na *NSSSF*.

Semina hiyo itafanya katika Ukumbi wa Pius Msekwa kuanzia saa 7.00 mchana, mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge. Waheshimiwa Wabunge, wote mnakaribishwa kuhudhuria semina hii muhimu.

**SPIKA:** Katibu.

**11 JUNI, 2026**

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2025 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

**SPIKA:** Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 127(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2025, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, kujadili na kupitisha Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa, mwaka 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2026/2027. Pamoja na hotuba hii ninawasilisha vitabu vya Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2025 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, taarifa hizi mbili ndizo zitakuwa msingi wa Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2026/2027 itakayowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika Bunge lako Tukufu, baadaye leo alasiri.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninamshukuru Mungu kwa neema ya uhai, afya, amani na utulivu, iliyotuwezesha kukutana hapa leo na katika kipindi chote cha Bunge hili la Bajeti, ambalo linaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa, ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa fursa aliyonipatia ya kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, ambayo imeniwezesha kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu, kuwasilisha taarifa hii kwa niaba yake na kwa niaba ya Serikali anayoiongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Emmanuela Mtatifikolo Kaganda kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Isimani. Ninamtakia mafanikio

makubwa katika kuwatumikia wananchi wa Jimbo la Isimani na Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake makini. Kipekee ninamshukuru na kumpongeza kwa ziara yake ya kihistoria na yenye mafanikio makubwa aliyoifanya hivi karibuni katika Taifa kubwa la Urusi, akiwa ni Rais wa Pili wa Tanzania kufanya ziara rasmi nchini Urusi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kuzingatia kuwa ziara ya Mheshimiwa Rais nchini Urusi ni sehemu ya utekelezaji wa falsafa yake ya kuifungua nchi au kile unachokiita *pragmatism* ambayo inazingatia uhalisia wa mambo kwa wakati husika katika kufanya maamuzi ya msingi ya kisera, kiuchumi, kisiasa na kijamii. Katika falsafa hii anapofanya ziara za nchi, Mheshimiwa Rais anaenda kutafuta washirika yaani *partners* wa maendeleo, haendi kutafuta wafadhili au wadhamini kwa maana ya *sponsor* au *patrons*. Mheshimiwa Rais anaenda nje kutafuta fursa za biashara na uwekezaji na sio kutafuta misaada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kusaka fursa za biashara na uwekezaji hatutachagua wapi pa kwenda, wala hatutakubali kuchagua rafiki wala adui, kama alivyowahi kusema Deng Xiaoping, Rais wa zamani wa China; *"It doesn't matter whether a cat is black or white as long as it catches mice."*

Mheshimiwa Spika, msimamo huu wa Rais wetu wa kukataa kuchagua marafiki wala adui sio mgeni kwa nchi yetu. Mara baada ya nchi nyingi za Afrika kupata uhuru miaka ya 1960 lilitokea wimbi na shinikizo kubwa la kuzisukuma nchi za Afrika kuchagua upande wa kushoto au wa kulia au upande wa magharibi au wa mashariki kama ilivyojulikana wakati huo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia shinikizo hilo Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Kwanza na Baba wa Taifa letu, aliweka msimamo wa wazi ambao ndio msimamo wetu unaotuongoza leo aliposema, ninaomba nimnukuu: *"We desire*

*friendship with the countries of the east as well as with those of the west and on the basis of mutual respect and non-interference in internal affairs we will not allow any of our friendships to be exclusive. Will not allow anyone to choose our friends or our enemies for us." (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wake ninaomba kutafsiri maneno hayo; "tunadhamiria kudumisha urafiki na nchi za mashariki na za magharibi kwa misingi ya kuheshimiana, usawa na kutokuingiliana katika masuala ya ndani ya mataifa mengine. Hatutaruhusu uhusiano wetu wa kirafiki na Taifa lolote kuwa wa kipekee wala hatutakubali Taifa lolote lituchagulie marafiki au maadui wetu." Hilo hilo ni jukumu letu sisi wenyewe kama Taifa huru na lenye mamlaka kamili juu ya maamuzi yake. Kwa hiyo basi, katika kusaka fursa za kiuchumi tutazingatia maslahi yetu mapana ya kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, ninaomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo. Kwanza nieleze muktadha wa uchumi wa dunia kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, ninapowasilisha Taarifa ya Hali ya Uchumi wa mwaka 2025 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2026 tupo katika kipindi ambacho dunia ipo katika hali ya mtikisiko mkubwa wa kiuchumi na kisiasa kutokana na migogoro mbalimbali inayoendelea duniani. Migogoro hii tunafahamu ni pamoja na vita unayoendelea katika Ukanda wa Mashariki ya Kati baina ya Marekani na Israel dhidi ya Iran na vita ya Urusi na Ukraine.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Mipango kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP)* imefanya utafiti kuhusu athari za vita ya uajemi katika uchumi wa Tanzania na fursa zinazotokana na vita hiyo. Taarifa ya matokeo haya iliwasilishwa tarehe 22 Mei, 2026. Taarifa hiyo inaonesha, pamoja na mengine kuwa vita dhidi ya Iran iliyoanza rasmi mwezi Februari, 2026 imesababisha taharuki katika masoko ya mafuta

duniani kufuatia hofu ya kuvurugika kwa usafirishaji wa mafuta kupitia ghuba ya uajemi.

Mheshimiwa Spika, taarifa inaonesha kuwa katika kipindi cha miezi mitatu ya vita dhidi ya Iran bei ya mafuta ghafi iliongezeka kwa wastani wa dola za Marekani 107.3 kwa pipa kati ya Februari, 2026 vita ilipoanza na Juni 5, 2026. Bei hizo za mafuta zilipanda kutoka dola za Kimarekani 100 kwa pipa mwezi Machi, zikaenda hadi dola 126 mwezi Aprili, 2026. Bei hizo zimeshuka hadi kufikia dola 90 mpaka 95 kwa Ukanda wa Bara la Afrika kwa Juni 8 hadi 9, 2026. Bei hizi hutegemea sana hali ya mashambulizi na mazungumzo yanayoendelea kati ya Marekani na Iran.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tanzania, kama unavyofahamu, huagiza mafuta yaliyosafishwa kwa 100% kutoka nje ya nchi, sawa na 13% ya thamani ya bidhaa zote tunazozioza toka nje. Sehemu kubwa ya mafuta haya, takribani 60% mpaka 70% huagizwa kutoka nchi za ghuba ya uajemi, hususan Umoja wa Falme za Kiarabu, Saudi Arabia, Kuwait pamoja na nchi za India na Singapore.

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa bei za mafuta kumeongeza gharama za uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa na huduma. Aidha, suala hili linaweza kuiathiri sekta ya utalii inayochangia takribani dola za Kimarekani bilioni 4.4 na kutoa ajira milioni 1.5 kupitia ongezeko la bei za tiketi za ndege na kuahirishwa kwa safari za ndege mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, nalihakikishia Bunge lako Tukufu, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na migogoro ya vita hizi. Hatua hizo ni pamoja na: -

(i) Kuendelea kuimarisha usimamizi wa sera ya fedha na bajeti ili kudhibiti mfumuko wa bei;

(ii) Kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala, kuimarisha uhifadhi wa akiba ya mafuta, pamoja na kuendelea

kutafuta masoko mbadala ya bidhaa zinazouzwa kutoka nje;

(iii) Vilevile Serikali inaendelea kuhamasisha uzalishaji wa ndani wa bidhaa muhimu ili kupunguza utegemezi wa bidhaa kutoka nje ya nchi, hususan mbolea na baadhi ya malighafi za viwandani;

(iv) Aidha jitihada zinaendelea kufanyika katika kuimarisha sekta za usafirishaji, biashara na uwekezaji ili kuongeza ustahimilivu wa uchumi wa Taifa dhidi ya misukosuko hiyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na athari hasi za migogoro inayoendelea duniani, hususan vita ya Marekani na Israel dhidi ya Iran, migogoro hiyo pia inatoa fursa za kiuchumi ambazo tukizitumia vizuri zinaweza kuleta manufaa ya kiuchumi kwa nchi yetu. Baadhi ya maeneo ya fursa ni pamoja na: -

(a) Kuongeza uzalishaji wa bidhaa ambazo soko lake limeathiriwa na mgogoro na hivyo kuongeza uwezo wetu wa ushindani wa kibiashara. Kwa mfano, ipo fursa katika kutoa huduma za upakuaji na uhifadhi wa shehena za mizigo kwa muda yaani *transshipment* kwa meli ambazo zimeshindwa kufikisha shehena hizo katika Bandari ya Mashariki ya Kati kutokana na uwepo wa vita; aidha

(b) Vita hii inatoa nafasi kwa nchi yetu kuvutia wawekezaji ambao sasa wanaona eneo la ghuba sio salama tena kwa uwekezaji wao ikiwemo kuvutia uwekezaji katika eneo la gesi ili kujilinda na athari za majanga kama hayo katika siku zijazo.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa hali ya uchumi kwa mwaka 2025; mwenendo huu umeelezwa kwa kirefu katika ukurasa wa tano hadi 27 wa vitabu ambavyo Waheshimiwa Wabunge wanavyo na tumegawa katika makundi makubwa

mawili; mapitio ya hali ya uchumi wa dunia na kikanda ambayo ipo ukurasa wa tano mpaka wa 10.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nijikite zaidi kwenye hali ya uchumi wa Taifa; mwaka 2025 Serikali kupitia Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilikamilisha maboresho ya takwimu za Pato la Taifa kwa kutumia mwaka 2016, kama mwaka wa kizio badala ya mwaka 2015. Kufuatia maboresho hayo mabadiliko kadhaa yalijitokeza, ikiwemo ukubwa wa Pato la Taifa, viwango vya ukuaji wa mchango wa sekta mbalimbali katika Pato la Taifa na uwiano wa viashiria mbalimbali kwa Pato la Taifa. Kwa mujibu wa takwimu mpya za mwaka wa kizio za mwaka 2019, pato halisi la Taifa lilikua kwa wastani wa 5.9% mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa 5.6% mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, kwa bei za mwaka husika Pato la Taifa lilifikia shilingi trilioni 238.104 mwaka 2025 sawa na dola za Kimarekani bilioni 91.81 ikilinganishwa shilingi trilioni 211.975 sawa na dola za Kimarekani bilioni 81.2 kwa mwaka 2024. Kutokana na mwenendo huo, wastani wa Pato wa Taifa kwa mtu uliongezeka kwa 7.4% na kufikia shilingi milioni 3,544,124 sawa na dola za Kimarekani 1,390 kwa mwaka 2025 ikilinganishwa na shilingi milioni 3,299,637 sawa na 1,264 kwa mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2025 sekta zilizokuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa zilikuwa kilimo ambacho kilichangia 24.3% ya pato ghafi la Taifa ikifuatiwa na ujenzi 11.9%, uchimbaji wa madini na mawe 10.3%, biashara na matengenezo 8.6% na usafirishaji na uhifadhi wa mizigo 8.3%. Sekta zilizoongoza kwa ukuaji ni fedha na bima 15.7%, umeme na gesi 11.8%, uchimbaji wa madini na mawe 9.4%, habari na mawasiliano 8.8%, sanaa na burudani 8.5% pamoja na usafirishaji na uhifadhi wa mizigo 8.0%.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2025 mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa 3.3% ikilinganishwa na 3.1% mwaka 2024. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuongezeka kwa bei za vyakula. Pamoja na ongezeko hilo, kiwango hicho kilikuwa ndani ya lengo la nchi la muda wa kati la 3.0% mpaka 5.0% na kukidhi vigezo vya

mtangamano wa kiuchumi kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki asilimia isiyozidi 8.0 pamoja na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika ambayo ni 3.0% mpaka 7.0%.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya hali ya uwekezaji ya dunia ya *UNCTAD* ya mwaka 2025 *(World Investment Report 2025)* uwekezaji kutoka nje ulifikia dola za Marekani bilioni 1.72 mwaka 2024 ukilinganisha na dola za Kimarekani bilioni 1.34 mwaka 2023 sawa na ukuaji wa 28.3%.

Mheshimiwa Spika, shughuli za uchimbaji madini na mawe ziliongoza kwa kuwa na uwekezaji mkubwa zaidi wenye thamani ya dola za Marekani milioni 442.2 ikifuatiwa na fedha na bima dola za Marekani milioni 401.3, uzalishaji bidhaa viwandani dola za Marekani milioni 223.1 na habari na mawasiliano dola za Marekani milioni 152.1.

Mheshimiwa Spika, shughuli hizo 12 zilichangia wastani wa 73.6% ya uwekezaji wote wa moja kwa moja kutoka nje. Aidha, shughuli za kilimo, ujenzi na usafirishaji na uhifadhi wa mizigo zilivutia uwekezaji wa moja kwa moja kwa 19.4% mwaka 2024 ikilinganishwa na 5.8% mwaka 2023. Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye ukuaji wa haraka wa uwekezaji Barani Afrika ikiwa imeshika nafasi ya 11 kwa kuvutia mitaji ya uwekezaji *(FDIs)*.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Taifa ya Takwimu, kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na wadau wengine imekamilisha utafiti wa mapato na matumizi ya kaya binafsi *(Household Budget Survey – HBS)* ya mwaka 2025, takwimu zitokanazo na utafiti huu hutumika katika kupanga, kutekeleza, kufuatilia na kutathmini programu na afua za maendeleo katika ngazi ya Taifa, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, takwimu hizi ndiyo chanzo kikuu cha kutoa viashiria vya upimaji na utekelezaji wa afua za kupunguza umaskini na kukuza uchumi nchini. Huu ni utafiti wa saba kwa Tanzania Bara na utafiti wa nne kwa Tanzania Zanzibar na ni utafiti wa kwanza ukihusisha pande zote za Muungano kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa Watanzania wanaoishi katika umaskini wa mahitaji ya msingi kwa Tanzania Bara ni 25.1%. Uchambuzi wa takwimu za mwenendo wa umaskini zinaonesha kuwa kiwango hicho kimekuwa kikipungua kutoka 34.4% mwaka 2007, 28.2% mwaka 2012, 26.4% mwaka 2018 na sasa 25.1% mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, mwenendo huu unaonesha kuwa jitihada zaidi zinahitajika katika kuongeza kasi ya kupunguza umaskini ili iendane na kasi ya ukuaji wa uchumi kama ilivyoainishwa katika Dira 2050.

Mheshimiwa Spika, kuhusu malengo na shabaha za msingi za uchumi jumla kwa mwaka 2026; malengo na shabaha za msingi za uchumi jumla ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa pato halisi la Taifa kufikia 6.3%;

(ii) Kuimarisha mfumuko wa bei uwe ndani ya wigo wa 3% hadi 5%;

(iii) Kuongeza mapato ya ndani kufikia 17.1% ya Pato la Taifa mwaka 2026/27;

(iv) Kuongeza mapato ya kodi kufikia 13.7% ya Pato la Taifa;

(v) Kuwa na nakisi ya bajeti isiyozidi 3.0% ya Pato la Taifa mwaka 2026;

(vi) Kiwango cha akiba ya fedha za kigeni kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne; na

(vii) Kuongeza uzalishaji wa ajira kufikia 1,700,000 mwaka 2026 kutoka ajira 981,000 zilizozalishwa mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2025/2026; Mpango

wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2025/2026 ni wa mwisho katika mfululizo wa mipango mitano ya muda mfupi iliyoandaliwa mahsusi kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Tatu wenye dhima ya Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu na ulikuwa ni nyenzo ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Hivyo, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2025/2026 ambao ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu, unahitimisha rasmi safari ya Dira 2025 na kuweka msingi wa kuanza utekelezaji wa Dira 2050 pamoja na nyenzo zake.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengi ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na mpango uliopita yameelezwa kwa ufasaha mkubwa na Mawaziri wakati wakiwasilisha hotuba za bajeti za Wizara zao. Katika muktadha huo, ninaomba kufanya majumuisho kwa kuweka muhtasari wa mafanikio ya utekelezaji wa mpango huo wa miaka mitano pamoja na mpango wa mwaka mmoja pamoja na miaka mitano ya mwanzo ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nimegawa mafanikio haya katika maeneo makubwa sita yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ni kufufua na kuimarisha wa ukuaji wa uchumi. Wakati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anaingia madarakani mwezi Machi, 2021 kama tunavyokumbuka sote, Tanzania kama ilivyokuwa kwa nchi zote duniani, ilikuwa inakabiliana na athari za ugonjwa wa UVIKO 19 na migogoro ya kidunia.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi chake cha miaka mitano ya mwanzo uchumi umeweza kukua kufikia 5.9% mwaka 2025 ukilinganisha na 4.7% mwaka 2021. Pili katika hilo, mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa nje ya nchi yameongezeka

kutoka dola za Marekani bilioni 6.4 mwaka 2021 alipoingia hadi kufikia dola za Kimarekani bilioni 10.6 mwaka 2025. Hayo ni mafanikio makubwa, *almost doubling export value in the last five years.*

Mheshimiwa Spika, pili; kukamilisha kwa mafanikio baadhi ya miradi mikubwa ya kielelezo na imetajwa na Waheshimiwa Mawaziri, niitaje tu kwa kukariri minne; *obviously,* ujenzi wa reli ya kisasa ya *SGR* ambapo wote tunaufahamu na huduma zinaendelea. Kilometa 680.38 zimeshakamilika na kazi inaendelea katika zote ambazo zimebaki.

Pili, kukamilishwa kwa utekelezaji wa mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere wenye uwezo wa kuzalisha *megawatts* 2,115. Hatua hii imewezesha uwezo wa kuzalisha umeme kuongezeka na kufikia *megawatts* 4,522.54 mwezi Machi, 2026 na kuifanya Tanzania kuwa nchi yenye kuzalisha kiasi kikubwa cha umeme katika ukanda huu wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, katika miaka 60 ya uhuru tuliweza kuzalisha umeme *megawatts* 1,600. Katika miaka mitano hii ya uongozi wa Awamu ya Sita ulioanzia Awamu ya Tano tumeweza kuzalisha zaidi ya *megawatts* 2,000.

Mheshimiwa Spika, mradi wa tatu ni ujenzi wa Daraja la JPM, *formally known as* Kigongo–Busisi umekamilika na umekuwa ni alama muhimu ya biashara na fursa katika Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa nne ni ununuzi wa meli na ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ya Kilwa ambayo *almost* imekamilika 97%, hatua ambayo itaanzisha na kuchochea rasmi uchumi wa buluu na kuweza kuongeza thamani katika sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu kuendelea kuimarika kwa mazingira ya biashara na uwekezaji kama nilivyoeleza na nne kuendelea kupanuka kwa fursa za ajira. Nitoe mifano michache hapa, nguvu kazi ya Tanzania kwa utafiti mpya wa *HBS* uliofanywa na *NBS* imefikia milioni 27.3 sawa na 73.2% ukilinganisha na 72.1%

mwaka 2020/2021. Kati ya hawa watu milioni 25.6 ndiyo wenye ujira ambapo 54.2% wameajiriwa katika sekta ya kilimo, 35.5% katika sekta ya huduma na 10.3% katika sekta uzalishaji viwandani.

Mheshimiwa Spika, utaona kwamba watu walioko katika sekta ya kilimo wamepungua kutoka 60% mwaka 2020/2021 na hiyo ni tabia ya nchi ambazo zinakuwa kuelekea uchumi wa kati. Hiyo haimaanishi kwamba umuhimu wa kilimo unapungua. Umuhimu wa kilimo upo palepale isipokuwa kilimo kinazidi kuwa cha kisasa na watu wengi wanajihusisha na sekta za uzalishaji viwandani pamoja na sekta ya huduma.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha ukosefu wa ajira *(unemployment)* kimepungua na kufikia 6.2% mwaka 2024, ukilinganisha na 8.7% kwa mwaka 2020/2021 na wastani wa ukuaji wa ajira kwa mwaka umeongezeka kufikia 7.8% mwaka 2024 ukilinganisha na 2.3% mwaka 2020/2021. Kwa hiyo, uwezo wetu wa kuzalisha ajira mwaka 2020/2021 ilikuwa 2.3% kwa mwaka, kwa sasa tumeongeza, tuna uwezo wa kuzalisha ajira angalau kwa 7.8%.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine takwimu hizi za kitakwimu inakuwa ngumu kuziona. Tuseme jambo moja muhimu hapa, kati ya mwaka 2016 na 2020 Serikali ilisitisha ajira na kupandishwa vyeo katika utumishi wa umma kwa miaka mitano. Hata hivyo, kama sehemu ya falsafa yake ya kuifungua nchi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alifungulia ajira na kupandishwa vyeo na madaraja katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, moja ya hatua ambazo Mheshimiwa Rais alizichukua mapema sana ni kufungulia ajira na kupandishwa kwa madaraja katika utumishi wa umma na katika kipindi cha miaka mitano iliyopita Serikali yake ya Awamu ya Sita imeshaajiri watumishi wa umma 32,833 ikiwemo walimu 7,000 na watumishi wa afya 5,000 waliaojiriwa kama sehemu ya kutekeleza ahadi za Mheshimiwa Rais ndani ya siku 100 baada ya kuapa

kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufuatia Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, tano ni kuendelea kupanuka kwa fursa na kuimarika kwa kiwango cha ubora wa huduma za jamii, ikiwemo:-

(i) Kupungua kwa vifo vya akina mama. Tumelisema hili mara nyingi;

(ii) Ujuzi wa kusoma na kuandika umeongezeka. Sasa umefikia 85.1%; na

(iii) Idadi ya wanafunzi wanaohitimu katika vyuo vikuu imeongezeka kufikia 62,570 kwa mwaka 2024, mwaka 2021 walikuwa wanafunzi 54,810.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Desemba, 2025 Serikali iliwekeza kwenye ujenzi wa miundombinu ya maji na usafi wa mazingira yenye uwezo wa kusambaza huduma ya maji vijijini kufikia 85.2% na kwa upande wa mijini kwa 92.5%.

Mheshimiwa Spika, sita kama sehemu ya muhtasari wa mafanikio; Serikali ya Awamu ya Sita imekamilisha kwa mafanikio makubwa maandalizi ya Dira 2050 na nyenzo zake zote za utekelezaji. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan anakuwa Rais anayekamilisha Dira ya 2025 na anayeanzisha utekelezaji wa Dira yetu mpya 2050.

Mheshimiwa Spika, sasa nieleze kuhusu malengo na vipaumbele vya mpango wa maendeleo wa taifa wa mwaka 2026/2027; katika kuyatekeleza malengo makuu ya Dira 2050, vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2026/2027 vimeandaliwa kwa kutohoa maeneo ya vipaumbele, malengo, shabaha, afua na viashiria muhimu vya utendaji vilivyoainishwa katika Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/2027 – 2030/2031 ambao dhima yake ni mageuzi kwa ajili ya ukuaji jumuishi wa uchumi na uzalishaji ajira na hicho kitakuwa kipimo kikubwa. Sekta zote na kila mtu

anachokifanya ni kwa kiasi gani anachangia kukuza uchumi jumuishi na kwa kiasi gani anazalisha ajira, ndilo litakuwa linatuongoza.

Mheshimiwa Spika, katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2026/2027, Serikali itatekeleza maeneo ya kipaumbele matano: -

(i) Kuimarisha utawala bora, demokrasia, amani na utulivu;

(ii) Kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani;

(iii) Kuimarisha uwezo wa watu na maendeleo ya jamii ikiwemo elimu, afya, maji, hifadhi ya jamii na makazi ya watu;

(iv) Kuimarisha uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu kwa mabadiliko ya tabianchi; na

(v) Kusimamia utekelezaji wa vichocheo vya mageuzi ikiwemo nishati, miundombinu ya usafiri na usafirishaji, utafiti na maendeleo, na mageuzi ya kidijiti.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza maeneo ya vipaumbele vilivyoainishwa hapo juu, Serikali imepanga kuanza kutekeleza programu na miradi mbalimbali ikiwemo miradi shikizi 38 kati ya 51 iliyopo katika programu saba za vielelezo vilivyoainishwa katika Mpango wa Nne wa Maendeleo ambao niliuwasilisha mwezi wa tatu.

Mheshimiwa Spika, gharama za utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2026/2027 zinakadiriwa kuwa shilingi trilioni 86.3 ambazo ni sawa na 18.1% ya gharama za kutekeleza Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambao gharama yake inatarajiwa kuwa shilingi trilioni 477.747.

Mheshimiwa Spika, gharama hizo 21 zitatokana na uwekezaji wa wadau wakubwa watatu; Serikali Kuu na Mamlaka

za Serikali za Mitaa, sekta binafsi na mashirika ya umma. Kati ya uwekezaji huo, sekta binafsi inatarajiwa kuchangia shilingi trilioni 60.1, sawa na 69.6%. Sekta ya umma kwa ujumla wake inatarajiwa kuchangia shilingi trilioni 26.2 sawa na 30.4% ambapo mashirika ya umma yanatarajiwa kuchangia shilingi trilioni 5.5. Serikali itachangia shilingi trilioni 20.8 itakayotengwa kutoka katika bajeti ya Serikali kama itakavyowasilishwa baadaye leo alasiri na Mheshimiwa Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wake katika kitabu chetu tunayo miradi ya maendeleo 366 na katika kitabu ambacho Waheshimiwa Wabunge wanacho ipo ukurasa wa 158 mpaka 171 na viashiria vya upimaji viko 304. Ufanisi wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2026/2027 utajengwa katika misingi nane ifuatayo: -

(i) Kuendelea kuwepo kwa demokrasia, amani, usalama na utulivu wa ndani na katika nchi jirani, inayowezesha shughuli za kiuchumi na uwekezaji kustawi;

(ii) Kudumisha misingi ya utawala bora na utawala wa sheria, ikiwa ni pamoja na uwajibikaji, uwazi na ufanisi katika matumizi ya rasilimali za umma;

(iii) Kuendelezwa kwa miundombinu ya nishati, bandari, barabara na reli ikiwa ni utekelezaji wa dhima ya kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara, viwanda na usafirishaji katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati;

(iv) Kuimarika kwa ubunifu na matumizi ya teknolojia za kidijiti katika kutoa huduma za kijamii na uzalishaji;

(v) Kuendelea kuimarika kwa mazingira ya biashara na uwekezaji yatakayochochea ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli za uchumi;

(vi) Kuendelea kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi na majanga ya asili na yasiyo ya asili ikiwemo ukame, mafuriko, vita, milipuko ya magonjwa na misukosuko ya

kiuchumi ya kimataifa kupitia mikakati ya kukabiliana na kupunguza athari zake;

(vii) Kuendelea kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa; na

(viii) Kuendelea kuimarika kwa upatikanaji na usalama wa chakula nchini.

Mheshimiwa Spika, nifanye hitimisho; hakuna shaka kwamba kazi kubwa imefanyika katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na katika miaka mitano ya Awamu ya Sita ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mafanikio yaliyopatikana na changamoto zilizojitokeza yameweka msingi imara katika kuanza utekelezaji wa Dira 2050 na mikakati yake.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2026 ni nyenzo ya kwanza katika kuanza utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo ya Taifa wa miaka mitano 2026/2027 – 2030/2031 na Dira 2050. Aidha, Serikali imekamilisha nyenzo zote muhimu za utekelezaji wa Dira 2050. Nyenzo hizo ni pamoja na Mpango Elekezi wa muda mrefu *(Longterm Perspective Plan)* 2026/2027 – 2050/2051, Mpango wa Nne wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano *(Fourth Five Year Development Plan)* 2026/2027 – 2030/2031, Mwongozo wa Kitaifa wa Uandaaji Mipango, Mwongozo wa Kitaifa wa Uidhinishaji wa Miradi ya Maendeleo, Mwongozo wa Kitaifa na Ufuatiliaji wa Tathmini ya Miradi ya Maendeleo *(National Monitoring Evaluation Learning and Accountability Framework)* na Mkakati wa Mawasiliano wa Dira 2050 wa miaka mitano yaani 2026/2027 – 2030/2031.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kufuatia kukamilika kwa nyenzo hizo, utekelezaji wa Dira 2050 kazi iliyo mbele yetu sasa ni moja tu, nayo ni kutekeleza. Tumeshapanga na Mheshimiwa Rais kwa mara ya kwanza amekamilisha dira kwa wakati mwaka 2000 tulikuwa na dira tu, hatukuwa na nyenzo za utekelezaji zimekuja

kupatikana miaka 10 baadaye. Safari hii dira ipo na nyenzo zote za utekelezaji zipo. Kwa hiyo, kama ambavyo umetuasa mara zote, sote Serikali, sekta binafsi, Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kazi iliyopo mbele yetu sasa ni moja tu, kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatilaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo, mafanikio ya utekelezaji wa Dira 2050 na mikakati yake, yatapimwa kwa kuzingatia viashiria vya matokeo *(key performance indicators)* kwa kila sekta. Hatutapimwa kwa wingi wa shughuli wala uhodari wa kukamilisha michakato, tutapimana kwa mujibu wa viashiria vya matokeo *(key performance indicators)*. Katika vitabu ambavyo tumetoa, kila sekta imepewa viashiria vyake. Zipo sekta kwa ujumla wake 22 na vipaumbele 12. Nivieleze hapa, tumevigawa katika maeneo matano kwa kuzingatia msingi mkuu wa dira, kuzingatia nguzo za dira na kwa kuzingatia vichocheo vya dira.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, eneo la utawala, amani, usalama na utulivu; ipo ukurasa wa 81 – 134 Sura ya Nane ya vitabu ambavyo tumewagawia Waheshimiwa Wabunge. Viashiria hapa vipo 26, viashiria vya uchumi imara jumuishi na shindani vipo 90; viashara vya uwezo wa watu na maendeleo ya jamii ikiwemo elimu, afya, maji, hifadhi ya jamii na ardhi na makazi vipo 141; mazingira ya ustahimilivu dhidi ya mabadiliko tabianchi vipo saba; na vichocheo, kwa maana ya nishati, TEHAMA, ujenzi, uchukuzi, sayansi na teknolojia 40. Jumla ya viashiria 304 na tumevigawa kwa kila sekta.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mnapotupima Waheshimiwa Wabunge tupimeni kwa mujibu wa viashiria hivyo na siyo namna tunavyoshughulika. Shughuli ni muhimu, lakini tunataka matokeo. Kwa hiyo, watu watapewa tuzo tupongezane kwa uhodari wa kutekeleza viashiria hivi na siyo kwa uhodari wa uchakarikaji, viashiria vya upimaji wa matokeo *(key performance indicators)*.

Mheshimiwa Spika, ninapohitimisha, ninapenda kurejea maelekezo ya CCM kuhusu maendeleo vijijini. Ilani ya CCM

ambacho ni chama tawala, ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 ilibaini kuwa wananchi wengi bado wanaishi vijijini na kwamba kasi ya maendeleo vijijini inahitaji kuongezeka na kupewa msukumo mpya. Aidha, CCM inatambua umuhimu wa kuimarisha maendeleo vijijini na kufanya vijiji vikue kiuchumi na katika huduma za jamii ili kupunguza wimbi la vijana kuhamia mijini kwa kukuza ajira. Hivyo basi, ningependa kuwakumbusha watekelezaji wote wa Ilani ya CCM na Mpango wa Maendeleo kuzingatia maelekezo 12 mahususi yaliyotolewa na Ilani ya CCM kuhusu kuongeza kasi ya maendeleo vijini kama ifuatavyo: -

(i) Kuendelea kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu ya barabara na madaraja vijijini ili kurahisisha usafiri na usafirishaji na kuunganisha maeneo ya uzalishaji na masoko. Hapa wahusika wakubwa ni Wizara ya Ujenzi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kupitia *TARURA* na *TANROADS;*

(ii) Kuanza programu maalum; Ilani imeagiza kuanza programu maalum ya ujenzi wa nyumba bora vijijini na wahusika hapa ni Wizara ya Ardhi pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI;

(iii) Kuimarisha huduma ya mawasiliano ili kuongeza kasi na kupanua wigo wa matumizi ya teknolojia ya habari kwa wananchi wa vijijini, ili kunufaika na fursa zitokanazo na shughuli za uzalishaji kiuchumi na kijamii. Ilani iliagiza kuweka sera za kikodi za kuvutia uwekezaji, kuimarisha huduma za mawasiliano vijijini;

(iv) Kuongeza kasi ya kusogeza huduma za msingi ikiwepo maji, afya, elimu na umeme vijijini. Wahusika hapo wakubwa ni Wizara yetu inayohusika na TEHAMA pamoja na Wizara ya Fedha;

(v) Kukuza stadi za maisha na ujuzi miongoni mwa vijana kwa kujenga na kuweka mazingira wezeshi ya ujenzi wa vyuo vya mafunzo ya amali, ili kukuza ajira katika kila

wilaya. Wahusika Wizara ya Elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI;

(vi) Kupitia upya mifumo ya uuzaji wa mazao ya kilimo, mifugo na misitu kwa lengo la kunufaisha wakulima, kurahisisha na kuwezesha mazingira ya kufanya biashara vijijini. Hapa tunahusika sote chini ya usimamizi Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI;

(vii) Kuweka mazingira maalum ya kuvutia ujenzi wa viwanda vidogo vidogo vijijini kwa lengo la kufanya uchakataji wa malighafi katika sekta za kimkakati zikiwemo kilimo, mifugo, uvuvi na misitu ili kuongeza fursa za ajira na kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno. Muda mfupi uliopita Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Mheshimiwa Waziri wa Uvuvi wameeleza wanavyofanya jambo hilo;

(viii) Kuimarisha usalama wa chakula kwa kuboresha uhifadhi wa mazao, kuwapatia wakulima teknolojia za kisasa za uhifadhi wa chakula na kuanzisha na kuendeleza kilimo cha mazao yanayohimili ukame na mabadiliko ya tabia nchi;

(ix) Kuimarisha miundombino ya masoko ikijumuisha vituo vya ukusanyaji na uongezaji wa thamani;

(x) Kuweka mfumo mpya wa upatikanaji wa fedha vijijini kwa kutekeleza mpango maalum wa kurahisisha utoaji wa huduma na kutoa mikopo yenye riba ndogo itakayowezesha wananchi kuwekeza katika kilimo cha kisasa na shughuli za ujasiriamali;

(xi) Kupanga matumizi bora ya ardhi matumizi bora ya ardhi, kupima na kumilikisha ardhi kwa wananchi ili kuwezesha kupata mikopo na motisha ya kuweka zaidi katika kilimo, ufugaji na shughuli nyingine za kiuchumi. CCM ilielekeza katika Ilani kwamba angalau asilimia 60

ya ardhi yote vijijini iwe imepimwa ifikapo mwaka 2030; na

(xii) Kuimarisha Vyama vya Ushirika kimuundo, utawala, uendeshaji na kirasiliamali kama vyombo muhimu vya sauti ya wakulima, wafugaji na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona nimalizie na maelekezo ya CCM kwa sababu Serikali hii ya Awamu ya Sita imeundwa na Chama Cha Mapinduzi na Serikali hii inawajibika kutekeleza maelekezo ya ilani kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, na nikiwaahidi, kwa niaba wenzangu Serikalini kwamba tutasimamia utekelezaji wa maelekezo yote ya Chama Cha Mapinduzi kupitia Ilani yake.

Mheshimiwa Spika, ninavyohitimisha, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wenzangu tunaofanya nao kazi; Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Pius Stepen Chaya, Mbunge wa Manyoni, kijana machachari sana, kwa usaidizi wake muhimu na umahiri wake katika kutusaidia. Nimshukuru sana Dkt. Tausi Mbaga Kida - Katibu Mkuu na Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango na timu yake wakiwepo Naibu Watendaji wa Tume kwa jinsi ambavyo wameandaa taarifa hizi makini, mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwashukuru *PST* Dkt. Natu Mwamba kwa ushirikiano katika kuandaa taarifa ya Hali ya Uchumi wa *Taifa Management* na wote ambao tunafanya nao kazi. Kipekee ninawashukuru sana wadau wa maendeleo ambao tumefanya nao kazi katika kuandaa taarifa hizi.

Mheshimiwa Spika, hotuba yetu hii inapatikana pia katika tovuti zetu za Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji pamoja na tovuti ya Tume ya Taifa ya Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ninayo heshima kuliomba Bunge lako likubali kupokea, kujadili na kupitisha Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2025 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2026/2027.

**11 JUNI, 2026**

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja.

**Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo (Mb.), akiwasilisha Bungeni Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/2027 – Kama Ilivyowasilishwa Mezani**

**Dodoma, Alhamisi 11 Juni 2026**

---

**I: UTANGULIZI**

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia Kanuni ya 127 (8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/2027. Pamoja na hotuba hii, ninawasilisha vitabu vya Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/2027. Taarifa hizi mbili ndiyo msingi wa Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2026/2027 itakayowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika Bunge lako Tukufu baadaye leo alasiri.

**2.** ***Mheshimiwa Spika***, awali ya yote, ninamshukuru Mungu kwa neema ya uhai, afya, amani na utulivu iliyotuwezesha kukutana hapa leo na katika kipindi chote cha Bunge hili la Bajeti.

**3.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa heshima kubwa, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa fursa aliyonipatia ya kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji) ambayo imeniwezesha kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha taarifa hii kwa niaba yake na kwa niaba ya Serikali anayoiongoza.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Emmanuela Kaganda Mtatifikolo kwa kuchaguliwa

kuwa Mbunge wa Jimbo la Isimani. Ninamtakia mafanikio makubwa katika kuwatumikia wananchi wa Jimbo la Isimani na watanzania kwa ujumla.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue nafasi hii pia kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake makini. Kwa kipekee, ninamshukuru na kumpongeza kwa ziara yake ya kihistoria na yenye mafanikio makubwa aliyoifanya hivi karibuni katika taifa kubwa la Urusi, akiwa ni Rais wa pili wa Tanzania kufanya ziara rasmi nchini Urusi.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** ni muhimu kuzingatia kuwa ziara ya Mheshimiwa Rais nchini Urusi ni sehemu ya utekelezaji wa falsafa yake ya kuifungua nchi au *pragmatizimu*, inayozingatia uhalisia wa mambo kwa wakati husika katika kufanya maamuzi ya msingi ya kisera za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Katika falsafa hii anapofanya ziara za nje, Mheshimiwa Rais anaenda kutafuta washirika (*partners*), sio wafadhili/wadhamini (*sponsors/patrons*). Mheshimiwa Rais anaenda nje kutafuta fursa za biashara na uwekezaji, na sio kutafuta misaada! Na katika kusaka fursa za biashara na uwekezaji hatutachagua wapi pa kwenda wala hatutakubali kuchaguliwa rafiki wala adui. Kama alivyowahi kusema Deng Xiaping, Rais wa zamani wa China, *"It doesn't matter whether a cat is black or white, as long as it catches mice."*

**7.** ***Mheshimiwa Spika***, msimamo huu wa Rais wetu wa kukataa kuchaguliwa marafiki sio mgeni kwa nchi yetu. Mara baada ya nchi nyingi za Afrika kupata uhuru miaka ya sitini lilitokea wimbi na shinikizo kubwa la kuzisukuma nchi za Afrika kuchagua upande wa kushoto au kulia, au upande wa magharibi au mashariki, kama ilivyojulikana wakati huo. Kufuatia shinikizo hilo, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa kwanza na Baba wa Taifa letu, aliweka msimamo wa wazi ambao ndiyo msimamo wetu hadi leo, aliposema:
*"We desire friendship with the countries of the East as well as with those of the West, and on the basis of mutual respect and non-interference in internal affairs. We will not allow any of our*

*friendships to be exclusive; we will not allow anyone to choose our friends or enemies for us."*

Kwa umuhimu wake ninaomba kutafsiri: *"Tunadhamiria kudumisha urafiki na nchi za Mashariki na za Magharibi kwa misingi ya kuheshimiana, usawa na kutokuingiliana katika masuala ya ndani ya mataifa mengine. Hatutaruhusu uhusiano wetu wa kirafiki na taifa lolote kuwa wa kipekee, wala hatutakubali taifa lolote lituchagulie marafiki au maadui wetu. Hilo ni jukumu letu sisi wenyewe kama taifa huru na lenye mamlaka kamili juu ya maamuzi yake."*

**8.** Hivyo basi, ***Mheshimiwa Spika,*** katika kusaka fursa za kiuchumi, tutazingatia maslahi yetu mapana kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya utangulizi huo ninaomba sasa kuwasilisha taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27 katika sehemu tano zifuatazo: *Muktadha wa Uchumi wa Dunia; Mwenendo wa Hali ya Uchumi Duniani, Kikanda na Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2025; Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26; Malengo na Vipaumbele katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27;* na *Hitimisho.*

**II: MUKTADHA WA UCHUMI WA DUNIA**

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninawasilisha taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27 katika katika kipindi ambacho dunia ipo katika hali ya mtikisiko mkubwa wa kiuchumi na kisiasa kutokana na migogoro mbalimbali inayoendelea. Migogoro hii ni pamoja na vita inayoendelea katika ukanda wa Mashariki ya Kati baina ya Marekani na Israel dhidi ya Iran na vita ya Urusi na Ukraine.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Taifa ya Mipango, kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), imefanya utafiti kuhusu athari za vita ya uajemi katika

uchumi wa Tanzania na fursa zinazotokana na vita hiyo (*Assessing the economic impacts of the gulf crisis on Tanzania: Risks, resilience, opportunities and strategic priorities*). Taarifa ya matokeo ya utafiti huo yaliwasilishwa na kujadiliwa na wadau mbalimbali wa maendeleo tarehe 22 Mei 2026 Jijini Dar es Salaam.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** taarifa ya utafiti huo unaonesha kuwa vita dhidi ya Iran iliyoanza rasmi mwezi Februari 2026 imesababisha taharuki katika masoko ya mafuta duniani kufuatia hofu ya kuvurugika kwa usafirishaji wa mafuta kupitia Ghuba ya Uajemi na maeneo mengine muhimu ya usafirishaji wa kimataifa. Kutokana na hali hiyo, bei za mafuta katika soko la dunia zimeendelea kupanda na kusababisha kupanda kwa gharama za uzalishaji, usafirishaji na huduma katika mataifa mengi duniani.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** taarifa inaonesha kuwa katika kipindi cha miezi mitatu ya vita dhidi ya Iran, bei ya mafuta ghafi iliongezeka kwa wastani wa dola za Marekani 107.3 kwa pipa kati ya 28 Februari 2026 vita ilipoanza na Juni 5, 2026. Bei hizo za mafuta zilipanda kutoka dola za Marekani 100 kwa pipa mwezi Machi 2026 hadi kufikia dola 126 mwezi Aprili 2026. Bei hizo zimeshuka hadi kufikia dola 90-95 kwa ukanda wa Ulaya na Afrika kwa Juni 8-9, 2026. Bei hizi hutegemea hali ya mashambulizi na mazungumzo yanayoendelea kati ya Marekani na Iran.

**14.** ***Mheshimiwa Spika***, vita ya Iran imeathiri pia minyororo ya usambazaji wa bidhaa na huduma duniani kwa kuongeza gharama za usafirishaji wa mizigo na muda wa usafirishaji. Aidha, baadhi ya kampuni za usafirishaji zimebadilisha njia za usafirishaji ili kuepuka maeneo yenye migogoro hali iliyoongeza gharama za biashara ya kimataifa. Hali hiyo imeathiri upatikanaji wa baadhi ya bidhaa muhimu zikiwemo mafuta, mbolea, malighafi za viwandani na bidhaa za chakula katika baadhi ya masoko duniani.

**15.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na kuongezeka kwa

gharama za nishati na usafirishaji, mfumuko wa bei duniani umeendelea kuwa katika viwango vya juu katika baadhi ya nchi. Aidha, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia inatarajiwa kupungua endapo mgogoro huo utaendelea kwa muda mrefu kutokana na kudorora kwa biashara, uwekezaji na matumizi ya walaji.

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, Taarifa hiyo inaonesha kuwa athari za vita ya Iran zimejitokeza kutokana na ongezeko la gharama za uagizaji wa mafuta, mbolea na bidhaa nyingine muhimu, pamoja na kuongezeka kwa gharama za usafirishaji. Aidha, baadhi ya nchi zinaweza kushuhudia kupungua kwa akiba ya fedha za kigeni kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya fedha za kuagiza bidhaa kutoka nje.

**17.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa Tanzania, athari za vita ya Iran zinajitokeza katika maeneo mbalimbali ya kiuchumi, hususan katika sekta za nishati, uchukuzi, viwanda, biashara na kilimo. Kwa upande wa mbolea, kwa mfano, Tanzania huagiza asilimia 30 hadi 40 ya mbolea (Urea na DAP) kutoka nchi za Ghuba (hususan Qatar). Vita inayoendelea inatarajiwa kusababisha ongezeko la bei ya mbolea hali ambayo itasababisha kuongezeka kwa bei katika soko la ndani na hivyo kuathiri shughuli za kilimo kwa msimu ujao wa mwaka 2026/27.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa mafuta, Tanzania huagiza kwa asilimia 100 bidhaa za petroli zilizosafishwa (*Refined Petroleum Products*) kutoka nje ya nchi (sawa na asilimia 13 ya thamani ya bidhaa zote zinazoagizwa nchini). Sehemu kubwa ya mafuta haya (60-70%) huagizwa kutoka nchi za Ghuba (husuani Umoja wa Falme za Kiarabu, Saudi Arabia, na Kuwait), India na Singapore.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na athari zingine, kuongezeka kwa bei za mafuta kumeongeza gharama za uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa na huduma. Aidha, suala hili linaweza kuiathiri sekta ya utalii inayochangia takribani dola za Marekani

milioni 4,410.6 na kutoa ajira takribani milioni 1.5 kupitia ongezeko la bei ya tiketi za ndege na kuahirishwa kwa safari za ndege.

**20.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na migogoro ya kidunia. Hatua hizo ni pamoja na kuendelea kuimarisha usimamizi wa sera za fedha na bajeti ili kudhibiti mfumuko wa bei; kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala; kuimarisha uhifadhi wa akiba ya mafuta; pamoja na kuendelea kutafuta masoko mbadala ya bidhaa zinazouzwa nje. Vile vile, Serikali inaendelea kuhamasisha uzalishaji wa ndani wa bidhaa muhimu ili kupunguza utegemezi wa bidhaa kutoka nje hususani mbolea na baadhi ya malighafi za viwandani. Aidha, jitihada zinaendelea kufanyika katika kuimarisha sekta za usafirishaji, biashara na uwekezaji ili kuongeza ustahimilivu wa uchumi wa Taifa dhidi ya mishtuko ya kiuchumi ya kimataifa.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na athari hasi za migogoro inayoendelea duniani, hususan vita ya Marekani na Israeli dhidi ya Iran, migogoro hiyo pia inatoa fursa za kiuchumi ambazo tukizitumia vizuri zinaweza kuleta manufaa ya kiuchumi kwa nchi yetu. Baadhi ya maeneo ya fursa ni pamoja na kuongeza uzalishaji wa bidhaa ambazo soko lake limeathiriwa na mgogoro na hivyo kuongeza uwezo wetu wa ushindani wa kibiashara. Kwa mfano, fursa ipo katika kutoa huduma za upakuaji na uhifadhi wa shehena za mizigo kwa muda (transhipment) kwa meli ambazo zimeshindwa kufikisha shehena hizo katika bandari za Mashariki ya kati kutokana na uwepo wa vita. Aidha, vita hii inatoa nafasi kwa nchi yetu kuvutia wawekezaji ambao sasa wanaona eneo la ghuba sio salama tena kwa uwekezaji wao, ikiwemo kuvutia uwekezaji katika eneo la gesi ili kujilinda na athari za majanga kama hayo katika siku zijazo.

**22.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa uchumi wa dunia na athari za migogoro ya kimataifa ili kuhakikisha kuwa hatua za kisera zinazochukuliwa zinaendelea kulinda uthabiti wa uchumi wa Taifa, ustawi wa wananchi na mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

## III: MWENENDO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2025

### a) Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Dunia na Kikanda

**23.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Aprili 2026, uchumi wa dunia umeendelea kukua kwa wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2025 kama ilivyokua kwa mwaka 2024. Hata hivyo, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia inatarajia kupungua na kufikia wastani wa asilimia 3.1 mwaka 2026.

**24.** ***Mheshimiwa Spika***, kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara iliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 4.4 mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.2 mwaka 2024. Ukuaji huu ulichangiwa na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi, hususan uwekezaji katika sekta ya umma; kuimarika kwa mauzo ya bidhaa nje; na utekelezaji madhubuti wa sera za kupunguza mfumuko wa bei. Ukuaji wa uchumi katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara unatarajiwa kupungua hadi wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2026 na kuongezeka hadi wastani wa asilimia 4.4 mwaka 2027.

**25.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika – SADC, uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 3.1 mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.2 mwaka 2024 na unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2026.

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika ukanda wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ukuaji uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 10.4 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 1.4 mwaka 2024. Ongezeko la kasi ya ukuaji wa uchumi wa ukanda wa EAC lilichangiwa na kupanda kwa uchumi wa nchi ya Sudani Kusini ambao ulikuwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 46.1 mwaka 2025 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 26.1 mwaka 2024. Ukuaji wa uchumi kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki unatarajiwa kupungua hadi wastani wa asilimia 5.2 mwaka 2026 na kuongezeka hadi asilimia 5.3 mwaka 2027.

**27.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa mujibu wa taarifa ya IMF ya Aprili 2026, mfumuko wa bei wa dunia ulipungua kutoka wastani wa asilimia 5.8 kwa mwaka 2024 hadi asilimia 4.1 mwaka 2025. Hii ilitokana na utekelezaji wa sera za fedha zilizolenga kuwa na utulivu wa mfumuko wa bei. Mwenendo huu unaonesha imani ya kufikia malengo ya kudhibiti mfumuko wa bei kwa nchi ya Marekani na nchi nyingine zilizoendelea.

**28.** ***Mheshimiwa Spika***, uchambuzi wa takwimu kwa kuzingatia makundi ya nchi unaonesha kuwa mfumuko wa bei kwa nchi zenye kipato cha chini ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 13.1 mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 19.9 mwaka 2024; kwa nchi zinazoibukia na zinazoendelea kiuchumi ulipungua hadi wastani wa asilimia 4.6 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 7.1 mwaka 2024; na kwa nchi zilizoendelea ulipungua kufikia wastani wa asilimia 2.7 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 2.9 mwaka 2024. Aidha, mfumuko wa bei wa dunia unatarajiwa kuongezeka kutoka asilimia 4.1 mwaka 2025 hadi asilimia 4.4 mwaka 2026.

**29.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 12.0 mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 54.5 mwaka 2024. Aidha, Katika ukanda wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), mfumuko wa bei umeendelea kutofautiana kati ya wanachama, ambapo Burundi ilikuwa na kiwango cha juu zaidi ya wastani wa asilimia 34.2 mwaka 2025, ikilinganishwa na asilimia 20.2 mwaka 2024. Kenya ikifikia asilimia 4.5, Uganda asilimia 3.6, Tanzania asilimia 3.3, na Rwanda asilimia 7.0 mwaka 2025.

### b) Hali ya Uchumi wa Taifa

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2025, Serikali kupitia Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilikamilisha maboresho ya takwimu za Pato la Taifa kwa kutumia mwaka 2019 kama mwaka wa kizio badala ya mwaka 2015. Kufuatia maboresho hayo, mabadiliko kadhaa yalijitokeza ikiwemo: ukubwa wa Pato la Taifa; viwango vya ukuaji na mchango wa sekta mbalimbali katika Pato la Taifa; na

uwiano wa viashiria mbalimbali kwa Pato la Taifa. Kwa mujibu wa takwimu mpya za mwaka wa kizio wa 2019, Pato halisi la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 5.9 mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.6 mwaka 2024.

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa bei za mwaka 2019, Pato la Taifa lilifikia shilingi Trilioni 234.104 mwaka 2025 (dola za Marekani bilioni 91.81), ikilinganishwa na Trilioni 211.975 (dola bilioni 81.2) kwa mwaka 2024. Kutokana na mwenendo huo, wastani wa Pato la Taifa kwa mtu uliongezeka kwa asilimia 7.4 na kufikia shilingi 3,544,124 (dola 1,390) mwaka 2025 ikilinganishwa na shilingi 3,299,637 (dola 1,264) mwaka 2024.

**32.** ***Mheshimiwa Spika***, mwaka 2025, sekta zilizokuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa zilikuwa kilimo ambacho kilichangia *asilimia 24.3* ya Pato Ghafi la Taifa, ikifuatiwa na ujenzi (*asilimia 11.9*), uchimbaji madini na mawe (*asilimia 10.3*), biashara na matengenezo (*asilimia 8.6*) na usafirishaji na uhifadhi wa mizigo (*asilimia 8.3*).

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** sekta zilizoongoza kwa ukuaji ni fedha na bima (*asilimia 15.7*); umeme na gesi (*asilimia 11.8*), uchimbaji wa madini na mawe (asilimia 9.4), habari na mawasiliano (*asilimia 8.8*), sanaa na burudani (*asilimia 8.5*), pamoja na usafirishaji na uhifadhi wa mizigo (*asilimia 8.0*).

**34.** ***Mheshimiwa Spika***, mwaka 2025, mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 3.3 ikilinganishwa na asilimia 3.1 mwaka 2024. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuongezeka kwa bei za vyakula. Pamoja na ongezeko hilo, kiwango hicho kilikuwa ndani ya lengo la nchi la muda wa kati la asilimia 3.0 hadi 5.0 na kukidhi vigezo vya mtangamano wa kiuchumi kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (asilimia isiyozidi 8.0) pamoja na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (asilimia 3.0 hadi 7.0).

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa taarifa ya hali ya uwekezaji ya Dunia ya UNCTAD ya mwaka 2025 (World Investment Report 2025), uwekezaji kutoka nje ulifikia dola za

Marekani bilioni 1.72 mwaka 2024, ukilinganisha na dola bilioni 1.34 mwaka 2023, sawa na ukuaji wa asilimia 28.3. Shughuli za uchimbaji madini na mawe ziliongoza kwa kuwa na uwekezaji mkubwa zaidi wenye thamani ya dola za Marekani milioni 442.2, ikifuatiwa na fedha na bima dola za Marekani milioni 401.3, uzalishaji bidhaa viwandani dola za Marekani milioni 223.1 na habari na mawasiliano dola za Marekani milioni 152.1. Shughuli hizo zilichangia wastani wa asilimia 73.6 ya uwekezaji wote wa moja kwa moja kutoka nje. Aidha, shughuli za kilimo, ujenzi, na usafirishaji na uhifadhi mizigo zilivutia uwekezaji wa moja kwa moja kwa asilimia 19.4 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 5.8 mwaka 2023. Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye ukuaji wa haraka wa uwekezaji barani Afrika (nafasi ya 11 kwa ukubwa wa FDIs).

**36.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa mujibu wa taarifa ya Mwongozo wa Biashara na Uwekezaji Tanzania ya mwaka 2026 (Tanzania Business and Investment Guide, 2026), Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi (TISEZA) ilisajili jumla ya miradi 915 mwaka 2025, yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 10.95 ikilinganishwa na miradi 901 yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 9.3 mwaka 2024 (sawa na ongezeko la asilimia 17.74 la thamani ya miradi iliyosajiliwa). Idadi hii ya miradi iliyosajiliwa imevunja rekodi ya usajili wa miradi tangu kuanzishwa kwa Kituo cha Uwekezaji (TIC) mwaka 1996 na baadaye TISEZA mwaka 2025. Miradi hiyo ipo katika sekta mbalimbali zikiwemo viwanda, ujenzi wa majengo ya biashara, usafirishaji, utalii na kilimo. Aidha, miradi iliyosajiliwa na TISEZA mwaka 2025 inatarajiwa kuzalisha ajira zaidi ya 162,895.

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (OCGS) na wadau wengine, imekamilisha utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi (*Household Budget Survey – HBS*) ya mwaka 2025. Takwimu zitokanazo na utafiti huu hutumika katika kupanga, kutekeleza, kufuatilia na kutathmini programu na afua za maendeleo katika ngazi ya Taifa, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, takwimu hizi ndio chanzo kikuu cha kutoa viashiria vya upimaji na utekelezaji wa afua za

kupunguza umaskini na kukuza uchumi. Huu ni utafiti wa saba kwa Tanzania Bara na utafiti wa nne kwa Tanzania Zanzibar, na ni utafiti wa kwanza ukihusisha pande zote za Muungano kwa wakati mmoja.

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** matokeo ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi Tanzania 2025 yanaonesha kuwa Watanzania wanaishi katika umaskini wa mahitaji ya msingi ambapo kwa Tanzania Bara ni asilimia 25.1 Uchambuzi wa takwimu za mwenendo wa umaskini zinaonesha kuwa idadi ya Watanzania wanaoishi katika umaskini wa mahitaji ya msingi kwa Tanzania Bara kimekuwa ikipungua kutoka asilimia 34.4 (mwaka 2007), asilimia 28.2 (mwaka 2012), asilimia 26.4 (mwaka 2018) na asilimia 25.1 (mwaka 2025). Mwenendo huu unaonesha kuwa jitihada zaidi zinahitajika katika kuongeza kasi ya kupunguza umaskini ili iendane na kasi ya ukuaji wa uchumi kama ilivyoainishwa katika Dira 2050.

**c) Malengo na Shabaha za Msingi za Uchumi Jumla kwa Mwaka 2026**

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** malengo na shabaha za msingi za uchumi jumla ni kama ifuatavyo:

(i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 6.3 mwaka 2026 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.9 kwa mwaka 2025;

(ii) Kuimarisha mfumuko wa bei katika wigo wa asilimia 3.0 – 5.0 katika kipindi cha muda wa kati, ili kulinda uwezo wa wananchi kumudu mahitaji muhimu;

(iii) Kuongeza mapato ya ndani kufikia asilimia 17.1 ya Pato la Taifa mwaka 2026/27, kutoka asilimia 16.8 mwaka 2025/26;

(iv) Kuongeza mapato ya kodi kufikia asilimia 13.7 ya Pato la Taifa mwaka 2026/27, kutoka asilimia 13.3 mwaka 2025/26;

(v) Kuwa na nakisi ya bajeti isiyozidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa mwaka 2026;

(vi) Kiwango cha akiba ya fedha za kigeni kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4); na

(vii) Kuongeza uzalishaji wa ajira kufikia 1,700,000 mwaka 2026 kutoka ajira 981,000 zilizozalishwa mwaka 2024.

## VI: TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2025/26

**40.** ***Mheshimiwa Spika***, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 ni wa mwisho katika mfululizo wa mipango mitano ya muda mfupi iliyoandaliwa mahususi kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26). Mpango wa Tatu wenye dhima ya "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu" ulikuwa nyenzo ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Hivyo, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 ambao ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu, unahitimisha safari ya Dira 2025 na kuweka msingi wa kuanza utekelezaji wa Dira 2050.

**41.** ***Mheshimiwa Spika***, mafanikio mengi ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano yameelezwa kwa ufasaha na waheshimiwa mawaziri wakati wakiwasilisha hotuba za bajeti za wizara zao. Katika muktadha huo, ninaomba kufanya majumuisho kwa kuweka muhtasari wa mafanikio ya utekelezaji wa Mpango huo na miaka mitano ya mwanzo ya Serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

i) ***Kufufua na kuimarisha wa ukuaji wa uchumi***: Wakati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anaingia madarakani mwezi Machi 2021 Tanzania, kama ilivyokuwa kwa nchi zingine duniani, ilikuwa inapambana na athari za ugonjwa wa UVIKO 19 na migogoro ya kidunia. Katika kipindi chake:

- Uchumi umeweza kukua kutoka asilimia 4.7 mwaka 2021 hadi kufikia asilimia 5.9 mwaka 2025, na unatarajiwa kukua kwa asilimia 6.3 mwaka huu.

- Mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa nje ya nchi yameongezeka kutoka dola za Marekani bilioni 6.4 mwaka 2021 hadi kufikia dola bilioni 10.6 mwaka 2025.

ii) Kukamilisha baadhi ya miradi mikubwa ya kielelezo, ikiwemo:

- Ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR ambapo jumla ya kilomita 680.38 zimejengwa na huduma tayari zimeanza kutolewa katika kipande cha Dar es Salaam hadi Dodoma.

- Kukamilishwa kwa utekelezaji wa mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere wenye uwezo wa kuzalisha Megawati 2,115. Hatua hii imewezesha uwezo wa kuzalisha umeme kuongezeka na kufikia MW 4,522.54 Machi, 2026. Huu ni uwekezaji mkubwa unaokwenda kubadilisha mazingira ya uzalishaji viwandani, kuongeza uhakika wa nishati, na kuimarisha ushindani wa uchumi wetu.

- Ujenzi wa Daraja la JPM (Kigongo–Busisi) umekamilika na kuwa alama ya uwezo wa Taifa katika kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati. Daraja hili limeunganisha watu, biashara na fursa

- Ununuzi wa meli na ujenzi wa bandari ya uvuvi ya Kilwa umefikia asilimia 97, hatua itakayochochea uchumi wa buluu na kuongeza thamani katika sekta ya uvuvi.

iii) Kuendelea kuimarika kwa mazingira ya biashara na uwekezaji kunakothibitishwa na kuendelea kukua kwa mitaji ya uwekezaji kama nilivyoeleza awali

iv) Kuendelea kupanuka kwa fursa za ajira ambapo:

- Nguvu kazi imefikia milioni 27.3 sawa na asilimia 73.2 ukilinganisha na asilimia 72.1 mwaka 2020/21. Kati ya

hawa, watu milioni 25.6 ndiyo wenye ujira, ambapo asilimia 54.2 wanafanya kazi katika sekta ya kilimo, asilimia 35.5 katika sekta ya huduma na asilimia 10.3 katika sekta uzalishaji viwandani.

- Kiwango cha ukosefu wa ajira (*unemployment)* kimepungua na kufikia asilimia 6.2 mwaka 2024, ukilinganisha na asilimia 8.7 kwa mwaka 2020/21. Wastani wa ukuaji wa ajira kwa mwaka umeongezeka kufikia asilimia 7.8 mwaka 2024 ukilinganisha na asilimia 2.3 mwaka 2020/21.

- Kati ya mwaka 2016 na 2020 ajira na kupandishwa vyeo ulisitishwa katika utumishi wa umma. Hata hivyo, kama sehemu ya falsafa ya kuifungua nchi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa awamu ya sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alifungulia ajira na kupandishwa vyeo na madaraja katika utumishi wa umma. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Serikali ya awamu ya sita imeshaajiri watumishi wa umma 32,833, ikiwemo walimu 7,000 na watumishi wa afya 5,000 waliaojiriwa kama sehemu ya kutekeleza ahadi za Mheshimiwa Rais ndani ya siku 100 baada ya kuapa kuwa Rais kufuatia uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

v) Kuendelea kupanuka kwa fursa na kuimarika kwa kiwango cha ubora wa huduma za jamii. Kwa mfano:

- Kupungua kwa vifo vya akina mama wajawazito ambapo uwiano wa vifo vya mama (Maternal Mortality Ratio) umefikia takribani vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2025 ikilinganishwa na vifo 556 mwaka 2021.

- Ujuzi wa kusoma na kuandika umeongezeka kufikia asilimia 85.1 ukilinganisha na asilimia 83.1 mwaka 2022

- Idadi ya wanafunzi wanaohitimu katika vyuo vikuu

imeongezeka kufikia 62,570 mwaka 2024 ukilinganisha na wahitimu 54,810 mwaka 2021.

- Hadi kufikia Desemba 2025, Serikali iliwekeza kwenye ujenzi wa miundombinu ya maji na usafi wa mazingira yenye uwezo wa kusambaza huduma ya maji vijijini kufikia asilimia 85.2 na mijini asilimia 92.5.

vi) Serikali ya awamu ya sita imekamilisha kwa mafanikio makubwa maandalizi ya Dira 2050 na nyenzo zake zote za utekelezaji.

**V: MALENGO NA VIPAUMBELE VYA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2026/27**

**42.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuyatekeleza malengo makuu ya Dira 2050, vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2026/27 vimeandaliwa kwa kutohoa maeneo ya vipaumbele, malengo, shabaha, afua na viashiria muhimu vya utendaji vilivyoainishwa katika Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31 wenye dhima ya "Mageuzi kwa ajili ya Ukuaji Jumuishi wa Uchumi na Uzalishaji Ajira" ambao ni wa kwanza katika utekelezaji wa Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2026/27 – 2050/51.

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27, Serikali itatekeleza maeneo ya kipaumbele matano kama yalivyoainishwa katika Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kama ifuatavyo:

i) Kuimarisha Utawala Bora, Demokrasia, Amani, na Utulivu;

ii) Kujenga Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani;

iii) Kuimarisha Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii;

iv) Kuimarisha Uhifadhi wa Mazingira na Ustahimilivu kwa Mabadiliko ya Tabianchi; na

v) Kusimamia utekelezaji wa vichocheo vya Mageuzi (ikiwemo nishati, miundombinu ya usafiri na usafirishaji, utafiti na maendeleo, na mageuzi ya kidigitali).

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza maeneo ya vipaumbele vilivyoainishwa hapo juu, Serikali imepanga kuanza kutekeleza programu na miradi mbalimbali ikiwemo miradi shikizi 38 kati ya 51 iliyopo katika programu saba (7) za kielelezo zilizoainishwa katika Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambazo ni kama ifuatavyo:

i) Mji wa Ikolojia ya Bahari Bagamoyo na Usafirishaji Fungamanishi: Programu hii ina jumla ya miradi shikizi kumi (10).

ii) Kitovu Changamani cha Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga: programu hii inajumuisha miradi shikizi saba (7).

iii) Programu ya Kitaifa ya Umwagiliaji na Mageuzi ya Viwanda vya Uchakataji wa Mazao ya Kilimo: Programu hii inajumuisha miradi shikizi nane (8).

iv) Kitovu cha Teknolojia na Uchakataji wa Madini Adimu –

v) Dodoma: Programu hii inajumuisha miradi shikizi saba (7).

vi) Kiwanda cha Kuchakata Gesi Asilia ya Kimiminika (LNG) –

vii) Lindi: Programu hii inajumuisha miradi shikizi mitatu (3).

viii) Kitovu cha Kisasa cha Viwanda na Uchumi wa Buluu katika Ukanda wa Maziwa Makuu: Programu hii inajumuisha miradi shikizi saba (7).

ix) Programu Shirikishi ya Uendelezaji wa Miji nchini: Programu hii inajumuisha miradi shikizi tisa (9).

**45.** ***Mheshimiwa Spika***, gharama za utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2026/2027 zinakadiriwa kuwa TZS trilioni 86.3 ambazo ni sawa na asilimia 18.1 ya gharama za kutekeleza Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambao unatarajiwa kutekelezwa kwa gharama ya TZS trilioni 477.747. Gharama hizo zitatokana na uwezeshaji wa wadau wakubwa watatu: serikali kuu na mamlaka za serikali za mitaa, sekta binafsi na mashirika ya umma.

**46.** ***Mheshimiwa Spika***, kati ya uwekezaji huo, sekta binafsi inatarajiwa kuchangia shilingi trilioni 60.1 (sawa na asilimia 69.6). Sekta ya umma kwa ujumla wake inatarajiwa kuchangia shilingi trilioni 26.2 (sawa na asilimia 30.4), ambapo mashirika ya umma yanatarajiwa kuchangia shilingi trilioni 5.5. Serikali itachangia shilingi trilioni 20.8, itakayotengwa kutoka katika Bajeti ya Serikali kama itakavyowasilishwa baadaye leo alasiri na Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**47.** ***Mheshimiwa Spika***, ufanisi wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2026/27 utajengwa katika misingi nane ifuatayo:

i) Kuendelea kuwepo kwa demokrasia, amani, usalama na utulivu wa ndani na katika nchi jirani, inayowezesha shughuli za kiuchumi na uwekezaji kustawi;

ii) Kudumisha misingi ya utawala bora na utawala wa sheria, ikiwa ni pamoja na uwajibikaji, uwazi na ufanisi katika matumizi ya rasilimali za umma;

iii) Kuendelezwa kwa miundombinu ya nishati, bandari, barabara na reli ikiwa ni utekelezaji wa dhima ya kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara, viwanda na usafirishaji katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati;

iv) Kuimarika kwa ubunifu na matumizi ya teknolojia za kidijitali katika huduma za kijamii na uzalishaji;

v) Kuendelea kuimarika kwa mazingira ya biashara na

uwekezaji yatakayochochea ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli za uchumi;

vi) Kuendelea kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi na majanga ya asili na yasiyo ya asili ikiwemo ukame, mafuriko, vita, milipuko ya magonjwa na misukosuko ya kiuchumi ya kimataifa kupitia mikakati ya kukabiliana na kupunguza athari zake;

vii) Kuendelea kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa; na

viii) Kuendelea kuimarika kwa upatikanaji na usalama wa chakula nchini.

## VI: HITIMISHO

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** hakuna shaka kwamba kazi kubwa imefanyika katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2020/21 – 2025/26) na katika miaka mitano ya awamu ya sita ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mafanikio yaliyopatikana na changamoto zilizijitokeza yameweka msingi imara katika kuanza utekelezaji wa Dira 2050 na mikakati yake ya utekelezaji.

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyoeleza awali, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026 ni nyenzo ya kwanza katika kuanza utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31 na Dira 2050. Aidha, Serikali imekamilisha nyenzo zote muhimu za utekelezaji wa Dira 2050. Nyenzo hizo ni Mpango Elekezi wa Muda Mrefu (*Long-Term Perspective Plan – LTPP* 2026/27 – 2050/51); Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Miaka Mitano (*Fourth Five Year Development Plan – FYDP* 2026/27 – 2030/31); Mwongozo wa Kitaifa wa Uandaaji Mipango; Mwongozo wa Kitaifa wa Uidhinishaji wa Miradi ya Maendeleo; Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo (*National Framework for Monitoring and Evaluation of Development*

*Projects*); na Mkakati wa Mawasiliano wa Dira 2050 wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31.

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia kukamilika kwa nyenzo hizo za utekelezaji wa Dira 2050, kazi iliyo mbele yetu sasa ni moja tu: KUTEKELEZA.

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo, mafanikio ya utekelezaji wa Dira 2050 na mikakati yake yatapimwa kwa kuzingatia ***viashiria vya matokeo*** (*Key Performance Indicators-KPIs*) kwa kila sekta na sio wingi wa shughuli au michakato ya utekelezaji. Katika kufikia azma hii, Sekretariati ya Tume itajielekeza na kujikita katika kusimamia utekelezaji wa mipango ya maendeleo (*Delivery Bureau*).

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapohitimisha ninapenda kurejea maelekezo ya CCM kuhusu maendeleo vijijini. Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 ilibaini kuwa wananchi wengi bado wanaishi vijijini na kwamba kasi ya maendeleo vijijini inahitaji kuongezeka na kupewa msukumo mpya. Aidha, CCM inatambua umuhimu wa kuimarisha maendeleo vijijini na kufanya vijiji vikue kiuchumi na katika huduma za jamii ili kupunguza wimbi la vijana kuhamia mijini kwa kukuza ajira. Hivyo, kuwakumbusha watekelezaji wote wa Ilani kuzingatia hatua 12 ambazo Ilani ya CCM imeelekeza kuchukuliwa katika kuongeza kasi ya maendeleo vijijini:

i) Kuendelea kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu ya barabara na madaraja vijijini ili kurahisisha usafiri na usafirishaji, na kuunganisha maeneo ya uzalishaji na masoko.

ii) Kuanza programu maalumu ya ujenzi wa nyumba bora vijijini

iii) Kuimarisha huduma ya mawasiliano ili kuongeza kasi na kupanua wigo wa matumizi ya teknolojia ya habari kwa wananchi wa vijijini ili kunufaika na fursa zitokanazo na shughuli za uzalishaji kiuchumi na kijamii. Serikali ya CCM itaweka sera za kikodi za kuvutia wawekezaji kuimarisha huduma ya mawasiliano vijijini;

iv) Kuongeza kasi ya kusogeza huduma za msingi zikiwemo maji, afya, elimu na umeme vijijini;

v) Kukuza stadi za maisha na ujuzi miongoni mwa vijana kwa kujenga na kuweka mazingira wezeshi ya ujenzi wa vyuo vya mafunzo ya amali ili kukuza ajira katika kila wilaya;

vi) Kupitia upya mifumo ya uuzaji wa mazao ya kilimo, mifugo, na misitu kwa lengo la kunufaisha wakulima, kurahisisha na kuwezesha mazingira ya kufanya biashara vijijini;

vii) Kuweka mazingira maalumu ya kuvutia ujenzi wa viwanda vidogo vidogo vijijini kwa lengo la kufanya uchakataji wa malighafi katika sekta za kimkakati zikiwamo kilimo, mifugo, uvuvi, na misitu ili kuongeza fursa za ajira na kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno;

viii) Kuimarisha usalama wa chakula kwa kuboresha uhifadhi wa mazao, kuwapatia wakulima teknolojia za kisasa za uhifadhi wa chakula, na kuanzisha na kuendeleza kilimo cha mazao yanayohimili ukame na mabadiliko ya tabianchi;

ix) Kuimarisha miundombinu ya masoko ikijumuisha vituo vya ukusanyaji na uongezaji thamani;

x) Kuweka mfumo mpya wa upatikanaji wa fedha vijijini kwa kutekeleza mpango maalumu wa kurahisisha utoaji wa huduma na kutoa mikopo yenye riba ndogo itakayowawezesha wananchi kuwekeza katika kilimo cha kisasa na shughuli za ujasiriamali;

xi) Kupanga matumizi bora ya ardhi, kupima na kumilikisha ardhi kwa wananchi ili kuwawezesha kupata mikopo na motisha ya kuwekeza zaidi katika kilimo, ufugaji, na shughuli nyingine za kiuchumi. CCM itaisimamia serikali kuhakikisha kuwa angalau 60% ya ardhi yote vijijini imepimwa ifikapo mwaka 2030; na

xii) Kuimarisha vyama vya ushirika kimuundo, kiutawala,

kiuendeshaji na kirasilimali kama vyombo muhimu vya sauti ya wakulima, wafugaji na wavuvi nchini.

**53.** ***Mheshimiwa Spika***, hotuba hii inapatikana katika Tovuti ya Ofisi ambayo ni www.popi.go.tz na www.planning.go.tz

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo, sasa naomba Bunge likubali kupokea, kujadili na kuridhia taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27.

**55.** ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba kutoa hoja.

Prof. Kitila Alexander Mkumbo **(Mb.),**
**WAZIRI WA NCHI**
**OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI**

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja hiyo imeungwa mkono. Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa hotuba. Hotuba zinazotekelezeka ni zile fupi, lakini ziko *clear*. Kuja hapa na hotuba *page* 800 halafu hakuna kilichofanyika...

Hongera sana Mheshimiwa Waziri wa Mipango kwa kazi nzuri unayoifanya. *(Makofi)*

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni waliokaa Jukwaa la Spika; wageni wa Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; Ndugu Monica Hangi - *Country Director Gatsby Africa*, karibu. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Profesa Mkumbo Menejimenti kutoka Tume ya Taifa ya Mipango, Wadau wa Maendeleo, Wajumbe wa Kamati ya Siasa Wilaya ya Ubungo, Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri ya Ubungo, Wenyeviti wa CCM Kata ya Jimbo la Ubungo, na majirani wa Mheshimiwa Waziri katika Jimbo la Ubungo, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Profesa Riziki Silas Shemdoe, Ndugu Abubakar Kunenge, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; mgeni wa Mheshimiwa Silvery Luboja Salvatory ambaye ni mwalimu na mpiga kura wake kutoka Wilaya ya Misungwi, Mwanza, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, leo ndiyo siku ya Bajeti, ninawaomba sana, saa tisa na nusu kila mtu awe amekwishakukaa kwenye kiti chake. Bajeti leo itaanza saa 10.00 jioni.

Ninasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni ya leo.

*(Saa 5.11 Asubuhi Bunge Lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

**SPIKA:** Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

*(Hapa Waziri wa Fedha aliingia Ukumbini akiambatana na Wapambe wa Bunge)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2026/2027. Uwasilishaji wa bajeti hii umezingatia Ibara ya 137 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ikisomwa pamoja na kifungu cha 23 (3) cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 na Kanuni ya 127 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Agosti, 2025.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii, ninawasilisha vitabu vinne vinavyoelezea kwa kina takwimu za Bajeti ya Serikali. kitabu cha kwanza kinahusu makadirio ya mapato yatakayowezesha utekelezaji wa shughuli za Kiserikali; kitabu cha pili kinahusu makadirio ya matumizi ya kawaida kwa Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali; kitabu cha tatu ni makadirio ya matumizi ya kawaida, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na kitabu cha nne kinahusu makadirio ya matumizi ya maendeleo kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Kiserikali, Ofisi za Wakuu wa Mikoa pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hotuba hii inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawasilisha pia Muswada wa Sheria za Fedha ya mwaka 2026; Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2026, Taarifa ya Bajeti yenye mrengo wa kijinsia na mkakati wa usimamizi wa vihatarishi vinavyoweza kuathiri utekelezaji wa bajeti itakayodhahirishwa na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninatanguliza shukrani kwa Mola wetu Mwenyezi, Rahimu na Karimu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki vyema Mkutano wa Tatu wa Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sichoki kuwapongeza viongozi wetu wakuu kwa mafanikio makubwa wanayoendelea kuleta kwenye nchi yetu. Ninaungana na Mawaziri wenzangu kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi kwa kuchaguliwa tena kwa kishindo

katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake mahiri na wa moyo wa kizalendo katika kuwatumikia wananchi. Sote tumeendelea kushuhudia matokeo ya kazi kubwa anayoifanya ya kuleta maendeleo ya nchi yetu kupitia kauli mbiu ya Kazi na Utu, Tunasonga Mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi wote kumuomba Mwenyezi Mungu aendelee kumjalia afya njema, hekima, maarifa na kumpa ulinzi zaidi Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza pia Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa weledi wake katika kuendelea kumsaidia na kumshauri Mheshimiwa Rais kuongoza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine tena kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Hii ni uthibitisho kwa kukubalika kwa uongozi wake mahiri na dhamira ya dhati ili kuendelea kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, kwanza kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Iramba Magharibi, pili, kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na hatimaye kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninampongeza pia kwa kuendelea kuratibu na kusimamia shughuli za Serikali kwa weledi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee na kwa mara nyingine tena, ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu

Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Mbunge na kunipa dhamana adhimu ya kumsaidia kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi katika nafasi ya Waziri wa Fedha. Hii ni imani na dhima kubwa kwangu. Njia pekee ya kuonesha kuwa ninaithamini ni kuitumikia kwa weledi, uaminifu na kwa maslahi ya Taifa letu. Ninachukua ahadi mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa nitafanya hivyo kwa muda wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa moyo wa simanzi na huzuni kubwa ninatoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwako binafsi, Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watanzania wote kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Watu Wenye Ulemavu na Mbunge wa Jimbo la Isimani; Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho na Mheshimiwa Halima Idd Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum. Tutaendelea kuwakumbuka kwa michango yao na utumishi uliotukuka ndani ya Bunge lako Tukufu na nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ninatoa pole kwa waumini wa Kanisa Katoliki pamoja na ndugu, jamaa na marafiki kwa kuondokewa na kiongozi wao mpendwa, Askofu Mkuu Mstaafu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo. Marehemu Kardinali Pengo atakumbukwa milele kwa mchango wake mkubwa alioutoa kwa Taifa, hususan katika uwakilishi wake wa kiroho kwa Kanisa Katoliki, ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, wapo Watanzania wenzetu waliofikwa na majanga mbalimbali yaliyosababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali na miundombinu kutokana na ajali za barabarani, maradhi na athari za mabadiliko ya tabianchi. Ninawaombea marehemu wote pumziko la amani na uponaji wa haraka kwa majeruhi wote ili waweze kurejea katika shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, aidha, ninatoa pole kwa Watanzania wote waliopoteza ndugu, jamaa, marafiki na mali zao kutokana

na majanga hayo. Tukiwa waja wa Mwenyezi Mungu tunapaswa kukumbuka kuwa sisi sote ni waja wake na kwake tutarejea, tujiandae kwa safari hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya ya utangulizi, ninaomba hotuba yangu yote iingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa hali ya uchumi; hali ya uchumi wa nchi yetu imeendelea kuimarika na kuwa himilivu pamoja na changamoto mbalimbali zinazoendelea kujitokeza duniani. Kwa kuwa Bunge lako Tukufu limepokea Hotuba ya Hali ya Uchumi asubuhi ya leo, ninaomba kwa kuwa kumbukumbu za kikao hiki uupokee Muhtasari wa Hali ya Uchumi kama ilivyowasilishwa katika aya ya 12 hadi ya 14 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utekelezaji wa bajeti ya Serikali, Bunge lako Tukufu liliidhinishia Serikali Bajeti ya jumla ya shilingi trilioni 56.49 kwa mwaka 2025/2026. Kati ya kiasi hicho, mapato ni shilingi trilioni 41.39, ikijumuisha misaada ya shilingi bilioni 925.1, pamoja na mikopo ya ndani na nje ya shilingi trilioni 15.1.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine matumizi yalijumuisha mishahara na stahiki za watumishi kwa shilingi trilioni 7.71; ununuzi wa bidhaa na huduma - shilingi trilioni 7.81; malipo ya riba za mikopo na mitaji - shilingi trilioni 14.21; ruzuku, michango, mafao, misaada ya kijamii na gharama nyingine - shilingi trilioni 23.98; pamoja na uwekezaji wa mali zisizo za kifedha - shilingi trilioni 2.78.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapato, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026 Serikali ilifanikiwa kukusanya mapato ya jumla ya shilingi trilioni 34.75 sawa na 101.8% ya lengo la kipindi hicho…

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, dakika moja.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Rais ameshajiunga moja kwa moja akiwa kama na yeye ni sehemu ya Bunge. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kati ya kiasi hicho, mapato ya kodi yalifikia shilingi trilioni 28.1 sawa na 105.1% ya lengo; mapato mengine yasiyo ya kodi na mapato yanayokusanywa na halmashauri shilingi trilioni 5.92 sawa na 89.5% ya lengo na misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo shilingi bilioni 740.5 sawa na 96.1% ya lengo.

Mheshimiwa Spika, ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya kodi umetokana na kuongezeka kwa wigo wa vyanzo vya mapato ya kodi kutokana na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi na kuongezeka kwa kiwango cha uwiano wa kulipa kodi kufuatia hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali ikiwemo kuimarisha kwa mifumo ya ukusanyaji wa mapato, utoaji wa elimu ya kodi kwa umma na mijadala ya pamoja kati ya Serikali na walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, ninatumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Watanzania wazalendo wanaotimiza wajibu wao wa kulipa kodi kwa hiari. Mwitikio huo mzuri umeendelea kuimarisha uwezo wa ndani wa Serikali kugharimia huduma muhimu za kijamii na kiuchumi nchini kwa zaidi ya 70%.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi, katika kipindi hicho cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026 jumla ya matumizi ya Serikali bila kujumuisha malipo ya mtaji wa deni yalikuwa shilingi trilioni 40.92 sawa na 98.8% ya lengo la kipindi hicho. Kiasi hicho kinajumuisha mishahara na stahiki za watumishi - shilingi trilioni 7.02; malipo ya riba - shilingi trilioni 5.09 na ununuzi wa bidhaa na huduma - shilingi trilioni 7.02. Matumizi mengine ni ruzuku, michango, mafao, misaada ya kijamii na gharama nyingine shilingi trilioni 19.741 na uwekezaji katika mali zisizo za kifedha shilingi trilioni 2.38.

Mheshimiwa Spika, hadi Aprili, 2026 Serikali ilikopa jumla ya shilingi trilioni 11.29 katika soko la ndani na nje sawa na 89.5% ya lengo. Kati ya kiasi hicho, mikopo ya ndani ilikuwa shilingi trilioni

5.08 ambapo shilingi trilioni 2.55 zilitumika kulipa hati fungani zilizoiva na shilingi trilioni 2.53 zilitumika kugharimia miradi ya maendeleo. Aidha, mikopo ya nje ilikuwa ni jumla ya shilingi trilioni 6.2 ambapo kati ya kiasi hicho mikopo nafuu ilikuwa shilingi trilioni 4.61 na mikopo yenye masharti kibiashara shilingi trilioni 1.59.

Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2026 Deni la Serikali lilifikia shilingi trilioni 114.34. Katika kiasi hicho deni la ndani lilikuwa shilingi trilioni 38.45 sawa na 33.6% na deni la nje lilikuwa shilingi trilioni 75.89 sawa na 66.4%. Deni hilo limetokana na mikopo iliyoelekezwa katika maeneo ya kimkakati yanayochochea ukuaji wa uchumi, ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji, nishati na mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya uhimilivu wa deni uliofanywa Novemba, 2025 imeonesha kuwa deni ni himilivu katika kipindi cha muda wa kati na muda mrefu. Thamani ya sasa ya deni la Serikali kwa Pato la Taifa ni 39.6% likilinganishwa na ukomo 55%. Deni la nje kwa Pato la Taifa ni 24.4% dhidi ya ukomo 40% na deni la nje kwa mauzo ya nje ni 123.1% dhidi ya ukomo 180%. Hali hii inaonesha kuwa nchi yetu ina uwezo mzuri wa kusimamia na kuhimili deni lake bila kuathiri uthabiti wa misingi ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na mafanikio hayo, kampuni kubwa za kimataifa za *Moody's* na *Fitch Ratings* zilifanya tathmini ya awamu ya kwanza ya uwezo wa nchi kukopa na kulipa madeni kwa mwaka 2026. Matokeo ya tathmini yalionesha kuwa Tanzania inakopesheka na ina uwezo mzuri wa kulipa madeni yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matokeo hayo yanatokana na ukuaji mzuri wa uchumi, utekelezaji wa mageuzi ya kimuundo yanayoboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, pamoja na nidhamu ya matumizi ya fedha za umma na ongezeko la mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masuala mtambuka; ninaomba Bunge lako Tukufu lipokee na kuzingatia masuala mtambuka

yanayobainishwa katika hotuba yangu ikiwa ni pamoja na athari za migogoro ya kimataifa, mabadiliko ya tabianchi na jinsia na ustawi wa jamii kama yalivyobainishwa kupitia aya ya 26 hadi ya 37 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Amri ya Rais, Uendelezaji wa Makao Makuu Dodoma; kupitia Amri ya Rais *(Presidential Decree)* Na. 320 ya mwaka 1973, Dodoma ilitangazwa kuwa Makao Makuu ya Taifa la Tanzania wakati wa Awamu ya Kwanza ya Serikali chini ya uongozi wa Baba wa Taifa, Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Aidha, mwezi Februari, 2026 tumetimiza miaka 30 toka Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhamia Dodoma na hivyo kuwa mhimili wa kwanza kuhamia rasmi makao makuu. Ninaomba nitumie fursa hii kulipongeza Bunge kupitia kwako Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mhimili wa Serikali ulihamia rasmi Dodoma mwaka 2017 wakati wa Serikali ya Awamu ya Tano iliyoongozwa na Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na kupitia kauli mbiu ya Kazi iendelee Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendeleza kwa kasi zaidi ujenzi wa Dodoma kama Makao Makuu ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa mihimili yote ya dola imeshahamia Dodoma ambapo mhimili wa Mahakama ukiwa na jengo la kisasa na la mfano Barani Afrika wakati Mji wa Serikali Mtumba ukiendelea kujengeka kwa hadhi ya kipekee. Vilevile, Ikulu ya Chamwino nayo imekamilika na kuendelea kutekeleza kazi zake za kuwa kituo kikuu cha uongozi wa Taifa letu. Hakika hii sasa ni Dodoma, Mji Mkuu unaoibukia vyema na siyo tena mji uliozama *(Idodomya)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wetu Serikali, sekta binafsi na hata Ofisi za Balozi na Mashirika ya Kimataifa kuendelea kuijenga Dodoma kuwa Mji Mkuu wa kisasa kwa karne ya 21 kwa Taifa linalojiamini na lenye matumaini makubwa. Badala ya kuwa makao makuu ya utawala wa nchi, Dodoma itaendelezwa kuwa alama muhimu ya nchi ya maendeleo ya kiuchumi, kitovu cha usafiri na usafirishaji kwa Tanzania na nchi jirani na mfano wa

maendeleo wa mikoa na majiji mengine nchini. Reli ya *SGR* na Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato vinatoa fursa muhimu ya kuharakisha kufikiwa ndoto hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka 2026/2027; bajeti ya mwaka 2026/2027 ni ya kwanza katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2050. Bajeti hii imeandaliwa kwa kuzingatia miongozo ya kitaifa, kikanda na kimataifa ikiwemo Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano; Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2025; Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2050; Ajenda ya Maendeleo ya Afrika ya mwaka 2063; Malengo ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030; pamoja na nyaraka, miongozo na makubaliano mengine ya kikanda na kimataifa ambayo Tanzania imeridhia.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii pia imezingatia hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa tarehe 14 Novemba, 2025 wakati wa kuzindua rasmi Bunge la Kumi na Tatu. Aidha, bajeti hii pia imezingatia maelekezo mahususi yaliyotolewa kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Madelu Nchemba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine, bajeti hii inawasilisha mapendekezo ya hatua mpya za kisera za mapato na matumizi kwa mwaka 2026/2027. Hatua hizo zinalenga kuchochea ukuaji wa uchumi, yaani kuwa na uchumi yaani kuwa na hatua ambazo ni *progress*, kuvutia uwekezaji, kulinda na kuimarisha sekta ya viwanda nchini *(pro-investment industrialization)*, kuongeza ukusanyaji wa mapato ili kujitegemea katika ugharamiaji wa sehemu kubwa wa bajeti ya Serikali, *fiscal sovereignty* na kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali na Umma kwa ujumla *(fiscal discipline)*.

Mheshimiwa Spika, viima na vipaumbele vya bajeti kwa mwaka 2026/2027; bajeti ya mwaka huu wa 2026/2027 ina dhima ya kujenga uchumi himilivu kupitia mageuzi ya kidijitali, uwekezaji wa kimkakati, na sera endelevu za kibajeti kwa ukuaji jumuishi wa

uchumi. Dhima hii imeandaliwa kwa kuzingatia maeneo matano ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/2027. Maeneo hayo ni pamoja na utawala, amani, usalama na utulivu.

Mheshimiwa Spika, pili, uchumi imara, jumuishi na shindani; tatu, uwezo wa watu na maendeleo ya kijamii; nne, uhifadhi wa mazingira na ustahamilivu wa mabadiliko ya tabianchi; na tano sekta ya vichecheo vya kimageuzi.

Mheshimiwa Spika, shabaha na misingi ya uchumi wa jumla; ninaomba Bunge lako Tukufu lipokee na kuzingatia taarifa ya shabaha na misingi ya uchumi jumla kama nilivyoiwasilisha kupitia aya 47 – 49 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa kuongeza mapato; takwimu za miaka ya karibuni zinaonesha kuwa, misaada kutoka nje imeendelea kupungua mwaka hadi mwaka na hivyo haiwezi kuwa chanzo cha kuaminika cha mapato katika utekelezaji wa bajeti yetu. Aidha, utekelezaji wa miradi kwa fedha za mikopo nao umeendelea kuleta changamoto kwa kuzingatia uhimilivu wa deni, gharama za mikopo na athari yake kwa uhuru wa Taifa letu. Hali hii inasababisha uhitaji wa kuongeza kasi yetu kwenye kujitegemea kiuchumi na mapato. Serikali itachukua hatua zaidi za kuimarisha ukusanaji wa mapato ya ndani kwa kuziba mianya upotevu na kuimarisha taasisi taasisi za ukusanyaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2026/2027, Serikali kupitia utekelezaji wa mkakati wa ukusanyaji wa mapato wa muda wa kati 2025/2026 – 2027/2028, itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha ukusaji wa mapato na miongoni mwake zikiwemo hizi zifuatazo: -

(i) Kuvutia uwekezaji zaidi wa ndani na nje kwa azma ya kutanua wigo wa kodi na kuongeza fursa za ajira;

(ii) Kuhamasisha ulipaji kodi kwa hiari kwa kuimarisha mahusiano baina ya sekta na baina ya Serikali na walipakodi kupitia majadiliano kwenye majukwaa

mbalimbali, ikiwemo Baraza la Taifa la Biashara na *CEOs Round Table*;

(iii) Kuendelea kusimamia na kuhimiza matumizi sahihi ya mashine za kutolea risiti za kielektroniki kupitia utoaji wa elimu na uendeshaji wa programu mbalimbali za hamasa;

(iv) Kuendelea kujenga na kuboresha mifumo ya TEHAMA ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya ndani, kutumia teknolojia ya kisasa ya akili unde, na matumizi ya taarifa *(big data)* na kuhakikisha mifumo yote inabadilishana taarifa;

(v) Kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa taasisi za umma ili kuhakikisha zinaongeza tija katika ukusanyaji wa maduhuli, pamoja na kuhakikisha zinawasilisha gawio na michango stahiki na kwa wakati katika Mfuko Mkuu wa Serikali;

(vi) Kuhakikisha bidhaa zote zinazozalishwa nchini, zinazoagizwa na kuuzwa ndani na nje ya nchi zinakuwa na msimbo pau *(barcode)*;

(vii) Kuendelea kufanya uchambuzi wa kina na kuanza utekelezaji wa baadhi ya mapendekezo 284 yaliyotolewa na Tume ya Rais ya Maboresho ya Mfumo wa Kodi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na mikakati hiyo, Serikali inakusudia kuanzisha programu ya tuzo ya uzalendo kupitia mfumo wa usimamizi wa risiti za kielektroniki inayotarajiwa kuzinduliwa rasmi Julai mwaka huu wa 2026. Lengo ni kuhamasisha tabia ya wananchi kudai risiti stahiki pindi wanapofanya ununuzi na wafanyabiashara kutoa risiti kwa hiari pale wanapofanya mauzo. Tuzo au zawadi hizo zitatolewa kwa mtindo wa bahati nasibu, ambapo zawadi mbalimbali zitatolewa kuchezesha *draw* ili kuwapata washindi waliotoa na waliodai risiti kwa kipindi husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba Bunge lako Tukufu lipokee na kuzingatia taarifa ya mikakati ya Serikali katika kuboresha na kuimarisha mazingira ya uwekezaji na biashara, urasimishaji wa sekta isiyo rasmi, huduma jumuishi za fedha, kupunguza matumizi ya fedha taslimu, na usimamizi wa matumizi ya fedha za umma kama ilivyoainishwa kupitia aya ya 53 – 69 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, maboresho ya mfumo wa kodi, ada, tozo na hatua nyingine za mapato; awali nilieleza haja ya kuwa na bajeti inayochochea mageuzi ya kiuchumi hasa ujenzi wa viwanda na kuwa na Taifa linalojitegemea.

Mheshimiwa Spika, sasa ninapenda kuwasilisha mapendekezo ya hatua mpya za kodi kwa mwaka 2026/2027, nikitarajia kuwa zitajibu maswali na kukidhi kiu ya wananchi, wafanyabiashara, wawekezaji kwa kuweka sera zitakazochea uwekezaji, uzalishaji, kulinda viwanda na kuchangia katika kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ikiyafanyia kazi kwa kina maoni yaliyotolewa na Tume ya Rais ya Maboresho ya Mfumo wa Kodi, mapendekezo ya kurekebisha mfumo wa kodi kwa mwaka 2026 yamezingatia baadhi ya maoni hayo. Maeneo yaliyopendekezwa kufanyiwa maboresho ni pamoja na haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kundi la kwanza, kustawisha sekta za uzalishaji katika mnyororo wa thamani wa mafuta ya kula, pamba, na nguo na mavazi. Mafuta ya kula ni bidhaa muhimu inayotumiwa kwa wingi nchini Tanzania na inatoa fursa kubwa ya kukuza uwekezaji, ajira, na mapato kupitia mnyororo wake wa thamani. Serikali imeweka vivutio mbalimbali vya kikodi ili kuhamasisha kilimo na matumizi ya mbegu za mafuta zinazozalishwa nchini, kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa hii kwa wananchi kwa gharama nafuu, pamoja na kuendeleza na kulinda viwanda vya ndani vinavyochakata na kuzalisha mafuta ya kula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua za kikodi zinazoendelea kutekelezwa kwa sasa ni pamoja na zifuatazo: -

(i) Msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye mafuta ya kula yaliyozalishwa kwa kutumia mbegu zinazozalishwa ndani ya nchi;

(ii) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha 10% kwenye mafuta ghafi ya kula yanayoingizwa nchini isipokuwa ya mchikichi;

(iii) Ushuhuru wa mauzo ya kusafirisha nje ya nchi *(export levy)* ya 10% kwenye mafuta ghafi ya alizeti na mbegu zake;

(iv) Ushuru wa Forodha wa asilimia sifuri kwenye mafuta ghafi ya kula ya mchikichi na 10% kwenye mafuta ya mchikichi yaliyochakatwa kwa kiwango cha kati; na

(v) Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha 35% au Dola za Marekani 300 kwa tani moja, kutegemea kiwango kilicho kikubwa badala ya kiwango cha 35% pekee kwenye mafuta ya kula ya aina zote yaliyochakatwa kwa kiwango cha mwisho *(refined edible oil)*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya mashauriano na wadau mbalimbali ikiwemo wazalishaji wa mafuta ya kula na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, inapendekezwa kufanya marekebisho yafuatayo: -

(i) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha 10% kwenye mafuta ghafi ya kula ya aina zote, ikiwemo ya mchikichi na mafuta yaliyochakatwa kwa kiwango kidogo *(semi refined palm oil)*. Hatua hii ina lengo la kuondoa changamoto ya udanganyifu wa uendeshaji wa bidhaa *(misdeclaration* na *misclassification)* unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara wasiowaaminifu ambao hutumia nafuu iliyopo kwenye mafuta ya mchikichi kuagiza yaliyochakatwa.

Matumizi ya kiwango hiki yanaendana na mwelekeo wa sera unaotumika na baadhi ya nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa sasa, ikiwemo Kenya na Uganda ambazo tayari zinatoza Ushuru wa Forodha wa kiwango cha 10% kwenye mafuta ya ghafi ya mchikichi kutoka nje ya jumuiya.

(ii) Kuendelea kutoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mafuta ya kula yaliyozalishwa kwa kutumia mbegu zinazozalishwa ndani ya nchi;

(iii) Kuendelea kutoza ushuru wa 35% kwa kiwango cha 35% au Dola za Marekani 300 kwa tani moja kwa mafuta safi, kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa. Aidha, Serikali imeandaa kanuni za uagizaji wa mafuta ya kula kwa lengo la kudhibiti uingizaji wa mafuta ya kula nchini ili kuhamasisha na kukuza tasnia ya mafuta ya kula yanayozalishwa na kutumika kutumia mbegu za ndani ya nchi; *(Makofi)*

(iv) Serikali kupitia Wizara ya Kilimo itaratibu utoaji wa vibali maalumu kwa waagizaji wa mafuta hayo kutoka nje ya nchi. Vibali hivyo vitatolewa baada ya kujiridhisha juu ya uwekezaji na uzalishaji wa mbegu za alizeti, pamba na michikichi chini ya Kanuni za *COPRA* za Mwaka 2026. Aidha, kwa kipindi cha miaka mitano ijayo Serikali itaendelea kutoa ruzuku ya mbegu ya alizeti na pamba, pamoja na miche milioni mbili kila mwaka kwa lengo la kukuza uzalishaji wa mbegu zinazotumika kuzalisha mafuta ya kula, na hivyo kuondoa kabisa uingizaji wa mafuta hayo kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mnyororo wa pamba nguo na vitambaa, sekta ya nguo na mavazi ni moja ya sekta inayohusisha mnyororo mrefu wa uongezaji wa thamani kwenye zao la pamba, yaani *ginning* (kusokota nyuzi) *spinning* (kusokota vitambaa), kufuma vitambaa, kuchapa na kuweka rangi, pamoja na kushona mavazi.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa sekta hii katika uchumi wa Tanzania, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa kuhamasisha matumizi ya pamba inayozalishwa ndani ya nchi katika uzalishaji wa nyuzi, vitambaa, nguo na mavazi, ikiwemo vivutio mbalimbali vya kikodi kwa wazalishaji wa nyuzi, vitambaa, nguo na mavazi nchini. Vivutio vya kikodi vinavyotekelezwa kwa sasa hivi ni pamoja na;

(i) Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha asilimia sifuri kwenye nguo na mavazi yanayozalishwa kwa kutumia pamba ya ndani ya nchi;

(ii) Unafuu wa ushuhuru wa forodha kwenye malighafi, mashine, na vipuri vinavyotumika katika uzalishaji wa vitambaa na nguo nchini;

(iii) Msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye uingizaji wa mashine zinazotumika kwenye viwanda vya uzalishaji wa mavazi;

(iv) Ushuru wa Forodha wa 25% kwenye nyuzi na pamba zinotoka nje ya jumuiya; na

(v) Uwepo wa kiwango maalumu cha Ushuru wa Forodha Dola za Marekani 0.25 kwa meta ya kitambaa kutegemea kiwango kilichokuwa kikubwa, ikilinganishwa na 25% ili kudhibiti udanganyifu na kulinda viwanda vya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa mchango wa tasnia ya pamba, nguo na mavazi katika uchumi, inapendekezwa kuendelea kulinda viwanda vya ndani vinavyozalisha vitambaa kwa kuchukua hatua zaidi zifuatazo:-

(i) Kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka 25% – 35% au Dola za Marekani 0.3 kwa meta ya kitambaa kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa; na

(ii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye nguo na mavazi yanayozalishwa kwa kutumia pamba inayozalishwa ndani ya nchi, kwa lengo la kuhamasisha matumizi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye matumizi ya nishati safi na mbadala katika vyombo vya moto na majumbani. Serikali imeendelea kuweka hatua mbalimbali za kodi zinazochochea matumizi ya nishati ya umeme na gesi asilia katika sekta ya usafiri na majumbani. Hatua zilizotekelezwa kwa sasa ni pamoja na hizi zifuatazo: -

(i) Msamaha wa ushuru wa bidhaa kwa kuzingatia uwezo wa injini kwenye magari yanayotumia umeme na gesi;

(ii) Msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye gesi asilia iliyoshindiliwa *(CNG)* inayotumika kwenye magari;

(iii) Msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vifaa vya usambazaji wa *CNG*, ikiwemo *CNG compressors, metering equipment, storage cascades*, na vifaa vingine vya magari pamoja na *dispensers;*

(iv) Msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye myororo mzima wa uzalishaji wa thamani;

(v) Msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vifaa vinavyotumika katika ubadilishaji wa mfumo wa matumizi ya mafuta ya petroli, kwa mfumo wa matumizi ya gesi na umeme kwenye magari;

(vi) Msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye uingizaji wa maligafi zilizotumika kutegemea kutengeneza mitungi ya gesi, kwa matumizi mbalimbali ikiwemo yanayotumika kwenye magari;

(vii) Kuweka unafuu wa Ushuru wa Forodha kwenye betri za umeme zinazotumiwa na wazalishaji au waunganisha wa magari na pikipiki za umeme; na

(viii) Unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa waunganisha na wazalishaji wa vyombo vya moto nchini, ikiwemo vinavyotumia umeme na gesi kwa kuzingatia kanuni za uunganishaji na uzalishaji wa bidhaa za Jumuiya ya Afrika Mashariki za mwaka 2025 ili kupunguza gharama za uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuchochea matumizi ya nishati ya umeme na gesi ya asilia, Serikali inapendekeza hatua zifuatazo kwa mwaka 2026/2027:-

(i) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vifaa vitakavyotumika katika vituo vya kuchaji magari yanayotumia umeme vinavyoingizwa nchini, vinavyotambulika kwa *HS Code 850400*;

(ii) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka 25% hadi 10% kwenye magari yanayotumia nishati ya umeme, yanayotambulika kwa *HS Codes* ambazo zimeoneshwa katika hotuba yangu. Aidha, Serikali inaendelea kufanya majadiliano na viwanda vya kuunganisha magari vilivyopo nchini ili kutoa unafuu wa kodi kwa waunganishaji wa magari ya umeme hapa nchini; *(Makofi)*

(iii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mita janja za gesi ya mitungi ya kupikia *(LPG smart meters)* zinazoingizwa nchini, zinazotambulika kwa *HS Code 9028.10.00*. Msamaha husika utatolewa kwa wasambazaji wa gesi ya kupikia pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu urasimishaji wa sekta isiyo rasmi. Mwaka 2026/2027 Serikali inaendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia urasimishaji wa sekta isiyo rasmi, ambayo inaajiri zaidi

vijana na wanawake. Katika kufanikisha azma hiyo, Serikali itatekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Kutoa msamaha wa Kodi ya Mapato kwa wafanyabiashara wapya kwa kipindi cha mwaka mmoja, tangu tarehe ya kupata namba ya utambulisho ya mlipakodi; na

(ii) Kufanya maboresho kwenye Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290 ili kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga 15% ya mapato yao ya ndani badala ya 10% iliyopo sasa ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Kati ya 15% itakayotengwa, 10% itaendelea kuelekezwa kwenye mikopo ya wanawake, vijana, na wenye ulemavu kwa uwiano kama ilivyokuwa awali, na asilimia tano ya ziada itatumika kwa ajili ya uwekezaji kwenye miradi ya ujenzi na maboresho ya masoko na maeneo ya biashara na ujasiriamali, ili kuvutia na kuongeza fursa za ajira hususan kwa vijana, wanawake, na makundi maalumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la *(d)* eneo la nne, kupunguza matumizi ya fedha taslimu ili kupunguza matumizi ya fedha taslimu katika mwaka 2026/2027 inapendekezwa kufanya maboresho yafuatayo:-

(i) Kuweka sharti la baadhi ya malipo ya huduma na biashara kufanyika kwa njia za kidijitali kama ilivyoainishwa katika aya ya 61 ya hotuba yangu;

(ii) Kusitisha usambazaji wa matumizi ya vocha za kukwangua za muda wa maongezi katika maeneo yote ya mijini yenye miundombinu wezeshi ya malipo ya kidijitali;

(iii) Kuweka sharti la matumizi ya vifaa vya malipo ya kidijitali (lipa namba na *TAN-QR*) kama moja ya kigezo wakati wa utoaji na uhuishaji wa leseni za biashara;

(iv) Kuweka sharti la kufungua akaunti ya benki kama moja ya kigezo kwa utoaji wa leseni kwa wafanyabiashara wanaoshiriki katika shughuli za madini, mifugo, mazao, mbao, na uvuvi na kuhakikisha miamala inafanyika kupitia akaunti husika; na

(v) Kuweka shati la uthibitisho wa malipo ya kidijitali kuwa rejea ya lazima itakayotumika kuidhinisha maombi ya uhamishaji wa mali kama vile ardhi, majengo, na magari, kama ambavyo imeelezwa katika aya ya 64 ya hotuba yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kundi la tano linahusu mapendekezo ya kiutawala ambayo yametolewa na Tume ya Rais ya Maboresho ya Kodi. Pamoja na mapendekezo ya maboresho ya sheria mbalimbali zikiwemo kodi yaliyotolewa na Tume ya Rais ya Maboresho ya Mfumo wa Kodi, Serikali pia imezingatia mapendekezo ya kiutawala yaliyotolewa na Tume hiyo. Katika mwaka 2026/2027, Serikali itatekeleza baadhi ya mapendekezo hayo kama ifuatavyo: -

(i) Mamlaka ya Mapato ya Tanzania kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA, akiliunde, *data* kubwa *(big data)*, na teknolojia ya *blockchain* ili kupunguza gharama za kiutawala, kuongeza ufanisi, kuhakikisha usalama na uwazi wa takwimu, na kuboresha huduma kwa walipa kodi kupitia teknolojia za kisasa. Aidha, hatua hii itapunguza ulazima wa mlipakodi kuonana uso kwa uso na watumishi wa *TRA*. *(Makofi)*

(ii) Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara wataweka utaratibu mahususi wa taasisi za udhibiti kufanya kaguzi za pamoja katika maeneo ya uwekezaji, biashara, na shughuli zote zinazosimamiwa na mamlaka za udhibiti ambao hautasababisha usumbufu wa wafanyabiashara na wawekezaji bila ya kuathiri majukumu ya msingi ya taasisi hizo; *(Makofi)*

(iii) Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, itatoa mwongozo wa utozaji tozo mbalimbali za Mamlaka za Serikali za Mitaa utakaotumika na mamlaka husika katika kuandaa sheria ndogo ndogo za utozaji wa tozo hizo. Aidha, mwongozo huo utaweka masharti muhimu ikiwemo ukomo wa kiwango cha tozo husika;

(iv) Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato *(TRA)* zitakamilisha ufungamanishaji wa mifumo, ikiwemo Mfumo wa Tausi na Mfumo wa Kodi za Ndani *(IDRAS)* ili ibadilishane taarifa moja kwa moja zikiwemo taarifa za leseni za biashara na cheti cha uthibitisho wa ulipaji kodi. Aidha, Serikali itaondoa sharti la mfanyabiashara kupakia cheti cha uthibitisho cha mlipa kodi kwenye Mfumo wa Tausi wakati wa kufanya maombi ya leseni za biashara, bali kitavutwa moja kwa moja kutoka kwenye mfumo wa *TRA; (Makofi)*

(v) Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kwa kushirikiana na *TRA* watakamilisha ujenzi wa moduli mahususi kwenye Mfumo wa Tausi kwa ajili ya usajili, utambuzi, na malipo ya kodi ili kuwezesha ukusanyaji wa kodi na tozo kulingana na matumizi ya jengo husika. Kanzidata hii itazingatia masuala yafuatayo: -

(a) Taarifa kamili za jengo ikiwa ni pamoja na hadhi ya usajili wa kiwanja, namba ya kiwanja, idadi ya nyumba, vyumba katika kiwanja na jengo husika, thamani ya jengo na matumizi ya jengo hilo, kama ni biashara au matumizi ya makazi na binafsi;

(b) Taarifa za mmiliki wa jengo ikiwa ni pamoja na namba ya *NIDA*, namba ya simu, baruapepe na taarifa nyingine kama ya mlipa kodi.

(c) Kanzidata itasomana moja kwa moja na mifumo mingine ya Serikali, ikiwa ni pamoja na *IDRAS* kwa *TRA* na mifumo ya Wizara ya Ardhi; na

(d) Kufanya mapitio ya taratibu na viwango vya na tozo ili kurahisisha urasimishaji wa umiliki wa ardhi.

(vi) Kuongeza idadi ya ofisi za *TRA* kwenye wilaya au vituo vya huduma kwa walipa kodi, pamoja na vituo vinavyotembea kwenye maeneo yenye shughuli nyingi za kiuchumi ili kusogeza huduma karibu na walipa kodi;

(vii) Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, itaongeza moduli maalumu katika Mfumo wa Tausi, itakayoruhusu watendaji wa mitaa na vijiji kusajili wafanyabiashara wote katika maeneo yao hata ambao hawana leseni za biashara; na *(Makofi)*

(viii) *TRA* itatengeneza programu tumizi *(application)* itakayotumika kwenye simu za mikononi vishikwambi au kompyuta, na kisha kutoa *app* hiyo bure kwa wafanyabiashara ili itumike kutoa risiti kama zile zinazotolewa na Mashine za *EFD*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapendekezo kwenye sheria mbalimbali za kodi ili kutambua vipengele vya msamaha wa kodi vilivyopo kwenye mikataba ya msingi *(framework agreements)*. Inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani; Sheria ya Kodi ya Mapato; Sheria ya Ushuru wa Bidhaa; na Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta ili kutambua vipengele vya msamaha wa kodi vilivyopo kwenye mikataba ya msingi *(framework agreements)* iliyosainiwa baina ya Serikali na wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii ni kutekeleza matakwa ya mikataba husika, kutimiza jukumu la Serikali la kusamehe kodi kwenye utekelezaji wa miradi hiyo na kuhakikisha miradi ya ubia inatekelezwa kwa wakati. Aidha, hatua hii itaenda sambamba na Serikali kuweka taratibu za usimamizi zitakazotoa mwongozo kuhusu utolewaji wa misamaha hiyo.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya kurekebisha mfumo wa kodi kwa mwaka 2026/2027 yanatarajiwa kuiongezea Serikali jumla ya shilingi trilioni 1.72.

Mheshimiwa Spika, marekebisho yanayopendekezwa yanahusu sheria zifuatazo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148; inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148 kama ifuatavyo:-

(i) Kuweka sharti la marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani *(VAT refunds)* kulipwa ndani ya siku 30 kutoka tarehe ya kuwasilishwa kwa maombi ya marejesho hayo. Hatua hii itaenda sambamba na kubainisha kuwa mlipakodi atakuwa na haki kisheria ya kulipwa riba pale ambapo marejesho husika hayatofanyika kwa wakati. Lengo la hatua hii ni kuchochea ulipaji kodi wa hiari na kuongeza uwajibikaji kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania; *(Makofi)*

(ii) Kujumuisha hati za kupandia ndege *(boarding pass)* kwenye wigo wa bidhaa zinazopata msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani. Lengo la hatua hii ni kutekeleza matakwa ya Mikataba ya Makubaliano ya Usafiri wa Anga ambayo Tanzania imeridhia;

(iii) Kujumuisha vifungashio vya maziwa vinavyotambulika kwa *HS Code* 3920.20.90 vinavyozalishwa na vinavyoingizwa kutoka nje ya nchi kwenye wigo wa bidhaa zinazopata msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani;

(iv) Kuondoa sharti la ukomo wa muda wa uahirishaji wa kodi ya ongezeko la thamani *(VAT deferment)* kwa bidhaa za mtaji zinazoingizwa nchini iliyopo sasa ili

kuanza kutekelezwa kwake tarehe 01 Julai, 2026; *(Makofi)*

(v) Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye vifaa vitakavyotumika katika vituo vya ku-*charge* magari yanayotumia umeme *(electric vehicles charging station)* vinavyoingizwa nchini na vinavyotambulika chini ya *HS Code* 8504.40.00;

(vi) Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye *turbojets, turbo-propellers* na *gas turbines* nyinginezo zinazotambulika kwa *HS Code Heading* 84.11; pamoja na matairi ya ndege yanayotambulika kwa *HS Code* 4011.30.00;

(vii) Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye mita janja za gesi ya mitungi ya kupikia zinazoingizwa nchini zinazotambulika kwa *HS Code* 9028.10.00. Msamaha huu husika utatolewa kwa wasambazaji wa gesi za kupikia pekee;

(viii) Kuendelea kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye mafuta ya kula yanayozalishwa ndani ya nchi kwa kutumia mbegu zinazozalishwa nchini kwa muda wa mwaka mmoja;

(ix) Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye nguo na mavazi yanayozalishwa kwa kutumia pamba inayozalishwa ndani ya nchi, kwa lengo la kuhamasisha matumizi ya pamba inayozalishwa nchini;

(x) Kufuta msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye nyavu za kuvulia samaki zinazoingizwa nchini, zinazotambulika kwa *HS Code* 5608.11.00; na

(xi) Kufuta msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye chakula cha mbwa na paka kinachotambulika kwa *HS Heading* 23.09

kinachozalishwa na kinachoingizwa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hatua zote za kodi ya ongezeko la thamani kwa ujumla wake zinatarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 26.6.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332; inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 kama ifuatavyo: -

(i) Kuweka msamaha wa kodi ya mapato kwa wafanyabiashara wapya kwa kipindi cha mwaka mmoja tangu tarehe ya kupata namba ya utambulisho kwa mlipakodi. Msamaha huo ni kwa ajili ya wafanyabiashara waliopo chini ya utaratibu wa makadirio *(presumptive regime)* pekee. Hatua hii inatofautiana na utaratibu wa sasa ambapo mfanyabiashara anaposajiliwa anafanyiwa tathmini ya mapato anayotarajia kuyakusanya na kupaswa kulipa kodi husika ndani ya miezi sita. Lengo la hatua hii ni kuwawezesha wafanyabiashara wapya kupata muda wa kutosha wa kujiandaa na mahitaji ya msingi, kuondoa usumbufu wakati wa kuanza biashara pamoja na kuhakikisha kuwa makadirio ya kodi yanazingatia uhalisia wa mapato yanayopatikana kutoka kwenye shughuli za biashara; *(Makofi)*

(ii) Kuongeza kima cha juu cha mauzo yanayotozwa kodi kwa utaratibu wa makadirio *(presumptive regime)* kutoka shilingi milioni 100 hadi shilingi milioni 200. Aidha, hatua hii itaenda sambamba na kuweka sharti la kuruhusu mlipakodi mwenye mauzo ya chini ya shilingi milioni 200 kuandaa vitabu vya hesabu pale atakapoona inafaa kwa lengo la kutumia utaratibu wa kujikadiria kodi *(self assessment)*. Lengo la hatua hii ni kuwianisha kima husika na kima cha usajili wa kodi ya ongezeko la thamani pamoja na kuboresha mfumo wa kodi;

(iii) Kuongeza kiwango cha kodi cha walipa kodi chini ya utaratibu wa makadirio wenye mauzo yanayozidi shilingi milioni 11 lakini yasiyozidi shilingi milioni 200 kutoka 3.5% hadi 4.5%. Lengo la hatua hii ni kuendana na kanuni za usawa za utozaji kwa kuhakikisha kodi husika inalipwa kwa kuzingatia uwiano wa mapato halisi yanayopatikana kwa walipakodi wenye mapato sawa na wale wanaotofautiana *(horizontal and vertical equity);*

(iv) Kuongeza kiwango cha kodi ya mapato kwenye malipo yanayofanywa kwa watoa huduma za kidijitali wa kigeni kutoka asilimia mbili hadi asilimia tatu;

(v) Kufanya marekebisho ya kifungu cha 33A cha Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 ili kupunguza kiwango cha faida ambayo haijagawanywa kwa wanahisa *(deemed retained earnings)* kinachotozwa kodi ya zuio kutoka 30C hadi 15%. Aidha, hatua hii itaenda sambamba na kuziondoa sekta ndogo za fedha, bima, kampuni zilizosajiliwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam pamoja na taasisi zenye mikataba ya utekelezaji na Serikali *(framework agreements)* katika utaratibu wa kutozwa kodi hiyo;

(vi) Kujumuisha *natural varnish, latex, resin, sap* na *gum* kwenye tafsiri ya neno mazao ya misitu ili viweze kutozwa kodi ya mapato kwa kiwango cha asilimia mbili kwenye mapato yanayotokana na uuzaji wa mazao hayo. Kiwango cha kodi husika kitalipwa kwa awamu moja kwa kila thamani ya mzigo;

(vii) Kuongeza kiwango cha kodi ya zuio kwenye mrabaha kwa Taasisi za Michezo au Shirikisho la Soka Tanzania kutoka asilimia tano hadi 10%;

(viii) Kuweka sharti la Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuzuia kodi ya mapato kwenye malipo

yanayofanywa kwenye ununuzi wa bidhaa nchini badala ya utaratibu wa sasa unaoweka sharti hilo kwa Taasisi za Serikali zinazojiendesha kwa kutegemea ruzuku kutoka Serikali Kuu kikamilifu au kwa kiasi kikubwa pekee. Lengo la hatua hii ni kuongeza wigo wa ukusanyaji wa kodi husika pamoja na kulinda mapato ya Serikali;

(ix) Kuanzisha utaratibu wa ulipaji wa kodi ya mapato ya awali kwa mkupuo mmoja kwa mnunuzi wa mazao ya kilimo. Katika utaratibu huu mnunuzi wa mazao ya chakula au biashara atawajibika kulipa kodi ya mapato kwa utaratibu pale ambapo anaponunua mazao, anapotaka kusafirisha mazao au anapohamisha umiliki wa mazao kutoka kwake kwenda kwa mtu mwingine. Kiwango cha kodi husika kitakuwa ni asilimia moja ya bei ya mazao husika katika eneo alikonunulia mazao na kitalipwa *TRA*. Kodi hii haitahusisha mkulima wa kawaida na mdogo, bali ni mnunuzi; na *(Makofi)*

(x) Kutoza kodi ya zuio kwa kiwango cha asilimia moja kwenye malipo yanayofanywa na kampuni au taasisi kwa muuzaji wa wanyama hai, maziwa ambayo hayajachakatwa, samaki ambao hawajachakatwa na mabondo. Aidha, kampuni au taasisi inayonunua mazao husika itakuwa wakala wa kukusanya kodi hiyo na kuiwasilisha kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato. Hivyo kodi hii vilevile haitamhusisha mfugaji au mvuvi wa kawaida nchini, bali ni mnunuzi wa mazao hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua hizi za kodi ya mapato kwa ujumla wake zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 174.48.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147; kwa mujibu wa kifungu cha 126(3) cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147, marekebisho ya viwango maalum vya ushuru

wa bidhaa *(specific excise duty rates)* yanaweza kufanyika kila baada ya miaka mitatu ili kuviwianisha na mfumuko wa bei na viashiria vingine vya uchumi jumla. Serikali ilianzisha utaratibu huo kuanzia mwaka 2023/2024 ili kuiwezesha nchi kuwa na sera za kodi zinazotabirika, kuchochea ukuaji wa uchumi pamoja na kuweka mazingira bora ya ufanyaji biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili ya utekelezaji wa utaratibu husika inatarajiwa kuanza mwaka 2026/2027 ambapo viwango vya ushuru vinatarajiwa kurekebishwa. Marekebisho hayo hayatahusisha viwango vya ushuru kwa bidhaa za petroli kutokana na kupanda kwa gharama za bidhaa husika katika soko la dunia kufuatia mgogoro baina ya Marekani, Israel na Iran na hivyo kuhitaji uwepo wa mikakati madhubuti nchini kwa lengo la kuzuia mfumuko wa bei, kupunguza ukali wa maisha kwa wananchi pamoja na kutoathiri ukuaji wa sekta zinazotegemea bidhaa za uendeshaji wa shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, licha ya utaratibu huo kuleta tija ikiwemo kuhakikisha uwepo wa mfumo wa utozaji unaotabirika imebainika kuwa ongezeko la ushuru wa bidhaa kwa kiwango kikubwa kwa mkupuo mmoja linaweza kuathiri ukuaji wa biashara na uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika, hivyo baada ya mashauriano ili kutatua changamoto zinazoweza kujitokeza na kufikia malengo yaliyokusudiwa, inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147 kuhusiana na utaratibu wa kurekebisha viwango vya ushuru kila baada ya miaka mitatu na badala yake viwango maalum vya ushuru viongezeke kwa asilimia nane kwa mwaka 2026/2027 na kwa miaka ya fedha ijayo, ongezeko litazingatia kiwango cha mfumuko wa bei kikijumlishwa na asilimia mbili.

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii ni kuakisi thamani ya mapato ya Serikali na kuiwezesha nchi kuwa na sera za kodi zinazotabirika na kuweka mazingira bora ya uwekezaji. Hatua hii inatarajia kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 251.54.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua hiyo, inapendekezwa pia kufanya marekebisho kwenye bidhaa nyingine kama ifuatavyo: -

(i) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha 20% kwenye maua ya bandia, matawi ya bandia, matunda ya bandia pamoja na bidhaa zinazofanana na hizo zinazoingizwa nchini zinazotambulika kwa *HS Heading* 67.02. Lengo la hatua hii ni kupunguza athari za kimazingira zinazotokana na matumizi ya bidhaa husika, kuongeza wigo wa kodi na mapato ya Serikali;

(ii) Kujumuisha watoa huduma wa kigeni kwa njia ya mtandao wasio na makazi ya biashara nchini wanaouza moja kwa moja kwa mtumiaji wa mwisho kwenye wigo wa utozaji ushuru wa bidhaa;

(iii) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha 10% kwenye mashine za kukaushia rangi za kucha zinazoingizwa nchini, zinazotambulika kwa *HS Code* 8516.779.070. Lengo la hatua hii ni kuzuia athari zinazotokea ikiwemo matatizo ya saratani; *(Makofi)*

(iv) Kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kutoka 10% hadi 15% kwenye bidhaa za urembo zinazoingizwa ndani ya nchi, zinazotambulika kwa *HS Heading* 33.03, 33.04, 33.05 na 33.07;

(v) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia tano kwenye pikipiki isipokuwa pikipiki za wagonjwa kwa dharura, pikipiki zinazotumia gesi asilia pamoja na pikipiki za umeme. Lengo la hatua hii ni kuendana na malengo ya Serikali ya kuhamasisha matumizi ya nishati safi kwenye vyombo vya moto nchini;

(vi) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha 10% kwenye viatu vya plastiki vinavyoingizwa nchini vinavyotambulika kwa *HS Code* 6402.99.00;

(vii) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia tano kwenye magari yanayotambulika kwa *HS Code* 8703.21.90 yenye ukubwa wa injini kuanzia 1,000 na kushuka chini;

(viii) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia tano kwenye thamani ya dau la kamari inayochezwa kwa njia ya michezo ya kubashiri ya ardhini au mtandaoni, michezo ya kasino ya ardhini au mtandanoni, mashine za *slot* 40 pamoja na michezo ya vikaragosi. Aidha, 10% ya mapato yatakayokusanywa kutoka kwenye chanzo hiki yatawasilishwa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha ili kuongeza ufanisi katika udhibiti wa michezo ya kubahatisha. Lengo la hatua hii ni kupunguza madhara yanayosababishwa na michezo ya kubahatisha ikiwemo uraibu na kupungua kwa nguvu kazi ya Taifa kutokana na baadhi ya vijana kujihusisha zaidi katika shughuli hizo badala ya shughuli za kiuchumi; na *(Makofi)*

(ix) Kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye magari yaliyotumika yanayoingizwa nchini kutoka 15% hadi 20% kwa magari yenye umri wa miaka nane, lakini hayazidi miaka 10 na kutoka 30% hadi 40% kwa magari yenye umri wa zaidi ya miaka kumi, lakini hayazidi miaka 20. Aidha, magari yenye miaka inayozidi 20 na kuendelea yatatozwa ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha 50%. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali pamoja na kupunguza uingizaji wa magari husika ambayo kwa kiasi kikubwa yanasababisha uchafuzi wa mazingira kutokana na uwepo wa taka ngumu ambazo hutumia gharama kubwa katika kuziteketeza.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi za ushuru wa bidhaa kwa ujumla wake zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 355.09.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438; napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438 ili kuweka sharti la Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kuruhusiwa kuuza bidhaa zinazoharibika haraka *(perishable goods)* zilizotaifishiwa au kushikiliwa kutokana na sababu mbalimbali za kikodi ikiwemo ukiukwaji wa taratibu za kodi na kushindwa kulipa deni la kodi, kwa utaratibu wa minada au uuzaji binafsi baada ya kutoa notisi kwa mlipakodi.

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii ni kuepuka kupoteza thamani ya bidhaa hizo kufuatia kukosekana kwa maghala ya kutosha ya kuhifadhia pamoja na kulinda mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura 339; inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania ili kuongeza kiwango cha tozo ya uchakataji wa nyaraka za uingizaji wa mizigo nchini kutoka 0.6% hadi asilimia moja. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali yatakayotumika katika kuboresha mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa kodi nchini. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 203.23.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290; katika jitihada za Serikali kuongeza fursa za ajira na kurasimisha sekta isiyo rasmi, inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 ili kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga 15% kama nilivyotangulia kusema ya mapato yao ya ndani badala ya 10% iliyokuwa awali ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kati ya hiyo 15% iliyotengwa, 10% itaendelea kutekelezwa kwenye mikopo ya wanawake, vijana na wenye ulemavu kwa uwiano kama ilivyokuwa awali na asilimia tano ya ziada itatumika kwa ajili ya uwekezaji kwenye miradi ya ujenzi wa maboresho ya masoko na maeneo ya biashara na ujasiriamali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mgawanyo wa mapato ya Mifuko ya Barabara, Nishati Vijijini, Maji na Reli; inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Nishati Vijijini, Sura 321; Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura 220; Sheria ya Reli, Sura 170; Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, Sura 272; pamoja na Sheria ya Petroli, Sura 392 ili kuweka mgawanyo wa mapato yatokanayo na vyanzo vya Mifuko ya Barabara, Nishati Vijijini, Maji na Reli na kuondoa changamoto ya sasa hivi iliyopo ya kutofikishwa mapato haya moja kwa moja katika mifuko hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapendekezo hayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, 70% ya makusanyo kutokana na mifuko hiyo kupelekwa moja kwa moja kwenye akaunti za mifuko tajwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mifuko husika; 25% kupelekwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina na asilimia tano kupelekwa kwenye akaunti maalum iliyopo Benki Kuu ya Tanzania kwa ajili ya kugharamia uwekezaji wa miundombinu katika Maeneo Maalum ya Uzalishaji wa Bidhaa kwa ajili ya mauzo nje *(EPZ)* na Maeneo Maalum ya Kiuchumi *(SEZ)* ikiwemo kulipia fidia kwa ardhi ya wananchi iliyochukuliwa kwa ajili ya ujenzi wa maeneo maalum ya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya yanalenga kuimarisha uwezo wa kifedha wa mifuko ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuhakikisha kuwa fedha zinaenda moja kwa moja, kuboresha miundombinu wezeshi katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji na kuiwezesha Serikali kuendelea kugharamia mahitaji ya lazima ikiwemo ulipaji wa madeni ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ardhi, Sura 113; inapendekezwa pia kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ardhi, Sura 113 ili kuweka mgawanyo wa 20% ya mapato yanayotokana na kodi ya pango la ardhi yanayorejeshwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza 10% ya kupelekwa Wizara yenye dhamana na masuala ya Ardhi na 10% kupelekwa Mamlaka za

Serikali za Mitaa. Lengo la hatua hii ni kuimarisha ushirikiano na kuongeza ufanisi katika upimaji wa ardhi na ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi. Aidha, Wizara ya Fedha itaweka utaratibu maalum wa matumizi ya fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura 197; katika kuendelea kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha za umma, Serikali inapendekeza kufanya maboresho ya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura 197 ili kupunguza kiwango cha ukomo wa mkopo wa muda mfupi *(overdraft)* ambao Serikali inachukua kutoka Benki Kuu kutoka 18% ya mapato halisi ya ndani ya mwaka wa fedha uliopita hadi 14%.

Mheshimiwa Spika, tunapunguza *overdraft* ambayo Serikali tunachukua kutoka Benki Kuu kutoka 18% ya mapato ya mwaka uliopita hadi 14% kuongeza nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapendekeza pia kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura 197 kwa kufuta kifungu cha 69 na kuandikwa upya ili kubainisha vigezo ambavyo benki inaweza kuruhusu mikopo ya muda mfupi kwa Serikali endapo kutatokea matukio yasiyotabirika au yasiyozuilika na kubainisha masuala yatakayochukuliwa kuwa ni matukio yasiyotabirika au yasiyozuilika.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Tume ya Mipango; inapendekezwa kufanya maboresho ya kifungu cha 6 cha Sheria ya Tume ya Mipango ili kuweka utaratibu wa miradi ya maendeleo ya kitaifa kutathminiwa kwa kuzingatia vigezo vya kiufundi, kifedha, kimazingira na kiuchumi kabla ya kuingizwa katika bajeti ya Serikali. Aidha, tathmini ya kimazingira itajumuisha tathmini ya athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha utafiti na uwekezaji katika sekta ya madini nchini, inapendekezwa Wizara ya Madini kuanzisha Mfuko wa Utafiti wa Madini nchini na kubakiza asilimia 10 ya mapato yatokanayo na sekta husika kwa ajili ya kugharamia tafiti hizo. Aidha, fedha hizo zitaingizwa kwenye

akaunti maalum itakayofunguliwa Benki Kuu na matumizi yake yatafanyika baada ya kupata idhini kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Rufaa za Kodi, Sura ya 408; inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Rufaa za Kodi, Sura ya 408 ili kuongeza muda wa kushughulikia utatuzi wa migogoro ya kodi nje ya mahakama kwa njia ya maridhiano, baina ya Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania na mlipakodi kutoka siku 60 hadi siku 90 tangu Bodi ya Rufaa ya Kodi *(TRAB)* na Baraza la Rufaa za Kodi *(TRAT)* lilipotoa amri ya kuruhusu shauri hilo kusubirishwa kwa utaratibu huo. Lengo la hatua hii ni kuhakikisha uwepo wa muda wa kutosha wa kutafuta suluhu ya migogoro ya kodi kwa njia ya maridhiano.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa na Mafuta, Sura ya 220; inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura ya 220 ili kutambua vipengele vya msamaha wa ushuru wa bidhaa na barabara na mafuta vilivyopo kwenye mikataba ya msingi *(framework agreements)* iliyosainiwa baina ya Serikali na wawekezaji wa madini, kama ilivyoelezwa hapo awali.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168; inapendekezwa kufanya marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168 ili kuruhusu magari au matela yaliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Usajili wa Tanzania Zanzibar kutumika Tanzania Bara yakiwa na namba za usajili za Tanzania Zanzibar pale ambapo kodi zote kwenye magari au matela husika imelipwa kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo. Aidha, kwa sasa utaratibu huu tayari unatumika kwa magari yanayotoka Tanzania Bara kwenda Tanzania Zanzibar. Lengo la hatua hii ni kutatua changamoto zilizopo kwenye matumizi ya vyombo hivyo, baina ya pande mbili za Muungano pasipo kuathiri mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kudhibiti Uingizaji wa Bidhaa Nchini, Sura ya 276; inapendekezwa kufanya marekebisho

kwenye Sheria ya Kudhibiti Uingizaji wa Bidhaa Nchini, Sura ya 276 kama ifuatavyo: -

(i) Kuweka sharti la tozo ya maendeleo ya viwanda kutotozwa kwenye bidhaa zinazozalishwa katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambazo zinakidhi vigezo vya usajili *(Rules of Origin)*. Aidha, hatua hii itaenda sambamba na kuruhusu vifungu na viwango vya utozaji kutumika kwa nchi mwanachama wa *EAC,* pale itakapobainika kuwa nchi husika imeweka vikwazo vya kibiashara kwa bidhaa zilizotoka Tanzania vikijumuisha vya kikodi, ada na tozo mbalimbali kwenye bidhaa hizo. Lengo la hatua hii ni kuendana na matakwa ya Itifaki ya Uanzishaji wa Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yanayoelekeza nchi wanachama kuzuia ubaguzi wa kikodi ili kuruhusu biashara huria na kuleta ushindani wa haki katika jumuiya yetu.

(ii) Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia tano kwenye madaftari yanayoingizwa nchini yanayotambuliwa kwa *HS Codes* ambazo zimetajwa.

(iii) Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia tano kwenye matela yanayoingizwa nchini, yanayotambuliwa kwenye *HS Codes* ambazo zimetajwa katika kitabu cha hotuba ya bajeti.

(iv) Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia kumi kwenye nyavu za kuvulia samaki zinazoingizwa nchini zinazotambuliwa kwenye *HS Code* ambayo imetajwa.

(v) Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia tano kwenye milango, madirisha, pamoja na *frame* zake zinazoingizwa nchini zinazotambulika kwa *HS Code* ambayo imetajwa.

(vi) Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia kumi kwenye bidhaa za chuma zinazoingizwa nchini zinazotambuliwa kwenye *HS Code* 7308.90.99.

(vii) Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia tano kwenye bidhaa za *aluminium* zinazotambulika kwenye *HS Code* 7610.10.00.

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hizi ni kuvutia uwekezaji nchini, kuchochea mauzo nje ya nchi na kulinda uzalishaji wa ndani kwa kuwa bidhaa husika zinazalishwa kwa wingi hapa nchini. Hatua hizi zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 37.04.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi, Sura ya 196; inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi, Sura ya 196 kama ifuatavyo:-

(i) Kutoza tozo ya usafirishaji wa bidhaa kwenda nje ya nchi kwa kiwango cha 30% ya thamani ya mizigo au shilingi 200 kwa kila kilo moja, kutegemeana na kiwango kitakachokuwa kikubwa, kwenye taka za karatasi zinazotambulika kwa *HS Code* 4707.00.00.

(ii) Kutoza tozo ya usafirishaji wa bidhaa kwenda nje ya nchi kwa kiwango cha 10% au shilingi 200 kwa kila kilo, kutegemeana na kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye madini ya *quartz* yanayotambulika kwa *HS Heading* 25.06 na *feldspar* inayotambulika kwa HS Code 2529.10.00.

(iii) Kutoza tozo ya usafirishaji wa bidhaa kwenda nje ya nchi kwa kiwango cha shilingi 50 kwa kila kilo ya pumba za ngano zinazotambulika kwa *HS Code* 2302.30.00, mashudu ya pamba yanayotambulika kwa *HS Code* ambayo imetajwa, pumba za mpunga, pumba za

mahindi na mashudu ya alizeti yanayotambulika kwa *HS Codes* ambazo zimetajwa katika hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hizi vilevile ni kuchochea uongezaji wa thamani nchini na kuhakikisha upatikanaji wa malighafi muhimu kwenye viwanda vya uchakataji na usindikaji hapa nchini. Hatua hizi kwa ujumla wake zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 24.44.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Stempu, Sura ya 189; Sheria ya Ushuru wa Stempu, Sura ya 189 ni moja ya sheria kongwe na ambayo imechukua muda mrefu kurekebishwa katika ushuru kwa baadhi ya hati na nyaraka. Inapendekeza kufanya marekebisho kwenye jedwali la sheria hiyo kama ifuatavyo: -

(i) Kuboresha tafsiri ya neno *lease* ili kujumuisha hati za ubadilishanaji wa mali zinazohamishika yaani *(moveable properties)* kwenye wigo wa utozaji wa ushuru wa stempu.

(ii) Kuongeza kima cha thamani ya utozaji wa ushuru wa stempu kwenye hati ya mauzo ya mali kwa njia ya dhamana *(bill of sale by way of of collateral security)* kutoka shilingi 1,000 hadi shilingi 10,000.

(iii) Kuongeza kima cha juu cha ukomo wa utozaji wa ushuru wa stempu wa hati ya mauzo kwa njia ya dhamana yaani *(bill of sale by way of security)* kutoka shilingi 10,000 hadi shilingi 100,000.

(iv) Kubadili wigo wa thamani wa mitaji kwenye hati za ubia, pamoja na viwango vya ushuru wa stempu kwenye hati husika kama ifuatavyo; kutoza kiwango cha shilingi 5,000 kwa hati zenye thamani ya mtaji isiyozidi shilingi 1,000,000 na kiwango cha shilingi 10,000 kwa hati zinazozidi thamani ya shilingi 1,000,000.

(v) Kuongeza kiwango cha ushuru wa stempu kwenye hundi kutoka shilingi 100 hadi shilingi 500.

(vi) Kuongeza kiwango cha ushuru wa stempu kwenye hati za kusitisha mikataba ya ukodishaji kutoka shilingi 1,000 hadi shilingi 2,000.

(vii) Kutoza ushuru wa stempu wa kiwango cha shilingi 50,000 kwenye hati za upandishaji wa mali.

(viii) Kutoza ushuru wa stempu kwa kiwango cha asilimia 0.5 kwenye hati za uhamishaji wa ardhi na matumizi ya kilimo badala ya kiwango maalum cha shilingi 500 kinachotozwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hizi ni kuendana na kanuni za usawa wa utozaji kodi, kuongeza wigo wa kodi, pamoja na kulinda thamani ya fedha kwa kuwa viwango husika havijabadilishwa kwa muda mrefu. Hatua hizi kwa pamoja zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 11.08.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Tume ya Ushindani, Sura ya 285; inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 88 cha Sheria ya Tume ya Ushindani, Sura ya 285 kwa kubainisha kuwa mapato ya Baraza la Ushindani yanajumuisha asilimia 0.5 ya mapato ya Mamlaka za Udhibiti yaliyoorodheshwa kwenye kifungu cha 88(1)(d) cha sheria husika, ikiwemo Mamlaka ya *EWURA, LATRA, TCRA* na *TCAA*. Hatua hii inalenga kutatua changamoto zilizopo ambapo sheria imebainisha vyanzo vya mapato ya taasisi ambazo zinapaswa kuwasilisha sehemu ya mapato yake Baraza la Ushindani bila kuweka kiwango husika.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi ya mwaka 2024; inapendekezwa kufanya marekebisho ya Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi ya mwaka 2024 ili kujumuisha vichwa vya matela vinavyotambulika kwenye *HS Codes* ambazo zimetajwa na kwenye orodha ya bidhaa zisizostahili msamaha wa kodi yaani *(negative list)*. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani, ajira na mapato ya Serikali. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 57.16.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004; napenda kufahamisha kuwa mkutano wa mashauriano kabla ya bajeti ya Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika tarehe 15 Mei, 2024 Jijini Arusha, pamoja na mambo mengine ulijadili na kupendekeza hatua mbalimbali za kisera, ikiwemo mabadiliko ya viwango vya pamoja vya ushuru wa forodha vya Jumuiya ya Afrika Mashariki vinavyopendekezwa kutekelezwa kwa mwaka 2026/2027. Aidha, mkutano huo ulipendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 kwa lengo la kutatua changamoto zilizopo katika utekelezaji wa sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizopendekezwa zinalenga kulinda viwanda vya ndani, kuvutia uwekezaji, kupunguza gharama za uzalishaji wa bidhaa nchini, kulinda walaji, kuongeza fursa za ajira, kuchochea ukuaji wa sekta mbalimbali za kiuchumi, kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa zinazotoka nje, pamoja na kuongeza mapato ya Serikali. Mapendekezo ya Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kufanya mabadiliko kwenye viwango vya pamoja vya ushuru wa forodha, yanahusisha hatua mpya na zinazoendelea kutekelezwa katika mwaka 2025/2026. Hatua hizo ni kama ifuatavyo: -

(i) Mapendekezo ya hatua mpya za mabadiliko ya viwango vya ushuru wa forodha: -

(a) Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha 35% au dola za Marekani mbili kwa mita za mraba kutegemeana na kiwango kilichokuwa kikubwa, badala ya 25% kwa mwaka mmoja kwenye mawe yanayotumika kama mapambo katika ujenzi, yanayotambulika kwa *HS Heading* 68.02 kwa lengo la kuhamasisha matumizi ya mawe yanayopatikana ndani ya nchi.

(b) Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha 25% au dola za Marekani 550 kwa tani, kutegemeana na kiwango kitakachokuwa kikubwa, badala ya 25% pekee kwenye bidhaa za *aluminium* zinazotambulika kwa *HS Heading* 76.04. Hatua hii inalenga kulinda viwanda vya ndani, kuhamasisha uwekezaji nchini, kuongeza mapato ya Serikali na kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa kutoka nje.

(c) Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha 35% au dola za Marekani 350 kwa tani, kutegemeana na kiwango kitakachokuwa kikubwa, badala ya 25% pekee kwenye sabuni zinazotambulika kwenye *HS Codes* ambazo zimetajwa. Hatua hii vilevile inalenga kulinda viwanda vya ndani vinavyozalisha bidhaa hii, kuhamasisha uwekezaji nchini na kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa.

(d) Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha 35% au dola za Marekani 250 kwa tani, kutegemeana na kiwango kitakachokuwa kikubwa, badala ya 25% pekee kwenye *stick* za kuchomea *(higher on welding electrodes)* zinazotambulika kwenye *HS Code* 8311.10.00.

(e) Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha 10% badala ya asilimia sifuri kwenye mafuta ghafi ya mchikichi kama ambavyo nimesema hapo awali.

(f) Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha 10% badala ya asilimia sifuri kwenye chokaa inayotambulika kwa *HS Code* 2836.50.00 kwa lengo la kulinda viwanda vya ndani pamoja na kuvutia uwekezaji katika sekta hii.

(g) Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha 35% au dola za Marekani 0.3 kwa kila mita moja kutegemeana na kiwango kilicho kikubwa badala ya 25% pekee kwa mwaka mmoja kwenye vitambaa ya pamba inayotambulika kwenye *HS Codes* ambazo zimeorodheshwa katika hotuba yangu ya bajeti. Lengo ni kuendelea kuongeza mapato ya Serikali, lakini zaidi ni kushajihisha maendeleo ya viwanda nchini na kulinda viwanda vilivyopo.

(h) Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha 35% badala ya 25% kwenye milango na madirisha ya plastiki yanayotambulika kwa *HS Code* 3925.20.00 kwa lengo la kulinda uzalishaji wa ndani.

(i) Kupunguza ushuru wa forodha kutoka 25% hadi 10% kwenye magari yanayotumia nishati ya umeme yanayotambulika kwenye *HS Codes* ambazo zimetajwa kama nilivyotangulia kusema.

(j) Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki vilevile zimekubaliana kubadilisha kiwango cha ushuru wa forodha kutoka kiwango cha 35% pekee hadi kiwango cha 35% au dola tatu za Marekani kwa kila mita moja ya mraba kutegemeana na kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye marumaru zinazotambulika kwenye *HS Codes* ambazo zimetajwa katika hotuba ya bajeti.

(k) Vilevile, kubadilisha kiwango cha ushuru wa forodha kutoka kiwango cha 35% pekee hadi kiwango cha 35% au dola za Marekani 350 kwa tani kutegemeana na kiwango

kitakachokuwa kikubwa kwenye misumari inayotambulika kwenye *HS Code* 7317.00.00.

(l) Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kwa kiwango cha 10% badala ya 25% kwa mwaka mmoja kwenye karatasi zinazotumiwa kwenye *HS Codes* ambazo zimetajwa, zinazotumika kutengeneza vifungashio aina ya maboksi. Lengo la hatua hii ni kuwapa unafuu wazalishaji wa vifungashio hivyo hapa nchini, ili wananchi waweze kuvipata kwa urahisi na kwa gharama nafuu.

(m) Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kwa kiwango cha asilimia sifuri badala ya 10% kwa mwaka mmoja kwenye karatasi zinazotambulika kwa *HS Codes* zilizotajwa zinazotumika kutengeneza vifungashio aina ya maboksi. Lengo ni lilelile kuimarisha viwanda vya ndani.

(n) Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu huu wa *duty remission* kwa kiwango cha asilimia sifuri badala ya 10% kwa mwaka mmoja kwenye malighafi zinazotambulika kwa *HS Codes* zilizotajwa zinazotumika kutengeneza vifungashio vya aina mbalimbali.

*(o)* Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kwa kiwango cha 10% badala ya 35% kwa mwaka mmoja kwenye malighafi zinazotambulika kwenye *HS Code* 3210.00.99 zinazotumika katika utengenezaji wa *aluminium products.*

(p) Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kwa kiwango cha

asilimia sifuri kwenye vifungashio vinavyotumiwa na wazalishaji wa madawa ya mifugo kwa mwaka mmoja.

(q) Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwa *duty remission* kwa kiwango cha 10% badala ya 25% kwenye nyaya zinazotambulika kwenye *HS Codes* ambazo zimetajwa, zinazotumika katika utengenezaji wa nguzo za umeme za zege. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za uzalishaji wa nguzo hizo ndani ya jumuiya ili kuwezesha zoezi la ubadilishaji wa nguzo za miti kwa kuweka nguzo za zege, pamoja na usambazaji wa umeme kufika vijijini na kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya kuendeleza viwango vya ushuru wa forodha; miongoni mwa mapendekezo ya viwango ambavyo tayari vipo, vinapendekezwa kuendelea tena kwa mwaka mwingine mmoja ambayo ni: -

(i) Kupunguza kiwango cha ushuru wa forodha kutoka 10% hadi asilimia sifuri kwa mwaka mwingine mmoja kwa vifaa vya kielektroniki, vinavyotumika kuhasibu mapato ya Serikali vinavyotambulika kwa *HS Code* 8470.50.00 na 8470.90.00.

(ii) Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha 10% badala ya asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kwenye unga wa kakao unaoingizwa kutoka nje unaotambuliwa kwa *HS Code* iliyotajwa.

(iii) Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha 10% badala ya asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kwenye fito za plastiki zitokanazo na *PVC profiles* zinazotambuliwa kwenye *HS Codes* zilizotajwa, zinazotumika kutengeneza fremu za milango na madirisha hapa nchini.

(iv) Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha 25% au dola za Marekani 1.35 kwa kila kilo moja, kutegemea kiwango kiwango kilichokuwa kimetajwa.

Mheshimiwa Spika, viwango hivyo vinapatikana katika hotuba yangu ambavyo vimetajwa kwa urefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua nilizozibainisha hapo juu, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kurekebisha kipengele cha kwanza cha Sehemu B ya Jedwali la Tano la Sheria ya Usimamizi wa Forodha ili kujumuisha karatasi zinazotumika kutolea hati ya kupandia *(boarding pass)* kama nilivyosema awali kwenye wigo wa msamaha wa ushuru wa forodha.

Mheshimiwa Spika, nchi wanachama vilevile zimekubaliana kurekebisha kipengele cha 20 cha Sehemu B ya Jedwali la Tano la Sheria ya Usimamizi wa Forodha ili kutambua mamlaka zote zinazosimamia majanga katika nchi mwanachama wa jumuiya kwa ajili ya kuwezesha au kurahisisha utoaji wa msamaha wa ushuru wa forodha kwa bidhaa zinazoingizwa nchini, kwa lengo la kutatua majanga yanapojitokeza.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2025 tulilifahamisha Bunge kuwa nchi wanachama zilikubaliana kuanzisha kanuni za uunganishaji na uzalishaji wa bidhaa za Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwamba utekelezaji wa kanuni hizo ulipangwa kuanza tarehe 1 Julai, mwaka 2026. Kanuni husika zinalenga kutoa mwongozo wa uzalishaji na usimamizi wa skimu za uunganishaji na uzalishaji wa bidhaa ndani ya nchi mwanachama ili kuongeza uzalishaji wa bidhaa ndani ya nchi mwanachama na kuongeza matumizi ya bidhaa zinazozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mkutano wa mashauriano kabla ya bajeti ya Mawaziri wa Fedha umekubaliana kusogeza mbele utekelezaji wa kanuni husika hadi tarehe 1 Julai, 2027 ili kutoa fursa kwa viwanda vya ndani kujipanga na kuanza uzalishaji wa bidhaa zinazopaswa kuzalishwa ndani ya jumuiya ambazo hazitopata

unafuu wa ushuru wa forodha endapo zitaagizwa kutoka nje ya jumuiya.

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu pamoja na wananchi kwamba kwa ujumla kuwa Novemba, 2025 nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zilikubaliana kuweka viwango maalum vya ushuru wa forodha kwenye baadhi ya bidhaa ikiwemo vilainishi, amira, karatasi zinazotumika kuchapisha na kutolea nakala, kwa lengo la kulinda viwanda vya ndani ya jumuiya pamoja na kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi.

Mheshimiwa Spika, viwango vipya vya ushuru wa forodha ambavyo vinategemewa kuanza kutekezwa kuanzia tarehe 01 Julai ni kama ifuatavyo:-

(i) 25% au dola za Marekani 0.46 kwa lita kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye vilainishi vinavyotambulika kwenye *HS Code* iliyotajwa badala ya kiwango cha 25% pekee;

(ii) 25% au dola za Marekani 660 kwa tani kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye hamira iliotambulika kwenye *HS Code* iliyotajwa badala ya kiwango cha 25% pekee;

(iii) 25% au dola za Marekani 200 kwa tani kutegemea kiwango kikubwa kwenye karatasi zilotumika kuchapishia na kutolea nakala zilizotambulika kwa *HS Code* iliyotajwa badala ya 25% pekee; na

(iv) 10% au dola za Marekani 80 kwa tani kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye karatasi inayotumika kuchapishia au kutolea nakala inambulia kwenye *HS Code* iliotajwa badala ya kiwango cha 10% pekee.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi kwa pamoja natarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 408.97.

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Sheria ya Wakala wa Vipimo mwaka 2025; inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Kanuni za Sheria ya Wakala wa Vipimo, 2025 ili kuongeza ada ya uhakiki wa mafuta kutoka shilingi 0.15 kwa kila lita ya mafuta hadi shilingi moja kwa lita ya mafuta. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya wakala wa vipimo kwa ajili ya kugharamia ununuzi wa vifaa vya kisasa vya udhibiti vinavyoendana na ukuaji wa teknolojia hususan katika tasnia ya biashara ya mafuta na hivyo kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa jukumu lake la uhakiki wa vipimo. Aidha, matumizi ya fedha yanayotokana na ada husika yatafanyika baada ya kupata ridhaa ya Mlipaji Mkuu wa Serikali kufuatia kuwasilishwa kwa mpango kazi wa matumizi hayo. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 21.96.

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Sheria Usajili na Utambuzi wa Watu, 2014; kumejitokeza mahitaji ya mara kwa mara ya taarifa kutoka *NIDA* yanayosababisha gharama kubwa ya uendeshaji, hivyo inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Kanuni za Sheria ya Usajili wa Utambuzi wa Watu, 2014 ili kuanzisha ada ya shilingi 500 kwa wananchi wanaoomba taarifa zake katika kanzidata ya *NIDA* kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, taarifa hizo ni pamoja na majina ya wazazi, shule uliyosoma, namba ya simu na taarifa nyingine zilizopo katika kanzidata ya Mamlaka. Aidha, kwa mwananchi atakayehitaji kupatiwa nakala ya taarifa hizo atalipia ada ya shilingi 1,000. Lengo la hatua hii ni kugharamia utoaji wa huduma hizo na kuongeza ufanisi wa Mamlaka ya *NIDA*. Hatua hii inatarajia kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 734.4.

Mheshimiwa Spika, Kanuni na Sheria ya Usalama Barabarani za mwaka 2024; pamoja na kuwepo mfumo maalum wa kulipia kodi kwa wafanyabiashara wadogo *(presumptive tax)* kumekuwa na ugumu wa kutekeleza mfumo huo kwenye biashara ya usafiri na wa vyombo vya miguu miwili; inapendekezwa kuendelea na utaratibu wa sasa wa kutowaingiza wafanyabiashara hao katika mfumo wa *presumptive tax*, badala yake imependekezwa

kufanya marekebisho kwenye Kanuni za Sheria za Usalama Barabarani za mwaka 2024 ili kuongeza ada ya mara moja tu ya usajili wa pikipiki wa miguu miwili kutoka shilingi 95,000 hadi 150,000.

Mheshimiwa Spika, lengo hatua hii ni kuongeza mapato wa Serikali bila ya kuathiri biashara hizo ndogo ndogo. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa shilingi bilioni 17.75.

Mheshimiwa Spika, uanzishaji wa vyanzo vya ziada vya mapato kwa ajili ya kuharamia bima ya afya kwa wote; Serikali inapendekeza kuongeza vyanzo vya mapato kwa ajili ya kugharamia Bima ya Afya kwa Wote na kufanya marekebisho kwenye sheria na kanuni mbalimbali. Kwanza, kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147 ili kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwa shilingi 20 kwa kila sigara 1,000 zinazotambulika kwenye *HS Heading* 2402 24.03 na pili kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Sukari, Sura 257 pamoja na kanuni zake ili kuongeza ada kwa shilingi 10 kwa kila kilo moja ya sukari iliyozalishwa ndani na inayoagizwa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, tozo hii itakusanywa na Bodi ya Sukari Tanzania na kuwasilishwa kwenye Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote. Hatua hizi kwa pamoja zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa shilingi bilioni 7.5.

Mheshimiwa Spika, maboresho ya ada na tozo mbalimbali ya taasisi za Serikali pamoja na utekelezaji wa mpango wa kuboresha mazingira; inapendekezwa kufanya maboresho ya sheria na kanuni mbalimbali kwa kufuta au kupunguza ada na tozo mbalimbali zinazotozwa na Wizara, Idara na Taasisi zanazojitegemea ili kuleta usimamizi bora wa sekta mbalimbali na kuboresha mazingira ya biashara nchini.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi ni moja ya sehemu za mwendelezo wa utekelezaji wa mpango wa kuboresha mazingira ya biashara nchini. Marekebisho hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Ada za huduma za maudhui mitandaoni; kufanya marekebisho kwenye kanuni za mawasiliano ya elektriniki na posta ili kupunguza ada za huduma za maudhui mitandaoni inayotumiwa zaidi na vijana kama ifuatavyo:-

(a) Ada ya maombi ya leseni ya huduma ya maudhui mtandaoni kupungua kutoka shilingi 50,000 hadi shilingi 10,000.

(b) Ada ya mwanzo za mwaka kwa ajili ya kuhuisha leseni ya huduma za maudhui mtandaoni kupunguzwa kutoka shilingi 500,000 hadi shilingi 50,000.

(c) Ada ya maombi ya leseni za kutengeneza maudhui mtandaoni nayo kupunguzwa kutoka shilingi 100,000 hadi shilingi 20,000; na

(d) Ada ya mwanzo ya mwaka kwa ajili ya kuhuisha na kutengeneza maudhui mtandaoni kupunguzwa kutoka shilingi 1,000,000 hadi shilingi 100,000.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wizara ya Maliasili na Utalii inapendekezwa kuanzisha ada ya usajili wa usimamizi wa makumbusho binafsi kama ifuatavyo:-

(i) Usajili wa makumbusho binafsi kwa raia wa Tanzania ada iwe shilingi 50,000

(ii) Usajili wa makumbusho binafsi kwa taasisi za Tanzania ada iwe shilingi laki 100,000.

(iii) Usajili wa makumbusho binafsi kwa raia ya kigeni ada shilingi laki 500,000.

(iv) Malipo ya leseni kwa ajili ya uendeshaji wa makumbusho binafsi kwa raia wa Tanzania shilingi 20,000 kwa mwaka.

(v) Malipo ya leseni kwa ajili ya uendeshaji wa makumbusho binafsi kwa taasisi za Tanzania wa kiwango cha shilingi 100,000 na;

(vi) Malipo ya leseni kwa ajili ya uendeshaji wa makumbusho binafsi kwa taasisi za kigeni ya shilingi 300,000.

Mheshimiwa Spika, marekebisho madogo madogo katika baadhi ya kanuni nyinginezo; kwa kufanya marekebisho mengine madogo katika kanuni mbalimbali sanjari na azma ya kurahisisha utekelezaji wake kama zilivyoainishwa kwenye kiambatisho namba moja, mbili na nne.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maboresho ya sheria mbalimbali yaliyofanywa na Serikali ili kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara kwa kupunguza mwingiliano wa majukumu baina ya taasisi na udhibiti na kufuta ama kupunguza ada ya tozo, bado kumekuwa na changamoto na taasisi nyingi za udhibiti za kusimamia sekta mbalimbali za ufanyaji biashara na uwekezaji kutokana na ada, tozo na adhabu mbalimbali zinazotozwa pamoja na kaguzi nyingi zisizokuwa na tija.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa kero hizo Serikali ipo katika hatua za kuanzisha mfumo wa pamoja wa ukusanyaji wa ada, tozo na adhabu za taasisi za udhibiti na kuweka utaratibu wa taasisi hizo kufanya kaguzi kwa namna ambayo haitaleta usumbufu bila kuathiri majukumu yao ya msingi kama nilivyotangulia kusema.

Mheshimiwa Spika, marekebisho madogo katika baadhi ya sheria za kodi, sheria nyingine; pamoja na mapendekezo mahsusi niliyoyabainisha hapo juu inapendekezwa pia kufanya marekebisho mengine madogo katika sheria mbalimbali za kodi, sheria nyingine pamoja na kanuni na sheria, sanjari na azma ya kurahisisha utekelezaji wake. Marekebisho haya yataainishwa katika Muswada wa Sheria wa Fedha wa mwaka 2026 na matangazo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, tarehe ya kwanza kutekeleza hatua hizo; hatua hizi za kikodi zinazopendekezwa zitaanza kutekelezwa tarehe 1 Julai, 2026 isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, Sura ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2026/2027; kwa mwaka 2026/2027 Serikali inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya shilingi trilioni 62.33 ikiwa ni ongezeko la 10.3% ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2025/2026. Mapato yanatarajiwa kuwa shilingi trilioni 46.79 ambapo mapato ya kodi ni shilingi trilioni 36.99 na mapato mengine ni shilingi trilioni 9.24 ikijumuisha mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa shilingi trilioni 1.97 na misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo shilingi bilioni 563.1.

Mheshimiwa Spika, ili kuendana na dhamira yetu ya kujitegemea katika uendeshaji wa Serikali na maendeleo takribani robo tatu ya bajeti yote ya mwaka 2026/2027 sawa na 74.2% inatarajiwa kugharamiwa na mapato ya ndani. Misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo inatarajiwa kupungua kwa 39.1% kwa mwaka 2026/2027 ikilinganishwa na fedha zilizoahidiwa kwa mwaka 2025/2026. Hali hii inatokana na kubadilika kwa sera za baadhi ya washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, tunawashukuru sana washirika wetu wa maendeleo kwa msaada wao pale walipoweza. Hata hivyo Tanzania ni Taifa letu na sisi tuna wajibu wa kulijenga, ni wajibu wa wananchi wote kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi, kulipa kodi kwa hiari na kushikamana na Serikali katika kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Spika, matumizi na uwekezaji katika mali zisizo za kifedha yanakadiriwa kufikia shilingi trilioni 54.5 pasipo kujumuisha malipo ya mtaji wa Deni la Serikali. Katika ya kiasi hicho stahiki za watumishi zikijumuisha michango ya pensheni ni shilingi trilioni 10.13, gharama za bidhaa na huduma shilingi trilioni 5.22, malipo ya riba ni shilingi trilioni 6.86, ruzuku shilingi trilioni 25.32, mafao na misaada ya kijamii shilingi trilioni 1.01, uwekezaji katika mali zisizo za kifedha shilingi trilioni 2.3 na gharama nyingine shilingi trilioni 3.63.

Mheshimiwa Spika, kulingana na makadirio ya mapato na matumizi hayo niliyoyaeleza, kunajitokeza nakisi kwenye bajeti ya shilingi trilioni 7.71, Serikali itaendelea kugharamia nakisi hii ya bajeti kwa kutumia mikopo kutoka vyanzo vya ndani na nje kwa kuzingatia mkakati wa muda wa kati wa kusimamia Deni la Serikali mwaka 2025/2026 – 2027/2028.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2026/2027 Serikali inatarajia kukopa jumla ya shilingi trilioni 15.54, kati ya kiasi hicho mikopo ya ndani ni shilingi trilioni 6.56 na mikopo ya nje yenye masharti nafuu ni shilingi trilioni 6.55 na mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara shilingi trilioni 2.43. Aidha, Serikali inakadiria kulipa malipo ya mtaji kwa mikopo iliyoiva ya shilingi trilioni 7.84.

Mheshimiwa Spika, sura ya bajeti inayopendekezwa kwa mwaka 2026/2027 imeainishwa katika jedwali namba moja.

Mheshimiwa Spika, vihatarishi vya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2026/2027 na hatua za kukabiliana na vihatarishi hivyo vimebainishwa kupitia aya ya 136 hadi aya ya 140 ya hotuba yangu ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, shukrani na pongeza; kabla ya kuhitimisha hotuba yangu kwanza naomba tena nikupongeze wewe binafsi Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Jimbo la Ilala; na Naibu Spika, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuliongoza Bunge letu Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha nampongeza Ndugu Baraka Leonard kwa kuendelea kuaminiwa kuwa Katibu wa Bunge na kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuratibu shughuli za chombo hiki cha wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Wenyeviti wa Bunge na Kamati zake walioaminiwa na kuteuliwa kuongoza vikao vya Bunge na shughuli za Kamati. Kipekee ninaishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake

Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi pamoja na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Ali Omar King, Mbunge wa Jang'ombe na Wajumbe wake wote kwa maoni na ushauri wao bora wakati wa maandalizi na utekelezaji wa bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha ninawashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Natumia pia fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge hili kwa kuaminiwa na kuchaguliwa au kuteuliwa kuhudumu katika nafasi za Ubunge kwenye Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kuwa sote tutaendelea kushirikiana katika kuwaletea maendeleo Watanzania wenzetu. Kipekee sana nakishukuru chama changu tawala, Chama Cha Mapinduzi kikiongozwa na Amiri Jeshi na Mwenyekiti wetu wa Chama Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini na kuwa sehemu utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, aidha na kwa kipekee kabisa ninawashukuru viongozi waandamizi wote wa Chama Cha Mapinduzi kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakinipatia kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yangu ndani ya Serikali. Mfumo wetu wa utawala unahusisha mihimili mitatu ya dola. Kwa maendeleo ya uchumi, Mahakama ni taasisi muhimu kwa utendaji bora wa soko. Niruhusu nimpongeze Mheshimiwa George Mcheche Masaju, Jaji Mkuu wa Tanzania pamoja na watendaji wote wa Mahakama kwa kazi nzuri na ya heshima wanayoifanya ya kusimamia mifumo ya utoaji wa haki kwa Watanzania wote na wawekezaji wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya tunayoendelea kuyapata yanatokana pia na utulivu na umahiri wa watumishi wote wa umma. Napenda kutoa shukrani na pongezi zangu za dhati kwa Katibu Mkuu Kiongozi Balozi Dkt. Moses Mpogole

Kusiluka, kwa utendaji wake mzuri katika kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali na Utumishi wa Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, ninawapongeza na kuwashukuru wakuu wote wa vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuendelea kulinda kwa umahiri mkubwa mipaka ya nchi yetu na kuhakikisha hali ya utulivu na usalama nchini kwetu. Utendaji wangu unapata msaada mkubwa kutoka kwa wasaidizi wangu wa karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru kwa dhati Waheshimiwa Naibu Mawaziri wa Fedha, Mheshimiwa Mhandisi Mshamu Ali Munde, Mbunge wa Jimbo la Liwale na Mheshimiwa Laurent Deogratius Luswetula, Mbunge wa Jimbo la Kavuu kwa ushirikiano wao na mchango mkubwa katika kunisaidia kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, aidha natoa pongezi na shukrani za dhati kwa Dkt. Natu El-Maamry Mwamba, Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali; Naibu Makatibu Wakuu Ndugu Elijah Greenton Mwandumbya na Ndugu Nsubili Akomeligwe Kajela Joshua kwa ushauri wao wa kitaalam na usimamizi makini wa majukumu ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii vilevile kumpongeza Ndugu Emmanuel Mpawe Tutuba, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania kwa kuendelea kusimamia kwa ufanisi utekelezaji wa sera ya fedha. Aidha, natumia fursa hii vilevile kuwapongeza Gavana Tutuba, Bodi ya Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Benki Kuu ya Tanzania kwa kutimiza miaka 60 toka Benki Kuu kuanzishwa. Ninawatakia kila la kheri katika kutekeleza majukumu yao kwa miaka 60 ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia Ndugu *CPA* Yusuph Juma Mwenda, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa jitihada kubwa anazofanya za kusimamia vyema ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Kama ilivyo kwa Benki Kuu tarehe 01 Julai, mwaka huu *TRA* nayo itatimiza miaka 30 tangu kuanzishwa kwake. Hivyo, natumia fursa hii kuwapongeza na

kuwatakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yao. Kwa miaka 30 ya uwepo wake *TRA* imepata mafanikio makubwa kutokana na ushirikiano inaoupata kutoka kwa walipakodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa walipakodi Julai, 2026 tunatarajia kwamba Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan atatoa tuzo kwa walipakodi mahiri ili kutambua mchango wao wa kizalendo na uhiari wa kulipa kodi kwa maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa pia shukrani na pongezi maalum kwa *CPA* Charles Edward Kichere, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa juhudi endelevu na kazi bora anayoifanya katika ukaguzi wa hesabu na taasisi za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nampongeza pia Dkt. Amina Suleiman Msengwa, Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa kuendelea kusimamia kwa weledi tafiti na uzalishaji wa takwimu rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadhalika, nawapongeza viongozi wengine na watumishi wote wa Wizara ya Fedha pamoja na taasisi zake kwa kazi nzuri ya maandalizi na usimamizi madhubuti wa utekezaji wa bajeti ya Serikali. Namshukuru Mheshimiwa Rais na najisikia kuwa nimependelewa kupatiwa moja ya timu bora kabisa ya utendaji. Kwa hakika hii ni *A-team* kama Arsenal, imekamilika katika idara zake zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani kwa viongozi na watendaji wa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa na wadau mbalimbali katika kuwezesha maandalizi na utekelezaji wa bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunawashukuru pia majirani zetu wa karibu nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Malawi, Msumbiji, Rwanda, Uganda na Zambia kwa ushirikiano wao wa kidiplomasia, kisiasa na kiuchumi. Msingi muhimu wa sera

yetu ya mambo ya nje ni kuendeleza na kuhudumisha ujirani mwema. Nachukua fursa hii kuwahakikishia majirani zetu kuwa Tanzania itaendelea kuwa jirani mwema kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niruhusu nitumie nafasi hii kuwashukuru washirika wetu wa maendeleo kwa misaada na ushirikiano wao wanaoendelea kutupatia katika harakati zetu za kujiletea maendeleo nchini. Naomba nizitambue nchi wahisani na taasisi mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni Australia, Austria, Brazil, Canada, China, Denmark, Finland, Hungary, India, Indonesia, Ireland, Italia, Jamhuri ya Cuba, Jamhuri ya Czech, Japan, Korea Kusini, Kuwait, Marekani, Norway, Oman, Poland, Qatar, Saudi Arabia, Singapore, Spain, Sweden, Belgium, France, Uholanzi Uingereza, Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu, Urusi na Uswisi.

Mheshimiwa Spika, taasisi na mashirika ya Kimataifa tunayoshirikiana nayo kwa karibu ni pamoja na Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Kimataifa, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Kiuchumi kwa Afrika, Mfuko wa Abu Dhabi, Mfuko wa Kimataifa kusaidia Mapambano dhidi ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria, Mfuko wa *OPEC*, *OFID,* Mfuko wa Mazingira Duniani, *GEF, Adaptation Fund,* Mfuko wa *Geothermal Risk Mitigation,* Umoja wa Mataifa na mashirika yake yote yaliyopo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Umoja wa Ulaya, Shirikisho la *GAVI, Global Partnership for Education (GPE), Nutrition International,* Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo wa Kimataifa *(IFAD)* na Mfuko wa Saudia. Ni matarajio yetu kuwa kwa washirika wetu waliotuahidi rasilimali wanatimiza ahadi zao kwa ukamilifu na kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha Serikali itaendelea kuimarisha uwajibikaji, uwazi na nidhamu katika usimamizi wa matumizi ya rasilimali zitakazotolewa ili kuhakikisha upatikanaji wa thamani halisi ya fedha na kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitambue pia mchango na ushirikiano wa Asasi Zisizo za Kiserikali ikiwa ni pamoja na asasi za kiraia, mashirika yasiyo ya kiserikali, taasisi za fedha, sekta binafsi, mashirika ya kidini pamoja na taasisi za elimu ya juu na utafiti katika kuchangia maendeleo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nitumie fursa hii kuishukuru familia yangu kwa maombi na faraja inayoniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi na kwa weledi. Kwa namna maalum na ya kipekee ninamshukuru sana mke wangu kipenzi na rafiki wangu mkuu, Bi. Nassra Ibrahim Ali, watoto wetu; Hafidh na Ashura Khamis na wakwe zetu; Abrarah Said Bakran na Hassan Juma Amour. Ninawashukuru pia wajukuu; Nassra, Khamis, Said na Maryam kwa Hafidh na Abrarah na mapacha; Malik na Malaak na Nasreen na Nazeen kwa Ashura na Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shukrani zangu za dhati ni kwa faraja na moyo wanaonipa na kuniombea kwa Mwenyezi Mungu kila siku ili niweze kutekeleza kwa uaminifu na uadilifu dhamana niliyopewa ya kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hitimisho; kama nilivyoeleza hapo awali bajeti hii ni ya kwanza katika utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa ambao ni sehemu ya utekelezaji wa Dira 2050. Ili kufikia malengo yaliyoainishwa katika dira hiyo ni muhimu kwetu sote kujituma na kuwa na umoja na mshikamano wa kitaifa katika utekelezaji wa mipango na maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, wananchi sote hatuna budi kuchangamkia kikamilifu fursa zinazojitokeza kwa utekelezaji wa bajeti. Fursa kama vile nchi yetu kuwa mwenyeji wa mashindano ya *AFCON* ili kujiongezea kipato na hivyo kuboresha ustawi wa jamii. Mashindano haya ya *AFCON* yanaleta fursa adhimu hususan katika utoaji wa huduma za vyakula, malazi, usafiri na utalii. *(Makofi)*

Pia fursa kubwa zitakazojitokeza katika miradi mikubwa inayotarajiwa kuwekezwa nchini ikiwemo ya *LNG*, uchimbaji wa makaa ya mawe na chuma na uchakataji wake wa chuma cha

pua. Pia na sekta ya ujenzi, usafirishaji, madini, nishati na gesi. Tuzichangamkie ipasavyo fursa zote hizo na nyingine zinazojitokeza nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoainisha hapo awali, Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini ikiwemo maboresho ya mfumo wa kodi kwa lengo la kuvutia uwekezaji, kuhamasisha urasimishaji wa sekta isiyo rasmi na uanzishaji wa biashara mpya na hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Serikali itarahisisha malipo kwa kupunguza matumizi ya fedha taslimu ili kuhakikisha kuwa mageuzi haya yanajenga uchumi wa kisasa pasipo kuacha nyuma wananchi katika gurudumu la ujenzi wa uchumi wa kidijitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimalizie kwa kulishukuru kundi muhimu na maalum katika jamii yetu. Kwa moyo wa dhati kabisa ninawashukuru viongozi wote wa dini kwa mchango wao mkubwa wanauotoa katika kujenga na kudumisha amani, maadili na mshikamano wa kitaifa. Imani yetu ya kiroho ni msingi muhimu wa umoja wetu na maendeleo ya nchi yetu. Tunawashukuru sana viongozi wetu kwa sala na dua zao za kuiombea nchi yetu, viongozi na wananchi kwa ujumla. Kwa hakika sala na dua hizo zimeendelea kuimarisha umoja, utulivu na mafanikio ya Taifa letu. Ninawaomba wasichoke, waendelee kuliombea Taifa letu, hasa pale shetani anapotupa majaribu yake.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili kuidhinisha Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2026/2027. Mungu ibariki Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**11 JUNI, 2026**

# HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA, MHESHIMIWA BALOZI KHAMIS MUSSA OMAR (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAPENDEKEZO YA SERIKALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2026/27 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## I. UTANGULIZI

## I. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2026/27. Uwasilishaji wa bajeti hii umezingatia Ibara ya 137 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, ikisomwa pamoja na Kifungu cha 23(3) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni 127 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Agosti 2025.

2. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na hotuba hii, ninawasilisha vitabu vinne vinavyoelezea kwa kina takwimu za Bajeti ya Serikali. **Kitabu cha Kwanza (I)** kinahusu makadirio ya mapato yatakayowezesha utekelezaji wa shughuli za Serikali; **Kitabu cha Pili (II)** kinahusu makadirio ya matumizi ya kawaida kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala wa Serikali; **Kitabu cha Tatu (III)** ni makadirio ya matumizi ya kawaida kwa Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na **Kitabu cha Nne (IV)** kinahusu makadirio ya matumizi ya maendeleo kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Ofisi za Wakuu wa Mikoa pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

3. **Mheshimiwa Spika**, nawasilisha pia: Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2026; Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2026; Taarifa ya Bajeti yenye Mrengo wa Kijinsia; na Mkakati wa Usimamizi wa Vihatarishi Vinavyoweza Kuathiri Utekelezaji wa Bajeti itakayoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

4. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote ninatanguliza shukrani kwa Mola wetu Mwenyezi, Rahimu na Karimu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki vyema Mkutano wa Tatu wa Bunge la Kumi na Tatu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

5. **Mheshimiwa Spika**, sichoki kuwapongeza viongozi wetu wakuu kwa mafanikio makubwa wanayoendelea kuleta kwenye nchi yetu. Ninaungana na mawaziri wenzangu kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi kwa kuchaguliwa kwa kishindo katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake mahiri na moyo wa kizalendo katika kuwatumikia wananchi. Sote tumeendelea kushuhudia matokeo ya kazi kubwa anayoifanya ya kuleta maendeleo kwa nchi yetu kupitia kauli mbiu ya ***"Kazi na Utu…Tunasonga Mbele"***. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi wote kumuomba Mwenyezi Mungu aendelee kumjalia afya njema, hekima, maarifa na kumpa ulinzi zaidi Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuwatumikia watanzania.

6. **Mheshimiwa Spika**, ninampongeza pia Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa weledi wake katika kuendelea kumsaidia na kumshauri Mheshimiwa Rais kuongoza Taifa letu. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Hii ni uthibitisho wa kukubalika kwa uongozi wake mahiri na dhamira ya dhati ya kuendelea kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

7. **Mheshimiwa Spika**, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, kwanza, kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Iramba Magharibi, pili, kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na hatimaye kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninampongeza pia kwa kuendelea kuratibu na kusimamia shughuli za Serikali kwa weledi mkubwa.

8. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee na kwa mara nyingine, ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Mbunge na kunipa dhamana adhimu ya kumsaidia kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika nafasi ya Waziri wa Fedha. Hii ni imani na dhima kubwa kwangu. Njia pekee ya kuonesha kuwa ninaithamini ni kuitumikia kwa weledi, uaminifu na kwa maslahi ya Taifa letu. Nachukua ahadi mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa nitafanya hivyo kwa muda wote.

9. **Mheshimiwa Spika**, kwa moyo wa simanzi na huzuni kubwa ninatoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwako binafsi Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge pamoja na watanzania wote kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) na Mbunge wa Jimbo la Isimani; Mheshimiwa Jenista Joackim Mhagama, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho; na Mheshimiwa Halima Iddi Nassor, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum. Tutaendelea kuwakumbuka kwa michango yao na utumishi uliotukuka ndani ya Bunge lako Tukufu na nchi kwa ujumla.

10. **Mheshimiwa Spika**, ninatoa pole kwa waumini wa Kanisa Katoliki pamoja na ndugu jamaa na marafiki kwa kuondokewa na kiongozi wao mpendwa, Askofu Mkuu Mstaafu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo. Marehemu Kardinali Pengo atakumbukwa milele kwa mchango wake mkubwa alioutoa katika Taifa, hususan katika uwakilishi wake wa kiroho kwa Kanisa Katoliki, ndani na nje ya nchi.

11. ***Mheshimiwa Spika***, wapo watanzania wenzetu waliofikwa na majanga mbalimbali yaliyosababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali na miundombinu kutokana na ajali za barabarani, maradhi na athari za mabadiliko ya tabianchi. Ninawaombea marehemu wote pumziko la amani na uponaji wa haraka kwa majeruhi wote ili waweze kurejea katika shughuli zao. Aidha, ninatoa pole kwa watanzania wote waliopoteza ndugu, jamaa, marafiki na mali zao kutokana na majanga hayo. Tukiwa waja, tunapaswa kukumbuka kuwa **sisi sote ni waja wa Mungu na kwake tutarejea**. **Tujiandae!**

## I. TATHMINI YA HALI YA UCHUMI NA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2025/26

### Mwenendo wa Uchumi

12. **Mheshimiwa Spika**, hali ya uchumi wa nchi yetu imeendelea kuimarika na kuwa himilivu pamoja na changamoto mbalimbali zinazoendelea kujitokeza duniani. Pato ghafi la Taifa lilifikia shilingi trilioni 234.1 mwaka 2025, sawa na dola za Marekani bilioni 91.8. Aidha, Pato halisi la Taifa lilikua kwa asilimia 5.9 mwaka 2025. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 3.4 ikiwa ndani ya lengo la nchi la kati ya asilimia 3.0 hadi 5.0; na mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka kwa wastani wa asilimia 20.2 na hivyo kuchachua shughuli za uchumi. Hadi Aprili 2026, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani bilioni 5.72, kiasi kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi 4.4, ambayo inaendana na lengo la kuwa na akiba ya kutosheleza uagizaji wa angalau miezi minne (4). Vilevile, thamani ya shilingi dhidi ya sarafu za nchi washirika wakuu wa kibiashara iliendelea kuimarika, ambapo kwa mwaka unaoishia Aprili 2026 thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani iliongezeka kwa wastani wa asilimia 2.7.

13. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, matokeo ya awali ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi nchini (IHBS) wa mwaka 2025 yanaonesha kuwa, umaskini wa mahitaji ya msingi umepungua kufikia asilimia 25.1 ya watu nchini ikilinganishwa na asilimia 26.4 mwaka 2017/18. Aidha, kulingana na matokeo hayo, kaya maskini zilizonufaika kupitia programu ya uwezeshaji wa kaya masikini - TASAF zimepungua na kufikia asilimia 6.7 ya watu nchini mwaka 2025 kutoka asilimia 8.4 mwaka 2017/18. Pamoja na mafanikio haya, taarifa hizi pia zinaashiria kuwa bado tuna kazi kubwa mbele yetu ya kuendelea na mapambano dhidi ya adui umasikini. *Tathmini ya kina ya mwenendo wa viashiria vya uchumi jumla ni kama ilivyobainishwa katika Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2025.*

## Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali

14. **Mheshimiwa Spika**, Bunge lako Tukufu liliidhinishia Serikali Bajeti ya jumla ya shilingi trilioni 56.49 kwa mwaka 2025/26. Kati ya kiasi hicho, mapato ni shilingi trilioni 41.39, ikijumuisha misaada ya shilingi bilioni 925.1, pamoja na mikopo ya ndani na nje shilingi trilioni 15.10. Kwa upande mwingine, matumizi yanajumuisha: Mishahara na stahiki za watumishi shilingi trilioni 7.71; ununuzi wa bidhaa na huduma shilingi trilioni 7.81; malipo ya riba za mikopo na mitaji shilingi trilioni 14.21; ruzuku, michango, mafao, misaada ya kijamii na gharama nyingine shilingi trilioni 23.98; pamoja na uwekezaji wa mali zisizo za kifedha shilingi trilioni 2.78.

## Mapato

15. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Serikali ilifanikiwa kukusanya mapato (ikijumuisha misaada) ya jumla ya shilingi trilioni 34.75, sawa na asilimia 101.8 ya lengo la kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho: Mapato ya kodi yalifikia shilingi trilioni 28.10, sawa na asilimia 105.1 ya lengo; mapato mengine (mapato yasiyo ya kodi na mapato yanayokusanywa na halmashauri) shilingi trilioni 5.92, sawa na asilimia 89.5 ya lengo; na misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo shilingi bilioni 740.5, sawa na asilimia 96.1 ya lengo.

16. **Mheshimiwa Spika**, ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya kodi umetokana na kuongezeka kwa wigo wa vyanzo vya mapato ya kodi kutokana na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi na kuongezeka kwa kiwango cha uhiari wa kulipa kodi kufuatia hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali ikiwemo kuimarishwa kwa mifumo ya ukusanyaji mapato, utoaji wa elimu ya kodi kwa umma na mijadala ya pamoja kati ya Serikali na walipakodi.

17. **Mheshimiwa Spika**, natumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati watanzania wazalendo wanaotimiza wajibu wao wa kulipa kodi kwa hiari. Mwitikio huo mzuri umeendelea kuimarisha uwezo wa ndani wa Serikali kugharamia huduma muhimu za kijamii na kiuchumi nchini kwa zaidi ya asilimia 70.0.

**Matumizi**

18. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, jumla ya matumizi ya Serikali bila kujumuisha malipo ya mtaji wa deni yalikuwa shilingi trilioni 40.92, sawa na asilimia 98.8 ya lengo la kipindi hicho. Kiasi hicho kinajumuisha: Mishahara na stahiki za watumishi shilingi trilioni 7.02; malipo ya riba shilingi trilioni 5.09 na ununuzi wa bidhaa na huduma shilingi trilioni 7.02. Matumizi mengine ni ruzuku, michango, mafao, misaada ya kijamii na gharama nyingine shilingi trilioni 19.41 na uwekezaji katika mali zisizo za kifedha shilingi trilioni 2.38.

19. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imefanya matumizi mahsusi kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi na huduma mbalimbali ikiwemo:

(i) Shilingi trilioni 2.86 kwa ujenzi wa barabara, madaraja, na viwanja vya ndege;

(ii) Shilingi trilioni 1.59 kwa miradi ya kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme ikiwemo mradi wa Gridi ya Taifa. Serikali imekamilisha na kuzindua mradi wa kuzalisha umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere lenye uwezo wa kuzalisha umeme wa megawati 2,115 na hivyo kusababisha uwezo wetu wa kuzalisha umeme kufikia megawati 4,522.54. Aidha, kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Serikali imetumia shilingi bilioni 521.3 na hivyo kufanya jumla ya vitongoji vilivyofikiwa na umeme kuwa 39,003;

(iii) Shilingi trilioni 1.58 kwa uimarishaji wa vyuo vya VETA, kukuza ujuzi kwa vijana na ujenzi wa miundombinu ya elimu pamoja na mikopo ya wanafunzi 284,487 wa elimu ya juu, na ugharamiaji wa elimumsingi bila ada iliyonufaisha wanafunzi 16,838,013;

(iv) Shilingi trilioni 1.27 kwa ujenzi na ukarabati wa reli ikiwemo shilingi trilioni 1.12 kwa ujenzi wa reli kwa kiwango cha kimataifa (SGR), katika kipindi hiki ujenzi wa reli ya SGR kati

ya Dar es Salaam na Dodoma ulikamilika na huduma za usafiri na usafirishaji zilizinduliwa rasmi;

(v) Shilingi bilioni 870.4 kwa utekelezaji wa miradi ya maji mijini na vijijini ikiwemo uendelezaji wa mradi wa Gridi ya Taifa ya Maji na ujenzi wa mabwawa, likiwemo la Kidunda litakalonufaisha mikoa mitatu ya Morogoro, Pwani na Dar-es-Salaam;

(vi) Shilingi bilioni 681.7 kwa ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya afya;

(vii) Shilingi bilioni 667.3 kwa ulipaji wa madeni yaliyohakikiwa ya wazabuni na watoa huduma, wakandarasi na washauri elekezi hususan wa ndani ya nchi; na

(viii) Shilingi bilioni 302.0 kwa ujenzi wa miundombinu na viwanja vya michezo na ushiriki kwa ajili ya mashindano ya AFCON 2027.

20. **Mheshimiwa Spika**, uwekezaji katika maeneo hayo umeongeza: Upatikanaji wa nishati ya umeme; huduma za kijamii ikiwemo elimu, afya na maji; ukuaji wa shughuli nyingine za kiuchumi kama vile viwanda, biashara, madini, mawasiliano, usafiri na usafirishaji; pamoja na kuongeza fursa za ajira. Tathmini ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ni kama ilivyowasilishwa katika hotuba za wizara za kisekta.

**Kugharamia Nakisi ya Bajeti**

21. **Mheshimiwa Spika**, hadi Aprili 2026, Serikali ilikopa jumla ya shilingi trilioni 11.29 katika soko la ndani na nje, sawa na asilimia 89.5 ya lengo. Kati ya kiasi hicho, mikopo ya ndani ilikuwa shilingi trilioni 5.08, ambapo shilingi trilioni 2.55 zilitumika kulipa hati fungani zilizoiva na shilingi trilioni 2.53 zilitumika kugharamia miradi ya maendeleo. Aidha, mikopo ya nje ilikuwa jumla ya shilingi trilioni 6.20, ambapo kati ya kiasi hicho, mikopo nafuu ilikuwa shilingi

trilioni 4.61 na mikopo yenye masharti ya kibiashara shilingi trilioni 1.59.

**Deni la Serikali**

22. **Mheshimiwa Spika**, hadi Machi 2026, Deni la Serikali lilifikia shilingi trilioni 114.34. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani lilikuwa shilingi trilioni 38.45, sawa na asilimia 33.6 na deni la nje lilikuwa shilingi trilioni 75.89 (asilimia 66.4). Deni hilo limetokana na mikopo iliyoelekezwa katika maeneo ya kimkakati yanayochochea ukuaji wa uchumi, ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji, nishati na mawasiliano.

23. **Mheshimiwa Spika**, tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanywa Novemba 2025 imeonesha kuwa deni ni himilivu katika kipindi cha muda wa kati na mrefu. Thamani ya sasa ya deni la Serikali kwa Pato la Taifa ni asilimia 39.6 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55; deni la nje kwa Pato la Taifa ni asilimia 24.4 dhidi ya ukomo wa asilimia 40; na deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 123.1 dhidi ya ukomo wa asilimia 180. Hii inaonesha kuwa nchi yetu ina uwezo mzuri wa kusimamia na kuhimili deni lake bila kuathiri uthabiti wa misingi ya uchumi.

24. **Mheshimiwa Spika**, sambamba na mafanikio hayo, kampuni kubwa za kimataifa za **Moody's** na **Fitch Ratings** zilifanya tathmini ya awamu ya kwanza ya uwezo wa nchi kukopa na kulipa madeni kwa mwaka 2026. Matokeo ya tathmini yalionesha kuwa Tanzania inakopesheka na ina uwezo mzuri wa kulipa madeni yake. Matokeo hayo yanatokana na ukuaji mzuri wa uchumi, utekelezaji wa mageuzi ya kimuundo yanayoboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, pamoja na nidhamu ya matumizi ya fedha za umma na ongezeko la mapato ya Serikali.

25. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na kuimarishwa kwa usimamizi wa deni la Serikali, Tanzania imeibuka mshindi wa jumla katika Tuzo ya Usimamizi wa Deni la Serikali katika nchi za Jumuiya ya Madola. Mafanikio haya yanatokana na maboresho ya kimfumo yaliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Jemedari wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, ikiwemo kuhakikisha matumizi sahihi ya mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kupitia Bunge lako Tukufu, ninapenda kuwahakikishia watanzania kuwa Serikali itaendelea kulinda uthabiti wa deni la Serikali na kudhibiti gharama za ukopaji kwa: Kuendeleza mageuzi ya uchumi; kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani; kutoa kipaumbele kwa mikopo yenye masharti nafuu; na kuongeza uzalishaji na thamani ya bidhaa za ndani ili kuongeza mauzo nje na hivyo kuongeza fedha za kigeni.

**II. MASUALA MTAMBUKA**
**Athari za Migogoro ya Kimataifa**

26. **Mheshimiwa Spika**, uchumi wa dunia umekuwa ukipitia vipindi tofauti vya misukosuko ikiwemo janga la UVIKO – 19; mgogoro wa Urusi na Ukraini; mgogoro wa ushuru na biashara baina ya Marekani na mataifa mengine hususan China; na hivi karibuni mgogoro unaoendelea baina ya Marekani, Israeli na Iran ulioanza mwishoni mwa Februari 2026.

27. **Mheshimiwa Spika**, Tanzania ni sehemu ya uchumi wa dunia hususan kupitia biashara za kimataifa na uwekezaji na hivyo uwepo wa misukosuko na vita hivyo umeathiri sekta za kiuchumi na kijamii nchini. Mathalani, katika jiji la Dar es Salaam bei ya mafuta ya petroli na dizeli zimeongezeka sanjari kwa asilimia 44 na 49 kati ya Machi na Mei 2026. Katika kipindi hicho, bei ya mbolea iliyoingizwa nchini nayo imeongezeka kwa asilimia 4 hadi asilimia 46 kulingana na aina ya mbolea. Tanzania hutegemea mbolea kutoka nje ya nchi kwa zaidi ya asilimia 80 ambapo asilimia 70 ya mbolea hiyo huagizwa kutoka nchi za Mashariki ya Kati.

28. **Mheshimiwa Spika**, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imeendelea kuifuatilia kwa makini hali hii na kuchukua hatua madhubuti kukabiliana na changamoto hizi ili kulinda ustawi wa wananchi na uthabiti wa uchumi wetu. Kwanza, Serikali imehakikisha uwepo wa kuaminika wa mafuta nchini kwa kuagiza mafuta kwa kiwango toshelevu na kwa wakati. Pili, Serikali inaendelea kusimamia kwa karibu mwenendo

wa bei za mafuta kupitia mamlaka husika, na imechukua hatua za kupunguza makali ya ongezeko hilo, ikiwemo kutoa ruzuku ya shilingi 259 na shilingi 535 kwa lita ya dizeli kwa mwezi Mei na Juni 2026 mtawalia. Tatu, kuimarisha usimamizi wa sera ya fedha na sera ya bajeti ili kudhibiti mfumuko wa bei kwa kushirikiana na taasisi za fedha na wadau wa sekta binafsi. Lengo ni kuhakikisha utulivu wa bei za bidhaa muhimu kwa wananchi.

29. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha muda wa kati, Serikali itaongeza kasi ya utekelezaji wa mradi wa hifadhi ya kimkakati ya mafuta (*Strategic Petroleum Reserve - SPR*) ili kuwezesha kuwa na akiba ya kutosha ya mafuta wakati wa migogoro ya kisiasa, kiuchumi na mabadiliko ya ghafla ya bei katika masoko ya mafuta duniani. Vilevile, Serikali itaongeza kasi ya uwekezaji katika nishati mbadala, ikiwemo gesi asilia na nishati jadidifu ili kupunguza utegemezi wa mafuta kutoka nje ya nchi.

30. **Mheshimiwa Spika**, katika sekta ya kilimo, Serikali inahamasisha: Uagizaji na matumizi ya mbolea mbadala za kukuzia zenye bei himilivu sokoni kama vile CAN na SA; kutekeleza mpango maalum wa ruzuku kwa wazalishaji wa ndani; na kuongeza matumizi ya mbolea za asili na za kimiminika ambazo hazina ruzuku. Aidha, Serikali itaendelea kulipa madai ya ruzuku ili kufanikisha upatikanaji wa mbolea kwa msimu wa 2026/27. Vilevile, Serikali inaendelea kuhamasisha na kuwezesha uzalishaji wa ndani katika sekta mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kupunguza utegemezi wa bidhaa za nje ambazo gharama zake zimeathiriwa na hali ya uchumi wa dunia.

**Mabadiliko ya Tabianchi**

31. **Mheshimiwa Spika**, nchi yetu nayo imeendelea kushuhudia athari za moja kwa moja za mabadiliko ya tabianchi. Hali hii inaathiri sekta muhimu za uchumi hususan kilimo, maji, afya, uchukuzi na nishati. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo matumizi ya utaratibu wa dharura (*Contingent Emergency Response Component - CERC*) chini ya Benki ya Dunia kwa ajili ya

kukabiliana na athari za majanga yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi. Kupitia utaratibu huo, Serikali imepokea jumla ya dola za Marekani milioni 320 katika kipindi cha mwaka 2024/25 hadi 2025/26 ili kuboresha na kurejesha miundombinu muhimu iliyoharibika kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa masuala ya mabadiliko ya tabianchi yanazingatiwa kikamilifu katika mipango na bajeti.

32. **Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea kutoa motisha katika matumizi ya nishati safi ikiwemo ujenzi wa miundombinu wezeshi kwa ajili ya matumizi katika shughuli mbalimbali ikiwemo kupikia, viwandani pamoja na usafiri na usafirishaji. Lengo ni kuhakikisha uwepo wa nishati salama na endelevu, kuokoa muda, kupunguza gharama pamoja na athari za kimazingira na kiafya kwa watumiaji.

**Jinsia na Ustawi wa Jamii**

33. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kuimarisha upangaji na utekelezaji wa bajeti kwa kuzingatia mahitaji halisi ya wananchi wote. Katika hatua hiyo, Serikali imeanza utekelezaji wa mfumo wa Bajeti yenye Mrengo wa Kijinsia (*Gender Responsive Budgeting – GRB*). Lengo ni kuhakikisha kuwa wanawake na wanaume, wasichana na wavulana pamoja na watu wenye mahitaji maalumu wananufaika kwa usawa na rasilimali pamoja na huduma zinazotolewa na Serikali katika kuleta maendeleo jumuishi na endelevu. *Taarifa kuhusu Bajeti yenye Mrengo wa Kijinsia kwa Mwaka 2026/27 kwa wizara tisa (9), mikoa miwili (2) na halmashauri mbili (2) imeambatishwa.*

34. **Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua umuhimu wa dhana ya ukuaji jumuishi wa uchumi, Serikali ya CCM inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeendelea kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kutoa mikopo kwa makundi mbalimbali ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu. Hadi Aprili 2026, Serikali imetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 135.8 kwa vikundi 13,062 kupitia mikopo itokanayo na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri.

35. **Mheshimiwa Spika**, Serikali pia imeanzisha Mfuko wa Machinga wa kuwezesha wafanyabiashara ndogo ndogo maarufu kama machinga, ambapo shilingi bilioni 18.5 zinaendelea kutumika kukopesha wafanyabiashara hao kwa mwaka 2025/26. Ili kuendelea kuimarisha Mfuko huo, shilingi bilioni 10.5 zitaongezwa kwa mwaka 2026/27. Aidha, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 200 kwa ajili ya Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi ambapo hadi Aprili 2026, shilingi bilioni 52.6 zimetolewa kwa ajili ya mikopo ya vijana walioko katika sekta mbalimbali waliokidhi vigezo.

36. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2025/26, Serikali imezindua Kituo cha Usaidizi wa Upatikanaji wa Vifaa/Bidhaa na Mauzo ya Nje. Kituo hiki kinatoa huduma kwa wajasiriamali wadogo na vijana, pamoja na wawekezaji wanaohitaji msaada katika kukuza shughuli za biashara na uwekezaji. Aidha, Kituo kinalenga kuwezesha upatikanaji wa mitaji, masoko ya nje kwa bidhaa zinazozalishwa nchini, kurahisisha usafirishaji wa mizigo kuingia na kutoka nchini, pamoja na kuwezesha upatikanaji wa malighafi, mashine na vifaa muhimu.

37. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, Serikali imeendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003, Toleo la 2024, inayolenga kuimarisha huduma za matunzo, afya na hifadhi ya jamii kwa wazee. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Serikali iligharamia huduma za matunzo kwa wazee na wasiojiweza katika makazi ya wazee yanayosimamiwa na Serikali, sambamba na kuwezesha upatikanaji wa bima ya afya na huduma za msamaha wa matibabu kwa wazee zenye thamani ya shilingi bilioni 3.2. Aidha, Serikali imeendelea kutambua na kuwajumuisha wazee katika Mpango wa Uwezeshaji wa Kaya Masikini (TASAF).

**Uendelezaji wa Makao Makuu Dodoma**

38. **Mheshimiwa Spika**, kupitia Amri ya Rais (*Presidential Decree*) Na. 320 ya mwaka 1973, Dodoma ilitangazwa kuwa makao makuu ya Taifa la Tanzania wakati wa awamu ya kwanza ya Serikali chini ya uongozi wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius

Kambarage Nyerere. Aidha, mwezi Februari 2026, tumetimiza miaka 30 tangu Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhamia Dodoma na hivyo kuwa Mhimili wa kwanza kuhamia rasmi makao Makuu. Naomba nitumie fursa hii kulipongeza Bunge kupitia kwako Mheshimiwa Spika.

39. **Mheshimiwa Spika**, Mhimili wa Serikali ulihamia rasmi Dodoma mwaka 2017 wakati wa Serikali ya Awamu ya Tano iliyoongozwa na Hayati Dkt. John Joseph Pombe Magufuli. Kupitia kaulimbiu ya **"Kazi iendelee"**, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendeleza kwa kasi zaidi ujenzi wa Dodoma kama makao makuu ya Taifa. Kwa sasa, mihimili yote ya Dola imeshahamia Dodoma ambapo Mhimili wa Mahakama ukiwa na jengo la kisasa na mfano barani Afrika wakati mji wa Serikali Mtumba ukiendelea kujengeka kwa hadhi ya kipekee. Vilevile, Ikulu ya Chamwino nayo imekamilika na kuendelea kutekeleza kazi zake za kuwa kituo kikuu cha uongozi wa Taifa letu. **Hakika hii sasa ni Dodoma, Mji Mkuu unaoibukia vyema na sio tena mji uliozama, Idodomya!**

40. **Mheshimiwa Spika**, ni wajibu wetu Serikali, sekta binafsi na hata ofisi za balozi na mashirika ya kimataifa, ni kuendelea kuijenga Dodoma kuwa mji mkuu wa kisasa wa karne ya 21 kwa Taifa linalojiamini na lenye matumaini makubwa. Badala ya kuwa makao makuu ya utawala wa nchi, Dodoma itaendelezwa kuwa alama muhimu ya maendeleo ya kiuchumi, kitovu cha usafiri na usafirishaji kwa Tanzania na nchi jirani, na mfano wa maendeleo kwa mikoa na majiji mengine nchini. Reli ya SGR na kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Msalato vinatoa fursa muhimu ya kuharakisha kufikiwa ndoto hizo.

**III. BAJETI YA MWAKA 2026/27**

41. **Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya mwaka 2026/27 ni ya kwanza katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Bajeti hii imeandaliwa kwa kuzingatia miongozo ya kitaifa, kikanda na kimataifa ikiwemo: Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27 - 2030/31); Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2025; Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2050; Ajenda ya Maendeleo ya

Afrika 2063; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; pamoja na nyaraka, miongozo na makubaliano mengine ya kikanda na kimataifa ambayo Tanzania imeridhia.

42. **Mheshimiwa Spika**, bajeti hii pia imezingatia Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa tarehe 14 Novemba 2025 wakati wa kufungua rasmi Bunge la 13. Miongoni mwa maeneo mahsusi yaliyozingatiwa ni: Kujenga uchumi imara, shindani na jumuishi; kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji; kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kimkakati; kuimarisha matumizi ya TEHAMA; kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, uvuvi, mifugo na madini yanayozalishwa nchini; kujenga uchumi unaozalisha fursa zaidi za ajira na maendeleo kwa vijana, wanawake na makundi mbalimbali ya jamii; kuongeza ufanisi katika matumizi ya rasilimali za umma; na kufanya mageuzi ya mashirika ya umma ili kuboresha ufanisi, uwazi na tija.

43. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na mambo mengine, bajeti hii inawasilisha mapendekezo ya hatua mpya za kisera za mapato na matumizi kwa mwaka 2026/27. Hatua hizo zinalenga kuchochea ukuaji wa uchumi (***pro-growth***), kuvutia uwekezaji, kulinda na kuimarisha sekta ya viwanda nchini (***pro-investment and industrialization***), kuongeza ukusanyaji wa mapato ili kujitegemea katika ugharamiaji wa sehemu kubwa ya Bajeti ya Serikali (***fiscal sovereignity***), na kuimarisha nidhamu ya matumizi ya Fedha za Serikali na umma kwa ujumla (***fiscal discipline***).

**Dhima na Vipaumbele vya Bajeti kwa Mwaka 2026/27**

44. **Mheshimiwa Spika**, tunaandaa na kuidhinisha mipango na bajeti kwa ajili ya ustawi wa watanzania kiuchumi na kijamii. Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 imeonesha kuwa takriban theluthi mbili (asilimia 65.1) ya watanzania wanaishi vijijini. Aidha, takriban idadi kama hiyo ya theluthi mbili ni watoto na vijana. Vilevile, baadhi ya majiji kama Dar es Salaam yanaendelea kupokea wakazi wengi zaidi na baadhi ya mikoa imebaki nyuma kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Hali hii inaashiria haja ya kuendelea kuwekeza katika: (i) Uhuishaji na maendeleo vijijini

(*rural revitalization and development*); (ii) mageuzi ya kilimo; (iii) uwekezaji wa maendeleo ya watu kupitia huduma bora za jamii; na (iv) hatua maalumu za kuinua kiuchumi mikoa iliyo nyuma zaidi.

45. **Mheshimiwa Spika**, bajeti ya mwaka 2026/27 ina dhima ya "***Kujenga uchumi himilivu kupitia mageuzi ya kidijitali, uwekezaji wa kimkakati na sera endelevu za kibajeti kwa ukuaji jumuishi wa uchumi***". Dhima hii imeandaliwa kwa kuzingatia maeneo matano (5) ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27. Maeneo hayo ni: (i) Utawala, amani, usalama na utulivu; (ii) uchumi imara, jumuishi na shindani; (iii) uwezo wa watu na maendeleo ya kijamii; (iv) uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi; na (v) sekta za vichocheo vya kimageuzi.

46. **Mheshimiwa Spika**, baadhi ya maeneo mahsusi katika bajeti ya mwaka 2026/27 ni: (a) Kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuibua vyanzo vipya, kuimarisha mifumo ya TEHAMA na hatua za kiutawala; (b) kukamilisha miradi na programu za maendeleo zinazoendelea; (c) kuendelea kuimarisha sekta za uzalishaji; (d) kuendelea kuimarisha huduma za jamii; (e) kuendelea kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini. Aidha, miradi mahsusi ya maendeleo itakayotekelezwa na Serikali katika bajeti ya mwaka 2026/27 imeainishwa kwa kina katika *Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27*.

**Shabaha na Misingi ya Uchumi Jumla**

47. **Mheshimiwa Spika**, maendeleo yanategemea ukuaji wa uchumi na namna unavyowanufaisha wananchi walio wengi. Shabaha za uchumi jumla kwa mwaka 2026/27 ni kama ifuatavyo:

(i) Ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 6.3 mwaka 2026 kutoka ukuaji halisi wa asilimia 5.9 mwaka 2025;

(ii) Mfumuko wa bei kubaki ndani ya wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0 katika muda wa kati;

(iii) Mapato ya ndani kufikia asilimia 17.1 ya Pato la Taifa mwaka 2026/27 kutoka makadirio ya asilimia 16.5 mwaka 2025/26;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.7 ya Pato la Taifa mwaka 2026/27 kutoka makadirio ya asilimia 13.2 mwaka 2025/26;

(v) Nakisi ya bajeti isiyozidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa mwaka 2026/27; na

(vi) Akiba ya fedha za kigeni kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

48. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na shabaha hizo za uchumi jumla, Serikali itaendeleza kwa haraka zaidi uwekezaji wa kimkakati na ujenzi wa uchumi mkubwa na wa kisasa kupitia viwanda vinavyotegemea sekta ya madini na nishati hususan madini adimu, gesi asilia, chuma na makaa ya mawe. Aidha, Serikali itaendeleza matumizi ya fursa ya kijiografia kwa kutekeleza mradi wa kuhuisha reli ya TAZARA na kuendeleza ujenzi wa reli ya SGR kutoka Dodoma hadi Mwanza na Isaka hadi Kigoma. Reli hizi pia zinatoa fursa maalum ya kuendeleza kiuchumi mikoa ambayo reli zinapita, mitano kwa TAZARA na minane kwa SGR.

49. **Mheshimiwa Spika**, uandaaji wa shabaha za uchumi jumla kwa mwaka 2026/27 umezingatia misingi ifuatayo: Kuelekea kwenye kujitegemea kwa mapato kwa kuhakikisha utekelezaji thabiti wa Mkakati wa Ukusanyaji Mapato wa Muda wa Kati - MTRS (2025/26 – 2027/28); kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji na biashara; kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili na yasiyo ya asili ikiwemo ukame, tetemeko la ardhi, magonjwa ya mlipuko, mafuriko na migogoro ya kivita na kibiashara; utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa; kuendelea kuimarika kwa upatikanaji na usalama wa chakula nchini; na uwepo wa amani, usalama, umoja na utulivu wa ndani na nchi jirani.

## Mikakati ya Kuongeza Mapato

50. **Mheshimiwa Spika**, takwimu za miaka ya karibuni zinaonesha kuwa misaada kutoka nje (*Official Development Assistance - ODA*) imeendelea kupungua mwaka hadi mwaka na hivyo haiwezi kuwa chanzo cha kuaminika cha mapato katika utekelezaji wa Bajeti. Aidha, utekelezaji wa miradi kwa fedha za mikopo nao umeendelea kuleta changamoto kwa kuzingatia uhimilivu wa deni, gharama za mikopo, na athari yake kwa uhuru wetu. Hali hii inasababisha uhitaji wa kuongeza kasi yetu kwenye kujitegemea kiuchumi na mapato. Serikali itachukua hatua zaidi za kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuziba mianya ya upotevu na kuimarisha taasisi za ukusanyaji.

51. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2026/27, Serikali kupitia utekelezaji wa Mkakati wa Ukusanyaji Mapato wa Muda wa Kati 2025/26 – 2027/28, itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha ukusanyaji wa mapato ikiwemo:

(i) Kuvutia uwekezaji zaidi wa ndani na nje kwa azma ya kutanua wigo wa kodi na kuongeza fursa za ajira;

(ii) Kuhamasisha ulipaji kodi wa hiari kwa kuimarisha mahusiano baina ya Serikali na walipakodi kupitia majadiliano kwenye majukwaa mbalimbali ikiwemo Baraza la Taifa la Biashara na *CEOs Round Table;*

(iii) Kuendelea kusimamia na kuhimiza matumizi sahihi ya mashine za kutolea risiti za kielektroniki (EFD) kupitia utoaji wa elimu na uendeshaji wa programu mbalimbali za hamasa;

(iv) Kuendelea kujenga na kuboresha mifumo ya TEHAMA ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya ndani, kutumia teknolojia ya kisasa ya Akili Unde – AI na matumizi ya taarifa (Big Data) na kuhakikisha mifumo yote inabadilishana taarifa;

(v) Kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa taasisi za umma ili kuhakikisha zinaongeza

(vi) Tija katika ukusanyaji wa maduhuli pamoja na kuhakikisha zinawasilisha gawio na michango stahiki kwa wakati katika Mfuko Mkuu wa Serikali;

(vii) Kuhakikisha bidhaa zote zinazozalishwa nchini, zinazoagizwa na kuuzwa ndani na nje ya nchi zinakuwa na msimbopau (barcode); na

(viii) Kuendelea kufanya uchambuzi wa kina na kuanza utekelezaji wa baadhi ya mapendekezo 284 yaliyotolewa na Tume ya Rais ya Maboresho ya Mfumo wa Kodi.

52. **Mheshimiwa Spika**, sambamba na mikakati hiyo, Serikali inakusudia kuanzisha programu ya Tuzo ya Uzalendo kupitia Mfumo wa Usimamizi wa Risiti za Kielektroniki itakayozinduliwa Julai 2026. Lengo ni kuhamasisha tabia ya wananchi kudai risiti stahiki pindi wanapofanya ununuzi, na wafanyabiashara kutoa risiti kwa hiari pale wanapofanya mauzo. Tuzo au zawadi hizo zitatolewa kwa mtindo wa bahati nasibu ambapo zawadi mbalimbali zitatolewa kwa kuchezesha droo ili kuwapata washindi waliotoa na waliodai risiti kwa kipindi husika.

**Mazingira ya Uwekezaji na Biashara**

53. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kutambua mchango mkubwa wa sekta binafsi kama nguzo muhimu ya ukuaji wa uchumi, uzalishaji wa ajira na utekelezaji wa miradi ya maendeleo nchini. Kupitia utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI I), Serikali imefanya maboresho katika sheria 55 ambapo pamoja na mambo mengine ada na tozo 374 zimepunguzwa au kufutwa. Hatua hii imechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza gharama za kufanya biashara, kuimarisha mazingira ya uwekezaji pamoja na kuongeza usajili wa biashara na uwekezaji nchini. Mathalani, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje uliongezeka kufikia dola za Marekani bilioni 21.7 mwaka 2024 kutoka dola za Marekani bilioni 14.1 mwaka 2018. Aidha, Serikali itaendelea kuwianisha tozo na ada mbalimbali zinazotozwa na taasisi na mamlaka mbalimbali za Serikali kwa lengo la kuzipunguza na kurahisisha ulipaji wake kupitia MKUMBI II ambayo ipo katika hatua za mwisho za ukamilishaji.

54. **Mheshimiwa Spika**, Serikali pia inaendelea kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi pamoja na kuimarisha ushirikiano na taasisi za fedha za ndani, kikanda na kimataifa ikiwemo benki za biashara, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Shirika la Kimataifa la Fedha kwa Sekta Binafsi (*International Finance Corporation - IFC*), Shirika la Fedha la Afrika (*Africa Finance Corporation - AFC*), Africa50 na Benki ya Uwekezaji wa Miundombinu ya Asia (*Asia Infrastructure Investment Bank - AIIB*) ili kuongeza fursa za upatikanaji wa mitaji, dhamana, utaalamu na teknolojia kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo nchini.

55. **Mheshimiwa Spika**, katika hatua za kuboresha upatikanaji wa mitaji na mikopo nafuu, Serikali imeanza mchakato wa kurasimisha Mifuko ya Dhamana ya Serikali iliyokuwa chini ya usimamizi wa Benki Kuu na kuanzisha Kampuni itakayosimamia mifuko hiyo. Kampuni hiyo itasaidia kuimarisha usimamizi na upatikanaji wa dhamana kwa wafanyabiashara wanaozalisha ndani ya nchi na kuuza katika masoko ya nje.

56. **Mheshimiwa Spika**, Serikali itaanzisha kituo cha fedha cha kimataifa nchini kitakachojulikana kama *Dar es Salaam International Financial Centre* (DIFC) kwa lengo la kuvutia mitaji kutoka nje ya nchi. Lengo la hatua hii ni kuendelea kuchochea ukuaji wa sekta mbalimbali nchini pamoja na kukuza mitaji.

**Urasimishaji wa Sekta Isiyo Rasmi**

57. **Mheshimiwa Spika**, mwaka 2026/27, Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia urasimishaji wa sekta isiyo rasmi ili kuongeza upatikanaji wa masoko na uwezo wa wafanyabiashara kupata huduma za kifedha hususan mikopo na bima pamoja na kuzalisha fursa za ajira hasa kwa vijana ikiwemo kupitia kujenga ujuzi na mafunzo ya amali (VETA). Katika kufanikisha azma hiyo, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kutenga na kuendeleza maeneo maalum ya uzalishaji na biashara (*Business Clusters/Centres*) kwa wajasiriamali wadogo na wa

kati, kwa kuyaunganisha na miundombinu muhimu kama vile TEHAMA, maji, umeme na barabara;

(ii) Kutoa mikopo, mafunzo ya ufundi stadi na huduma za kisheria kwa wajasiriamali wadogo na wa kati kama motisha ya kuhamasisha urasimishaji wa shughuli za kiuchumi;

(iii) Mamlaka ya Mapato Tanzania kuendelea kutoa huduma ya elimu ya kodi na uendeshaji wa biashara kupitia Dawati la Kuwezesha Biashara;

(iv) Kuratibu taasisi za udhibiti ili zifanye kaguzi za pamoja katika baadhi ya maeneo ya biashara na hivyo kuondoa usumbufu kwa wafanyabiashara bila kuathiri majukumu ya msingi ya taasisi hizo; na

(v) Kuendelea kusajili na kutoa kitambulisho kimoja kwa wafanyabiashara ndogo ndogo (machinga) kilichounganishwa na mifumo mingine ikiwemo Kitambulisho cha Taifa kwa ajili ya utambuzi na kupunguza utitiri wa vitambulisho.

**Huduma Jumuishi za Fedha**

58. **Mheshimiwa Spika**, katika hatua ya kuongeza huduma jumuishi za fedha nchini, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ikiwemo kutunga Kanuni za Benki na Taasisi za fedha za mwaka 2025 ili kuwezesha benki na taasisi za fedha zisizotoza riba kutoa huduma za fedha kwa kuzingatia misingi ya sharia. Aidha, Benki Kuu ya Tanzania imefanya maboresho ya kanuni za kumlinda mlaji za mwaka 2019 kwa: Kuongeza muda wa akaunti kulala kutoka miezi mitano (5) hadi miezi 12; kuzuia makato ya mwezi kwa akaunti zisizotumika; na kuzuia makato na adhabu kwa malipo yaliyochelewa pamoja na kupanda kwa riba pasipo makubaliano ya mteja.

## Kupunguza Matumizi ya Fedha Taslimu

59. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuimarisha ufanisi wa mifumo ya malipo, kuongeza usalama pamoja na kuwezesha mwingiliano wa mifumo ya malipo. Katika kipindi cha mwaka 2025/26, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania imeboresha mfumo wa malipo ya papo kwa hapo (*Tanzania Instant Payment Systems - TIPS*) na kufanikiwa kuongeza huduma mbalimbali kufanyika kupitia mfumo huo ikiwemo malipo ya Serikali kupitia benki na mitandao ya simu pamoja na malipo ya wafanyabiashara kupitia msimbomilia (*QR Code*). Aidha, mfumo wa TIPS umeboreshwa na kuwezesha miamala ya uhamisho wa fedha kutoka nje ya nchi.

60. **Mheshimiwa Spika**, jitihada hizo zimechangia ongezeko la matumizi ya huduma za fedha kwa njia za kidijitali ambapo kwa mwaka 2025 miamala katika mfumo wa TIPS ilikuwa milioni 651 yenye thamani ya shilingi trilioni 54.95 ikilinganishwa na miamala milioni 453 mwaka 2024 iliyokuwa na thamani ya shilingi trilioni 29.82.

61. **Mheshimiwa Spika**, maboresho katika mifumo ya malipo yatachangia katika juhudi za Serikali za kupunguza matumizi ya fedha taslimu katika uchumi ili kuleta ufanisi wa miamala na kuzuia vitendo vya uhalifu pamoja na gharama zisizo za lazima ikiwemo: Utakatishaji fedha; kupunguza gharama za kutunza, kusafirisha na kuchapisha fedha; pamoja na kurahisisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Hivyo, kuanzia mwaka 2026/27, ninaelekeza malipo yote katika maeneo yafuatayo yafanyike kwa njia ya kidijitali:

(i) Tozo, ushuru na nauli za mabasi ya mwendokasi, vivuko, madaraja, mabasi yaendayo masafa marefu, taxi mtandao, usafiri wa anga na reli pamoja na maeneo ya maegesho;

(ii) Biashara zinazofanyika kwenye majengo makubwa ya biashara (*shopping malls)*, maeneo ya mazoezi (*Gyms*), vituo vya kuonesha sinema, vituo vya mafuta, uuzaji na ununuzi wa magari, kumbi za mikutano na sherehe, viwanja vya

michezo pamoja na maeneo ya maonesho ya biashara ya kimataifa kama vile SabaSaba na Nane Nane;

(iii) Ada na michango yote ya huduma za elimu kuanzia shule za awali, shule za msingi, sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu;

(iv) Gharama za malazi, chakula na vinywaji katika hoteli, migahawa na huduma zote zinazohusiana na utalii;

(v) Biashara ya upangishaji na ununuzi wa majengo, viwanja na mashamba; na

(vi) Shughuli za sekta ya kilimo zinazotekelezwa kupitia vyama vikuu vya ushirika na AMCOS katika mazao ya kimkakati (pamba, korosho, kahawa, chai, katani na tumbaku pamoja na pembejeo na viuatilifu).

62. **Mheshimiwa Spika**, sambamba na hatua hizo, Serikali pia kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania - TCRA itaondoa vocha za simu za kukwangua kwa mkono ambapo zoezi hili litaanza katika maeneo yote ya mijini. Hatua hii itasaidia kujifunza kabla ya kutekeleza pendekezo hili kwa maeneo mengine ya nchi.

63. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya fedha itaendelea kuimarisha miundombinu itakayowezesha malipo kufanyika kwa njia za kidijitali ikiwemo kuongeza kasi ya utoaji wa nyenzo za malipo ya kidijitali (LIPA NAMBA, QR Codes) kwa wafanyabiashara wadogo (boda boda na baba/mama lishe, masoko ya wazi). Aidha, wafanyabiashara wanaotumia njia za kidijitali kupokea malipo watapata sifa za ziada wakati wa kuomba mikopo inayotolewa na Serikali pamoja na watoa huduma za fedha. Pamoja na hatua hizi, Serikali pia inasisitiza masuala yafuatayo:

(i) Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kuanza utekelezaji wa programu ya Jamii Namba kama ilivyoelekezwa katika Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali nchini (*Tanzania Digital Economy Strategic Framework 20242034*) kwa lengo la kuongeza uwazi na utambuzi wa taarifa mbalimbali; na

(ii) Taasisi zinazotoa vibali kuweka sharti la kufungua akaunti ya benki kama moja ya vigezo vya utoaji wa leseni kwa wafanyabiashara wanaoshiriki katika shughuli za madini, mifugo, mazao, mbao na uvuvi na kuhakikisha miamala inafanyika kupitia akaunti husika.

64. **Mheshimiwa Spika**, kuanzia mwaka 2026/27, Serikali itaweka sharti la uthibitisho wa malipo ya kidijitali kuwa rejea ya lazima itakayotumika kuidhinisha maombi ya uhamishaji wa mali kama vile ardhi, majengo na magari. Hivyo, taasisi zote za umma, kama vile Mamlaka ya Mapato Tanzania, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, BRELA na nyingine zitalazimika kupokea uthibitisho wa kidijitali kuidhinisha uhamishaji wa mali. Hatua hii itaanza tarehe 1 Julai 2026.

**Usimamizi wa Matumizi ya Fedha za Umma**

65. **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2024/25, taasisi 555 kati ya 562, sawa na asilimia 98.8 za Serikali Kuu zilipata hati safi. Kwa upande wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, jumla ya taasisi 219 kati ya 221, sawa na asilimia 99.1 zilipata hati safi. Haya ni mafanikio ya kujivunia yakiashiria: Ujenzi na kuimarika kwa mifumo ya usimamizi wa fedha za umma; ubora wa taarifa za kifedha; nidhamu ya matumizi ya fedha; na kuongezeka kwa uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma.

66. **Mheshimiwa Spika**, licha ya mafanikio hayo, bado taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaonesha kuwa bado kuna changamoto baadhi ya maeneo katika usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Miongoni mwa changamoto hizo ni: Matumizi ya fedha yaliyofanyika pasipo kufuata taratibu; ukiukwaji wa taratibu za zabuni; kuchelewa kukamilika kwa miradi; na kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa miradi.

67. **Mheshimiwa Spika**, kama sehemu ya kuimarisha nidhamu katika usimamizi wa fedha za umma, Serikali ya Awamu ya Sita imedhamiria kuendeleza maboresho katika usimamizi wa matumizi kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) Kuendelea kusimamia na kutekeleza miongozo mbalimbali ya usimamizi wa fedha za umma ikiwemo Waraka wa Hazina Na. 1 kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Serikali;

(ii) Kuimarisha mipango ya ununuzi, mifumo ya udhibiti wa ndani, mifumo ya ufuatiliaji, usimamizi na utekelezaji wa matakwa ya kisheria;

(iii) Kuimarisha mifumo ya ukaguzi wa ndani kwa kuhakikisha kuwa taasisi zote zinatambua na kudhibiti vihatarishi vinavyoweza kuathiri matumizi ya fedha za umma;

(iv) Kufanya mageuzi ya kidijitali kwa kuendelea kuunganisha mifumo yote ya fedha za umma, ikiwemo mifumo ya mapato, matumizi, mali na madeni;

(v) Kuimarisha usimamizi wa miradi ya maendeleo kwa kufungamanisha maandalizi na utekelezaji wa mipango na bajeti ili kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa wakati na gharama stahiki;

(vi) Kuhakikisha upangaji, ugawaji na utoaji fedha unazingatia maeneo yenye matokeo, tija na mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi na ustawi wa wananchi;

(vii) Kudhibiti zaidi matumizi ya safari za nje na ndani pamoja na kupunguza semina, warsha na makongamano yenye gharama kubwa bila tija ya moja kwa moja;

(viii) Kuendelea kujenga uwezo wa wataalamu wa ndani ili kuimarisha usimamizi wa mifumo ya TEHAMA katika utekelezaji wa shughuli za Serikali;

(ix) Kuimarisha usimamizi wa mali za umma kwa kuhakikisha kuwa mali zote za Serikali zinatambuliwa, zinatunzwa na kutumika kwa tija, pamoja na kuzuia upotevu na matumizi yasiyo sahihi;

(x) Kuendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi na utendaji kazi katika Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma kwa kuboresha mikataba ya utendaji kazi, miundo ya taasisi na usimamizi wa bodi;

(xi) Kuhakikisha taasisi na mashirika ya umma hususan mashirika yanayojiendesha kibiashara yanaandaa na kutekeleza mikakati ya kuondokana na utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu;

(xii) Kuwezesha mashirika ya umma yanayojiendesha kwa faida kujiorodhesha katika Soko la Hisa la Dar es Salaam kwa lengo la kuongeza mtaji na kupunguza utegemezi kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali;

(xiii) Kuimarisha uandaaji na usimamizi wa mikataba ili kupunguza, kuondoa na kudhibiti gharama zinazotokana na mashauri ya kimahakama;

(xiv) Kutoingia mikataba bila kuwa na kasma zilizoidhinishwa na Bunge kwa mujibu wa kifungu cha 51 na 45(b) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439;

(xv) Kufanya uchambuzi wa gharama za miradi ya maendeleo kabla ya kujumuishwa kwenye mpango na bajeti ya Serikali ili kuhakikisha kuwa gharama za miradi zinaendana na uhalisia (value for *money*) na uwezo wa Serikali kugharamia;

(xvi) Kuandaa mikakati ya kuzalisha, kulea na kukuza wajasiriamali wadogo, wa kati na wakubwa kupitia ushirikishaji katika utekelezaji wa dhana ya wazawa (Local Content) katika utekelezaji wa miradi na huduma zinazotolewa na Serikali;

(xvii) Kupunguza kadiri itakavyowezekana uhamisho wa bajeti baina ya mafungu ili kuongeza uwazi na uwajibikaji na kuhakikisha utekelezaji wa mipango na bajeti unafanyika kama ilivyopangwa;

(xviii) Kusimamia ufanisi wa fedha zote zilizo nje ya Mfuko Mkuu wa Serikali zikiwemo za Mifuko iliyolindwa kama vile Mfuko wa

Barabara, Mfuko wa Reli, Mfuko wa Maji, Mfuko wa REA na kuhakikisha matumizi yake yanaendana na mipango na vipaumbele vya Serikali kwa mwaka husika; na

(xix) Kusimamia na kudhibiti uanzishwaji wa mifuko mipya inayopunguza uwezo wa Serikali kugharamia miradi na huduma muhimu za kijamii kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 135.

68. **Mheshimiwa Spika**, katika hatua nyingine, Serikali inazielekeza taasisi za umma kuanza kuzingatia ununuzi wa magari mapya yanayotumia teknolojia ya umeme na gesi katika mipango na bajeti zao. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali kutokana na utegemezi wa nishati za mafuta kutoka nje ya nchi.

69. **Mheshimiwa Spika**, hatua hizi zinalenga kuboresha usimamizi wa fedha za umma kwa kuhakikisha kuwa rasilimali za Taifa zinatumika kwa tija, ufanisi na kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma ili kufikia malengo ya Taifa ya kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani na hatimaye kufikia malengo yaliyoainishwa katika Dira 2050. Vilevile, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa bajeti kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti, Sura 439 ikisomwa pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika Muda wa Kati (2026/27 - 2028/29), Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348, Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290 na Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410, pamoja na miongozo mingine.

## IV. MABORESHO YA MFUMO WA KODI, ADA, TOZO NA HATUA NYINGINE ZA MAPATO

70. **Mheshimiwa Spika**, awali nilieleza haja ya kuwa na Bajeti inayochochea mageuzi ya kiuchumi hasa ujenzi wa viwanda na kuwa na Taifa linalojitegemea. Sasa ninapenda kuwasilisha mapendekezo ya hatua mpya za kodi kwa mwaka 2026/27 nikitarajia kuwa yatajibu maswali na kukidhi kiu ya wananchi, wafanyabiashara na wawekezaji kwa kuweka sera

zinazochochea uwekezaji, uzalishaji, kulinda viwanda na kuchangia katika kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 (DIRA 2050). Maboresho haya, pamoja na mambo mengine, yanalenga kukuza uchumi, kuongeza fursa za ajira na hatimaye kupunguza ukali wa maisha ya wananchi. Aidha, hatua hizo zinalenga pia kuimarisha usimamizi, ukusanyaji wa mapato ya ndani na kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali.

71. **Mheshimiwa Spika**, wakati Serikali ikiyafanyia kazi kwa kina maoni yaliyotolewa na Tume ya Rais ya Maboresho ya Mfumo wa Kodi, mapendekezo ya kurekebisha mfumo wa kodi kwa mwaka 2026/27 yamezingatia baadhi ya maoni hayo. Maeneo yanayopendekezwa kufanyiwa maboresho ni:

**A. Kustawisha Sekta za Uzalishaji katika Mnyororo wa Thamani wa Mafuta ya Kula na Pamba, Nguo na Mavazi**

**Tasnia ya Mafuta ya Kula**

72. **Mheshimiwa Spika**, mafuta ya kula ni bidhaa muhimu inayotumiwa kwa wingi nchini Tanzania na inatoa fursa kubwa ya kukuza uwekezaji, ajira na mapato kupitia mnyororo wake wa thamani. Serikali imeweka vivutio mbalimbali vya kikodi ili kuhamasisha kilimo na matumizi ya mbegu za mafuta zinazozalishwa nchini, kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa hii kwa wananchi kwa gharama nafuu pamoja na kuendeleza na kulinda viwanda vya ndani vinavyochakata na kuzalisha mafuta ya kula. Hatua za kikodi zinazoendelea kutekelezwa kwa sasa ni pamoja na zifuatazo:

(i) Msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye mafuta ya kula yaliyozalishwa kwa kutumia mbegu zinazozalishwa ndani ya nchi (*locally grown seeds*);

(ii) Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye mafuta ghafi ya kula yanayoingizwa nchini isipokuwa ya mchikichi;

(iii) Ushuru wa mauzo ya kusafirisha nje ya nchi (*export levy*) wa asilimia 10 kwenye mafuta ghafi ya alizeti na mbegu zake;

(iv) Ushuru wa forodha wa asilimia 0 kwenye mafuta ghafi ya kula ya mchikichi na asilimia 10 kwenye mafuta ya mchikichi (*Crude Palm Oil – CPO*) yaliyochakatwa kwa kiwango cha kati [*palm olein, fractions (semi-refined*)]; na

(v) Ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 35 au dola za Marekani 300 kwa tani moja kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya kiwango cha asilimia 35 pekee kwenye mafuta ya kula ya aina zote yaliyochakatwa kwa kiwango cha mwisho *(refined edible oil)*.

73. **Mheshimiwa Spika**, Serikali baada ya kufanya mashauriano na wadau mbalimbali ikiwemo wazalishaji wa mafuta ya kula na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, inapendekezwa kufanya marekebisho yafuatayo:

(i) Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye mafuta ghafi ya kula ya aina zote ikiwemo ya mchikichi (*crude palm oil)* na mafuta yaliyochakatwa kwa kiwango kidogo (semi-*refined palm oil*). Hatua hii inalenga kuondoa changamoto ya udanganyifu wa uainishaji wa bidhaa (*misdeclaration/misclassification*) unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu ambao hutumia nafuu iliyopo kwenye mafuta ya mchikichi (*crude palm oil)* kuingiza yaliyochakatwa (*semi refined palm oil*). Matumizi ya kiwango hiki yanaendana na mwelekeo wa sera unaotumika na baadhi ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa sasa, ikiwemo Kenya na Uganda ambazo zinatoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye mafuta ghafi ya mchikichi kutoka nje ya Jumuiya;

(ii) Kuendelea kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye mafuta ya kula yaliyozalishwa kwa kutumia mbegu zinazozalishwa ndani ya nchi (*locally grown seeds*);

(iii) Kuendelea kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 35 au dola za Marekani 300 kwa tani moja ya ujazo wa mafuta safi (*refined edible oil)* kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa. Aidha, Serikali imeandaa kanuni za uagizaji wa mafuta ya kula kwa lengo la kudhibiti uingizaji wa mafuta ya kula nchini ili kuhamasisha na kukuza tasnia ya mafuta ya kula yanayozalishwa kwa kutumia mbegu za ndani ya nchi; na

(iv) Serikali kupitia Wizara ya Kilimo itaratibu utoaji wa vibali maalum kwa waagizaji wa mafuta hayo kutoka nje ya nchi. Vibali hivyo vitatolewa baada ya kujiridhisha juu ya uwekezaji na uzalishaji wa mbegu za alizeti, pamba na michikichi, chini ya Kanuni za COPRA za mwaka 2026. Aidha, kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali itaendelea kutoa ruzuku ya mbegu za alizeti na pamba pamoja na miche milioni mbili kila mwaka kwa lengo la kukuza uzalishaji wa mbegu zinazotumika kuzalisha mafuta ya kula na hivyo kuondoa kabisa uingizaji wa mafuta hayo kutoka nje ya nchi.

**Mnyororo wa Pamba, Nguo na Vitambaa**

74. **Mheshimiwa Spika**, sekta ya nguo na mavazi ni moja ya sekta inayohusisha mnyororo mrefu wa uongezaji thamani kwenye zao la pamba (*ginning*), kusokota nyuzi (*spinning*), kuseketa vitambaa (*weaving*), kufuma vitambaa (*knitting*), kuchapa na kuweka rangi (*dyeing and printing*) pamoja na kushona mavazi (*garments*).

75. **Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua umuhimu wa sekta hii katika uchumi wa Tanzania, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa kuhamasisha matumizi ya pamba inayozalishwa ndani ya nchi katika uzalishaji wa nyuzi, vitambaa, nguo na mavazi ikiwemo vivutio mbalimbali vya kikodi kwa wazalishaji wa nyuzi, vitambaa, nguo na mavazi nchini. Vivutio vya kikodi vinavyotekelezwa kwa sasa ni pamoja na:

(i) Kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha asilimia sifuri (*zero rated*) kwenye nguo na mavazi

yanayozalishwa kwa kutumia pamba ya ndani ya nchi (*locally grown cotton*);

(ii) Unafuu wa ushuru wa forodha kwenye malighafi, mashine na vipuri vinavyotumika katika uzalishaji wa vitambaa na nguo nchini;

(iii) Msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye uingizaji wa mashine zinazotumika kwenye viwanda vya uzalishaji wa mavazi (*textile industry*);

(iv) Ushuru wa forodha wa asilimia 25 kwenye nyuzi za pamba zinazotoka nje ya Jumuiya; na

(v) Uwepo wa kiwango maalum cha ushuru wa forodha wa dola za Marekani 0.25 kwa mita ya kitambaa kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa ikilinganishwa na asilimia 25 ili kudhibiti udanganyifu na kulinda viwanda vya ndani.

76. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia umuhimu wa mchango wa tasnia ya pamba, nguo na mavazi katika uchumi, inapendekezwa kuendelea kulinda viwanda vya ndani vinavyozalisha vitambaa kwa kuchukua hatua zifuatazo:

(i) Kuongeza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 35 au dola za Marekani 0.30 kwa mita ya kitambaa kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa; na

(ii) Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye nguo na mavazi yanayozalishwa kwa kutumia pamba inayozalishwa ndani ya nchi (*locally grown cotton*) kwa lengo la kuhamasisha matumizi yake.

**B. Matumizi ya nishati safi na mbadala katika vyombo vya moto na majumbani**

77. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuweka hatua mbalimbali za kodi zinazochochea matumizi ya nishati ya umeme na gesi asilia katika sekta ya usafiri na majumbani. Hatua zinazotekelezwa kwa sasa ni pamoja na:

(i) Msamaha wa ushuru wa bidhaa kwa kuzingatia uwezo wa injini kwenye magari yanayotumia umeme na gesi;

(ii) Msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye gesi asilia iliyoshindiliwa (*Compressed Natural Gas - CNG*) inayotumika kwenye magari;

(iii) Msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye vifaa vya usambazaji wa CNG, ikiwemo *CNG compressors, CNG metering equipment, CNG storage cascades, CNG special transportation vehicles* na *CNG dispensers*;

(iv) Msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye mnyororo mzima wa uzalishaji wa CNG;

(v) Msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye vifaa vinavyotumika katika ubadilishaji wa mfumo wa matumizi ya mafuta ya petroli kuwa mfumo wa matumizi ya gesi na umeme kwenye magari;

(vi) Msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye uingizaji wa malighafi zinazotumika kutengeneza mitungi ya gesi kwa matumizi mbalimbali ikiwemo inayotumika kwenye magari;

(vii) Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwenye betri za umeme zinazotumiwa na wazalishaji au waunganishaji wa magari na pikipiki za umeme; na

(viii) Unafuu wa ushuru wa forodha kwa waunganishaji na wazalishaji wa vyombo vya moto nchini ikiwemo vinavyotumia umeme na gesi kwa kuzingatia kanuni za uunganishaji na uzalishaji wa bidhaa za Jumuiya ya Afrika Mashariki za mwaka 2025 (EAC Assembling and

Manufacturing *of Products Regulations, 2025*) ili kupunguza gharama za uzalishaji.

78. **Mheshimiwa Spika**, katika kuchochea matumizi ya nishati ya umeme na gesi asilia, Serikali inapendekeza yafuatayo kwa mwaka 2026/27:

(i) Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye vifaa vitakavyotumika katika vituo vya kuchaji magari yanayotumia umeme (*electric vehicles charging station*) vinavyoingizwa nchini vinavyotambulika kwa *HS Code* 8504.40.00;

(ii) Kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10 kwenye magari yanayotumia nishati ya umeme yanayotambulika kwa *HS Codes* 8702.40.19; 8702.40.22; 8702.40.29; 8702.40.99; 8703.80.90 na 8704.60.90. Aidha, Serikali inaendelea kufanya majadiliano na viwanda vya kuunganisha magari vilivyopo nchini ili kutoa unafuu wa kodi kwa waunganishaji wa magari ya umeme nchini; na

(iii) Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye mita janja za gesi ya mitungi ya kupikia (*LPG smart meter*) zinazoingizwa nchini zinazotambulika kwa *HS Code* 9028.10.00. Msamaha husika utatolewa kwa wasambazaji wa gesi ya kupikia pekee (*LPG distributors*).

**C. Urasimishaji wa Sekta Isiyo Rasmi**

79. **Mheshimiwa Spika**, mwaka 2026/27, Serikali inaendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia urasimishaji wa sekta isiyo rasmi ambayo inaajiri zaidi vijana na wanawake. Katika kufanikisha azma hiyo, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) Kutoa msamaha wa kodi ya mapato kwa wafanyabiashara wapya kwa kipindi cha mwaka mmoja tangu tarehe ya kupata namba ya utambulisho wa mlipakodi; na

(ii) Kufanya maboresho kwenye Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290, ili kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa

kutenga asilimia 15 ya mapato yao ya ndani badala ya asilimia 10 iliyopo sasa ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Kati ya asilimia 15 itakayotengwa, asilimia 10 itaelekezwa kwenye mikopo ya wanawake, vijana na wenye ulemavu kwa uwiano kama ilivyokuwa awali na asilimia tano (5) itatumika **kwa ajili ya uwekezaji kwenye miradi ya ujenzi na maboresho ya masoko na maeneo ya biashara na ujasiriamali** ili kuvutia na kuongeza fursa za ajira hususan kwa vijana, wanawake na makundi maalum.

**D. Kupunguza Matumizi ya Fedha Taslimu**

79. **Mheshimiwa Spika**, ili kupunguza matumizi ya fedha taslimu katika mwaka 2026/27 inapendekezwa kufanya maboresho yafuatayo:

(i) Kuweka sharti la baadhi ya malipo ya huduma na biashara kufanyika kwa njia za kidijitali kama ilivyoainishwa katika Aya Na. 61;

(ii) Kusitisha usambazaji na matumizi ya vocha za kukwangua za muda wa maongezi (*scratch cards*) katika maeneo yote ya mijini yenye miundombinu wezeshi ya malipo ya kidijitali;

(iii) Kuweka sharti la matumizi ya vifaa vya malipo ya kidijitali (Lipa Namba na TANQR) kama moja ya kigezo wakati wa utoaji na uhuishaji wa leseni ya biashara;

(iv) Kuweka sharti la kufungua akaunti ya benki kama moja ya vigezo vya utoaji wa leseni kwa wafanyabiashara wanaoshiriki katika shughuli za madini, mifugo, mazao, mbao na uvuvi na kuhakikisha miamala inafanyika kupitia akaunti husika; na

(v) Kuweka sharti la uthibitisho wa malipo ya kidijitali kuwa rejea ya lazima itakayotumika kuidhinisha maombi ya uhamishaji wa mali kama vile ardhi, majengo na magari kama ilivyoainishwa katika Aya Na. 64.

## E. Mapendekezo ya Kiutawala ya Tume ya Rais ya Maboresho ya Kodi

81. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imezingatia mapendekezo ya kiutawala yaliyotolewa na Tume ya Rais ya Maboresho ya Mfumo wa Kodi. Katika mwaka 2026/27, Serikali itatekeleza mapendekezo yafuatayo:

(i) Mamlaka ya Mapato Tanzania kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA, akili unde (*Artificial Intelligence - AI*), data kubwa (*big data*) na *blockchain*, ili kupunguza gharama za kiutawala, kuongeza ufanisi, kuhakikisha usalama na uwazi wa takwimu, na kuboresha huduma kwa walipakodi kupitia teknolojia za kisasa. Aidha, hatua hii itapunguza ulazima wa mlipakodi kuonana uso kwa uso na watumishi wa TRA;

(ii) Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara wataweka utaratibu mahsusi kwa taasisi za udhibiti kufanya kaguzi za pamoja katika maeneo ya uwekezaji, biashara na shughuli zote zinazosimamiwa na mamlaka za udhibiti ambao hautasababisha usumbufu kwa wafanyabiashara na wawekezaji bila kuathiri majukumu ya msingi ya taasisi hizo;

(iii) Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI itatoa mwongozo (guidelines) wa utozaji tozo mbalimbali za Mamlaka za Serikali za Mitaa utakaotumika na Mamlaka husika katika kuandaa sheria ndogo za utozaji wa tozo hizo. Aidha, mwongozo huo utaweka masharti muhimu ikiwemo ukomo wa kiwango cha tozo husika;

(iv) Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kwa kushirikiana na TRA zitakamilisha ufungamanishaji wa mifumo ikiwemo mfumo wa TAUSI na mfumo wa kodi za ndani (IDRAS) ili ibadilishane taarifa moja kwa moja, zikiwemo za leseni za biashara na Cheti cha Uthibitisho wa Ulipaji Kodi (Tax Clearance Certificate). Aidha, Serikali itaondoa sharti la mfanyabiashara kupakia cheti cha uthibitisho wa mlipakodi

kwenye mfumo wa TAUSI wakati wa kufanya maombi ya leseni ya biashara bali kitavutwa moja kwa moja kutoka kwenye mfumo wa TRA;

(v) Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kwa kushirikiana na TRA watakamilisha ujenzi wa moduli mahsusi kwenye mfumo wa TAUSI kwa ajili ya usajili, utambuzi na malipo ya kodi ili kuwezesha ukusanyaji wa kodi na tozo kulingana na matumizi ya jengo husika. Kanzidata hii itazingatia masuala yafuatayo:

(a) Taarifa kamili za jengo ikiwa ni pamoja na hadhi ya usajili wa kiwanja, namba ya kiwanja, idadi ya nyumba/vyumba katika kiwanja/jengo husika, thamani ya jengo, na matumizi (biashara au makazi binafsi);

(b) Taarifa za mmiliki wa jengo/majengo ikiwa ni pamoja na namba ya NIDA, namba ya simu, barua pepe na namba ya mlipakodi - TIN;

(c) Kanzidata itasomana na moja kwa moja na mifumo mingine ya Serikali ikiwa ni pamoja na IDRAS na mfumo wa Wizara ya Ardhi; na

(d) Kufanya mapitio ya taratibu na viwango vya ada na tozo ili kurahisisha urasimishaji wa umiliki wa ardhi.

(vi) Kuongeza idadi ya ofisi za TRA kwenye wilaya au vituo vya huduma kwa walipakodi (Tax Service Centres) pamoja na vituo vinavyotembea (mobile centres) kwenye maeneo yenye shughuli nyingi za kiuchumi ili kusogeza huduma karibu na walipakodi;

(vii) Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI itaongeza moduli maalumu katika mfumo wa TAUSI itakayoruhusu watendaji wa mitaa na vijiji kusajili wafanyabiashara wote katika maeneo yao hata ambao hawana leseni za biashara; na

(viii) TRA itengeneze programu tumizi *(application)* itakayotumika kwenye simu za mkononi, vishikwambi au kompyuta na kisha kutoa *App* hiyo bure kwa wafanyabiashara ili itumike kutoa risiti kama zile zinazotolewa na mashine za EFD.

82. **Mheshimiwa Spika**, mapendekezo ya kurekebisha mfumo wa kodi kwa mwaka 2026/27 yanatarajiwa kuiongezea Serikali jumla ya shilingi **trilioni 1.72**. Marekebisho yanayopendekezwa yanahusu sheria zifuatazo:

**1. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani,** SURA 148

83. **Mheshimiwa Spika**, inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148 kama ifuatavyo:

(i) Kuweka sharti la marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani (*VAT refunds*) kulipwa ndani ya siku 30 kutoka tarehe ya kuwasilishwa kwa maombi ya marejesho hayo. Hatua hii itaenda sambamba na kubainisha kuwa, mlipakodi atakuwa na haki kisheria ya kulipwa riba pale ambapo marejesho husika hayatofanyika kwa wakati. Lengo la hatua hii ni kuchochea ulipaji kodi wa hiari na kuongeza uwajibikaji kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania;

(ii) Kujumuisha hati za kupandia ndege (boarding pass) kwenye wigo wa bidhaa zinazopata msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani. Lengo la hatua hii ni kutekeleza matakwa ya Mikataba ya Makubaliano ya Usafiri wa Anga ambayo Tanzania imeridhia, yanayoitaka Serikali kusamehe kodi kwenye hati husika kama ilivyobainishwa kwenye miongozo ya usafiri wa anga ya kimataifa;

(iii) Kujumuisha vifungashio vya maziwa (dairy packaging materials) vinavyotambulika kwa HS Code 3920.20.90 vinavyozalishwa na vinavyoingizwa kutoka nje ya nchi kwenye wigo wa bidhaa zinazopata msamaha wa kodi

ya ongezeko la thamani. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwenye sekta ya maziwa nchini na kuwawezesha wazalishaji wa ndani kushindana kwenye masoko ya kikanda na kimataifa. Hatua hii inatarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 17.8;

(iv) Kuondoa sharti la ukomo wa muda wa uahirishaji wa kodi ya ongezeko la thamani (*VAT Deferment*) kwa bidhaa za mtaji zinazoingizwa nchini. Pendekezo hilo linazingatia matokeo ya tathmini iliyofanyika ambayo yalionesha kuwa uzalishaji wa ndani wa bidhaa hizo haukidhi mahitaji ya soko. Hivyo, lengo la hatua hii ni kuendelea kupunguza gharama za uwekezaji kwa kuhakikisha kuwa bidhaa mtaji zinaingizwa nchini kwa bei nafuu. Mapendekezo hayo yanatarajiwa kuanza kutekelezwa tarehe 1 Julai 2026;

(v) Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye vifaa vitakavyotumika katika vituo vya kuchaji magari yanayotumia umeme (*electric vehicles charging station*) vinavyoingizwa nchini vinavyotambulika kwa *HS Code* 8504.40.00. Hatua hii inatarajiwa **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **bilioni 5.97**;

(vi) Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye turbojets, turbo-propellers na gas turbines nyinginezo zinazotambulika kwa HS Heading 84.11; pamoja na matairi ya ndege yanayotambulika kwa HS Code 4011.30.00. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za uendeshaji na kuchochea uwekezaji kwenye sekta ya anga nchini. Hatua hii inatarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 14.84;

(vii) Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye mita janja za gesi ya mitungi ya kupikia (LPG smart meter) zinazoingizwa nchini zinazotambulika kwa HS Code 9028.10.00. Msamaha husika utatolewa kwa wasambazaji wa gesi ya kupikia pekee (LPG distributors).

Hatua hii inatarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 16.8;

(viii) Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye mafuta ya kula yanayozalishwa ndani ya nchi kwa kutumia mbegu zinazozalishwa nchini kwa muda wa mwaka mmoja. Msamaha huu ulitolewa kwa kipindi cha mwaka mmoja kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2025 na ukomo wake ni tarehe 30 Juni 2026. Lengo la hatua hii ni kuendelea kuleta unafuu wa bei ya mafuta ya kula nchini;

(ix) Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye nguo na mavazi yanayozalishwa kwa kutumia pamba inayozalishwa ndani ya nchi (locally grown cotton) kwa lengo la kuhamasisha matumizi ya pamba inayozalishwa nchini. Hatua hii inatarajiwa kuokoa mapato ya Serikali yanayotokana na marejesho kwa mlipakodi (VAT refund) kwa kiasi cha shilingi bilioni 6.30;

(x) Kufuta msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye nyavu za kuvulia samaki zinazoingizwa nchini zinazotambulika kwa HS Code 5608.11.00. Hatua hii inaenda sambamba na kuweka msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye nyuzi za polyester zinazotambulika kwa HS Code 5402.20.00 zinazotumika kwenye uzalishaji wa nyavu za kuvulia samaki. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za uzalishaji na kuvutia uwekezaji nchini. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 2.55;

(xi) Kufuta msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye chakula cha mbwa na paka kinachotambulika kwa HS Heading 23.09 kinachozalishwa na kinachoingizwa kutoka nje ya nchi. Lengo la hatua hii ni kuendana na azma ya Serikali ya kupunguza misamaha isiyo na tija ili kulinda mapato ya Serikali pamoja na kupunguza matumizi yanayohusiana na utoaji wa misamaha ya kodi (tax expenditure). Hatua hii

inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 6.73; na

(xii) Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ongezeko la Thamani, ili kutambua vipengele vya msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani vilivyopo kwenye Mikataba ya Msingi (Framework

(xiii) Agreements) iliyosainiwa baina ya Serikali na wawekezaji wa madini, baada ya kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri. Lengo la hatua hii ni kuwezesha utekelezaji wa miradi ya ubia ya uchimbaji wa madini nchini. Aidha, hatua hii itaenda sambamba na Serikali kuweka taratibu za usimamizi zitakazotoa mwongozo kuhusu utolewaji wa msamaha huo. Lengo la hatua hii ni kutekeleza matakwa ya mikataba husika, kutimiza jukumu la Serikali la kusamehe kodi kwenye utekelezaji wa miradi hiyo na kuhakikisha miradi ya ubia inatekelezwa kwa wakati na kuharakisha maendeleo yetu.

84. **Mheshimiwa Spika**, hatua zote za kodi ya ongezeko la thamani kwa ujumla wake zinatarajiwa **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 26.6**.

**2. Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332**

85. **Mheshimiwa Spika**, inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 kama ifuatavyo:

(i) Kuweka msamaha wa kodi ya mapato kwa wafanyabiashara wapya kwa kipindi cha mwaka mmoja tangu tarehe ya kupata namba ya utambulisho wa mlipakodi. Msamaha huo ni kwa ajili ya wafanyabiashara waliopo chini ya utaratibu wa makadirio (*presumptive regime*) pekee. Hatua hii inatofautiana na utaratibu wa sasa ambapo mfanyabiashara anaposajiliwa anafanyiwa tathmini ya mapato anayotarajia kuyakusanya na kupaswa kulipa kodi husika ndani ya miezi sita. Aidha, baada ya kipindi cha muda wa mpito, wafanyabiashara husika watapaswa kuanza kulipa kodi kwa mujibu wa

sheria. Lengo la hatua hii ni kuwawezesha wafanyabiashara wapya kupata muda wa kutosha wa kujiandaa na mahitaji ya msingi, kuondoa usumbufu wakati wa kuanza biashara pamoja na kuhakikisha kuwa makadirio ya kodi yanazingatia uhalisia wa mapato yanayopatikana kutoka kwenye shughuli za biashara;

(ii) Kuongeza kima cha juu cha mauzo yanayotozwa kodi kwa utaratibu wa makadirio (*presumptive regime*) kutoka shilingi milioni 100 hadi shilingi milioni 200. Aidha, hatua hii itaenda sambamba na kuweka sharti la kuruhusu mlipakodi mwenye mauzo ya chini ya shilingi milioni 200 kuandaa vitabu vya hesabu (*financial statements*) pale atakapoona inafaa kwa lengo la kutumia utaratibu wa kujikadiria kodi (*self assesment*). Lengo la hatua hii ni kuwianisha kima husika na kima cha usajili wa kodi ya ongezeko la thamani pamoja na kuboresha mfumo wa kodi. Hatua hii inatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **bilioni 111.13**;

(iii) Kuongeza kiwango cha kodi kwa walipakodi chini ya utaratibu wa makadirio (*presumptive regime*) wenye mauzo yanayozidi shilingi milioni 11 lakini yasiyozidi shilingi milioni 200 kwa mwaka kutoka asilimia 3.5 hadi asilimia 4.5. Lengo la hatua hii ni kuendana na kanuni za usawa za utozaji kwa kuhakikisha kodi husika inalipwa kwa kuzingatia uwiano wa mapato halisi yanayopatikana kwa walipakodi wenye mapato sawa na wale wanaotofautiana (*horizontal and vertical equity*). Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **bilioni 75.11**;

(iv) Kuongeza kiwango cha kodi ya mapato kwenye malipo yanayofanywa kwa watoa huduma za kidijitali wa kigeni kutoka asilimia 2 hadi asilimia 3. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 1.44;

(v) Kufanya marekebisho ya kifungu cha 33A cha Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 ili kupunguza kiwango cha faida ambayo haijagawanywa kwa wanahisa (*deemed retained earnings*) kinachotozwa kodi ya zuio kutoka asilimia 30 hadi asilimia 15. Aidha, hatua hii itaenda sambamba na kuziondoa sekta ndogo ya fedha, bima, makampuni yaliyosajiliwa kwenye soko la hisa la Dar es Salaam pamoja na taasisi zenye mikataba ya utekelezaji na Serikali (*Framework Agreements*) katika utaratibu wa kutozwa kodi hiyo. Hatua hii inatarajiwa **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **bilioni 23.59**;

(vi) Kujumuisha natural varnish, latex, resin, sap na gum kwenye tafsiri ya neno mazao ya misitu ili viweze kutozwa kodi ya mapato kwa kiwango cha asilimia 2 kwenye mapato yanayotokana na uuzaji wa mazao hayo. Kiwango cha kodi husika kitalipwa kwa awamu moja (Single Installment Tax) kwa kila thamani ya mzigo. Lengo la hatua hii ni kuongeza wigo wa kodi na kuendana na kanuni za usawa za utozaji kodi kwa kuzingatia kuwa, tayari mazao mengine ya misitu yakiwemo mbao, magogo na mirunda yanatozwa kodi ya mapato kwa utaratibu huo. Hatua hii inatarajia kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 433.2;

(vii) Kuongeza kiwango cha kodi ya zuio kwenye mrabaha kwa Taasisi za Michezo au Shirikisho la Soka Tanzania kutoka asilimia 5 hadi asilimia 10. Lengo la hatua hii ni kuendana na kanuni za usawa za utozaji kodi kwa kuwa kiwango husika kinatozwa kwenye mrabaha kwa tasnia ya filamu. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 1.44;

(viii) Kuweka sharti la Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuzuia kodi ya mapato kwenye malipo yanayofanywa kwenye ununuzi wa bidhaa nchini badala ya utaratibu wa sasa unaoweka sharti hilo kwa Taasisi za Serikali zinazojiendesha kwa kutegemea ruzuku kutoka

Serikali kuu kikamilifu au kwa kiasi kikubwa pekee. Lengo la hatua hii ni kuongeza wigo wa ukusanyaji wa kodi husika pamoja na kulinda mapato ya Serikali;

(ix) Kuanzisha utaratibu wa ulipaji wa kodi ya mapato ya awali kwa Mkupuo Mmoja (Advance Single Instalment Tax) kwa mnunuzi wa mazao ya kilimo (food and cash crops). Katika utaratibu huu mnunuzi wa mazao ya chakula au biashara atawajibika kulipa kodi ya mapato kwa utaratibu huu pale ambapo anaponunua mazao, anapotaka kusafirisha mazao au anapohamisha umiliki wa mazao kutoka kwake kwenda kwa mtu mwingine. Kiwango cha kodi husika kitakuwa ni asilimia moja ya bei ya mazao husika katika eneo alikonunulia mazao na kitalipwa TRA. Mara baada ya kufanya malipo mnunuzi atapewa cheti cha malipo ya kodi kwa mkupuo mmoja kama uthibitisho wa malipo hayo. Mnunuzi ataruhusiwa kutumia cheti hicho wakati wa usafirishaji wa mazao husika. Kwa kuwa kodi ni ya awali mnunuzi ataruhusiwa kuidai wakati analipa kodi ya mapato ya mwaka mzima. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 99.87;

(x) Kutoza kodi ya zuio kwa kiwango cha asilimia moja (1) kwenye malipo yanayofanywa na makampuni au taasisi kwa muuzaji wa wanyama hai, maziwa ambayo hayajachakatwa, samaki ambazo hazijachakatwa na mabondo (fish maws). Aidha, kampuni au taasisi inayonunua mazao husika itakuwa wakala wa kukusanya kodi hiyo na kuiwasilisha kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Lengo la hatua hii ni kuongeza wigo wa kodi, kuendana na kanuni za usawa za utozaji kodi na kuendelea kurasimisha sekta isiyo rasmi. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 49.49; na

(xi) Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato, ili kutambua vipengele vya msamaha wa kodi ya mapato vilivyopo kwenye Mikataba ya Msingi

(Framework Agreements) iliyosainiwa baina ya Serikali na wawekezaji wa madini, baada ya kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri. Lengo la hatua hii ni kuwezesha utekelezaji wa miradi ya ubia ya uchimbaji wa madini nchini. Aidha, hatua hii itaenda sambamba na Serikali kuweka taratibu za usimamizi zitakazotoa mwongozo kuhusu utolewaji wa msamaha huo. Lengo la hatua hii ni kutekeleza matakwa ya mikataba husika, kutimiza jukumu la Serikali la kusamehe kodi kwenye utekelezaji wa miradi hiyo na kuhakikisha miradi ya ubia inatekelezwa kwa wakati.

86. **Mheshimiwa Spika**, hatua hizi za kodi ya mapato kwa ujumla wake zinatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **bilioni 174.48**.

**3. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa kifungu cha 126 (3) cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147 marekebisho ya viwango maalum vya ushuru wa bidhaa (*specific excise duty rates*) yanaweza kufanyika kila baada ya miaka mitatu ili kuviwianisha na mfumuko wa bei na viashiria vingine vya uchumi jumla. Serikali ilianzisha utaratibu huo kuanzia mwaka 2023/24 ili kuiwezesha nchi kuwa na sera za kodi zinazotabirika, kuchochea ukuaji wa uchumi pamoja na kuweka mazingira bora ya ufanyaji biashara na uwekezaji.

87. **Mheshimiwa Spika**, awamu ya pili ya utekelezaji wa utaratibu husika inatarajiwa kuanza mwaka 2026/27, ambapo viwango vya ushuru vinatarajiwa kurekebishwa. Marekebisho hayo hayatahusisha viwango vya ushuru kwa bidhaa za petroli kutokana na kupanda kwa gharama za bidhaa husika katika soko la dunia kufuatia mgogoro baina ya Marekani, Israel na Iran na hivyo kuhitaji uwepo wa mikakati madhubuti nchini kwa lengo la kuzuia mfumuko wa bei, kupunguza ukali wa maisha kwa wananchi pamoja na kutoathiri ukuaji wa sekta zinazotegemea bidhaa za petroli katika uendeshaji wa shughuli zake.

88. **Mheshimiwa Spika**, licha ya utaratibu huo kuleta tija ikiwemo kuhakikisha uwepo wa mfumo wa utozaji unaotabirika imebainika

kuwa, ongezeko la ushuru wa bidhaa kwa kiwango kikubwa kwa mkupuo mmoja linaweza kuathiri ukuaji wa biashara na uwekezaji nchini. Hivyo, ili kutatua changamoto zinazoweza kujitokeza na kufikia malengo yaliyokusudiwa, inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147, kuhusiana na utaratibu wa kurekebisha viwango vya ushuru kila baada ya miaka mitatu na badala yake viwango maalumu vya ushuru (*specific excise duty rates*) viongezeke kwa asilimia 8 kwa mwaka 2026/27 na, kwa miaka ya fedha ijayo, ongezeko litazingatia kiwango cha mfumuko wa bei kikijumlishwa na asilimia 2. Lengo la hatua hii ni kuakisi thamani ya mapato ya Serikali na kuiwezesha nchi kuwa na sera za kodi zinazotabirika na kuweka mazingira bora ya uwekezaji. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **bilioni 251.54**;

89. **Mheshimiwa Spika**, sambamba na hatua hiyo, inapendekezwa pia kufanya marekebisho kwenye bidhaa nyingine kama ifuatavyo:

(i) Kufanya maboresho kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, ili kutambua vipengele vya msamaha wa ushuru wa bidhaa vilivyopo kwenye Mikataba ya Msingi (*Framework Agreements*) iliyosainiwa baina ya Serikali na wawekezaji wa madini, baada ya kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri. Lengo la hatua hii ni kuwezesha utekelezaji wa miradi ya ubia ya uchimbaji wa madini nchini. Aidha, hatua hii itaenda sambamba na Serikali kuweka taratibu za usimamizi zitakazotoa mwongozo kuhusu utolewaji wa msamaha huo.

Lengo la hatua hii ni kutekeleza matakwa ya mikataba husika, kutimiza jukumu la Serikali la kusamehe kodi kwenye utekelezaji wa miradi hiyo na kuhakikisha miradi ya ubia inatekelezwa kwa wakati;

(ii) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 20 kwenye maua ya bandia (*artificial flowers*), matawi ya bandia (*foliage*), matunda ya bandia pamoja na bidhaa zinazofanana na hizo zinazoingizwa nchini zinazotambulika kwa *HS Heading* 67.02. Lengo la hatua

hii ni kupunguza athari za kimazingira zinazotokana na matumizi ya bidhaa husika, kuongeza wigo wa kodi na mapato ya Serikali. Hatua hii inatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 852.8**;

(iii) Kujumuisha watoa huduma wa kigeni kwa njia ya mtandao wasio na makazi ya bishara nchini (*non-resident suppliers of digital and electronic exciseable services*) wanaouza moja kwa moja kwa mtumiaji wa mwisho (B2C) kwenye wigo wa utozaji ushuru wa bidhaa. Lengo la hatua hii ni kuendana na kanuni za usawa za utozaji kodi pamoja na kuhakikisha ushindani wa haki baina ya watoa huduma wa kawaida na wa mtandao. Hatua hii inatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **bilioni 1.63**;

(iv) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye mashine za kukaushia rangi za kucha (*ultraviolet/light-emitting diodes*) zinazoingizwa nchini zinazotambulika kwa *HS Code* 8516.79.00. Lengo la hatua hii ni kupunguza athari za kiafya zinazoweza kujitokeza kutokana na matumizi ya bidhaa husika ikiwemo ugonjwa wa saratani na kuongeza wigo wa kodi. Hatua hii inatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 566.5**;

(v) Kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kutoka asilimia 10 hadi asilimia 15 kwenye bidhaa za urembo zinazoingizwa ndani ya nchi zinazotambulika kwa *HS Heading 33.03; 33.04; 33.05* and *33.07*. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali na kuwianisha kiwango husika na viwango vinavyotozwa na baadhi ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwemo Kenya, Uganda na Rwanda. Hatua hii inatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **bilioni 1.91**;

(vi) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 5 kwenye pikipiki isipokuwa pikipiki za wagonjwa wa

dharura (*motorcycle ambulances*), pikipiki zinazotumia gesi asilia pamoja na pikipiki za umeme. Lengo la hatua hii ni kuendana na malengo ya Serikali ya kuhamasisha matumizi ya nishati safi kwenye vyombo vya moto nchini. Hatua hii inatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **bilioni 30.40**;

(vii) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye viatu vya plastiki (*plastic or rubber clogs*) vinavyoingizwa nchini vinavyotambulika kwa *HS Code 6402.99.00*. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani vinavyozalisha viatu vya plastiki na kuchochea uwekezaji ndani ya nchi. Hatua hii inatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **bilioni 10.58**;

(viii) Kutoza ushuru wa bidhaaa kwa kiwango cha asilimia 5 kwenye magari yanayotambulika kwa HS Code
(ix) 8703.21.90 yenye ukubwa wa injini (CC) kuanzia 1,000 kushuka chini. Lengo la hatua hii ni kuongeza wigo wa kodi na mapato ya Serikali. Hatua hii inatarajia kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 5.71;

(x) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 5 kwenye thamani ya dau la kamari (gaming) inayochezwa kwa njia ya michezo ya kubashiri ya ardhini au mtandaoni (land/internet based sports betting), michezo ya kasino ya ardhini au mtandanoni (land based/internet casino), mashine za sloti arobaini (forty machine) pamoja na michezo ya vikaragosi (virtual games operations). Aidha, asilimia 10 ya mapato yatakayokusanywa kutoka kwenye chanzo hiki (ushuru wa asilimia 5) yatawasilishwa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha (GBT) ili kuongeza ufanisi katika udhibiti wa michezo ya kubahatisha. Lengo la hatua hii ni kupunguza madhara yanayosababishwa na michezo ya kubahatisha ikiwemo uraibu na kupungua kwa nguvu kazi ya Taifa kutokana na baadhi ya vijana

kujihusisha zaidi katika shughuli hizo badala ya shughuli za kiuchumi. Vilevile, hatua husika itaongeza mapato ya Serikali ambayo pamoja na masuala mengine yanatumika katika kugharamia utekelezaji wa shughuli za kiuchumi. Hatua hii inatarajia kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 74.50; na

(xi) Kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye magari yaliyotumika yanayoingizwa nchini kutoka asilimia 15 hadi asilimia 20 kwa magari yenye umri wa miaka nane lakini hayazidi miaka 10 na kutoka asilimia 30 hadi asilimia 40 kwa magari yenye umri wa zaidi ya miaka kumi lakini hayazidi miaka 20. Aidha, magari yenye miaka inayozidi 20 na kuendelea yatatozwa ushuru wa bidha kwa kiwango cha asilimia 50. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali pamoja na kupunguza uingizaji wa magari husika ambayo kwa kiasi kikubwa yanasababisha uchafuzi wa mazingira kutokana na uwepo wa taka ngumu ambazo hutumia gharama kubwa katika kuziteketeza. Hatua hii inatarajia kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 106.70.

91. **Mheshimiwa Spika**, hatua hizi za ushuru wa bidhaa kwa ujumla wake zinatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **bilioni 355.09**.

**4. Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438**

92. **Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438 ili kuweka sharti la Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kuruhusiwa kuuza bidhaa zinazoharibika haraka (*perishable goods*) zilizotaifishiwa au kushikiliwa (*distrained or seized*) kutokana na sababu mbalimbali za kikodi ikiwemo ukiukwaji wa taratibu za kodi na kushindwa kulipa deni la kodi, kwa utaratibu wa minada (*public auction*) au uuzaji binafsi (*private treaty)* baada ya kutoa notisi kwa mlipakodi. Lengo la hatua hii ni kuepuka kupoteza

thamani ya bidhaa hizo kufuatia kukosekana kwa maghala ya kutosha ya kuhifadhia pamoja na kulinda mapato ya Serikali.

**5. Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, SURA 399**

93. **Mheshimiwa Spika**, inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura 399 ili kuongeza kiwango cha tozo ya uchakataji wa nyaraka za uingizaji wa mizigo nchini (*Customs Processing Fees*) kutoka asilimia 0.6 hadi asilimia 1. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali yatakayotumika katika kuboresha mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa kodi nchini. Hatua hii inatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **bilioni 203.23**.

**6. Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, SURA 290**

94. **Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za Serikali za kuongeza fursa za ajira na kurasimisha sekta isiyo rasmi, inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290, ili kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga asilimia 15 ya mapato yao ya ndani badala ya asilimia 10 iliyokuwa awali ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Kati ya asilimia 15 itakayotengwa, asilimia 10 itaelekezwa kwenye mikopo ya wanawake, vijana na wenye ulemavu kwa uwiano kama ilivyokuwa awali na asilimia tano (5) itatumika kwa ajili ya uwekezaji kwenye miradi ya ujenzi na maboresho ya masoko na maeneo ya biashara na ujasiriamali ili kuongeza fursa za ajira.

**7. Mgawanyo wa Mapato ya Mifuko ya Barabara, Nishati Vijijini, Maji, na Reli**

95. **Mheshimiwa Spika**, inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Nishati Vijijini, Sura 321; Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura 220; Sheria ya Reli, Sura 170; Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, Sura 272; pamoja na Sheria ya Petroli, Sura 392; ili kuweka mgawanyo wa mapato yatokanayo na vyanzo vya mifuko ya Barabara, Nishati Vijijini, Maji, na Reli kama ifuatavyo:

(i) Asilimia 70 kupelekwa moja kwa moja kwenye akaunti za mifuko tajwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mifuko husika;

(ii) Asilimia 25 kupelekwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali; na

(iii) Asilimia 5 kupelekwa kwenye akaunti maalum iliyopo Benki Kuu ya Tanzania kwa ajili ya kugharamia uwekezaji wa miundombinu katika maeneo maalum ya uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya mauzo ya nje (EPZ) na maeneo maalum ya kiuchumi (SEZ) ikiwemo kulipa fidia kwa ardhi ya wananchi iliyochukuliwa kwa ajili ya ujenzi wa maeneo maalum ya uzalishaji.

96. **Mheshimiwa Spika**, marekebisho haya yanalenga kuimarisha uwezo wa kifedha wa mifuko ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuhakikisha fedha zinaenda moja kwa moja, kuboresha miundombinu wezeshi katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji (EPZ na SEZ), na kuiwezesha Serikali kuendelea kugharamia mahitaji ya lazima ikiwemo ulipaji wa madeni ya Serikali.

**8. Sheria ya Ardhi, SURA 113**

97. **Mheshimiwa Spika**, inapendekezwa pia kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ardhi, Sura 113 ili kuweka mgawanyo wa asilimia 20 ya mapato yanayotokana na kodi ya pango la ardhi (*land rent*) yanayorejeshwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kama ifuatavyo: asilimia 10 kupelekwa Wizara yenye dhamana na masuala ya Ardhi na asilimia 10 kupelekwa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Lengo la hatua hii ni kuimarisha ushirikiano na kuongeza ufanisi katika upimaji wa ardhi na ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi. Aidha, Wizara ya Fedha itaweka utaratibu maalumu wa matumizi ya fedha hizo.

**9. Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, SURA 197**

98. **Mheshimiwa Spika**, katika kuendelea kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha za umma, Serikali inapendekeza kufanya maboresho ya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura 197 ili kupunguza kiwango cha ukomo wa mkopo wa muda mfupi (*overdraft*) kutoka asilimia 18 ya mapato halisi ya ndani ya mwaka wa fedha uliopita hadi asilimia 14.

99. **Mheshimiwa Spika**, ninapendekeza pia kufanya maboresho kwenye Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura 197 kwa kufuta kifungu cha 69 na kuandikwa upya ili kubainisha vigezo ambavyo Benki inaweza kuruhusu mikopo ya muda mfupi kwa Serikali endapo kutatokea matukio yasiyotabirika au yasiyozuilika, na kubainisha masuala yatakayochukuliwa kuwa matukio yasiyotabirika au yasiyozuilika.

**10. Sheria ya Tume ya Mipango**

100. **Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya maboresho ya Kifungu cha 6 cha Sheria ya Tume ya Mipango ili kuweka utaratibu kwa miradi ya maendeleo ya Kitaifa kutathminiwa kwa kuzingatia video vya kiufundi, kifedha, kimazingira na kiuchumi kabla ya kuingizwa katika bajeti ya Serikali. Aidha, Tathmini za kimazingira zitajumuisha tathmini za athari za mabadiliko ya tabianchi.

**11. Utafiti na Uwekezaji katika Sekta ya Madini**

101. **Mheshimiwa Spika**, ili kuimarisha utafiti na uwekezaji katika sekta ya madini nchini, inapendekezwa Wizara ya Madini kuanzisha mfuko wa utafiti wa madini nchini na kubakiza asilimia 10 ya mapato yatokanayo na sekta husika kwa ajili ya kugharamia tafiti hizo. Aidha, fedha hizo zitaingizwa kwenye akaunti maalum itakayofunguliwa Benki Kuu na matumizi yake yatafanyika baada ya kupata idhini ya Mlipaji Mkuu wa Serikali.

**12. Sheria ya Rufaa za Kodi, SURA 408**

102. **Mheshimiwa Spika**, inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Rufaa za Kodi, Sura 408 ili kuongeza muda wa

kushughulikia utatuzi wa migogoro ya kodi nje ya mahakama kwa njia ya maridhiano (*amicable settlement*) baina ya Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania na mlipakodi kutoka siku 60 hadi siku 90 tangu Bodi ya Rufaa ya Kodi (TRAB) au Baraza la Rufaa ya Kodi (TRAT) lilipotoa amri ya kuruhusu shauri hilo kusuluhishwa kwa utaratibu huo. Lengo la hatua hii ni kuhakikisha uwepo wa muda wa kutosha wa kutafuta suluhu ya migogoro ya kodi kwa njia ya maridhiano.

**13. Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, SURA 220**

103. **Mheshimiwa Spika**, inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura 220 ili kutambua vipengele vya msamaha wa ushuru wa barabara na mafuta vilivyopo kwenye Mikataba ya Msingi (*Framework Agreements*) iliyosainiwa baina ya Serikali na wawekezaji wa madini, baada ya kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri. Lengo la hatua hii ni kuwezesha utekelezaji wa miradi ya ubia ya uchimbaji wa madini nchini. Aidha, hatua hii itaenda sambamba na Serikali kuweka taratibu za usimamizi zitakazotoa mwongozo kuhusu utolewaji wa msamaha huo. Lengo la hatua hii ni kutekeleza matakwa ya mikataba husika, kutimiza jukumu la Serikali la kusamehe kodi kwenye utekelezaji wa miradi hiyo na kuhakikisha miradi ya ubia inatekelezwa kwa wakati.

**14. Sheria ya Usalama Barabarani, SURA 168**

104. **Mheshimiwa Spika**, inapendekezwa kufanya marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani, Sura 168 ili kuruhusu gari au trela iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria za usajili za Tanzania Zanzibar kutumika Tanzania Bara likiwa na namba za usajili za Tanzania Zanzibar, pale ambapo kodi zote kwenye gari au trela husika zimelipwa kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo. Aidha, kwa sasa, utaratibu huu unatumika kwa magari yanayotoka Tanzania Bara kwenda Tanzania Zanzibar. Lengo la hatua hii ni kutatua changamoto zilizopo kwenye matumizi ya vyombo hivyo baina ya pande mbili za Muungano pasipo kuathiri mapato ya Serikali.

**15. Sheria ya Kudhibiti Uingizwaji wa Bidhaa Nchini, SURA 276**

105. **Mheshimiwa Spika**, inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kudhibiti Uingizwaji wa Bidhaa Nchini, Sura 276 kama ifuatavyo:

(i) Kuweka sharti la tozo ya maendeleo ya viwanda kutotozwa kwenye bidhaa zinazozalishwa katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC Partners States*) ambazo zinakidhi vigezo vya uasili (*Rules of Origins*). Aidha, hatua hii itaenda sambamba na kuruhusu vifungu na viwango vya utozaji kutumika kwa nchi mwanachama wa EAC pale itakapobainika kuwa, nchi husika imeweka vikwazo vya kibiashara kwa bidhaa zinazotoka Tanzania vikijumuisha kutoza kodi, ada na tozo mbalimbali kwenye bidhaa hizo. Lengo la hatua hii ni kuendana na matakwa ya Itifaki ya Uanzishwaji wa Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yanayoelekeza nchi wanachama kuzuia ubaguzi wa kikodi ili kuruhusu biashara huria na kuleta ushindani wa haki;

(ii) Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia 5 kwenye madaftari (*excercise books na notebooks*) yanayoingizwa nchini yanayotambulika kwa *HS Codes* 4820.10.00 na 4820.20.00. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shillingi **milioni 978.5**;

(iii) Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia 5 kwenye trela (*trailers*) zinazoingizwa nchini zinazotambulika kwa *HS Codes* 8716.31.90, 8716.39.90 na 8716.40.90. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shillingi **bilioni 16.66**;

(iv) Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye nyavu za kuvulia samaki zinazoingizwa nchini zinazotambulika kwa *HS Code* 5608.11.00;

(v) Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia 5 kwenye milango, madirisha, pamoja na fremu zake

zinazoingizwa nchini zinazotambulika kwa *HS Code* 7610.10.00. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shillingi **milioni 280.3**;

(vi) Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye bidhaa za chuma (*steel structure*) zinazoingizwa nchini zinazotambulika kwa *HS Code* 7308.90.99. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shillingi **bilioni 16.86**; na

(vii) Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia 5 kwenye *aluminium structures* zinazotambulika kwa *HS Code* 7610.10.00. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shillingi **bilioni 1.14**;

106. **Mheshimiwa Spika**, lengo la hatua hizi ni kuvutia uwekezaji nchini, kuchochea mauzo nje ya nchi na kulinda uzalishaji wa ndani kwa kuwa bidhaa husika zinazalishwa kwa wingi nchini. Hatua hii inatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **bilioni 37.04**.

**16. Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi, SURA 196**

107. **Mheshimiwa Spika**, inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi, Sura 196 kama ifuatavyo:

(i) Kutoza tozo ya usafirishaji wa bidhaa kwenda nje ya nchi kwa kiwango cha asilimia 30 ya thamani ya mzigo (FOB) au shilingi 200 kwa kila kilo moja kutegemeana na kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye taka za karatasi (*waste paper*) zinazotambulika kwa *HS Code* 4707.00.00. Lengo la hatua hii ni kuchochea uongezaji wa thamani nchini na kuhakikisha upatikanaji wa malighafi hiyo kwa wazalishaji wa karatasi na maboksi nchini. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 415.0**;

(ii) Kutoza tozo ya usafirishaji wa bidhaa kwenda nje ya nchi kwa kiwango cha asilimia 10 au shilingi 200 kwa kila kilo

kutegemeana na kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye madini ya *quartz* yanayotambulika kwa *HS Heading* 25.06 na *Feldspar* zinazotambulika kwa *HS Code* 2529.10.00. Lengo la hatua hii ni kuhakikisha uwepo wa malighafi za kutosha kwa wazalishaji wa marumaru na vioo nchini. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **bilioni 6.08**; na

(iii) Kutoza tozo ya usafirishaji wa bidhaa kwenda nje ya nchi kwa kiwango cha shilingi 50 kwa kila kilo ya: pumba za ngano (*wheat bran*) zinazotambulika kwa *HS Code* 2302.30.00; mashudu ya pamba (cotton cake) yanayotambulika kwa *HS Code* 2306.10.00; pumba za mpunga (*rice bran*) zinazotambulika kwa *HS Code* 2302.40.00; pumba za mahindi (*maize bran*) zinazotambulika kwa *HS Code* 2302.10.00; na mashudu ya alizeti (*sunflower cake*) yanayotambulika kwa *HS Code* 2306.30.00. Lengo hatua hii kuhakikisha upatikanaji wa kutosha wa bidhaa husika ambazo ni malighafi muhimu kwenye uzalishaji wa vyakula vya mifugo. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **bilioni 17.95**.

108. **Mheshimiwa Spika**, hatua hizi kwa ujumla wake zinatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **bilioni 24.44**.

**17. Sheria ya Ushuru wa Stempu, SURA 189**

109. **Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Ushuru wa Stempu, Sura 332 ni moja ya sheria kongwe na ambayo imechukua muda mrefu kurekebishwa katika ushuru wa baadhi ya Hati na nyaraka. Inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Jedwali la sheria hiyo kama ifuatavyo:

(i) Kuboresha tafsiri ya neno *lease* ili kujumuisha hati za ubadilishanaji wa mali zinazohamishika (*moveable property*) kwenye wigo wa utozaji wa ushuru wa stempu;

(ii) Kuongeza kima cha thamani ya utozaji wa ushuru wa stempu kwenye Hati ya Mauzo ya mali kwa njia ya dhamana (*bills of sale by way of collateral security*) kutoka shilingi 1,000 hadi shilingi 10,000;

(iii) Kuongeza kima cha juu cha ukomo wa utozaji wa ushuru wa stempu kwenye Hati ya Mauzo kwa njia ya dhamana (*bills of sale by way of security*) kutoka shilingi 10,000 hadi shilingi 100,000;

(iv) Kubadili wigo wa thamani ya mitaji kwenye Hati za Ubia (*partnership deeds*) pamoja na viwango vya ushuru wa stempu kwenye Hati husika kama ifuatavyo: kutoza kiwango cha shilingi 5000 kwa Hati zenye thamani ya mitaji isiyozidi shilingi 1,000,000 na kiwango cha shilingi 10,000 kwa Hati zinazozidi thamani ya mitaji ya shilingi 1,000,000. Aidha, utaratibu wa awali ulihusisha kutoza kiwango cha shilingi 1,000 kwa Hati zenye thamani ya mitaji isiyozidi shilingi 10,000; shilingi 5,000 kwa Hati zenye thamani inayozidi shilingi 100,000 lakini haizidi shilingi 1,000,000 pamoja na shilingi 10,000 kwenye Hati zenye thamani inayozidi shilingi 1,000,000;

(v) Kuongeza kiwango cha ushuru wa stempu kwenye hundi (*cheque*) kutoka shilingi 100 hadi shilingi 500;

(vi) Kuongeza kiwango cha ushuru wa stempu kwenye Hati za Kusitisha Mikataba ya Ukodishaji (*surrender of lease*) kutoka shilingi 1000 hadi shilingi 2000;

(vii) Kutoza ushuru wa stempu kwa kiwango cha shilingi 5000 kwenye hati za ubadilishanaji (*bills of exchange*) wa mali; na

(viii) Kutoza ushuru wa stempu kwa kiwango cha asilimia 0.5 kwenye hati ya uhamishaji wa ardhi ya matumizi ya kilimo badala ya kiwango maalumu cha shilingi 500 kinachotozwa kwa sasa.

110. **Mheshimiwa Spika**, lengo la hatua hizi ni kuendana na kanuni za usawa za utozaji kodi, kuongeza wigo wa kodi pamoja na kulinda thamani ya fedha kwa kuwa viwango husika havijabadilishwa kwa muda mrefu. Hatua hizi kwa pamoja zinatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shillingi **bilioni 11.08**.

**18. Sheria ya Tume ya Ushindani, SURA 285**

111. **Mheshimiwa Spika**, inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 88 cha Sheria ya Tume ya Ushindani, Sura 285 kwa kubainisha kuwa, mapato ya Baraza la Ushindani (FCT) yanajumuisha asilimia 0.5 ya mapato ya mamlaka za udhibiti zilizoorodheshwa kwenye kifungu cha 88(1)(d) cha Sheria husika ikiwemo EWURA, LATRA, TCRA na TCAA. Hatua hii inalenga kutatua changamoto zilizopo ambapo sheria imebainisha vyanzo vya mapato na Taasisi zinazopaswa kuwasilisha sehemu ya mapato yake Baraza la Ushindani (FCT) bila kuweka viwango husika.

**19. Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi ya Mwaka 2024**

112. **Mheshimiwa Spika**, inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi ya Mwaka 2024 ili kujumuisha vichwa vya trela (*road tractors for semi-trailers*) vinavyotambulika kwa *HS Codes* 8701.21.90, 8701.22.90, 8701.23.90, na 8701.24.90 kwenye orodha ya bidhaa zisizostahili msamaha wa kodi (*negative list*). Lengo hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani, ajira na mapato ya Serikali. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **bilioni 57.16**.

**20. Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004**

113. **Mheshimiwa Spika**, ninapenda kukufahamisha kwamba, mkutano wa Mashauriano Kabla ya Bajeti wa Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*Meeting of the EAC Pre-Budget Consultations of Ministers/Cabinet Secretary of Finance*) uliofanyika tarehe 15 Mei 2026 jijini Arusha, pamoja na masuala mengine ulijadili na kupendekeza hatua mbalimbali za kisera ikiwemo mabadiliko ya Viwango vya Pamoja vya Ushuru wa Forodha vya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC Common External Tariff*) zinazopendekezwa kutekelezwa kwa mwaka 2026/27.

Aidha, mkutano huo ulipendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 kwa lengo la kutatua changamoto zilizopo katika utekelezaji wa sheria hiyo.

114. **Mheshimiwa Spika**, hatua zinazopendekezwa zinalenga kulinda viwanda vya ndani, kuvutia uwekezaji, kupunguza gharama za uzalishaji wa bidhaa nchini, kulinda walaji, kuongeza fursa za ajira, kuchochea ukuaji wa sekta mbalimbali za kiuchumi, kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa zinazotoka nje pamoja na kuongeza mapato ya Serikali.

115. **Mheshimiwa Spika**, mapendekezo ya Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ya kufanya mabadiliko kwenye Viwango vya Pamoja vya Ushuru wa Forodha yanahusisha hatua mpya na zinazoendelea kutekelezwa katika mwaka 2025/26. Hatua hizo ni kama ifuatavyo:

**(i) Mapendekezo ya hatua mpya za mabadiliko ya Viwango vya Ushuru wa Forodha ni kama ifuatavyo:**

(a) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 au dola za Marekani mbili (2) kwa mita za mraba (SQM) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye mawe yanayotumika kama mapambo katika ujenzi (*monumental or building stone)* yanayotambulika kwa *HS Heading* 68.02 kwa lengo la kuhamasisha matumizi ya mawe yanayopatikana ndani ya nchi;

(b) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 au dola za Marekani 550 kwa tani kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 25 pekee kwenye bidhaa za aluminium (*aluminium bars, rods and profiles*) zinazotambulika kwa *HS Heading* 76.04. Hatua hii inalenga kulinda viwanda vya ndani, kuhamasisha uwekezaji nchini, kuongeza mapato ya Serikali na

kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo kutoka nje;

(c) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 au dola za Marekani 350 kwa tani kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 25 pekee kwenye sabuni zinazotambulika kwa *HS Codes* 3402.49.00; 3402.50.00; na 3402.90.00. Hatua hii inalenga kulinda viwanda vya ndani vinavyozalisha bidhaa hii, kuhamasisha uwekezaji nchini na kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo kutoka nje;

(d) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 au dola za Marekani 250 kwa tani kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 25 pekee kwenye stiki za kuchomea (*welding electrodes*) zinazotambulika kwa HS Code 8311.10.00. Hatua hii inalenga kulinda viwanda vya ndani vinavyozalisha stiki hizi, kuhamasisha uwekezaji nchini na kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo kutoka nje;

(e) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 0 kwenye mafuta ghafi ya mchikichi (*Crude Palm Oil – CPO*) yanayotambulika kwa HS Code 1511.10.00 kwa lengo la kuhamasisha matumizi ya mbegu zinazozalishwa ndani ya nchi katika kuchakata mafuta ya kula na kuvutia uwekezaji. Hatua hii pia inalenga kuondoa changamoto ya udanganyifu wa uainishaji wa bidhaa unaofanywa na baadhi ya waagizaji wasio waaminifu ambao hutumia nafuu iliyopo kwenye mafuta ghafi ya mchikichi kuingiza mafuta ya mchikichi yaliyochakatwa kwa kiwango cha kati (*semi refined palm oil*);

(f) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 0 kwenye chokaa inayotambulika kwa *HS Code* 2836.50.00 kwa lengo la kulinda viwanda

vya ndani pamoja na kuvutia uwekezaji zaidi katika sekta hii;

(g) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 au dola za Marekani 0.30 kwa kila mita moja kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 25 pekee kwa mwaka mmoja kwenye vitambaa vya pamba (*cotton grey fabric*) vinavyotambulika kwa *HS Codes* 5208.11.00; 5208.12.00; 5208.13.00; 5208.19.00; 5209.11.00; 5209.12.00; 5209.19.00; 5210.11.00; 5210.19.00; 5211.11.00; 5211.12.00; 5211.19.00; 5212.11.00; na 5212.21.00. Lengo la hatua hii ni kuchochea uzalishaji wa vitambaa hivyo kwa kutumia pamba inayozalishwa hapa nchini, kuongeza ajira na mapato ya Serikali pamoja na kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo kutoka nje;

(h) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwenye milango na madirisha ya plastiki yanayotambulika kwa HS Code 3925.20.00 kwa lengo la kulinda wazalishaji wa bidhaa hizo hapa nchini;

(i) Kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10 kwenye magari yanayotumia nishati ya umeme yanayotambulika kwa *HS Codes* 8702.40.19; 8702.40.22; 8702.40.29; 8702.40.99; 8703.80.90 na 8704.60.90. Hatua hii inalenga kuhamasisha matumizi ya nishati ya umeme katika sekta ya usafiri ili kupunguza utegemezi wa mafuta ya petroli na dizeli nchini;

(j) Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kubadilisha kiwango cha Ushuru wa Forodha kutoka kiwango cha asilimia 35 pekee hadi kiwango cha asilimia 35 au dola za Marekani 3.0 kwa kila mita moja ya mraba (*square meter*) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye marumaru zinazotambulika kwa HS Codes 6907.21.00; 6907.22.00; 6907.23.00; 6907.30.00; na 6907.40.00. Hatua hii inalenga kulinda viwanda vya ndani ya Jumuiya vinavyozalisha

marumaru, kuhamasisha uwekezaji pamoja na kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo kutoka nje;

(k) Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kubadilisha kiwango cha Ushuru wa Forodha kutoka kiwango cha asilimia 35 pekee hadi kiwango cha asilimia 35 au dola za Marekani 350 kwa tani kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye misumari inayotambulika kwa *HS Code* 7317.00.00. Hatua hii inalenga kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hizo ndani ya Jumuiya, kuhamasisha uwekezaji, kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo kutoka nje pamoja na kuongeza mapato ya Serikali;

(l) Kuweka unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye karatasi zinazotambulika kwa *HS Codes* 4805.24.00; na 4805.25.00 zinazotumika kutengeneza vifungashio aina ya maboksi (*corrugated boxes*). Lengo la hatua hii ni kuwapa unafuu wazalishaji wa vifungashio hivyo hapa nchini ili wananchi waweze kuvipata kwa urahisi na kwa gharama nafuu;

(m) Kuweka unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye karatasi zinazotambulika kwa *HS Codes* 4804.19.00; 4804.39.00 na 4804.52.00 zinazotumika kutengeneza vifungashio aina ya maboksi (*corrugated boxes*). Lengo la hatua hii ni kuwapa unafuu wazalishaji wa vifungashio hivyo hapa nchini ili wananchi waweze kuvipata kwa urahisi na kwa gharama nafuu;

(n) Kuweka unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10 au asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye

malighafi zinazotambulika kwa *HS Codes* 3506.91.00 na 3920.10.10 zinazotumika kutengeneza vifungashio vya aina mbalimbali. Lengo la hatua hii ni kuwapa unafuu wazalishaji wa vifungashio hapa nchini ili wananchi waweze kuvipata kwa urahisi na kwa gharama nafuu;

(o) Kuweka unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi zinazotambulika kwa *HS Codes* 3210.00.99 zinazotumika katika utengenezaji wa *aluminium profile*. Lengo la hatua hii ni kuwapa unafuu wazalishaji wa bidhaa za *aluminium* hapa nchini na kuhamasisha uwekezaji;

(p) Kuweka unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 kwenye vifungashio vinavyotumiwa na wazalishaji wa madawa ya mifugo (*acaricides*) kwa mwaka mmoja. Hatua hii inalenga kupunguza gharama za uzalishaji wa dawa za mifugo nchini, kuhamasisha uwekezaji, na kuongeza ajira;

(q) Kuweka unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 25 kwenye nyaya (*prestressed steel wire or spiral PC wire*) zinazotambulika kwa *HS Codes* 7217.10.00 na 7217.90.00 zinazotumika katika utengenezaji wa nguzo za umeme za zege. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za uzalishaji wa nguzo hizo ndani ya Jumuiya ili kuwezesha zoezi la ubadilishaji wa nguzo za miti kwa kuweka nguzo za zege pamoja na usambazaji wa umeme kwa wananchi;

**(ii) Mapendekezo ya kuendelea na utekelezaji wa Viwango vya Ushuru wa Forodha vilivyokuwa vinatekelezwa mwaka 2025/26 ni kama ifuatavyo:**

(a) Kupunguza kiwango cha Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye

vifaa vya kielektroniki vinavyotumika kuhasibu mapato ya Serikali *(Cash registers, Electronic Fiscal Device (EFD) Machines and Point of Sale (POS)* machines) vinavyotambulika kwa *HS Codes* 8470.50.00 na 8470.90.00. Lengo la hatua hii ni kuwezesha upatikanaji wa vifaa hivi kwa gharama nafuu na kuhamasisha matumizi ya vifaa husika katika kuhasibu mapato ya Serikali;

(b) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye unga wa kakao unaoingizwa kutoka nje unaotambulika kwa *HS Code* 1805.00.00. Hatua hii inalenga kuhamasisha kilimo cha zao la kakao, uongezaji wa thamani wa zao hilo nchini pamoja na kuongeza mapato ya Serikali;

(c) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye fito za plastiki zijulikanazo kama *PVC Profiles* zinazotambulika kwa *HS Codes* 3916.10.00; 3916.20.00; na 3916.90.00 zinazotumika kutengenezea fremu za milango na madirisha. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali pamoja na kuzuia udanganyifu unaofanywa na waagizaji wasio waaminifu kwa kuwa bidhaa hizo ni mbadala wa bidhaa za aluminium zinazotozwa kiwango kikubwa cha ushuru wa forodha;

(d) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 au dola za Marekani 1.35 kwa kila kilo moja kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 25 pekee kwenye viberiti (safety match) vinavyotambuliwa kwa HS Code 3605.00.00 kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha viberiti nchini dhidi ya bidhaa zenye ruzuku kutoka nje na hivyo kuwa na ushindani sawa katika soko;

(e) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 60 badala ya asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye maji

ya kunywa (mineral and aerated waters) yanayotambulika kwa *HS Code* 2201.10.00. Hatua hii inalenga kulinda viwanda vinavyozalisha maji ya kunywa nchini;

(f) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 0 kwenye Gypsum Powder inayotambulika kwa HS Code 2520.20.00 kwa mwaka mmoja kwa lengo la kulinda wazalishaji wa bidhaa hiyo hapa nchini;

(g) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 pekee badala ya asilimia 35 au dola za Marekani 0.40 kwa kilo moja kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwa mwaka mmoja kwenye mitumba inayotambulika kwa HS Codes 6309.00.10; 6309.00.20; na 6309.00.90. Hatua hii inalenga kuweka unafuu kwa watumiaji wa bidhaa hii hapa nchini;

(h) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye matairi mapya ya pikipiki (new pneumatic tyres of rubber) yanayotambulika kwa HS Code 4011.40.00. Lengo la hatua ni kuhamasisha uzalishaji wa matairi hayo nchini kwa kuwa kuna malighafi za kutosha;

(i) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye taulo za watoto (baby diapers) zinazotumbulika kwa HS code 9619.00.90. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hii nchini, kuhamasisha uwekezaji pamoja na kuongeza mapato ya Serikali;

(j) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye nyuzi za pamba (cotton yarns) zinazotambulika kwa HS Headings 52.05, 52.06 na 52.07 isipokuwa nyuzi za pamba zinazotambulika kwa HS Code 5205.23.00. Lengo la hatua ni kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hiyo

na kuongeza thamani ya zao la pamba pamoja na kuhamasisha uwekezaji nchini;

(k) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwenye mazao ya bustani ikiwemo matunda yanayotambulika kwa *HS Codes* 0604.20.00; 0604.90.00; 0808.10.00; na 0808.30.00 kwa mwaka mmoja. Hatua hii inalenga kulinda wazalishaji wa mazao hayo hapa nchini;

(l) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwenye kamba zinazotengenezwa kwa nyuzi zenye asili ya plastiki (*Twine of other synthetic fibers*) zinazotambulika kwa *HS Code* 5607.50.00 kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hii hapa nchini pamoja na kuongeza ajira;

(m) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye kadi janja (*smart cards*) zinazotambulika kwa *HS Code* 8523.52.00 zitakazoingizwa nchini na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). Hatua hii inalenga kupunguza gharama za uingizaji wa kadi hizo ili kurahisisha upatikanaji wa vitambulisho vya Taifa kwa wananchi;

(n) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka kiwango cha asilimia 50 hadi asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye vitenge vinavyotambulika kwa *HS Codes* 5208.51.10; 5208.52.10; 5209.51.10; 5210.51.10; 5211.51.10; 5212.15.10; 5212.25.10; 5513.41.10 na 5514.41.10. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu kwenye uagizaji wa vitenge ili kuwezesha upatikanaji wa bidhaa hiyo kwa wananchi na kwa gharama nafuu;

(o) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwenye karatasi za kutolea risiti za kielektroniki zinazotambulika kwa HS Code 4811.90.00 kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda

viwanda vya ndani vinavyozalisha bidhaa hii pamoja na kuhamasisha uwekezaji nchini;

(p) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 badala ya asilimia 100 au dola za Marekani 460 kwa kila tani kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwa mwaka mmoja kwenye sukari ya matumizi ya kawaida inayotambulika kwa HS Code 1701.14.90 inayoagizwa kutoka nje ya nchi kwa vibali maalum kutoka Bodi ya Sukari Tanzania kwa lengo la kuziba pengo la uzalishaji wa sukari hapa nchini;

(q) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 badala ya asilimia 10 kwenye vioo vya kawaida na vioo vigumu (*float and toughened glasses*) vinavyotambulika kwa *HS Codes* 7005.10.00; 7005.21.00; 7005.29.00; 7005.30.00; 7007.19.00; 7007.29.00 na 7008.00.00 kwa mwaka mmoja. Hatua hii inalenga kulinda wazalishaji wa vioo hivyo hapa nchini ili viweze kuwa shindani dhidi ya vioo kutoka nje ya nchi;

(r) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 50 badala ya asilimia 35 kwenye chumvi inayotambulika kwa HS Code 2501.00.90 kwa mwaka mmoja ili kulinda wazalishaji wa chumvi nchini;

(s) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 kwa mwaka mmoja badala ya asilimia 0 kwenye mafuta ghafi ya soya, karanga, nazi, mnyonyo, haradali na mengineyo yanayotambulika kwa HS Codes 1507.10.00; 1508.10.00; 1513.11.00; 1513.21.00; 1514.11.00; 1514.91.00 na 1515.11.00. Lengo la hatua hii ni kuoanisha viwango vya mafuta ghafi haya vifanane na viwango vya mafuta ghafi ya alizeti, pamba, mahindi na mafuta ghafi mengineyo ambayo viwango vyake ni asilimia 10. Aidha, hatua hii pia inalenga kulinda na kuhamasisha uzalishaji wa mbegu za mafuta ya kula nchini, kuongeza ajira pamoja na kulinda fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mafuta hayo nje ya nchi;

(t) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye karatasi zinazotambulika kwa HS Code 4804.51.00 kwa lengo la kulinda viwanda vinavyozalisha karatasi hizo hapa nchini;

(u) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye mabasi ya abiria yanayotumia mafuta ya petroli, dizeli na gesi yanayotambulika kwa *HS Codes* 8702.10.99; 8702.20.99 na 8702.90.99 yanayoingizwa nchini kwa ajili ya mradi wa mabasi yaendayo haraka. Hatua hii inalenga kupunguza gharama za uingizaji wa mabasi hayo ili kurahisisha huduma ya usafiri kwa wananchi;

(v) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa ya mbao ikiwemo *Medium Density Fibreboard (MDF)* zinazotambulika kwa *HS Heading* 44.11 kwa lengo la kulinda wazalishaji wa ndani;

(w) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye vinia na mbao laini (veneered panels and plywood) zinazotambulika kwa HS Heading 44.12 kwa lengo la kulinda wazalishaji wa ndani;

(x) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 au dola za Marekani 300 kwa kila tani moja kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye mafuta ya kula yaliyochakatwa kwa kiwango cha mwisho (refined edible oils) yanayotambulika kwa HS Codes 1507.90.00; 1508.90.00; 15.09; 15.10; 1511.90.30; 1511.90.90; 1512.19.00; 1512.29.00; 1513.19.00; 1513.29.00; 1514.19.00; 1514.99.00; 1515.19.00; 1515.29.00; 1515.50.00; 1515.60.00 na 1515.90.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani na kuhamasisha uchakataji wa mbegu

zinazozalishwa ndani ya nchi na mafuta ghafi yaliyoingizwa nchini ili kuongeza thamani ya bidhaa, kukuza ajira, pamoja na kuongeza mapato ya Serikali;

(y) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 au dola za Marekani 125 kwa kila tani kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 10 pekee kwenye bidhaa za chuma kwa mwaka mmoja. Bidhaa hizi zinatambulika kwa *HS Codes* 7209.16.00; 7209.17.00; 7209.18.00; 7209.25.00 7209.26.00; 7209.27.00; 7209.28.00; 7209.90.00; 7211.23.00; 7211.90.00; 7225.50.0 na 7226.92.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani vinavyozalisha bidhaa hizo, kuhamasisha uwekezaji, kuongeza mapato ya Serikali, kukuza ajira nchini na kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo kutoka nje;

(z) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 au dola za Marekani 500 kwa kila tani kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 35 kwenye mabati yanayotambulika kwa *HS Codes* 7210.30.00 na 7210.41.00 kwa mwaka mmoja. Hatua hii inalenga kulinda viwanda vinavyozalisha mabati hayo ndani ya nchi, kuhamasisha uwekezaji, kuongeza ajira na mapato ya Serikali na kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo kutoka nje;

(aa) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 au dola za Marekani 350 kwa kila tani kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 25 au dola za Marekani 200 kwa kila tani kwa mwaka mmoja kwenye mabati yanayotambulika kwa *HS Codes* 7210.49.00; 7210.61.00; 7210.69.00; 7210.70.00; na 7210.90.00. Hatua hii inalenga kulinda viwanda vya ndani, kuongeza ajira na mapato ya Serikali pamoja na kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo kutoka nje;

(bb) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 au dola za Marekani 125 kwa kila tani moja kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 10 pekee kwenye mabati yanayotambulika kwa *HS Code* 7212.20.00 kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani, kuhamasisha uwekezaji, kuongeza ajira na mapato ya Serikali na kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo kutoka nje;

(cc) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 au dola za Marekani 300 kwa kila tani moja kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 25 au dola za Marekani 200 kwa kila tani moja kwa mwaka mmoja kwenye mabati yanayotambulika kwa *HS Code* 7212.30.00. Hatua hii inalenga kulinda viwanda vya ndani, kuongeza ajira na mapato ya Serikali pamoja na kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo kutoka nje;

(dd) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 au dola za Marekani 350 kwa kila tani moja kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye mabati yanayotambulika kwa HS Codes 7212.40.00; na 7212.50.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani, kuongeza ajira na mapato ya Serikali pamoja na kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo kutoka nje;

(ee) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 au dola za Marekani 300 kwa kila tani moja kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 10 pekee kwa mwaka mmoja kwenye mabati yanayotambulika kwa HS Code 7212.60.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani, kuhamasisha uwekezaji katika sekta hii, kuongeza ajira na mapato ya Serikali pamoja na kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo kutoka nje;

(ff) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 au dola za Marekani 250 kwa kila tani moja kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 25 au dola za Marekani 200 kwa kila tani moja kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye nondo zinazotambulika kwa HS Codes 7213.10.00; 7213.20.00; na 7213.99.00 kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha nondo hapa nchini, kuhamasisha uwekezaji, kuongeza ajira na mapato ya Serikali pamoja na kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo kutoka nje;

(gg) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 au dola za Marekani 250 kwa kila tani moja kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 35 pekee kwa mwaka mmoja kwenye nondo zinazotambulika kwa *HS Heading* 72.14. Hatua hii inalenga kulinda viwanda vya ndani, kuvutia uwekezaji, kuongeza ajira na mapato ya Serikali pamoja na kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo kutoka nje;

(hh) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 au dola za Marekani 300 kwa kila tani moja kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 10 pekee kwenye bidhaa za chuma zinazotambulika kwa HS Codes 7225.91.00; 7225.92.00; na 7225.99.00 kwa mwaka mmoja.
Hatua hii inalenga kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hizo hapa nchini, kuhamasisha uwekezaji, kuongeza ajira na mapato ya Serikali na kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo kutoka nje;

(ii) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 au dola za Marekani 300 kwa kila tani moja kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 10 pekee kwenye bidhaa za chuma zinazotambulika kwa HS Code 7226.99.00 kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua

hii ni kulinda viwanda vya ndani, kuongeza ajira, kuvutia uwekezaji, kuongeza mapato ya Serikali pamoja na kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo kutoka nje;

(jj) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 au dola za Marekani 250 kwa kila tani moja kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 25 pekee kwenye bidhaa za chuma ikiwemo bomba za chuma zinazotambulika kwa HS Codes 7306.30.00; 7306.50.00; 7306.61.00; 7306.69.00; na 7306.90.00 kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hizo hapa nchini, kuhamasisha uwekezaji, kuongeza ajira na mapato ya Serikali na kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo kutoka nje;

(kk) Kuweka unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye ngano inayotambulika kwa *HS Codes* 1001.99.10; na 1001.99.90 kwa lengo la la kupunguza gharama kwa viwanda vinavyozalisha unga wa ngano nchini ili kurahisisha upatikanaji wa bidhaa hiyo kwa wananchi;

(ll) Kuweka unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa Duty Remission kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi ya kutengeneza sabuni ijulikanayo kama RBD Palm Stearin inayotambulika kwa HS Code 1511.90.40 kwa lengo la kutoa unafuu kwa wazalishaji wa sabuni nchini;

(mm) Kuweka unafuu wa Ushuru wa Forodha kwenye malighafi, vipuri na mashine vinavyotumika katika utengenezaji wa nguo na viatu vya ngozi. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha ukuaji wa sekta ya nguo na ngozi nchini;

(nn) Kuweka unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa Duty Remission kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10 au asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza sabuni (organic surface-active agents including LABSA) zinazotambulika kwa HS Codes 3402.31.00; 3402.39.00; 3402.49.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa sabuni nchini;

(oo) Kuweka unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa Duty Remission kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10 au asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kuchakata ngozi zinazotambulika kwa HS Codes 3208.20.10; 3208.20.20; 3208.90.20 na 3210.00.10. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu kwa wachakataji wa ngozi nchini;

(pp) Kuweka unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa Duty Remission kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwa waunganishaji wa pikipiki za matairi matatu bila kujumuisha fremu (CKD for threewheelers motorcycles excluding chassis and its components) zinazotambulika kwa HS Code 8704.21.90 ili ziweze kutengenezwa na kuunganishwa hapa nchini.
Lengo la hatua hii ni kuwapa unafuu waunganishaji wa pikipiki hizo nchini ili kurahisisha usafirishaji wa mizigo pamoja na kuhamasisha uwekezaji nchini;

(qq) Kuweka unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa Duty Remission kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza sabuni (toilet soap) zinazotambulika kwa HS Code 3401.20.10. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu kwa wazalishaji wa sabuni nchini, kuhamasisha uwekezaji na kuongeza ajira;

(rr) Kuweka unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa Duty Remission kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10 na asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza nyaya za umeme (electrical

cables) zinazotambulika kwa HS Codes 7312.10.00; 7217.20.00; 7408.19.00; 7409.11.00; 7605.21.00; 2710.19.56; 3815.90.00; 5402.19.00; 5903.90.00; 7907.00.00; na 2712.10.00. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu kwa watengenezaji wa nyaya hizo pamoja na kuvutia uwekezaji nchini;

(ss) Kuweka unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa Duty Remission kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 35, asilimia 25 au asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza rejeta za vyombo vya moto zinazotambulika kwa *HS Codes* 7409.11.00; 7409.19.00; 7409.21.00; 7410.11.00; 7410.12.00; 8001.10.00; 3810.90.00. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu pamoja na kuchochea uwekezaji katika uzalishaji wa rejeta hapa nchini;

(tt) Kuweka unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye betri za umeme (*lithium-ion electric accumulators*) zinazotambulika kwa *HS Code* 8507.60.00 zinazotumiwa na wazalishaji au waunganishaji wa magari na pikipiki za umeme nchini. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu pamoja na kuchochea uwekezaji katika uzalishaji au uunganishaji wa magari na pikipiki za umeme nchini ili kuwezesha upatikanaji wa bidhaa ya mwisho kwa gharama nafuu;

(uu) Kuweka unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi zinazotumiwa na wazalishaji wa *optical fiber cables* zinazotambulika kwa HS Codes 3215.19.00; 3403.99.00; 3506.91.00; 3818.00.00; 3907.99.00; 3916.90.00; 3917.39.00; 3919.90.90; 3920.69.90; 3920.99.90; 3921.14.90; 3921.90.90; 5402.11.00; 5404.90.00; 7019.90.90; 8536.90.00; na 8544.49.00. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu kwa wazalishaji wa *optical fiber cables* nchini ili kurahisisha upatikanaji wa mawasiliano kwa

gharama nafuu, kuongeza ajira pamoja na kuhamasisha uwekezaji kwenye sekta ya mawasiliano;

(vv) Kuweka unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye karatasi zinazotambulika kwa *HS Code* 4811.90.00 zinazotumiwa na wazalishaji wa lebo na karatasi za kutolea risiti za kielektroniki. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwenye viwanda vinavyotumia malighafi hii;

(ww) Kuweka unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi zinazotambulika kwa *HS Codes* 2713.20.00; 5603.14.00; 2710.19.59; na 3920.10.10 zinazotumiwa na wazalishaji wa *waterproofing membranes*. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu kwenye viwanda vinavyotumia malighafi hizi katika uzalishaji wa *waterproofing membranes*;

(xx) Kuweka unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa Duty Remission kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi zinazotambulika kwa HS Code 6802.99.00 zinazotumiwa na wazalishaji inayozuia kupitisha maji (waterproofing membranes). Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu kwenye viwanda vinavyotumia malighafi hizi katika uzalishaji wa waterproofing membranes;

(yy) Kuweka unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa Duty Remission kwa kiwango asilimia 0 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya chai iliyochakatwa vinavyotambulika kwa HS Codes 4819.20.90 na 5407.44.00. Hatua hii inalenga kutoa unafuu kwa wachakataji wa chai (tea blenders) nchini pamoja na kuhamasisha uwekezaji katika zao hili;

(zz) Kuweka unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa Duty Remission kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vinavyotambulika kwa HS Codes 7310.21.00; na 6305.10.00 vinavyotumiwa na viwanda vya kusaga kahawa nchini. Hatua hii inalenga kuongeza thamani zao la kahawa na kutoa unafuu wa gharama kwenye viwanda vinavyosaga kahawa hapa nchini;

(aaa) Kuweka unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa Duty Remission kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya mbegu vinavyotambulika kwa *HS Codes* 4819.40.00; 6304.91.90; 6305.10.00; 6305.20.00; 6305.33.00; 7310.29.90; na 7607.19.90. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu kwa wazalishaji wa mbegu hapa nchini na kuhamasisha uwekezaji katika uzalishaji wa mbegu;

(bbb) Kuweka unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25 au asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vinavyotumiwa na wazalishaji wa maziwa kwa joto la juu yanayodumu kwa muda mrefu (*UHT Milk*), mtindi (*yoghurt)* na maziwa ya unga vinavyotambulika kwa *HS Codes* 3923.50.90; 4819.20.90; 4819.30.00; 4819.50.00; 4821.90.00; na 7607.19.90. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu kwa wazalishaji wa maziwa hapa nchini, kuongeza ajira pamoja na kuhamasisha uwekezaji kwenye sekta ya maziwa nchini;

116. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na hatua nilizobainisha hapo juu, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kurekebisha Kipengele cha Kwanza (1) cha Sehemu B cha Jedwali la Tano la Sheria ya Usimamizi ya Forodha ya EAC ili kujumuisha karatasi zinazotumika kutolea hati ya kupandia ndege (*boarding pass*) kwenye wigo wa msamaha wa ushuru wa forodha ili kuendana na matakwa ya kimataifa katika huduma za usafiri wa anga na kuheshimu mikataba iliyoingiwa na

Serikali inayohusu masuala ya anga (*Bilateral Air Services Agreements - BASA*).

117. **Mheshimiwa Spika**, nchi wanachama wa Jumuiya zimekubaliana pia kurekebisha Kipengele cha 20 cha Sehemu B ya Jedwali la Tano la Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kutambua mamlaka zote zinazosimamia majanga katika nchi wanachama wa Jumuiya kwa ajili ya kuwezesha au kurahisisha utoaji wa msamaha wa ushuru wa forodha kwa bidhaa zinazoingizwa nchini kwa lengo la kutatua majanga yatakayojitokeza.

118. **Mheshimiwa Spika**, mwaka 2025 tulikufahamisha kuwa, nchi wanachama zilikubaliana kuanzisha Kanuni za Uunganishaji na Uzalishaji wa Bidhaa za Jumuiya ya Afrika Mashariki, 2025 (*The EAC Assembling and Manufacturing of Products Regulations, 2025*) na utekelezaji wa Kanuni hizo ulipangwa kuanza tarehe 1 Julai 2026. Kanuni husika zinalenga kutoa mwongozo wa uanzishaji na usimamizi wa skimu za uunganishaji na uzalishaji wa bidhaa ndani ya nchi wanachama ili kuongeza matumizi ya bidhaa zinazozalishwa ndani ya Jumuiya.

119. **Mheshimiwa Spika**, mkutano wa Mashauriano Kabla ya Bajeti wa Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya uliofanyika tarehe 15 Mei 2026, nchi wanachama zimekubaliana kusogeza mbele utekelezaji wa Kanuni husika hadi tarehe 1 Julai 2027 ili kutoa fursa kwa viwanda vya ndani kujipanga na kuanza uzalishaji wa bidhaa zinazopaswa kuzalishwa ndani ya Jumuiya ambazo hazitopata nafuu ya ushuru wa forodha (*exclusion list*) endapo zitaagizwa kutoka nje ya Jumuiya.

120. **Mheshimiwa Spika**, ninapenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu pamoja na wananchi kwa ujumla kuwa, Novemba 2025 nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zilikubaliana kuweka viwango maalum vya ushuru wa forodha kwenye baadhi ya bidhaa ikiwemo vilainishi (*lubricants*), hamira (*yeast*), karatasi zinazotumika kuchapishia na kutolea nakala (*photocopy and printing paper*) kwa lengo la kulinda viwanda vya ndani ya Jumuiya pamoja na kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya

bidhaa hizo kutoka nje. Viwango vipya vya ushuru wa forodha vilivyokubalika vitaanza kutekelezwa tarehe 1 Julai 2026. Viwango hivyo ni kama ifuatavyo:

(i) Asilimia 25 au dola za Marekani 0.46 kwa lita kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye vilainishi vinavyotambulika kwa *HS Code* 2710.19.51 badala ya kiwango cha asilimia 25 pekee;

(ii) Asilimia 25 au dola za Marekani 660 kwa tani kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye hamira inayotambulika kwa *HS Code* 2102.10.00 badala ya kiwango cha asilimia 25 pekee;

(iii) Asilimia 25 au dola za Marekani 200 kwa tani kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye karatasi zinazotumika kuchapishia na kutolea nakala zinazotambulika kwa *HS Code* 4802.56.00 badala ya kiwango cha asilimia 25 pekee; na

(iv) Asilimia 10 au dola za Marekani 80 kwa tani kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye karatasi zinazotumika kuchapishia na kutolea nakala zinazotambulika kwa *HS Code* 4802.57.00 badala ya kiwango cha asilimia 10 pekee.

121. **Mheshimiwa Spika**, hatua hizi kwa pamoja zinatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shillingi **bilioni 408.97**.

**21. Kanuni za Sheria ya Wakala wa Vipimo za Mwaka 2025**

122. **Mheshimiwa Spika**, inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Kanuni za Sheria ya Wakala wa Vipimo za Mwaka 2025 ili kuongeza ada ya uhakiki wa mafuta (*petroleum verification fee*) kutoka shilingi 0.15 kwa kila lita ya mafuta hadi shilingi 1 kwa kila lita ya mafuta. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Wakala wa Vipimo (WMA) kwa ajili ya kugharamia ununuzi wa vifaa vya kisasa vya udhibiti vinavyoendana na ukuaji wa teknolojia hususan katika tasnia ya biashara ya mafuta na hivyo, kuongeza

ufanisi katika utekelezaji wa jukumu lake la uhakiki wa vipimo. Aidha, matumizi ya fedha zinazotokana na ada husika yatafanyika baada ya kupata ridhaa ya Mlipaji Mkuu wa Serikali kufuatia kuwasilishwa kwa mpango kazi wa matumizi. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **bilioni 21.96**.

**22. Kanuni za Sheria ya Usajili na Utambuzi wa Watu za Mwaka 2014**

123. **Mheshimiwa Spika**, kumejitokeza mahitaji ya mara kwa mara ya taarifa kutoka NIDA yanayosababisha gharama kubwa za uendeshaji. Hivyo, inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Kanuni za Sheria ya Usajili na Utambuzi wa Watu za mwaka 2014 ili kuanzisha tozo ya shilingi 500 kwa wananchi wanaomba taarifa zake katika Kanzidata ya NIDA kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Taarifa hizo ni pamoja na majina ya wazazi, shule aliyosoma, namba ya simu na taarifa nyingine zilizopo katika kanzidata ya Mamlaka. Aidha, kwa mwananchi atakaehitaji kupatiwa nakala ya taarifa hizo (*print out extracts*) atalipia ada ya shilingi 1,000. Lengo la hatua hii ni kugharamia utoaji huduma hizo ikiwemo gharama za uchapishaji na matumizi ya mifumo na kuhakikisha uendelevu wa huduma za utambuzi kwa wananchi. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 734.4**.

**23. Kanuni za Sheria ya Usalama Barabarani za mwaka 2024**

124. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwepo Mfuko maalum wa kulipia kodi kwa wafanyabiashara wadogo (*presumptive tax*), kumekuwa na ugumu wa kutekeleza Mfuko huo kwenye biashara ya usafiri wa vyombo vya miguu miwili (*motorcycles*). Inapendekezwa kuendelea na utaratibu wa sasa wa kutowaingiza wafanyabiashara hao katika mfumo wa *presumptive tax*. Badala yake, inapendkezwa kufanya marekebisho kwenye Kanuni za Sheria ya Usalama Barabarani za mwaka 2024 ili kuongeza ada ya mara moja tu ya usajili wa pikipiki ya miguu miwili kutoka shilingi 95,000 hadi shilingi 150,000. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali bila ya kuathiri

biashara hizo ndogo ndogo. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **bilioni 17.75**.

**24. Uanzishaji wa Vyanzo vya Ziada vya Mapato kwa Ajili ya Kugharamia Bima ya Afya kwa Wote**

125. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inapendekeza kuongeza vyanzo vya mapato kwa ajili ya kugharamia bima ya afya kwa wote kwa kufanya marekebisho kwenye sheria na kanuni mbalimbali kama ifuatavyo:

(i) Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147 ili kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwa shilingi 20 kwa kila sigara 1,000 (*per mil*) zinazotambulika kwa *HS Heading* 24.02 na 24.03; na

(ii) Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Sukari Sura 251 pamoja na Kanuni zake ili kuongeza tozo kwa shilingi 10 kwa kila kilo moja ya sukari inayozalishwa ndani na inayoagizwa kutoka nje ya nchi. Tozo hii itakusanywa na Bodi ya Sukari Tanzania na kuwasilishwa kwenye Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote.

126. **Mheshimiwa Spika**, hatua hizi kwa pamoja zinatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa shilingi **bilioni 7.5**.

**25. Maboresho ya Ada na Tozo mbalimbali za Taasisi za Serikali pamoja na Utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara (*Blueprint*)**

127. **Mheshimiwa Spika**, inapendekezwa kufanya maboresho ya sheria na kanuni mbalimbali kwa kufuta au kupunguza ada na tozo mbalimbali zinazotozwa na Wizara, Idara na Taasisi zinazojitegemea ili kuleta usimamizi bora wa sekta mbalimbali na kuboresha mazingira ya biashara nchini. Hatua hizi pia ni moja ya sehemu ya mwendelezo wa utekelezaji wa Mpango wa

Kuboresha Mazingira ya Biashara Nchini (MKUMBI). Marekebisho hayo ni kama ifuatavyo:

**(i) Ada za Huduma za Maudhui Mtandaoni**

Kufanya marekebisho kwenye Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui Mtandaoni) ili kupunguza ada za huduma za maudhui mtandaoni zinazotumiwa zaidi na vijana kama ifuatavyo:

(a) Ada ya maombi ya leseni ya huduma za maudhui mtandaoni kutoka shilingi 50,000 hadi shilingi 10,000;

(b) Ada za mwanzo (*initial*), za mwaka na kwa ajili ya kuhuisha leseni ya huduma za maudhui mtandaoni kutoka shilingi 500,000 hadi shilingi 50,000;

(c) Ada ya maombi ya leseni ya mtengeneza maudhui mtandaoni (*Online Content Aggregator*) kutoka shilingi 100,000 hadi shilingi 20,000; na

(d) Ada za mwanzo (*initial*), mwaka na kwa ajili ya kuhuisha mtengeneza maudhui mtandaoni (*Online Content Aggregator*) kutoka shilingi 1,000,000 hadi shilingi 100,000.

**(ii) Wizara ya Maliasili na Utalii**

Kuanzisha ada ya usajili, usimamizi na uendeshaji wa makumbusho binafsi kama ifuatavyo:

(a) Usajili wa makumbusho binafsi kwa raia wa Tanzania kwa kiwango cha shilingi 50,000;

(b) Usajili wa makumbusho binafsi kwa taasisi za Tanzania kwa kiwango cha shilingi 100,000;

(c) Usajili wa makumbusho binafsi kwa raia wa kigeni kwa kiwango cha shilingi 500,000;

(d) Malipo ya leseni kwa ajili ya uendeshaji wa makumbusho binafsi kwa raia wa Tanzania kwa kiwango cha shilingi 20,000 kwa mwaka;

(e) Malipo ya leseni kwa ajili ya uendeshaji wa makumbusho binafsi kwa taasisi ya Tanzania kwa kiwango cha shilingi 100,000 kwa mwaka; na

(f) Malipo ya leseni kwa ajili ya uendeshaji wa makumbusho binafsi kwa taasisi za kigeni kwa kiwango cha 300,000 kwa mwaka.

**(iii) Marekebisho madogo madogo katika baadhi ya Kanuni mbalimbali.**

Kufanya marekebisho mengine madogo madogo katika kanuni mbalimbali sanjari na azma ya kurahisisha utekelezaji wake kama zilivyoambatishwa kwenye **Kiambatisho Na. 1, 2, 3** na **4**.

128. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na maboresho ya sheria mbalimbali yaliyofanywa na Serikali ili kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara kwa kupunguza mwingiliano wa majukumu baina ya taasisi za udhibiti nchini na kufuta na kupunguza ada na tozo kero, bado kumekuwa na changamoto ya taasisi nyingi za udhibiti zinazosimamia sekta mbalimbali kuongeza kero za ufanyaji biashara na uwekezaji kutokana na ada, tozo na adhabu mbalimbali wanazotoza pamoja na kaguzi nyingi na zisizokuwa na tija. Ili kuondoa kero hizo, Serikali ipo katika hatua za kuanzisha mfumo wa pamoja wa ukusanyaji wa ada, tozo na adhabu za taasisi za udhibiti (*Single Window Payment System*) na kuweka utaratibu kwa taasisi hizo kufanya kaguzi kwa namna ambayo haitaleta usumbufu na bila kuathiri majukumu ya msingi yanayofanywa na taasisi husika.

**26. Marekebisho madogo madogo katika baadhi ya Sheria za Kodi, Sheria nyingine na Kanuni mbalimbali**

129. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na mapendekezo mahsusi niliyobainisha hapo juu, inapendekezwa pia kufanya marekebisho mengine madogo madogo katika sheria mbalimbali za kodi, sheria nyingine pamoja na kanuni za sheria mbalimbali sanjari na azma ya kurahisisha utekelezaji wake. Marekebisho hayo yataainishwa katika Muswada wa **Sheria ya Fedha ya mwaka 2026** na Matangazo ya Serikali (*Government Notices*).

**27. Tarehe ya Kuanza Kutekeleza Hatua Mpya za Kodi.**

130. **Mheshimiwa Spika**, hatua hizi za kikodi zinazopendekezwa zitaanza kutekelezwa tarehe 1 Julai, 2026, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo.

**V. SURA YA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2026/27**

131. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2026/27 Serikali inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya shilingi trilioni 62.33, ikiwa ni ongezeko la asilimia 10.3 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2025/26.

132. **Mheshimiwa Spika**, mapato yanatarajiwa kuwa shilingi trilioni 46.79 ambapo mapato ya kodi ni shilingi trilioni 36.99, mapato mengine ni shilingi trilioni 9.24 (ikijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa shilingi trilioni 1.97) na misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo shilingi bilioni 563.1. Ili kuendana na dhamira yetu ya kujitegemea katika uendeshaji wa Serikali na maendeleo, takribani robo tatu ya bajeti yote ya mwaka 2026/27, sawa na asilimia 74.2 inatarajiwa kugharamiwa na mapato ya ndani.

133. **Mheshimiwa Spika**, misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo inatarajiwa kupungua kwa asilimia 39.1 kwa mwaka 2026/27 ikilinganishwa na fedha zilizoahidiwa mwaka 2025/26. Hali hii inatokana na kubadilika kwa sera za baadhi ya washirika wa maendeleo. Tunawashukuru sana washirika wetu wa maendeleo kwa msaada wao pale walipoweza. Hata hivyo, Tanzania ni Taifa

letu; na sisi ndio wenye wajibu wa kulijenga. Ni wajibu wa wananchi wote kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi, kulipa kodi kwa hiari, na kushikamana na Serikali katika kuleta maendeleo.

134. **Mheshimiwa Spika**, matumizi na uwekezaji katika mali zisizo za kifedha yanakadiriwa kuwa shilingi trilioni 54.50 pasipo kujumuisha malipo ya mtaji wa deni la Serikali. Kati ya kiasi hicho, stahiki za watumishi ikijumuisha michango ya pensheni ni shilingi trilioni 10.13, gharama za bidhaa na huduma shilingi trilioni 5.22, malipo ya riba ni shilingi trilioni 6.86, ruzuku shilingi trilioni 25.32, mafao na misaada ya kijamii shilingi trilioni 1.01, uwekezaji katika mali zisizo za kifedha shilingi trilioni 2.33 na gharama nyingine shilingi trilioni 3.63.

135. **Mheshimiwa Spika**, kulingana na makadirio ya mapato na matumizi hayo niliyoyaeleza, **kunajitokeza nakisi kwenye bajeti ya shilingi trilioni 7.71**. Serikali itaendelea kugharamia nakisi ya bajeti kwa kutumia mikopo kutoka vyanzo vya ndani na nje kwa kuzingatia Mkakati wa Muda wa Kati wa Kusimamia Deni la Serikali (2025/26 – 2027/28). Katika mwaka 2026/27, Serikali inatarajia kukopa jumla ya shilingi trilioni 15.54. Kati ya kiasi hicho, mikopo ya ndani ni shilingi trilioni 6.56, mikopo ya nje yenye masharti nafuu shilingi trilioni 6.55 na mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara shilingi trilioni 2.43. Aidha, Serikali inakadiria kulipa malipo ya mtaji kwa mikopo iliyoiva shilingi trilioni 7.84. Sura ya bajeti inayopendekezwa kwa mwaka 2026/27 imeainishwa katika **Jedwali Na. 1.**

**Jedwali Na.1: Mapendekezo ya Sura ya Bajeti kwa Mwaka 2026/27**

*Shilingi milioni*

| | **2026/27** |
|---|---|
| **A: Mapato** | **46,791,299** |
| Mapato ya kodi | 37,022,030 |
| Misaada/Michango | 563,139 |

| | |
|---|---|
| Mapato mengine | 9,206,129 |
| o/w Mamlaka za Serikali za Mitaa | 1,966,193 |
| | |
| **B: Matumizi** | **52,169,947** |
| **Mishahara na stahiki za watumishi** | **10,127,295** |
| o/w Mishahara kwa watumishi wa Serikali Kuu | 6,327,227 |
| Michango ya hifadhi za jamii | 2,131,009 |
| **Gharama za bidhaa na huduma** | **5,215,408** |
| **Malipo ya riba** | **6,859,541** |
| Malipo ya riba nje | 2,829,241 |
| Malipo ya riba ndani kwa taasisi zisizo Serikali Kuu | 4,030,301 |
| **Ruzuku kwenye taasisi za uwekezaji** | **2,791,970** |
| **Ruzuku na michango** | **22,528,163** |
| Kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa | 9,029,943 |
| o/w Mishahara ya watumishi | 5,312,016 |
| Ununuzi wa samani na uwekezaji | 2,200,313 |
| Kwa taasisi za umma | 11,006,544 |
| o/w Mishahara ya watumishi | 2,320,445 |
| Ununuzi wa samani na uwekezaji | 5,936,233 |
| Ruzuku ya vyanzo maalumu inayoenda moja | |

| | |
|---|---|
| kwa moja kwe | 1,843,130 |
| **Mafao na misaada ya kijamii** | **1,007,689** |
| **Gharama nyingine** | **3,639,880** |
| | |
| **Salio la Mapato na Matumizi** | **(5,378,648)** |
| | |
| **C: Uwekezaji katika mali zisizo za kifedha** | **2,328,661** |
| Gharama za majengo, miundombinu, mashine n.k | 2,319,500 |
| Mali zisizozalishwa/mali za asili | 9,161 |
| | |
| **Nakisi ya Bajeti bila Misaada** | **(8,270,449)** |
| | |
| **Nakisi ya bajeti ikijumuisha misaada** | **(7,707,309)** |
| | |
| **Ugharamiaji wa nakisi ya bajeti** | **7,707,309** |
| | |
| **D: Mikopo ya ndani** | **3,272,349** |
| D1 - Mikopo ya ndani | 6,557,744 |
| D2 - Malipo ya mikopo ya ndani | (3,285,395) |
| | |
| **E: Mikopo ya nje** | **4,434,960** |
| E1 - Mikopo ya nje | 8,985,150 |

| | |
|---|---|
| o/w Mikopo ya Kibiashara | 2,430,372 |
| E2 - Malipo ya mikopo ya nje | (4,550,190) |
| | |
| **Jumla ya Bajeti ( A + D1 + E1)** | **62,334,193** |
| **Nakisi ya bajeti/Pato la Taifa** | **2.9%** |

***Chanzo***: *Wizara ya Fedha*

**VI. VIHATARISHI VYA UTEKELEZAJI WA BAJETI**

136. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2026/27 unaweza kuathiriwa na vihatarishi tofauti ikiwemo: Mabadiliko ya viwango vya riba za mikopo; mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma; kushuka kwa thamani ya shilingi; na mabadiliko ya sera za washirika wa maendeleo. Vihatarishi vingine ni: Madeni sanjari; mabadiliko ya tabianchi na majanga ya asili; migogoro ya kisiasa na vita za kimataifa; mashambulio ya mifumo ya TEHAMA; na kihatarishi cha kiutendaji.

137. **Mheshimiwa Spika**, iwapo vitatokea, athari za vihatarishi hivyo ni pamoja na: Kuongezeka kwa viwango vya riba pamoja na gharama za mikopo kwa sekta ya umma na sekta binafsi; kuongezeka kwa matumizi ya fedha za kigeni katika kugharamia bidhaa na huduma; kupungua kwa kasi ya uzalishaji na shughuli za kiuchumi; kupungua kwa ufanisi wa utoaji wa huduma; na kuongezeka kwa nakisi ya bajeti na mfumuko wa bei.

138. **Mheshimiwa Spika**, athari nyingine zinazoweza kujitokeza ni: Ongezeko la mzigo wa kibajeti kwa ajili ya kugharamia madai na deni la Serikali; kupungua kwa uwezo wa Serikali katika kugharamia miradi ya maendeleo na uendeshaji wa shughuli za kawaida; vifo, uharibifu wa miundombinu, mali na mifumo ya ikolojia; na kuathirika kwa upatikanaji wa misaada, mikopo na uwekezaji kutoka nje.

**Hatua za Kukabiliana na Vihatarishi**

139. **Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea kukabiliana na vihatarishi hivyo kwa: Kusimamia kwa uthabiti sera za fedha na

bajeti; kuimarisha mazingira ya uwekezaji na biashara; kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kuimarisha Upatikanaji wa fedha za Kigeni; kuimarisha Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo pamoja na kuwekeza kwenye kilimo cha kisasa; kuwekeza kwenye uzalishaji wa nishati mbadala ya petroli kama vile gesi na umeme; kupanua wigo wa vyanzo vya mapato ya ndani; na kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia.

140. **Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea pia: Kuimarisha usimamizi wa Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana, Sura 134 na Sheria ya Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Sura 103; kutekeleza Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 - 2032), Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa 2022 – 2027, Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati safi ya Kupikia (2024 – 2034); kuimarisha mifumo ya utawala bora na utawala wa sheria; kujenga uwezo na kuimarisha usalama wa mtandao wa Serikali; kuimarisha mifumo ya ukaguzi wa ndani, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi; pamoja na kushirikisha sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya umma yenye sifa za kibiashara. *Maelezo ya kina kuhusu vihatarishi yapo katika Mkakati wa Usimamizi wa Vihatarishi katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2026/27 uliyoambatishwa.*

## VII. SHUKRANI NA PONGEZI

141. **Mheshimiwa Spika**, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, ninakupongeza tena wewe binafsi Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Jimbo la Ilala, na Naibu Spika Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini, kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuliongoza Bunge letu Tukufu. Aidha, nampongeza Bw. Baraka Leonard kwa kuendelea kuaminiwa kuwa Katibu wa Bunge na kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuratibu shughuli za chombo hiki cha wananchi. Nawapongeza pia wenyeviti wa Bunge na kamati zake walioaminiwa na kuchaguliwa kuongoza vikao vya Bunge na shughuli za kamati.

142. **Mheshimiwa Spika**, kipekee ninaishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki - Mbunge wa Maswa Magharibi, pamoja na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Ali

Omar King - Mbunge wa Jang'ombe, na wajumbe wake wote, kwa maoni na ushauri wao bora wakati wa maandalizi na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali.

Aidha, niwashukuru na kuwapongeza waheshimiwa mawaziri na manaibu waziri wote kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Natumia pia fursa hii kuwapongeza waheshimiwa wabunge wote kwa kuaminiwa na kuchaguliwa au kuteuliwa kuhudumu katika nafasi za ubunge kwenye Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni imani yangu kuwa sote tutaendelea kushirikiana katika kuwaletea maendeleo watanzania wenzetu.

143. **Mheshimiwa Spika**, mfumo wetu wa utawala unahusisha mihimili mitatu ya Dola. Kwa maendeleo ya uchumi, mahakama ni taasisi muhimu kwa utendaji wa soko. Niruhusu nimpongeze Mheshimiwa George Mcheche Masaju, Jaji Mkuu wa Tanzania pamoja na watendaji wote wa Mahakama kwa kazi nzuri na ya heshima wanayoifanya ya kusimamia mifumo ya utoaji wa haki kwa watanzania wote na wawekezaji wetu.

144. **Mheshimiwa Spika**, mafanikio tunayoendelea kuyapata yanatokana pia na utulivu na umahiri wa watumishi wa umma. Napenda kutoa shukrani na pongezi zangu za dhati kwa Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Dkt. Moses Mpogole Kusiluka, kwa utendaji wake mzuri katika kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali na utumishi wa umma. Aidha, nawapongeza na kuwashukuru wakuu wote wa vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuendelea kulinda kwa umahiri mkubwa mipaka ya nchi yetu na kuhakikisha hali ya utulivu na usalama nchini.

145. **Mheshimiwa Spika**, utendaji wangu unapata msaada mkubwa kutoka kwa wasaidizi wangu wa karibu. Nawashukuru kwa dhati Manaibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mhandisi Mshamu Ali Munde – Mbunge wa Jimbo la Liwale na Mheshimiwa Laurent Deogratius Luswetula – Mbunge wa Jimbo la Kavuu kwa ushirikiano wao na mchango mkubwa katika kunisaidia kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi. Aidha, ninatoa pongezi na shukrani za dhati kwa Dkt. Natu El-Maamry Mwamba, Katibu

Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Naibu Makatibu Wakuu, Bw. Elijah Greenton Mwandumbya na Bw. Nsubili Akomeligwe Kajela Joshua kwa ushauri wao wa kitaalam na usimamizi makini wa majukumu ya Wizara.

146. **Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii pia kumpongeza Bw. Emmanuel Mpawe Tutuba, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania kwa kuendelea kusimamia kwa ufanisi utekelezaji wa sera ya fedha. Aidha, natumia fursa hii kuwapongeza Gavana Tutuba, Bodi ya Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Benki Kuu ya Tanzania kwa kutimiza miaka 60 tangu kuanzishwa kwake. Ninawatakia kila la kheri katika kutekeleza majukumu yao kwa miaka ijayo.

147. **Mheshimiwa Spika,** namshukuru pia Bw. Yusuph Juma Mwenda, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa jitihada kubwa anazofanya za kusimamia vyema ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Kama ilivyo kwa Benki Kuu, tarehe 1 Julai 2026, TRA nayo itatimiza miaka 30 tangu kuanzishwa kwake. Hivyo, natumia fursa hii kuwapongeza na kuwatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao. Kwa miaka 30 ya uwepo wake, TRA imepata mafanikio makubwa kutokana na ushirikiano wanaoupata kutoka kwa walipakodi. Kwa kutambua umuhimu wa walipakodi, Julai 2026 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anatarajiwa kutoa tuzo kwa walipakodi mahiri ili kutambua mchango wao wa kizalendo na uhiari wa kulipa kodi kwa maendeleo ya nchi.

148. **Mheshimiwa Spika**, natoa shukrani na pongezi maalum kwa CPA Charles Edward Kichere, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa juhudi endelevu na kazi bora anayoifanya katika ukaguzi wa hesabu za taasisi za Serikali. Aidha, nimpongeze pia Dkt. Amina Suleiman Msengwa, Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa kuendelea kusimamia kwa weledi tafiti na uzalishaji wa takwimu rasmi. Kadhalika, nawapongeza viongozi wengine na watumishi wote wa Wizara ya Fedha pamoja na taasisi zake kwa kazi nzuri ya maandalizi na usimamizi madhubuti wa utekelezaji wa bajeti ya Serikali. Namshukuru Mheshimiwa Rais na najisikia kuwa nimependelewa kupatiwa moja ya timu bora kabisa ya

utendaji. Kwa hakika, hii ni “***ATeam***” – imekamilika katika idara zake zote.

149. **Mheshimiwa Spika**, napenda pia kutoa shukrani kwa: Viongozi na watendaji wa wizara; Idara Zinazojitegemea; Wakala na Taasisi za Serikali; Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na wadau mbalimbali katika kuwezesha maandalizi na utekelezaji wa bajeti ya Serikali.

150. **Mheshimiwa Spika**, tunawashukuru pia majirani zetu wa karibu, nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Malawi, Msumbiji, Rwanda, Uganda, na Zambia kwa mashirikiano ya kidiplomasia, kisiasa na kiuchumi. Msingi muhimu wa Sera yetu ya Mambo ya Nje ni kuendeleza na kudumisha ujirani mwema. Nachukua fursa hii kuwahakikishia majirani zetu kuwa Tanzania itaendelea kuwa jirani mwema kwao.

151. **Mheshimiwa Spika**, niruhusu nitumie nafasi hii kuwashukuru washirika wetu wa maendeleo kwa misaada na mashirikiano yao wanayoendelea kutupatia katika harakati zetu za kujiletea maendeleo nchini. Naomba nizitambue nchi wahisani na taasisi mbalimbali kama ifuatavyo: Australia, Austria, Brazil, Canada, China, Denmark, Finland, Hungary, India, Indonesia, Ireland, Italia, Jamhuri ya Cuba, Jamhuri ya Czech, Japan, Korea Kusini, Kuwait, Marekani, Norway, Oman, Poland, Qatar, Saudi Arabia, Singapore, Spain, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu – UAE, Urusi na Uswisi.

152. **Mheshimiwa Spika**, taasisi na mashirika ya kimataifa tunayoshirikiana nayo kwa karibu ni pamoja na: Benki ya Dunia; Shirika la Fedha la Kimataifa; Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi katika Afrika (BADEA); Mfuko wa Abu Dhabi (ADFD); Mfuko wa Kimataifa wa Kusaidia Mapambano Dhidi ya Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria (Global Fund); Mfuko wa OPEC kwa Maendeleo ya Kimataifa (OFID); Mfuko wa Mazingira Duniani (GEF); Adaptation Fund; Mfuko wa Geothermal Risk Mitigation Facility (GRMF); Umoja wa Mataifa na mashirika yote yaliyopo chini yake; Umoja wa Ulaya (EU); Shirikisho la GAVI; Global Partnership for Education (GPE);

Nutrition International; Mfuko wa Maendeleo wa Kilimo wa Kimataifa (IFAD) na Mfuko wa Saudi.

153. **Mheshimiwa Spika**, ni matarajio yetu kuwa kwa washirika wetu waliotuahidi rasilimali, watatimiza ahadi zao kwa ukamilifu na kwa wakati. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha uwajibikaji, uwazi na nidhamu katika usimamizi na matumizi ya rasilimali zitakazotolewa ili kuhakikisha upatikanaji wa thamani halisi ya fedha na kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

154. **Mheshimiwa Spika**, naomba nitambue pia michango na ushirikiano wa Asasi Zisizo za Kiserikali ikiwa ni pamoja na Asasi za Kiraia, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, taasisi za fedha, sekta binafsi, mashirika ya kidini pamoja na taasisi za elimu ya juu na utafiti katika kuchangia maendeleo nchini.

155. **Mheshimiwa Spika**, kipekee nitumie fursa hii kuishukuru familia yangu kwa maombi na faraja inayoniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi na weledi. Kwa namna maalum na ya kipekee, namshukuru mke wangu kipenzi na rafiki yangu mkuu, Bi. Nassra Ibrahim Ali, watoto wetu Hafidh na Ashura Khamis, na wakwe zetu, Abrarah Said Bakran na Hassan Juma Amour. Nawashukuru pia wajukuu – Nassra, Khamis, Said, Maryam kwa Hafidh na Abrarah; na mapacha Malik na Malaak, na Nasreen na Nazeen kwa Ashura na Hassan. Shukrani zangu za dhati ni kwa faraja na moyo wanaonipa na kuniombea kwa Mwenyezi Mungu kila siku ili niweze kutekeleza kwa uaminifu na uadilifu dhamana niliyopewa ya kuwatumikia watanzania.

## VIII. HITIMISHO

156. **Mheshimiwa Spika**, kama nilivyoeleza hapo awali, bajeti hii ni ya kwanza katika utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31 ambao ni sehemu ya utekelezaji wa Dira 2050. Ili kufikia malengo yaliyoainishwa katika Dira 2050, ni muhimu kwetu sote kujituma na kuwa na umoja na mshikano wa kitaifa katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo. Aidha, wananchi sote hatuna budi kuchangamkia kikamilifu fursa zinazojitokeza kwa utekelezaji wa bajeti, nchi yetu kuwa mwenyeji wa mashindano ya AFCON ili kujiongezea kipato na hivyo kuboresha ustawi wa jamii.

Mashindano ya AFCON yanaleta fursa adhimu hususan katika utoaji wa huduma za vyakula, malazi, usafiri na utalii. Fursa kubwa zitajitokeza katika miradi mikubwa inayotarajiwa kuwekezwa ya LNG, uchimbaji wa makaa ya mawe na chuma na uchakataji wake kuwa chuma cha pua pamoja na sekta za ujenzi, usafirishaji, madini, nishati na gesi. Tuzichangamkie ipasavyo fursa zote hizo na nyingine zinazojitokeza nchini kwetu.

157. **Mheshimiwa Spika**, kama nilivyoainisha hapo awali, Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini ikiwemo maboresho ya mfumo wa kodi kwa lengo la kuvutia uwekezaji, kuhamasisha urasimishaji wa sekta isiyo rasmi na uanzishaji wa biashara mpya na hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi. Serikali pia itarahisisha malipo kwa kupunguza matumizi ya fedha taslimu ili kuhakikisha kuwa mageuzi haya yanajenga uchumi wa kisasa pasipo kuacha nyuma wananchi katika gurudumu la ujenzi wa uchumi wa kidijitali.

158. **Mheshimiwa Spika**, naomba nimalizie kwa kulishukuru kundi muhimu na maalumu katika jamii yetu. Kwa moyo wa dhati kabisa, ninawashukuru viongozi wote wa dini kwa mchango wao mkubwa katika kujenga na kudumisha amani, maadili na mshikamano wa kitaifa. Imani yetu ya kiroho ni msingi muhimu wa umoja wetu na maendeleo ya nchi yetu. Tunawashukuru sana viongozi wetu kwa sala na dua zenu za kuiombea nchi yetu, viongozi na wananchi kwa ujumla. Kwa hakika, sala na dua hizo zimeendelea kuimarisha umoja, utulivu na mafanikio ya Taifa letu. Nawaomba wasichoke, waendelee kuliombea Taifa letu hasa pale shetani anapotupa majaribu yake.

159. **Mheshimiwa Spika**, naomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2026/27.

**Mungu ibariki Tanzania.**

160. **Mheshimiwa Spika**, kwa heshima na taadhima, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, na mimi nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Waziri wa Fedha kwa bajeti ambayo ameisoma hapa, ikiwa ni bajeti ya kwanza ya Dira 2050; hongera sana. *(Makofi)*

Niwapongeze wote ambao tuko ndani kupata fursa hii kwa kundi la kwanza la Bunge hili kuweza kushughulikia Dira 2050. Ninamshukuru Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maelekezo na Dira hii. Tuna kazi kubwa sana ya kufanya. Tutafanikiwa kwa kushirikiana na tutafanikiwa kwa kuweka uzalendo, utu na ubinadamu kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Baada ya maneno hayo, tunao wageni Bungeni jioni hii; wageni waliokaa Jukwaa la Spika; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu Mstaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Anne Semamba Makinda, Spika Mstaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Balozi. Dkt. Moses Mpogole Kusiluka, Katibu Mkuu Kiongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rosemary Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Stephen Wassira, Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM). *(Makofi/Vigelegele)*

Profesa Elisante Ole-Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama. *(Makofi)*

Dkt. Jim James Yonazi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu, Bunge na Wenye Ulemavu. *(Makofi)*

Dkt. Natu El-Maamry Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge Mstaafu. *(Makofi)*

Jenerali Jacob John Mkunda, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi *(CDF)*. *(Makofi)*

Inspekta Jenerali Camillus Wambura, Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania *(IGP)*. *(Makofi)*

Ndugu Daniel Barago, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa *(DGIS)*. *(Makofi)*

Kamishna Jenerali Jeremiah Yoramu Katungu, Mkuu wa Jeshi la Magereza *(CGP)*. *(Makofi)*

Kamishna Jenerali John William Masunga, Mkuu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji *(CGF)*. *(Makofi)*

Dkt. Anna Makakala, Kamishna Jenerali wa Uhamiaji. *(Makofi/Vigelegele)*

Ndugu Crispin Francis Chalamila, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). *(Makofi)*

Ndugu Abel Mwajeka, Mwakilishi wa Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Dawa za Kulevya *(DCEA)*. *(Makofi)*

Ndugu Charles Edward Kichere, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)*. *(Makofi)*

Ndugu Yusuph Juma Mwenda, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*. *(Makofi)*

Jaji Mstaafu Sivangilwa Sikalalilwa Mwangesi, Kamishna wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. *(Makofi)*

Jaji wa Rufaa Jacobs Mwambegele, Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi *(INEC)*. *(Makofi)*

Ndugu Ramadhani Kailima, Mkurugenzi wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi *(INEC)*. *(Makofi)*

Ndugu Mohamed Ahmed, Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa. *(Makofi)*

Ndugu Mgonya Benedicto, Mwakilishi wa Gavana wa Benki Kuu *(BOT)*. *(Makofi)*

Ndugu Agathon Kipandula, Mwakilishi wa Msajili wa Hazina. *(Makofi)*

Balozi Ombeni Yohana Sefue, Mjumbe Tume ya Taifa ya Mipango. *(Makofi)*

Ndugu Raymund Kahumba, mgeni wa Mheshimiwa Naibu Spika. *(Makofi)*

Ndugu Azza Mnzava, mgeni wa Mheshimiwa Naibu Spika. *(Makofi)*

Ndugu Nasra Ibrahim Ally, mke wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha. *(Makofi/Vigelegele)*

Ndugu Hafidh Khamis Mussa, mtoto wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Ndugu Ashura Khamis Mussa, mtoto wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Ndugu Abrarah Said Bakran, mkwe wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha

Ndugu Hassan Juma Amour, mkwe wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Utambulisho wa makundi; Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu wa Wizara, karibuni sana. *(Makofi)*

Mabalozi, Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa na Washirika wa Maendeleo; *H.E. Dr. Ahamada El Badaoui Mohamed Fakih, Ambassador and Dean of the Diplomatic Corps, Union of the Comoros. (Makofi)*

*H.E. Mahayub Buyema Mafud, Ambassador, Saharawi Arab Democratic Republic. (Makofi)*

*H.E. Yordenis Despaigne Vera, Ambassador, Republic of Cuba. (Makofi)*

*H.E. Andrey Avetisyan, Ambassador, Russian Federation. (Makofi)*

*H.E. Saud Hilal Al Shidhani, Ambassador, Sultanate of Oman. (Makofi)*

*H.E. Col. (Rtd.) Fred Mwesigye, High Commissioner Republic of Uganda. (Makofi)*

*H.E. Mr. Mathews Jere, High Commissioner, Republic of Zambia. (Makofi)*

*H.E. Gustavo Martins Nogueira, Ambassador, Federative Republic of Brazil. (Makofi)*

*H.E. Yahya Ahmed Okeish, Ambassador, Kingdom of Saudi Arabia. (Makofi)*

*H.E. Leontine Nzeyimana, Ambassador, Republic of Burundi. (Makofi)*

*Ambassador General Patrick Nyamvumba, Ambassador, Republic of Rwanda. (Makofi)*

*H.E. Fekadu Beyene Ayana, Ambassador, Federal Democratic Republic of Ethiopia. (Makofi)*

*H.E. Sherif Ismail, Ambassador, Arab Republic of Egypt. (Makofi)*

*H.E. Dr. Mohamed Abdalla Abdelhameed, Ambassador, Republic of the Sudan. (Makofi)*

*H.E. Domingos De Almeida Da Silva Coelho, Ambassador, Republic of Angola. (Makofi)*

*H.E. Jesper Kammersgaard, Ambassador, Kingdom of Denmark. (Makofi)*

*H.E. Catherine Karemu, High Commissioner Republic of Kenya. (Makofi)*

*Mr. Alba Espino Gómez, Deputy Head of Mission Kingdom of Spain. (Makofi)*

*Mr. Taher Jomast, Deputy Head of Mission, Islamic Republic of Iran. (Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni.

*Ms. Sandra Diesel, Chargé d'affaires ad interim, Kingdom of Sweden. (Makofi)*

*Mr. Abdulla Saeed Al Naimi, Chargé d'affaires, State of Qatar. (Makofi)*

*Mr. Hipolito Roia, Chargé d'affaires, Republic of Mozambique. (Makofi)*

*Ms. Muzeyyen Inci, Deputy Head of Mission, Republic of Türkiye. (Makofi)*

*Dr. Wendelin Kibwe, Executive Director, World Bank. (Makofi)*

*Mr. Firas Raad, Division Director, World Bank. (Makofi)*
*Ms. Nimo Mohamed, Political Advisor, Federal Republic of Somalia. (Makofi)*

*Mr. Chelaus Rutachururwa, Economist, International Monetary Fund (IMF). (Makofi)*

*Ms. Susan Ngongi Namondo, Resident Coordinator, UN System. (Makofi)*

*Mr. Shigeki Komatsubara, Resident Representative, United Nations Development Programme (UNDP). (Makofi)*

*Mr. Godfrey Mulisa, Head of UNDP Dodoma Sub- Office, United Nations Development Programme (UNDP). (Makofi)*

*Dr. Majaliwa Marwa, Assistant Representative, United Nations Population Fund (UNFPA). (Makofi)*

*Ms. Elke Wisch, Country Representative, United Nations Children's Fund (UNICEF). (Makofi)*

*Mr. Amin Mawji, Representative, Aga Khan Development Network (AKDN). (Makofi)*

*Mr. Ashraf Hassan, Chief of Mission, International Organization for Migration (IOM). (Makofi)*

*Ms. Christine Mendes, Deputy Country Director, World Food Programme (WFP). (Makofi)*

*Mr. Zulqarnain Hussain Anjum, Deputy Representative, United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR). (Makofi)*

*Mr. Firas Raad, Division Director, World Bank. (Makofi)*

*Ms. Godfrida Magubo, Representative, United Kingdom, Dodoma Office. (Makofi)*

*Mr. Wang Yong, Minister Counsellor, People's Republic of China. (Makofi)*

*Dr. Remember Benjamin, Minister Counsellor, Republic of Zimbabwe. (Makofi)*

*Mr. Frans van Aardt, Counsellor, Republic of South Africa. (Makofi)*

*Ms. Maria Ochs, First Secretary, Republic of Namibia. (Makofi)*

*Mr. Mwamina Ngwale, First Secretary, Republic of Zambia. (Makofi)*

*Ms. Zhou Zihan, Desk Officer, People's Republic of China. (Makofi)*

*Mr. Shekhar Kanabar, Honorary Consul, Republic of Lithuania. (Makofi)*

*Mr. Hussein Hamad, Honorary Consul, Republic of Sierra Leone. (Makofi)*

*Mr. Gilman Kasiga, Honorary Consul, Czech Republic. (Makofi)*

*Ms. Johanna Omere, Honorary Consul, Austria. (Makofi)*

*Mr. Munezero Kanyangemu, Liaison Officer, German Development Cooperation. (Makofi)*

*Mr. Solomon Michael, Country Director, Trade Mark Africa. (Makofi)*

Viongozi wa Dini wa Kitaifa na Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Wakuu wa Mashirika ya Umma, sekta binafsi na taasisi za fedha. *(Makofi)*

Wakuu wa taasisi za elimu kutoka Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Wawakilishi wa Vyama vya Siasa vyote. *(Makofi)*

Wakuu wa taasisi na vyombo vya habari. *(Makofi)*

Maafisa kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)*. *(Makofi)*

Watendaji wa Wizara ya Fedha na taasisi zake. *(Makofi)*

Menejimenti ya Ofisi ya Bunge. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia kuwa Ofisi ya Bunge kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, imeandaa Tamasha la *Grand Bunge Bonanza* litakalofanyika siku ya Jumamosi, tarehe 20 Juni, 2026 katika Uwanja wa Jamhuri, Dodoma. Bonanza hili litakuwa la kihistoria kwa kuwa litawashirikisha Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Mabalozi wa nchi mbalimbali zinazowakilisha hapa nchini. Viongozi wa Serikali, watumishi Ofisi za Bunge, wananchi, taasisi za umma zilizoalikwa na wadhamini wakuu wa *CRDB Bank*.

Bonanza hili litatanguliwa na matembezi yatakayoanzia Bungeni saa 12.30 asubuhi na kuelekea Uwanja wa Jamhuri. Baadhi ya michezo ya ushindani ya burudani itakayofanyika ni mpira wa miguu, mpira wa pete, mpira kikapu, mpira wa wavu, mbio, kuvuta kamba, kukimbiza kuku, drafti na karata.

Kauli mbiu ni: "Pamoja *AFCON,* Tanzania Tuko Tayari."

Waheshimiwa Wabunge, wote mnahimizwa kuendelea kufanya mazoezi kwa ajili ya kushiriki bonanza hili muhimu.

Waheshimiwa Wabunge, ninatangaza kuwa siku ya Ijumaa tarehe 12 Juni kutakuwa na mdahalo kuhusu bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Mdahalo huo utafanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa kuanzia saa 4.00 asubuhi. Waheshimiwa Wabunge, wote mnakaribishwa kuhudhuria mdahalo huo muhimu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupokea maelezo kuhusu Hali ya Uchumi na Hotuba ya Bajeti ya Serikali kesho siku ya Ijumaa tarehe 12 Juni, 2026 hakutakuwa na Kikao cha Bunge. Siku hii itatumiwa na Wabunge kusoma na kutafakari kwa kina hotuba zote mbili zilizowasilishwa muda mfupi uliopita siku ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, mjadala wa jumla utaanza siku ya Jumatatu tarehe 15 Juni, 2026. Mjadala huu utakuwa wa siku zisizozidi saba na utamalizika siku ya Jumanne tarehe 23 Juni ambapo Wabunge watapata nafasi ya kupiga kura ya wazi kwa mujibu wa Kanuni ya 128 ya Kanuni za Kudumu ya Bunge, 2025.

Waheshimiwa Wabunge, mnasisitizwa kutumia siku ya kesho vizuri kwa kupitia nyaraka zote zilizowasilishwa ambazo zipo kwenye vishikwambi vyenu ili wakati wa mjadala muweze kuishauri Serikali ipasavyo. Inaelekezwa kwamba, kama Wabunge walivyojaa leo kwenye ukumbi huu na kwa heshima ya bajeti hii ambayo inakwenda kutoa mwanga kwa Watanzania inasisitizwa kuwepo kwa Wabunge wote kama mlivyokuwa humu ndani leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno haya ninamshukuru sana na kumpongeza Waziri wa Fedha na timu yake, peke yake asingeweza, ameshirikiana na watu na Kamati zetu za Bunge zote ambazo zimeshiriki katika kuandaa bajeti hii na kutoa ushauri mbalimbali kwa Serikali.

Ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka tarehe 15 Juni, siku ya Jumatatu, saa 3.00 asubuhi.

**11 JUNI, 2026**

*(Saa 12.06 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 15 Juni, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA